Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

### MKUTANO WA NNE

**Kikao cha Ishirini na Nane – Tarehe 24, Julai, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Kabla ya kuendelea na shughuli nina matangazo machache tu ya utangulizi.

Waziri wa Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Shukuru Kawambwa, anao wageni ambao wametoka Jimboni kwake kuhudhuria Kikao cha leo cha Bunge wako kumi na nne (14).

Katibu wa CCM Wilaya ya Bagamoyo naomba asimame pale alipo. Katibu wa Vijana, Katibu wa Wazazi, Katibu wa Jumuiya ya Wanawake (UWT) na Madiwani wote wa Jimbo la Uchaguzi la Bagamoyo wakiongozwa na Mheshimiwa Almasi Masukuzi, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Bagamoyo, wale pale karibuni sana. Waheshimiwa, tunashukuru sana mmeona ni vema mje muungane nasi kushuhudia shughuli za Bunge letu. (*Makofi*)

Kwa umuhimu huo huo naomba nimtambulishe Mama Kawambwa, mkewe Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na watoto wao watatu, nadhani ni wale pale. Karibuni sana Bungeni.(*Makofi*)

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007.

**MHE. JOYCE N. MACHIMU – (k.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO NA ARDHI):**

Maoni ya Kamati ya Kilimo na Ardhi Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara Hiyo kwa Mwaka 2006/2007.

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa ni Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu sekta ya kilimo na ardhi.(*Makofi*)

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI:**

Maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, Pamoja na Maoni Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Waziri hiyo kwa Mwaka 2006/2007.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 260

### Vifaa Vya Kinga kwa Wazoa Taka

**MHE. MWAKA ABDULRAHAMAN RAMADHAN** aliuliza:-

Kwa kuwa kuna utaratibu wa Afya ya Wafanyakazi *Occupational Health*, Mfanyakazi anahitaji kujikinga na madhara ya kiafya anapofanya kazi O*ccupational Hazard* anatakiwa avae vitendea kazi vya kinga:-

(a) Je, kwanini wazoa takataka katika magari ya taka hasa wa Magomeni Mapipa wanazoa taka bila vitendea kazi vitakavyowalinda kama vile *gloves* na *mask* za pua?

(b) Je, wafanyakazi hao huwa wanapimwa afya zao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa, Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwaka Abdulrahaman Ramadhan, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna utaratibu wa uwekaji Kinga ya Afya na ajali kwa wafanyakazi wanapokuwa kazini. Aidha, wafanyakazi wote kutegemea mazingira ya kazi wanazofanya wanatakiwa kutumia vifaa vya kinga ya afya na ajali. Kwa upande wa wafanyakazi wa wanaozoa taka wanatakiwa wavae vifaa vya kinga ya

mdomo (*masks*), mikono (*gloves*), sare (*reflectors*) kofia (*headgear)* pamoja na viatu imara (kama, *gumboots)* ili kujikinga na uwezekano wa kupatwa na magonjwa ama kupatwa na ajali yoyote wanapokuwa kazini.

Mheshimiwa Spika, ni kweli pia kulikuwa na tatizo la wazoa taka kufanya kazi bila vifaa vya kinga katika magari ya taka ya Magomeni Mapipa na kwingineko katika Manispaa ya Kinondoni. Kwa hivi sasa kazi ya uzoaji taka katika maeneo mbalimbali ya Manispaa imetolewa kwa sekta binafsi. Kutokana na hatua hii tatizo la wafanyakazi kutotumia vifaa vya kinga kidogo limepungua. Hata hivyo ili kuhakikisha kuwa kuna mazingira salama ya wafanyakazi, hatua zifuatazo zimechukuliwa na Halmashauri husika:-

(i) Manispaa kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (*ILO*) imeanzisha programu ya uhamasishaji inayofanyika katika ngazi zote za Utawala ili kusisitiza matumizi ya vifaa vya kinga ya afya kwa wafanyakazi wanao zoa taka.

(ii) Manispaa imeweka taratibu za ufuatiliaji wa karibu kuona kwamba makampuni ya kuzoa taka yanatekeleza suala la vifaa vya kinga kwa wafanyakazi wao.

(iii) Manispaa imeendelea kuimarisha mfumo wake wa ukaguzi wa huduma za usafirishaji, msisitizo mkubwa ukiwa kwenye kufuatilia namna bora ya matumizi ya vifaa vya kinga ya afya na ajali kwa wazoa taka.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli vikundi na Makampuni yanayotoa huduma ya uzoaji taka yameboresha zaidi hali ya matumizi ya vifaa vya kinga kwa wafanyakazi ingawa bado hawajafikia kiwango cha juu cha matumizi hayo. Hata hivyo kuna baadhi ya wafanyakazi wa kuzoa taka wamekuwa wazembe kuvitumia vifaa hivyo na hivyo kuhatarisha afya zao. Aidha ni wazi kuwa matandao wa ufuatiliaji haujafanikiwa kufika katika maeneo yote ya Manispaa, hivyo tunawaomba wadau wote waonapo kasoro kama hizi waiarifu Mamlaka husika ili waajiri wa wazoa taka hao waweze kuchukuliwa hatua zinazostahili mara moja.

(b) Mheshimiwa Spika, ni jukumu la kampuni husika kuhakiki kuwa wafanyakazi wao wana afya njema kwa kuwapa vifaa vya kinga ya afya zao na kuwawekea bima ya afya na pia kuwapima afya zao mara kwa mara. Hata hivyo imebainika kuwa wengi wa wazoa taka ni wafanyakazi wa muda yaani vibarua wa siku na hivyo hawapimwi afya zao. Manispaa ya Kinondoni kwa kushirikiana na sekta binafsi, wanaendelea kuboresha mazingira ya kazi ya uzoaji taka ili kuwavutia wafanyakazi wa ajira ya muda mrefu ambao pia watawekewa Bima na kupimwa afya zao mara kwa mara.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa sio tu Dar es Salaam peke yake na maeneo mengi afya ya mfanyakazi na kuvaa vifaa vinavyomtakia ajikinge imeonekana si suala linalochukuliwa umuhimu wake. Unajikuta hata wanaofanya kazi ya vumbi wanapewa maziwa badala ya kuwekewa bima.

Je, kuna chombo au sheria inayofuatilia suala hili kuwa watu wasipofuatilia suala hili la *Occupational Heath* wachukuliwe hatua?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Usalama yaani *Occupational Health and Safety* ya mwaka 2004 kifungu namba 24.(2) kinasisitiza juu ya umuhimu wa kuvaa vifaa salama ili kujikinga na maradhi. Pia katika kila Halmashauri kuna Sheria ndogo ndogo ambazo pia zinahusu usafi na mazingira. Vilevile Serikali katika Manispaa au Halmashauri mbalimbali kuna wakaguzi wa afya wanapita sehemu mbalimbali ili kuhakikisha kwamba wafanyakazi au hao wazoa taka wanavaa vifaa vya kinga kama vile nilivyovitaja hapo juu, *gloves*, *Helmet* na pia *gumboots* na makoti ili kujikinga na afya zao.

Lakini ninachosisitiza ni kwamba naomba wadau mbalimbali tushirikiane kuhakikisha kwamba hao wafanyakazi wanavaa vifaa hivyo, wengi hawapendi kutumia vifaa hivyo. Kwa hiyo, naomba wadau mbalimbali tushirikiane, sheria zipo na Serikali inasisitiza ili kuhakikisha kwamba hao wafanyakazi wanakuwa salama.

Na.261

**Kilimo cha Umwagiliaji – Bonde la Mto Bubu.**

**MHE. PASCHAL C. DEGERA** aliuliza:-

Kwa kuwa utafiti uliofanywa mara nyingi umeonyesha kuwa Bonde la Mto Bubu linafaa kwa kilimo cha umwagiliaji

Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati muafaka wa kutekeleza mradi huo ili kuwapunguzia wananchi wa Mkoa wa Dodoma umaskini iliokithiri?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paschal Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua tafiti mbalimbali zilizokwishafanywa katika Bonde la Mto Bubu kuanzia Kondoa hadi Bahi.

Mheshimiwa Spika, kaitka miaka ya 1970 baada ya Serikali kuanzisha Mipango wa Maendeleo ya Uwiano ya Mikoa (*RIDEPS*), na baada ya mji wa Dodoma kutangazwa rasmi kuwa Makao Makuu ya Serikali, tafiti zilianza upya katika Bonde la Mto Bubu kwa kutumia wataalam Wazalendo wa iliyojulikana *Water Development and Irrigation Division (WD&ID).*

Aidha kati ya mwaka 1974 na 1977 wakati wa Serikali inaandaa *Dodoma Region Water Master Plan,* iliyokuwa Wizara ya Maji, Madini na Nishati ilifanya uchunguzi mwingine katika Bonde la Mto wa Bubu kwa lengo la kupata maji ambayo yangekidhi mahitaji ya maji wa Dodoma na Vijijini vinavyouzunguka mji.

Mheshimiwa Spika, kilele cha tafiti za Mto Bubu zilihitimishwa na kampuni ya Ujerumani inayoitwa *Agrar-Und Hudrotechnic (GMBH)* ambayo mwaka 1984 iliandaa usanifu na makisio ya ujenzi wa mabwawa ya Farkwa na Upendo kwa ajili ya kumwagilia mashamba yenye ukubwa wa hekta 10,000.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 1984 gharama za mradi mzima zilikadiriwa kuwa *USD* milioni 75 na shilingi bilioni 3.011 za Tanzania. Kwa wakati huo Serikali haikuwa na uwezo wa kutekeleza mradi huu kutokana na gharama yake kubwa sana kwa kuzingatia vipaumbele vingine vya maendeleo vilivyokuwepo wakati huo. Muda mrefu umepita, baadhi ya malengo, mikakati na gharama za utekelezaji vimebadilika; vitahitajika kuchunguzwa na kuboreshwa upya ili vizingatie mikakati mingine mipya kama vile MKUKUTA, athari kwa mazingira, nishati mbadala na kadhalika.

Mheshimiwa Spika , Bonde la Mto Bubu limetambuliwa na kuainishwa na Wizara katika Mpango Kamambe wa Kilimo cha Umwagiliaji Maji. *(National Irrigation Master Plan (NIMP)* uliokamilika mwaka 2003. Miradi iliyoainishwa chini ya *NIMP* inaanza kutekelezwa katika programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo *(ASDP)* ambayo katika utekelezaji wake kwa kipindi cha miaka saba unaanza mwaka huu, 2006/2007.

Katika programu hii sekta ndogo ya umwagiliaji itatumia takribani shilingi trilioni 1.4 na mradi ya umwagiliaji itakayoibuliwa katika Bonde la Mto Bubu itaendelezwa chini ya Programu hii. Wazira itaendelea kushirikiana na Halmashauri za Mkoa wa Dodoma kuchambua miradi ya umwagiliaji inayoweza kutekelezwa kwa gharama nafuu na kuiweka katika Mipango ya Maendeleo ya Wilaya (*DADPs*) ili iombewe fedha za utekelezaji kwa awamu ili hatimaye Bonde la Mto Bubu liendelezwe kwa ujumla. *(Makofi)*

Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na wananchi wote wa Kondoa na Mkoa wa Dodoma kwa ujumla kwamba nia ya kuendeleza Kilimo cha umwagiliaji katika Bonde la Mto Bubu bado ipo pale pale na itatekelezwa kwa utaratibu niliyoueleza. *(Makofi)*

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa katika majibu yake, Naibu Waziri amekiri kwamba mradi huu kama utatekelezwa utakuwa wa manufaa makubwa sana kwa wananchi wa Mkoa wa Dodoma kwa ujumla; na kwa kuwa amesema kwamba kutokana na gharama za mradi wenyewe mradi unatakiwa utekelezwe kwa awamu.

Je Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba tuanze na ujenzi wa bwawa lenyewe ambalo lina gharama ndogo sana kuzui maji ili wananchi waanze kunufaika na huduma ya maji ya matumizi ya nyumba, mifugo, ufugaji wa samaki na umwagiliaji mdogo mdogo

La pili, kwa kuwa mradi huu unagusa Wizara nyingi, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Wizara ya Miundombinu kwa sababu kuna ujenzi wa daraja pale, Wizara ya Nishati na Madini kwa sababu kuna uzalishaji wa umeme na Wizara ya Maliasili na Utalii kwa sababu kuna ufugaji wa samaki. Je Mheshimiwa Naibu Waziri haoni haja ya kushirikisha wadau wote hawa ili wote waweze kuchangia utekelezaji wa mradi huu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE)**: Mheshimiwa Spika, kuhusu pendekezo la Mheshimiwa Mbunge kwamba kama awamu nilizozitaja hapa zianze na ujenzi wa bwawa, niseme tu kwamba nimeeleza hapa kwamba utaratibu wa uibuaji wa hii miradi unatakiwa uanzie na Halmashauri zetu za Wilaya kwa kushirikiana na Ofisi zetu za Kanda za umwagiliani zilizoko huku kwenye Kanda zetu na kwenye Kanda ya eneo hili la Dodoma ni Kanda ya Manyara Mtaalam yuko kule Babati. Kwa hiyo, nishauri kwamba endapo wananchi wataona umuhimu wa kwanza katika utekelezaji wa mradi huu uanzie bwawa Serikali haitakuwa na kipingamizi isipokuwa itabidi utafiti rasmi ufanyike kuona uwezekano wa utekelezaji wa jambo hili.

Mheshimiwa Spika la pili nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba mradi ule wa Mto Bubu kama ulivyofanyiwa utafiti awali ulikuwa unagusa Wizara nyingi kama alivyosema, na kama nilivyoeleza katika jibu la msingi kwamba vipaumbele vya wakati ule hivi sas vimebadirika. Kwa mfano wakati ule ilikuwa imefikiriwa kwamba mradi ule wa Mto Bubu ndiyo ungewezesha kuleta maji ya kutosheleza mji wa Dodoma hapa na vijiji vya jirani.

Lakini hivi sasa kama wote tunavyofahamu maji ya hapa Dodoma sasa hivi yako kiwango cha ziada na miradi mingine ambayo inaweza itaingia katika utekelezaji huu ni hiyo ya barabara kama alivyokua amesema. Sasa kwa sababu miradi hii ambayo ni miradi mtambuka mimi nakubaliana naye kwamba tunaweza tukashirikiana na Wizara nyingine wakati wa utekelezaji utakapofika.

Na 262.

**Mahitaji ya Umeme Kisesa**

**MHE. LUHAGA J. MPINA** aliuliza:-

Kwa kuwa, wananchi wa Jimbo la Kisesa wanajishughulisha na kilimo, biashara, ufugaji na kadhalika na kwa kuwa kuna vituo vya afya shule, zahanati na kadhalika lakini hakuna umeme.

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme kwenye Makao Makuu ya Jimbo na maeneo mengine?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika naomba kujibu swali la Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mbunge wa Kisesa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Makao Makuu ya Jimbo la Kisesa ni kati ya maeneo kadhaa ya vijiji vya Mkoa wa Shinyanga vilivyopendekezwa kupatiwa umeme chini ya mpango wa kusambaza umeme unaojulikana kama *Energizing Rural Transformation (ERT).* Jumla ya shilingi milioni 544/- zinahitajika kupeleka umeme kwenye Makao Makuu ya Jimbo yaani Mwandoya, pamoja na maeneo yaliyojirani. Mradi huu utatekelezwa baada ya kuanza kwa utekelezaji wa mpango wa *ERT*.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona, kwa kuwa wananchi wa Kata ya Mgandu nao wanajishughulisha sana na masuala ya kilimo na biashara; na kwa kuwa wana hospitali wanayoitegemea ya pale Mitundi pamoja na shule ya sekondari. Je, Wizara imepanga vipi kusogeza umeme kutoka Itigi kwenda Mitundu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni lengo la Wizara yangu kuhakikisha kwamba Makao Makuu zote za Wilaya hapa nchini zipate umeme chini ya mipango mbalimbali ikiwemo *ERT.* Ningemwomba Mheshimiwa Mbunge kama akitaka kufahamu kama maeneo ya vijiji alivyovitaja vitakuja kupata umeme aje ofisini kwangu tuangalie mipango ya *ERT* na mipango mbalimbali ili tuweze kumfahamisha vizuri. *(Makofi)*

Na. 263

**Uzalishaji wa Umeme wa Upepo**

**MHE. LAUS O. MHINA** aliuliza:-

Kwa kuwa uzalishaji wa umeme nchini hutegemea sana maji yatokanayo na mvua na njia nyingine zinazotarajiwa kutumika ni *gas*, mafuta na makaa ya mawe na kwa kuwa tafiti mbalimbali zimeonesha kuwa upepo unaweza kuwa nishati nzuri, rahasi na isiyoharibu mazingira katika kuzalisha umeme na pia Tanzania inayo maeneo mengi yenye upepo mkali kwa mfano Dodoma, Iringa na Kilimanjaro na kwa kuwa teknolojia hiyo inatumika na imeonyesha mafanikio katika nchi nyingi za Afrika na kwingineko:-

Je, Serikali haioni kuwa kuna umuhimu wa kuwashawishi wawekezaji kuwekeza kwenye nishati hii rahisi, isiyochafua mazingira wala kuhitaji mafuta?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Laus Mhina, Mbunge wa Korogwe Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa upepo ni chanzo kizuri na salama kwa mazingira katika uzalishaji wa umeme. Hata hivyo, baadhi ya vyanzo vya nishati mbadala hasa upepo, ni *site-specific* vikilinganishwa na nishati ya jua ambayo iko kila mahali. Kwa mfano, sehemu ambazo zingependekezwa kwa ajili ya *wind power generation* utakuta kasi ya upepo iko chini sana katika eneo husika. Hivyo, teknolojia ya nishati ya upepo inahitaji kufanyiwa tathimini ya kutosha kabla ya kufikia uamuzi wa kuzalisha umeme kwa mfumo wa *wind farms* kama ilivyo katika baadhi ya nchi kama Marekani, Denmark, Ujerumani, Uholanzi, India na kadhalika. Katika baadhi ya sehemu nishati ya upepo hutumika kwa kusukuma maji *(Mechanical not electrical power for water pumping)*. Hapa nchini, upepo umekuwa ukitumika maeneo mengi kwa ajili ya kusukuma pampu za maji hasa katika Mikoa ya Arusha, Singida na Dodoma. Kitaalamu upepo unaohitajika kwa ajili ya kuzalisha umeme unatakiwa uwe wa kasi ya juu zaidi kuliko ule ambao ungetakiwa kuendesha pampu kwa ajili ya kusukuma maji.

Mheshimiwa Spika, suala la uendelezaji wa nishati ya upepo kwa ajili ya kuzalisha umeme limepewa kipaumbele ambapo miaka mitatu iliyopita, Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Denmark ziliwezesha upimaji wa kasi ya upepo kufanyika katika maeneo manne nchini. Maeneo hayo ni Gomvi Mkoani Dar es Salaam, Mkumbara Mkoani Tanga, Litembe Mkoani Mtwara na Karatu Mkoani Manyara. Katika utafiti huu vituo vya Mkumbara na Karatu vilionyesha kuwa upepo unaofaa kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Spika, Wizara na *TANESCO*, wanaendelea na maandalizi ya kufanya awamu ya pili ya utafiti *(economic feasibility)* kwa kuchagua maeneo halisi huko Mkumbara na Karatu ambayo yatafanya uzalishaji uvutie kibiashara. Sambamba na jitihada hizo, Serikali ino mpango wa kuainisha maeneo mengine nchini yenye kasi kubwa ya upepo ili kuangalia uwezekano wa kazilisha umeme pia.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, asante, Wizara ya Nishati na Madini kwa kutumia shirika lake la *TANESCO* wamefanya kazi nzuri sana pale Makambako ya kuangalia kasi ya upepo na hivi sasa wako pale na kuna mategemeo ya kutumia upepo ule kutoa umeme. Labda Mheshimiwa Naibu Waziri hiyo taarifa hakuwa nayo kama hakuwa nayo, je anakubaliana kwamba kuna kituo hivi vile vile?

**SPIKA:** Mheshimiwa Makwetta swali lako halikusikika nadhani ulikuwa mbali na chombo cha sauti. Tafadhili rudia.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA**: Mheshimiwa Spika, nimesema kwamba, Wizara ya Nishati na Madini kwa kutumia shirika lake la *TANESCO* wamefanya kazi nzuri sana pale Makambako ya kuangalia kasi ya upepo na hivi sasa wako pale na kuna

mategemeo ya kutumia upepo ule kutoa umeme na kuna matumaini kwamba upepo wa pale ni wa kasi kupita maeneo mengine mengi ya Tanzania. Swali lilikuwa kwamba Naibu Waziri alisahau kituo hiki au alikuwa hana habari kama hakuwa na habari ajue kuna hiki, je atakubalina na suala hilo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi, Wizara yangu pamoja na *TANESCO* inafanya kazi sasa hivi kuanisha maeneo mbalimbali katika nchi ambayo yana kasi ya upepo wa kutosha ikiwemo Makambako.

Lakini utafiti wa Makambako haujakamilika na pale utakapo kamilika tutahakikisha kwamba tutamfahamisha Mheshimiwa Makwetta kama eneo la Makambako lina kasi ya upepo wa kutosha kuzalisha umeme kibiashara.

Na. 264

**Barabara ya Mtwara – Masasi**

**MHE. JUMA A. NJWAYO** aliuliza:-

Kwa kuwa Wilaya za Tandahimba, Newala, Masasi na Mtwara Vijiji ni wazalishaji wakubwa wa korosho, zao ambalo linachangia kwa kiwango kikubwa pato la Taifa lakini barabara ya kutoka Mtwara – Tandahimba – Newala – Masasi ambayo hutegemewa kwa usafirishaji wa zao hilo ni mbovu, korofi na ngumu kupitika:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuiweka lami barabara hiyo?

**NAIBU WAZIRI WIZARA YA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mbunge wa Tandahimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba barabara ya mkoa ya Mtwara – Newala hadi masasi ni muhimu sana kwa uchumi wa Mkoa wa Mtwara kwa sababu ndiyo inayosafirisha mazao ya biasahara kwenda Bandari ya Mtwara. Ni kweli pia kwamba hali ya barabara hiyo ni mbaya hasa wakati wa majira ya mvua ikizingatiwa kuwa barabara hiyo ni ya udongo na haijapata matengenezo makubwa kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa mwaka huu haina uwezo wa kuijenga barabara hiyo yote ya kilomita 211 kwa kiwango cha lami kwa sababu ya ufinyu wa Bajeti, lakini itaishughulikia kwa kiwango cha changarawe kwa sehemu ili ipitike wakati wa mvua.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya umuhimu wa barabara hii, katika mwaka wa fedha 2005/2006 Serikali ilitenga fedha kiasi cha shilingi milioni 440 kwa ajili ya matengenezo maalum. Matengenezo haya yalihusisha uwekaji wa lami eneo la Mpeta hadi Masasi, Milima ya Nanyamba na Namaleche na pia uimarishaji wa madaraja ya

Mwiti na Nyakato. Serikali pia ilitenga fedha kwa ajili ya matengenezo ya kawaida kiasi cha shilingi milioni 79. Aidha, kiasi cha shilingi milioni 200 zilitengwa kwa ajili ya kuijenga kwa kiwango cha changarawe sehemu ya barabara hiyo yenye urefu wa kilometa 13.3 kati ya vijiji vya Mbawala na Maranje. Kazi hizo karibu zote zimekamilika pamoja na kilomita 6 kati ya Masasi na Mpeta.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha 2006/2007, kilometa 50 za barabra hiyo kuanzia Maranje hadi Tandahimba zitafanyiwa matengenezo makubwa kwa kiwango cha changarawe. Shilingi mbilioni 1.056 zimetengwa kwa ajili hiyo. Pia matangenezo makubwa yatafanyika kati ya Newala na Mahuta kilometa 10.6 kwa gharama ya shilingi milioni 190.89. Kwa matengenezo haya, sehemu kubwa ya barabara hii itakuwa imepata matengenezo makubwa ya kuifanya iweze kupitika wakati wote.

**MHE. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, ni seara ya Serikali kwamba kila Makao Makuu ya Mkoa yafikike kwa lami. Na barabara inayozungumzwa, ndiyo inayopita katika Wilaya zote tano za Mkoa wa Mtwara yaani Nanyumbu, Masasi, Newala, Tandahimba na Mtwara. Je, Serikali ina majibu gani kuhusu azimio la Bodi ya barabara ya Mkoa wa Mtwara iliyopendekeza barabara ile kurudishiwa hadhi yake ya zamani kama barabara inayomilikiwa na Serikali Kuu badala ya *Regional Manager* wa *TANROADS* na hatimaye kuweka lami? Nini majibu ya Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya lami kufika katika makao makuu ya mkoa, kwa sasa barabara ya lami ambayo inafika Mtwara ni ya Masasi – Mnazi Mmoja – Mtwara. Kwa hiyo, kuna barabara ya lami inayounganisha Makao Makuu ya Mkoa wa Mtwara. Lakini, ni kweli kwamba barabara hiyo aliyoitaja inapita katika Wilaya nyingi, lakini kama nilivyosema katika jibu la msingi, kwa sasa Serikali nitaendelea kuboresha barabara hiyo inayopitia Tandahimba kwa kiwango cha changarawe ili iweze kupitika wakati wote. Lakini katika siku zinazokuja, kama uwezo utakuwepo, barabara hiyo inaweza kufikiriwa kuwekwa lami, lakini kwa sasa turidhike kwamba tutaendelea kuikarabati kwa kiwango cha changarawe na maeneo korofi sana tutaweka lami kama ambavyo nimesema kwenye jibu langu la msingi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maamuzi au mapendekezo ya Bodi ya Barabara ya Mkoa, hayo yatashughulikiwa kwa utaratibu wake pale tutakapokuwa tumepokea mapendekezo hayo.

Na. 265

**Kuzidisha Abiria – Vyombo vya Baharini**

**MHE. MGENI J. KADIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa vipo vyombo vingi vya usafiri majini ambavyo hupakia abiria zaidi ya uwezo wake na hivyo kuhatarisha maisha ya abiria hao, na kwa kuwa vyombo hivyo mara nyingi huwa vichakavu:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa hali hiyo inahatarisha maisha ya watu na mali zao?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kukomesha tabia hiyo ili kunusuru maisha ya watumiaji wa vyombo hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge wa Vita Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Usafiri Majini (*Merchant Shipping Act)* ya mwaka 2003, ndiyo Sheria mama inayosimamia usalama wa usafiri majini. Kifungu cha 155 cha sheria hiyo kinamtaka mwenye meli, nahodha na hata Wakala wa meli kuhakikisha kuwa chombo chake ni salama kahakijapakia abiria au mizigo. Na ni wajibu wa Mkaguzi wa Meli kufanya ukaguzi mkubwa wa meli mara moja kwa mwaka kwa ajili ya kutoa cheti cha ubora wa meli na ukaguzi wa chombo mara uharibifu au matatizo ya aina yoyote yanapoweza kujitokeza wakati wowote.

Mheshimiwa Spika, ni marufuku kabisa kwa wamiliki wa vyombo vya usafiri majini kupakiza abiria zaidi ya uwezo wake. Wote wanapaswa kuzingatia vyema sheria hiyo na taratibu zilizowekwa ili kuepusha ajali zinazoweza kutokea. Wizara kupitia mdhibiti wa vyombo hivyo, *SUMATRA* itaendelea kuelimisha jamii na wenye vyombo hivyo, ili waelewe madhara yanayotokana na kupanda chombo chenye abiria kuzidi uwezo wake, umuhimu wa kuwa na vifaa vinavyotakiwa kuwemo katika vyombo hivyo na namna ya kuvitumia pindipo mahitaji ya dharura yatakapojitokeza na kuendelea kuvikagua kama sheria na taratibu zinavyoeleza.

Serikali itasimamia vyema *SUMATRA* kuona wamefungua Ofisi Mikoani zitakazoshughulikia lusalama wa vyombo vya majini katika maeneo husika, hii ni pamoja na kuwepo katika magati wakati vyombo hivyo vinapofanya kazi ya kupakia na kupakua abiria na mizigo. Adhabu zinazohusika kutolewa kwa wale wote wanaoenda kinyume na Sheria hizi zimeelezwa wazi katika Sheria inayosimamia usafiri majini ya mwaka 2003 na tutahakikisha zinachukuliwa.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kumekuwa kukitokea ajali kama ya vyombo majini kwa mfano Mwanza, ilitokea katika Ziwa Victoria mwaka 1996. Je, hao wanaomiliki hivyo vyombo vya majini, huwa wanakuwa wamewawekea Bima abiria wao wanapowachukua kabla ya kuondoka?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, kimsingi, wenye meli wanapaswa kukata Bima ya meli kwa abiria zao na meli yao.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Nami napenda niulize Swali dogo kama ifuatavyo: Kwa kuwa, tatizo la uchakavu wa vyombo vya majini, ni kutokana na uwezo mdogo wa wale wanaomiliki vyombo vyao katika Ziwa au Bahari. Na kwa kuwa ujazaji wa abiria wengi ni kutokana na uchache wa vyombo vyenyewe katika Ziwa au Bahari. Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuwasaidia wananchi niseme kwa mfano hasa wanaoishi katika maeneo yanayozunguka Ziwa walio na nia ya kuwekeza katika usafiri wa Ziwa, maanake kwenye Ziwa vinavyotumika sana ni mitumbwi inayotumia *engine*, siyo meli, mitumbwi ambayo inamilikiwa na wananchi binafsi. Je, Serikali inawasaidia vipi ili wananchi wengi waweze kununua mitumbwi na *engine* kwa wingi waache kujazana kwenye vyombo hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, kwanza labda nimfahamishe Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, kwamba uchakavu ni uchakavu wa vyombo, lakini hauhusiani kabisa na uwezo mdogo wa wenye meli. Kwa hiyo, wanaomiliki meli wanapaswa wawe na uwezo na uzoefu wa kufanya shughuli hizo ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, Serikali itaendelea kuweka mazingira mazuri kwa wananchi wanaoweza kuwekeza katika maeneo hayo, waweze kufanya shughuli hizo ipasavyo ikiwa ni pamoja na kutengeneza magati ili shughuli za kupakua na kupakia mizigo iwe salama na kitengo cha uwekezaji cha *TICKS* kiko kwa ajili ya kufanya shughuli hizo.

Na. 266

**Ukarabati wa Bwawa la Kalemawe**

**MHE. ANNE K. MALECELA** aliuliza:-

Kwa kuwa Kata ya Ndungu imebahatika kuwa na Bwawa la asili la Kalemawe ambalo linasaidia wananchi wa Kata ya Ndungu, Kihurio, mpaka Bendera kwa shughuli za kilimo, matumizi ya nyumbani na kuwapatia wananchi samaki. Na kwa kuwa, bwawa hilo limepoteza hadhi yake kabisa na kushindwa kuwasaidia wananchi kikamilifu katika kilimo, matumizi yao ya nyumbani pamoja na kitoweo;

Je, Serikali ya awamu ya nne yenye lengo kuu la kuleta maisha bora kwa wananchi ina mpango wa nguvu na wa uhakika wa kusaidia kiutaalamu kulikarabati Bwawa hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Jimbo la Same Mashariki, naomba kutoa maelezo yafutayo:-

Mheshimiwa Spika, Bwawa la Kalemawe, lililopo katika Kijiji cha Ndungu, lilianza kujengwa mwaka 1957 na kukamilika mwaka 1959 likiwa na mita za ujazo milioni 34.5. Lengo la kujenga Bwawa hili lilikuwa ni kuzuia mafuriko yasitokee, wakati wa mvua nyingi za masika, kwenye vijiji vilivyopo ukanda wa tambarare hasa vijiji vya Bendera na Mkomazi. Aidha, lengo lingine lilikuwa ni kuimarisha kilimo cha umwagiliaji wakati wa kiangazi kwenye eneo la hekari 6,000 katika vijiji vya Kihurio, Kalemawe na Mkomazi na ufugaji wa samaki kwa ajili ya biashara na kitoweo.

Mheshimiwa Spika, mafuriko yaliyotokea mwaka 1977 yalifanya uharibu wa Bwawa ambapo Serikali ilifanya matengenezo ya Bwawa hilo kwa gharama ya shilingi 1,200,000/=. Aidha, katika mafuriko ya mwaka 1993, Bwawa liliharibika tena na Serikali kufanya matengenezo kwa gharama ya shilingi 7,586,000/=.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukarabati ambao ulifanyika kwa vipindi viwili tofauti, bado nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kuwa Bwawa hili linahitaji ukarabati. Hivyo, Serikali ya awamu ya nne itashirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Same kufanya tathmini na uchunguzi wa kina, ili kupata gharama halisi za ukarabati.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshauri na kumwomba Mheshimiwa Mbunge, kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya, watoe kipaumbele kwa Bwawa hilo na kuliingiza kwenye Bajeti ya Wilaya, katika kipindi kijacho cha Bajeti ili Wizara tuweze kulishughukia. Aidha, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge awahamasishe wananchi wanaoishi maeneo ya juu *(upstream)* na yale yanayozunguka Bwawa kuacha kulima katika maeneo hayo kama inavyoelekezwa na wataalamu wa maji ili kupunguza udongo unaoingia kwenye Bwawa na kuathiri kina cha Bwawa na hivyo kupunguza wingi wa maji.

**SPIKA:** Kabla sijamwita Mheshimiwa Anne Kilango Malecela aulize swali la nyongeza, nashangaa Waheshimiwa Wabunge mnaonekana mmepoa sana, mmetulia! Ninapenda niseme kwamba mkiendelea hivi, mtanisononesha, kwa sababu leo ni Siku Kuu ya Kuzaliwa ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta. Sasa, hali hii ya kununa kwenu, hailingani. Naomba mniunge mkono kuifurahia siku hii. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Nashukuru kwa majibu ya Naibu Waziri. Lakini kwa kuwa swali hili linalohusu Bwawa la Kalemawe, nilishaliuliza kwenye Bunge hili mwaka 2004 na nikaonyesha ni *serious* kiasi gani Bwawa hili linahitaji mkono wa Serikali. Na kwa kuwa kipindi hicho cha mwaka 2004 nikiwa Mbunge wa Taifa, nilipewa majibu mazuri sana ya kutia matumaini na aliyekuwa Waziri wa Maji wa kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, naomba kulijulisha Bunge lako hili kwamba kwa kweli Halmashauri ya Wilaya ya Same haina uwezo wa kuboresha Bwawa hili. Je, kwa kuwa nilishapewa majibu mazuri sana na Waziri wa Maji wa kipindi kile kwamba Serikali kuu itakwenda kuliona Bwawa hili na kupeleka wataaalam, leo Serikali inaniambia nini kuhusu kupeleka wataalamu na yenyewe Serikali Kuu kwenda.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa wananchi wa Kata ya Kihurio, Ndungu, Bendera na mpaka Mkomazi walishatumia nguvu zao kutengeneza mifereji miwili ili kuchukua maji kutoka kwenye Bwawa hili kwa ajili ya umwagiliaji kwenye mashamba yao. Na kwa kuwa sasa hivi wanakwama na wanakumbwa na matatizo ya njaa. Je, Serikali haioni kwamba kwa kutokuchukua hatua ya dharura, ni yenyewe inasababisha njaa kwa wananchi hawa?

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahadi ilikwishatolewa na sisi tunatoa ahadi kwa kuahidi tena kwamba tunapeleka wataalamu kwenda kufanya tathmini na nataka kumhakikishia Mheshimiwa Anne K. Malecela kwamba wataalamu hao watakwenda muda siyo mrefu, mara tu baada ya Bunge hili ili kufanya tathmini itakayotuwezesha kujua namna tunavyoweza kukarabati Bwawa hilo na kuhakikisha kwamba haliwezi kuendelea tena kuathirika kutokana na mafuriko. Ili kulizuia lisipate mafuriko tena, inabidi utaalamu wa hakika ufanyike na hatuwezi kuufanya bila kufanya tathmini. Kwa hiyo naahidi watalaamu wataenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la njaa, tutawasiliana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa sababu wanao mpango wa umwagiliaji ambao umeelezwa vizuri ndani ya Bunge hili wakati wa Bajeti. Nadhani kwa kushirikiana Wizara hizi mbili, tunaweza tukafanya kazi ambayo itafanya wananchi wa maeneo hayo waweze kunufaika na Bwawa hilo. Kwa hiyo, tuvute subira. *(Makofi)*

**SPIKA:** Swali linalofuata Wizara hiyo hiyo linaulizwa na Mheshimiwa Mbaruk K. Mwandoro, Mbunge wa Mkinga.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Spika, ahsante!

**SPIKA:** Hebu tulia kwanza. Tulia tu kwanza kidogo. Ninafahamu Mheshimiwa Mbaruk K. Mwandoro ulipata mtihani kidogo wa afya na wiki iliyopita ulilazwa hospitali. Ni furaha kwa sisi Wabunge wote na kwa niaba yao nasema hivyo, kukuona tena ukiwa na afya njema na unashughulika. *(Makofi)*

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kabla sijauliza swali langu, naomba uniruhusu nichukue fursa hii nitoe salaam za pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kufikisha *Birth Day* yake leo. Hongera sana. sana

Na. 267

**Upungufu wa Maji**

**MHE. MBARUK K. MWANDORO** aliuliza:-

Kwa kuwa upungufu mkubwa wa maji umebainika kuwa kero kubwa sana takriban nchi nzima vijiji na mijini:-

(a) Je, isingekuwa vema Serikali kuutazama upya mpango kabambe wa maji kwa kuwashirikishaWabunge ili waupe kipaumbele, kuurekebisha ipasavyo na kuuwekea progaramu thabiti ya utekelezaji?

(b) Je, ni lini Serikali itaanzisha mfuko wa kuendeleza maji kama ilivyo kwa Mfuko wa barabara, MMEM na MMES hasa kwa kuzingatia mahitaji makubwa ya maji kwenye Kilimo cha umwagiliaji?

(c) Je, kama mpango huo umekwisha kurekebishwa, programu ya utekelezaji kukamilishwa na Mfuko wa maji wa Taifa kuundwa, Serikali inaweza kufikisha taarifa hizo rasmi Bungeni?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mbaruk K. Mwandoro, Mbunge wa Jimbo la Mkinga, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza vizuri Sera ya Maji ya mwaka 2002 na kufikia malengo ya MKUKUTA na yale ya Milenia, Wizara yangu imekamilisha maandalizi ya mkakati wa kuendeleza Sekta ya maji. Aidha, maandalizi ya mkakati huo yamehusisha wadau wa sekta ya maji na tayari umewasilishwa Serikalini kwa ajili ya kupitishwa. Aidha, Wizara yangu pia iko kwenye hatua za mwisho za kukamilisha maandalizi ya programu ya sekta ya maji. Programu hii ni mpango kabambe kwa kusambaza huduma ya maji hapa nchini na itaanza kutekelezwa katika kipindi cha mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbaruk K. Mwandoro, Mbunge wa Mkinga, swali lake lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na wazo la Mheshimiwa Mbunge la kuwashirikisha Wabunge katika kupitia na kutoa maoni juu ya programu ya sekta ya maji kwani wao ndio wawakilishi na wadau wakuu yaani wananchi. Wizara yangu iliendesha semina ya Waheshimiwa Wabunge tarehe 22 Julai, 2006 kwa lengo la kuwashirikisha na itaendelea kufanya hivyo kwa wadau wengine katika ngazi mbali mbali.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu bado ipo katika hatua za maandalizi ya kuanzisha Mfuko wa Maji chini ya Sheria ya Maji ambayo inatarajiwa kuwasilishwa Bungeni mwaka huu. Sheria hiyo ikipita, itatupa nafasi ya kuanzisha Mfuko huo kisheria.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali itafikisha Bungeni taarifa za kukamilika kwa programu za uanzishwaji wa Mfuko wa Maji itakapokuwa tayari. Aidha, Serikali itawashirikisha Waheshimiwa Wabunge katika mchakato wa kukamilisha na kusimamia programu pamoja na Mfuko wa Maji.

**MHE. MBAROUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri pamoja nashughuli nzuri ambazo Wizara ilifanya kuandaa semina ambayo imefafanua juu ya suala hili. Kwa vile katika programu ya kitaifa ya maji na usafi wa mazingira vijijini imelelezwa katika sura ya 27 kwamba fedha zitatolewa kwa kila Wilaya kwa kuzingatia uwiano wa mahitaji halisi. Je, kwa msingi huu, Serikali itafikiria yale maeneo ambayo yako pembezoni na yana shida kubwa sana ya maji?

Mheshimiwa Spika, pili, mgao uliofanyika hapo awali ulizingatia kila Wilaya ipate miradi 10. Kwa kuwa sasa baadhi ya Wilaya hizo zimegawanyika katika Wilaya mbili. Je, Serikali itafikiria upya na hizi Wilaya mpya zilizokuja zikafikiriwa kupata miradi ya ziada?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kufuatana na Sera inaeleza kwamba tutatenga fedha kufuatana na mahitaji ya kila Wilaya. Ni kweli hilo ndilo linalotendeka. Lakini kinachofanyika ni kwamba tumewapa fursa na uwezo kila Halmashauri ya Wilaya yenyewe iangalie kipaumbele mambo ambayo wanaona kwamba kwa kweli ndiyo yafanyiwe haraka. Pia, kwa hali hiyo ni kwamba Wilaya zenyewe zikiishaamua, sisi Wizara tunaheshimu na kuona kwamaba hayo ndiyo matakwa ya Wilaya na hiyo ndiyo Bajeti yao.

Mheshimiwa Spika, lakini hata hivyo pia tunazo pesa ambazo napenda niwakumbushe Waheshimiwa wabunge juzi katika Semina tulieleza kuna pesa zile zinaitwa *Quick Wings* ambapo pia kuna baadhi ya miradi ambayo katika Wilaya iliyokuwa na kasoro kwa sasa hivi pia tunaihudumia kwa kutumia pesa hizo kufuatana na Wilaya yenyewe kuziombea. Kwa hali hiyo, hata kimradi ile ya ukame nayo sisi Wizara tunaiheshimu na kuishughulikia kufuatana na matakwa ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, baada ya jibu hilo, napenda Mheshimiwa Mbunge anifahamishe tena kipengele cha pili ambacho sikukisikia kulikuwa kuna makelele nyuma yangu.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Spika, kabla ya Sera hii haijatolewa rasmi, palikuwa na utaratibu wa Mradi wa Benki ya Dunia ambapo kila Wilaya ilipewa Miradi 10. Maendeleo yaliyotokea baadaye ni kwamba baadhi ya Wilaya hizo zimegawanywa sasa. Sasa hizi Wilaya Mpya zimekuja na zile za zamani zina miradi pungufu ukizingatia msimamo huo. Je, Serikali italifikiria upya suala hili ukizingatia mabadiliko yaliyotokea?

**SPIKA:** Kuhusu ike Miradi 10 ya Beki ya Dunia.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna baadhi ya Wilaya ambazo sasa hivi zimegawanyika, au zimeongekea. Kwa mfano katika Wilaya ya Muheza ambako Mheshimiwa Mbunge anatoka, Wilaya ile kwa sasa hivi imegawanyika. Pia kuna mfano mwingine wa Wilaya zingine za Mikoa mingine kama Kilindi na Handeni ambapo Kilindi kwa sasa yenyewe imeishaweza Kujitegemea na yenyewe inakuwa na miradi yake peke yake. Kwa upande wa Wilaya ya Muheza ambapo Wilaya Mpya ya Mkinga ndio tunasubiri kwa kipindi cha sasa wenzetu wa TAMISEMI wakiisha wakamilishia taratibu zote waweze kuwa na Wilaya kamili na watendaji wa kutosha, ndipo hapo kwenye Halmashauri yao ikiwa ya kutosha, ndipo na wenyewe wataweza kufanyiwa kila kitu na kwa hivi sasa tunaomba subira waendelee kutumia huduma kutoka katika Wilaya mama.

Na. 268

**Soko la Mbamba Bay**

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA (K.n.y. MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne alihudhunishwa na kitendo cha wafanyabiashara pale *Mbamba Bay* kuvusha mahindi kwenda Malawi bila utaratibu maalum wa kuliingizia taifa mapato; na kwa kuwa hii ilidhihirisha wazi kuwa soko la *Mbamba Bay* ni ufumbuzi na utatuzi wa umaskini unaowakabili wananchi wa Ruvuma;

(a) Je, huu sasa si wakati muafaka wa kujenga soko la kisasa pale *Mbamba Bay* kwa dhamira ya kuendeleza ukanda wa bonde la Ziwa Nyasa?

(b) Je, si vema sasa ujumbe kutoka Wizara husika na wale wa kamati husika na Bunge wakatembelea fukwe za Ziwa Nyasa upande wa Malawi ili kuona wenzetu wamefanya nini?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa kukosekana kwa masoko ya kisasa katika maeneo ya mipakani, kumekuwepo kwa biashara zisizo rasmi na taifa kukosa takwimu sahihi za biashara katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha ujenzi wa soko la kisasa eneo la *Mbamba Bay* kwa dhamira ya kuendeleza ukanda wa bonde la Ziwa Nyasa, Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga ibainishe na kuingiza katika mipango yake ya maendeleo ujenzi wa soko hilo. Wizara yangu iko tayari kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga kufanya tathmini ya umuhimu wa soko na aina ya soko linalofaa kujengwa katika eneo la *Mbamba Bay*. Aidha, tathmini hii itaiwezesha Wizara yangu kwa kushirikiana na

Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga kuwashawishi wafadhili na wadau wengine kuchangia fedha ili kufanikisha ujenzi huo.

(b)Mheshimiwa Spika, Wizara ya Viwanda, Biashara na masoko, iko tayari kupeleka Wataalamu wake kutembelea fukwe za Ziwa Nyasa upande wa Malawi ili kuona wenzetu wamefanya nini kuhusiana na uendelezaji wa Biashara kati ya Tanzania na Malawi. Aidha Wizara inaunga mkono wazo la kuwajumuisha Wabunge wa kamati husika kushiriki katika ziara hiyo.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:**Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa bidhaa zinazopelekwa pale sasa hivi zinawekwa kwenye mchanga na hakuna nyumba au *godown* zozote na hata samaki wanaovuliwa kule wanawekwa kwenye michanga na kwenye matete. Je, Serikali haioni iko haja ya kujenga *godowns* kule ili kuhifadhi mazao hayo na samaki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Capt. John D. Komba, rudia naona haikusikika vizuri.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, swali ni hivi, kwa kuwa kuna bidhaa nyingi kama mahindi, maharage na samaki wanaouvuliwa pale wanawekwa kwenye mchanga, hakuna sehemu ya kuhifadhia mazao hayo na samaki hao. Je, Serikali haioni iko haja sasa ya kujenga *godowns* pale ili samaki na bidhaa hizo zihifadhiwe vizuri?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuongezea jibu zuri la Naibu Waziri. Kama alivyoeleza Naibu Waziri, mipango yote inatoka kwenye Halmashauri, ndiyo chimbuko lake. Kwa hiyo, wale ndio wanajua kitu gani ambacho wanataka. Kwa hiyo, tukipokea ile mipango kutoka Halmashauri, tutaweza kuhusisha wadau husika ili kuweza kuona ni kitu gani kinahitajika. Unaweza ukasema *godown*, kumbe unachokitaka, ni samaki anahitaji *refrigeration*. Kwa hiyo, ili kujua hiyo yote, kitu gani kinahitajika, lazima patoke mipango kutoka Wilayani kule ili tuweze kuichukua kutoka Wilayani kuhusisha na wadau wengine, tuweze kuifikisha na kuijadili na kuona ni kitu gani kinahitajika. *(Makofi)*

Na. 269

**Utafiti jinsi ya Kupunguza Mazalio ya Mbu**

**MHE. USSI AMME PANDU** aliuliza: -

Kwa kuwa, ugonjwa wa malaria ni tatizo kubwa sana nchini na vifo vingi vimekuwa vikitokea kwa sababu ya ugonjwa huo; na kwa kuwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kupitia Kitengo cha Utafiti *(NIMR)* Amani Tanga ulifanya utafiti ili kuona uwezekano wa kupunguza mazalio ya mbu: -

(a) Je, utafiti huo umefikia hatua gani?

(b) Je, ni mafanikio gani yaliyopatikana katika utafiti huo ambao ulikuwa na lengo la kupunguza ongezeko la mazalio ya mbu?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ussi Amme Pandu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Ussi kwamba malaria ni ugonjwa ambao unachukua vifo vingi, vifo vya Watanzania laki moja kwa mwaka. Wizara hii kupitia Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu, Kituo cha Amani imekuwa inaendelea kufanya utafiti kuhusu mazalio ya mbu ili kutafuta mbinu bora za kupambana na kutokomeza malaria na magonjwa mengi yanayoambukizwa na mbu hususan mabusha na matende.

Mheshimiwa Spika, utafiti huu umehusu udhibiti wa mazalio ya mbu na umeendelea kufanyika ukilenga katika matumizi ya viini hai ili kutokomeza mbu waambukizao magonjwa. Aidha, aina hii ya udhibiti inalenga kulinda mazingira na kuwa hakuna madhara yanayotokea kwa mazingira ikiwa ni pamoja na viumbe hai vingine wanaoishi pamoja na viluilui katika mazalio.

Mheshimiwa Spika, tunashirikiana na Serikali ya Cuba katika utafiti huu na matokeo ya awali yametuwezesha kuanza majaribio na sasa hivi kazi hiyo imeanza kutekelezwa katika Wilaya za Bagamoyo na Mvomero na baadaye tunatarajia kuhamia Mafia. Viini hai vinavyotumika vinaitwa *bacillus thuringiensis* na *bacillus sphaericus.*

Mheshimiwa Spika, mpango wa Wizara ni kutumia matokeo haya ya awali na kuona uwezekano wa kusambaza teknolojia hii ya kutokomeza viluilui vya mbu katika nchi nzima. Ikiwa majaribio haya yataonyesha mafanikio, basi Serikali ya Cuba imekubali kuhamisha utaalam huo, yaani *technology transfer* kwa kutengeneza viuatilifu uweze kufanyika hapa nchini kwa ajili ya matumizi ya ndani na pia kwa soko letu katika nchi za jirani za Afrika. Pamoja na utafiti huo, kituo chetu cha Amani kinaendelea kufanya utafiti ili kuweza kutumia vivutio vya mbu katika mazalio mbalimbali. Vivutio vya aina hiyo vimeweza kugunduliwa na watafiti wetu kwa mbu wa jamii ya *Culex* ambao wanaambukiza matende na mabusha. Aina hii ya utafiti sasa inaelekezwa kwa mbu wa jamii ya *Anopheles* ambao wanaambukiza malaria. Ni matumaini yetu kwamba kemikali zinazowavutia mbu kuzaliana katika maeneo fulani zinaweza kutumiwa kuwavutia mbu hao watage katika maeneo ambayo tayari tumeshaweka viuatilifu na hivyo tupate uwezo wa kutokomeza kabisa.

**SPIKA:** Nitaruhusu swali moja tu la muuliza swali maana muda wa maswali sasa umekaribia kumalizika. Mheshimiwa Ussi, swali la nyongeza.

**MHE. USSI AMME PANDU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, vifo bado vinaendelea katika nchi yetu ya Tanzania kutokana na malaria. Pamoja na utafiti huo ambao unaendelea nataka kujua. Je, utafiti huo utamalizika lini?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, swali la Mheshimiwa Ussi ni gumu kidogo kwa sababu hatuwezi kusema utafiti utakwisha lini. Hata tukifikia hatua ya utekelezaji tutaendelea tu kuboresha na kuboresha na vinginevyo tutafunga kituo tukisema utafiti umekwisha. Naomba tu uamini kwamba sasa hivi tumefikia hatua nzuri na tunafanya utafiti wa kuua hivyo vijidudu katika maeneo fulani na kama nilivyosema, tukiona kwamba vinatupatia matokeo mazuri tutaanza kusambaa kwenda katika maeneo mengine ya Tanzania.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha. Nimearifiwa kwamba Mheshimiwa Balozi wa Uingereza tuko naye hapa, *The United Kingdom High Commissioner to Tanzania,* karibu sana. *You are very much welcome Sir; we are always pleased when we see our developing cooperating partners take interest in our proceedings here. Thanks very much. (Makofi)*

Upande wa kushoto, wageni wa Mheshimiwa Lukuvi kutoka Ismani, ni walimu na wanafunzi wa Shule ya Msingi ya Mtera naomba wasimame ili tuwatambue. Pia, wapo Viongozi wa Kijiji cha Migori na Katibu wa Jimbo la Ismani, karibuni sana. Pia, tuna mgeni wa Mheshimiwa Chacha Wangwe ambaye ni Katibu wa Wilaya wa CHADEMA kutoka Tarime. Katibu wa CHADEMA Tarime, yule pale. Karibu sana. Mheshimiwa Ruth Msafiri ana mgeni wake ambaye anaitwa Shadrack Msafiri. Sielewi uhusiano ni upi, lakini kwenye *note* hapa anasema ni wa Kanisa na *Calvary Assemblies of God. (Kicheko/Makofi)*

Nawafahamisha kwamba Mheshimiwa Naibu Spika amekwenda safari ndefu. Tarehe 21 Julai, 2006 aliondoka kwenda Dar es Salaam, halafu anakwenda Ghana kwenye mkutano. Anatuwakilisha kwenye Mkutano wa *Commonwealth Parliamentary Association Accra, Ghana.* Baada ya hapo, tarehe 12 Agosti, 2006 anaenda likizo na pia tarehe 15 Septemba, 2006 atahudhuria mkutano wa Umoja wa Mataifa kule New York. Kwa hiyo, hatarudi nchini mpaka Septemba. Basi tumtakie mema katika safari ndefu hiyo. *(Makofi)*

Mkutano ambao ulikuwa umepangwa wa Kamati ya Uongozi na Tume ya Huduma za Bunge kwa pamoja kukutana na Serikali saa 7:30 umeahirishwa hadi hapo tutakapoarifiwa baadaye, kwa hiyo haupo. Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii anawatangazia wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo tarehe 24 Julai, 2006 kutakuwa na kikao saa 5 asubuhi, chumba namba 432. Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, anawatangazia wajumbe kwamba kutakuwa na kikao cha Kamati ya Huduma za Jamii saa 7.00 leo mchana, ukumbi namba 231. Mheshimiwa William Kusilla, Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama anaomba wajumbe wa Kamati hiyo ya Ulinzi na Usalama wakutane leo asubuhi hii saa 5, chumba namba 133.

Baada ya matangazo hayo, Katibu endelea na *Order Paper.*

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2006/2007**
**Wizara ya Maendeleo ya Mifugo**

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu baada ya kuzingatia taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kisekta ya Kilimo na Ardhi lipokee na kujadili Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo kwa mwaka wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hiki ni kikao cha kwanza cha Bajeti tangu Bunge lako Tukufu lichaguliwe kufuatia Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani uliofanyika mwezi Desemba, 2005, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi na wananchi wa Tanzania kuwa Rais wetu wa Awamu ya Nne. Ushindi wa kishindo alioupata ni kielelezo cha imani waliyonayo wananchi kwake. Katika muda mfupi wa uongozi wake, ameonyesha kwa vitendo uwezo wa kuongoza, kusimamia na kuendeleza amani, utulivu, uchumi na maendeleo ya nchi yetu. Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kuchaguliwa kwake katika awamu hii, ni kielelezo cha sifa, uwezo na ukomavu aliokuwa nao katika uongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa kunipa heshima kubwa sana, kuniteua kuwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo. Naahidi kupitia Bunge lako Tukufu kuwa nitaitumia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uwezo wangu wote. Vile vile, napenda kuchukua nafasi hii kukipongeza Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa kufanikisha Uchaguzi wake mkuu.

Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi sana kuwa Mwenyekiti wa CCM. Pia, nampongeza Luteni Mstaafu Yusuph Makamba, kwanza kwa kuteuliwa kuwa Mbunge na pia kwa kuchaguliwa kuwa Katibu Mkuu mpya wa CCM. Aidha, naipongeza sekretarieti nzima ya CCM kwa kuchaguliwa kwao *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, napenda kumpongeza Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, Mbunge wa Monduli na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuteuliwa kwake na Mheshimiwa Rais na baadaye kuthibitishwa kwa kura nyingi na Bunge lako Tukufu kushika wadhifa huu mkubwa. Kuteuliwa kwake kunaonyesha imani kubwa aliyonayo Mheshimiwa Rais juu ya uwezo na utendaji wake wa kazi katika kusimamia majukumu ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie pia nafasi hii, kukupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Samuel John Sitta, Mbunge wa Urambo Mashariki, pamoja na Naibu Spika,

Mheshimiwa Anne S. Makinda Mbunge wa Njombe Kusini, kwa kuchaguliwa kwenu kwa kura nyingi kuliongoza Bunge hili Tukufu. Ushindi wenu ni kielelezo cha imani kubwa waliyonayo Waheshimiwa Wabunge kwenu katika kusimamia shughuli za Bunge hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo na Ardhi chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Gideon Asimulike Cheyo, Mbunge wa Ileje, iliyojadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu tarehe 29 Mei, 2006 na kuyapitisha baada ya kutoa ushauri, mapendekezo na maoni mbalimbali.

Aidha, katika kipindi kifupi tangu iteuliwe, Kamati imekutana na viongozi, wataalam na wadau wa Sekta ya Mifugo na kutoa maoni na ushauri. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Wizara yangu itazingatia na kutekeleza ushauri, mapendekezo na maoni yaliyotolewa na Kamati na yale yatakayotolewa na Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii pia kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa kuteuliwa kwao na Mheshimiwa Rais kuongoza Wizara mbalimbali. Aidha, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa na walioteuliwa kuingia katika Bunge hili Tukufu. *(Makofi)*

Pia, napenda kuwashukuru wapigakura na wananchi wa Jimbo la Bagamoyo kwa kunichagua kuwa Mbunge wao na kwa hivyo kunipa heshima kubwa ya kuliwakilisha Jimbo letu. Nawaahidi kupitia Bunge lako Tukufu kuwa nitawatumikia kwa juhudi kubwa na Wizara yangu itashirikiana nao katika kuendeleza Sekta ya Mifugo nchini. *(Makofi)*

Naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dr. Charles Ogesa Mlingwa, Mbunge wa Shinyanga Mjini na Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo, kwa msaada wake wa karibu katika kusimamia kazi za Wizara yangu.

Aidha, napenda nitoe shukrani zangu kwa Katibu Mkuu wa Wizara yangu, Dr. Charles Nyamrunda na Naibu Katibu Mkuu Dr. Jonas Melewas, wakurugenzi, wataalam na watumishi wote wa Wizara kwa ushirikiano, uadilifu, kunishauri na kuandaa mipango mizuri ya bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2006/2007. Naomba waendelee kutekeleza majukumu tuliyojipangia kwa ari hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii pia kutoa shukrani zangu nyingi na za dhati kwa mke wangu Saumu kwa kuwa nami katika kila ngazi ya maisha yetu. Shukrani hizo nazitoa pia kwa watoto wetu Asha, Mariam, Karim na Malick kwa kunipa upendo mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, Mbunge wa Monduli, kwa hotuba yake nzuri ya bajeti ambayo imetoa malengo

na mwelekeo wa utekelezaji wa kazi za Serikali kwa mwaka 2006/2007. Nawapongeza pia Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Mheshimiwa Dr. Juma Alifa Ngasongwa, Mbunge wa Ulanga Magharibi na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Zakia Hamdani Meghji, Mbunge wa Kuteuliwa kwa hotuba zao zilizoainisha kwa makini mwelekeo wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2006/2007.

Napenda pia kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia masuala ya maendeleo ya mifugo kupitia hotuba hizo. Pia, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote waliotangulia kwa hotuba zao nzuri ambazo zimeainisha maeneo mbalimbali tunayoshirikiana nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu ya Sekta ya Mifugo, Wizara yangu inazingatia maelekezo yaliyomo katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005. Ilani inatambua mchango mkubwa unaoweza kutolewa na Sekta ya Mifugo katika kuwapunguzia wananchi umaskini na kuongeza Pato la Taifa. Ilani inatamka kuwa, nanukuu:-

"Pamoja na kwamba Tanzania ina mifugo mingi sana; mchango wa mifugo kwenye uchumi wa Taifa ni mdogo. Kwa lengo la kuendeleza Sekta ya Mifugo ili ichangie zaidi ukuaji wa uchumi wa Taifa na kuwaongezea kipato wafugaji, Serikali za CCM zitaendeleza kwa msisitizo zaidi lengo la kuzingatia zaidi ubora kuliko wingi pekee katika ufugaji. Ili kufikia lengo hilo, hatua zifuatazo zitachukuliwa katika kipindi cha mwaka 2005 - 2010:-

(a) Kujenga mazingira ya kuvutia uwekezaji katika viwanda vya kuongezea thamani mazao ya mifugo kama vile ukataji nyama, usindikaji wa maziwa na utengenezaji wa bidhaa za ngozi na kadhalika.

(b) Kuwashawishi Watanzania wale nyama na mayai na kunywa maziwa kwa wingi zaidi kwa ajili ya kujenga afya zao na kukuza soko la ndani la bidhaa hizo.

(c) Kufufua na kujenga mabwawa na majosho mapya kwa ajili ya mifugo.

(d) Kuwaelimisha wafugaji umuhimu wa kuuza sehemu ya mifugo yao ili wajipatie mapato.

(e) Kuwahimiza wafugaji kutekeleza kanuni za ufugaji bora na kwa ujumla kuwawezesha kuingia katika ufugaji wa kisasa.

(f) Kuhifadhi mazingira kwa kuzingatia ufugaji endelevu usioharibu mazingira, raslimali muhimu kama ardhi na vyanzo vya maji kote nchini.

(g) Kuendelea kukuza na kuendeleza masoko ya ndani ya mifugo na mazao yake.

(h) Kuendeleza mikakati ya kukuza Sekta ya Mifugo kupitia ugani, tiba, kinga, usambazaji wa maji na uboreshaji wa malisho.

(i) Kuimarisha vituo vya uzalishaji wa mbegu bora za ng'ombe na mifugo mingine na kuongeza ufanisi katika usambazaji wa mbegu hizo.

(j) Kuendelea kutenga maeneo ya wafugaji kwa lengo la kupunguza migogoro baina ya wakulima na wafugaji.

(k) Kuendelea kuhamasisha uimarishaji na uanzishaji wa vikundi vya ushirika wa wafugaji". Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatekeleza kwa makini maagizo ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoyatoa wakati akizindua Bunge lako Tukufu tarehe 30 Desemba, 2005. Katika hotuba yake, Mheshimiwa Rais alitamka yafuatayo kuhusu ufugaji nchini, nanukuu:-

"Tutachukua hatua za dhati kuboresha ufugaji wetu. Hatuna budi tutoke kwenye uchungaji wa kuhamahama na kuwa wafugaji wa kisasa. Tutachukua hatua za kuboresha malisho na huduma za madawa, majosho na minada.

Ni wajibu wa mamlaka zote za Mikoa na Wilaya nchini, hususan kule kwenye mifugo mingi, kutenga maeneo maalum kwa ajili ya mifugo katika mipango yao ya matumizi ya ardhi. Tanzania ina mifugo mingi sana na tukiboresha ufugaji, itatoa mchango mkubwa katika Pato la Taifa na maendeleo ya wafugaji". Mwisho wa kunukuu.

Aidha, Mheshimiwa Rais alipofanya ziara ya kutembelea Wizara yangu mnamo tarehe 18 Januari, 2006 alitoa maagizo yanayolenga kuleta mapinduzi ya ufugaji nchini. Maagizo hayo yalihusu: -

(i) Kuongeza mchango wa Sekta ya Mifugo katika Pato la Taifa;
(ii) Kudhibiti uhamishaji holela wa mifugo;
(iii) Kuimarisha huduma za ugani;
(iv) Kufufua ranchi zilizopo na kuhakikisha zinafanya kazi iliyokusudiwa;
(v) Kutoka kwenye uchungaji wa kuhamahama na kwenda kwenye ufugaji wa kisasa na kibiashara;
(vi) Kupata masoko ikiwa ni pamoja na masoko ya nje ya kuuza mifugo na mazao yake; na
(vii) Kufikisha madawa na huduma za mifugo kwa wafugaji.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza maagizo ya Mheshimiwa Rais, Wizara yangu imezingatia na kuyaingiza katika Mpango wa Muda wa Kati na Bajeti ya Serikali *(MTEF)* kwa mwaka 2006/2007 hadi 2008/2009 na katika Mpango wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2005-2010).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, kumekuwepo na matukio muhimu yanayogusa Sekta ya Mifugo kwa ujumla. Naomba nitaje baadhi ya matukio hayo.

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuhusu hali ya ukame. Nchi yetu ilikumbwa na ukame kati ya mwezi Agosti, 2005 hadi mwezi Machi, 2006. Ukame huu uliathiri zaidi Mikoa ya Arusha, Dodoma, Kilimanjaro (Same na Mwanga), Manyara, Mara, Mwanza, Shinyanga, Singida na Tabora. Maeneo hayo yanakadiriwa kuwa na asilimia 75 ya mifugo yote nchini. Takriban ng'ombe 250,900, mbuzi 133,237, kondoo 122,069 na punda 744 wanaokadiriwa kuwa na thamani ya Shilingi bilioni 45.3 waliripotiwa kufa kutokana na ukosefu wa maji na malisho  Aidha, mifugo takriban milioni 3 ilidhoofika kutokana na hali ya ukame.

Mheshimiwa Spika, ili kunusuru mifugo, wafugaji walilazimika kuhamia katika maeneo yaliyokuwa na unafuu wa malisho na maji ikiwa ni pamoja na Mikoa ya Kilimanjaro (Rombo na Siha), Tanga, Kagera, Rukwa, Ruvuma, Lindi, Pwani, Kigoma, Morogoro, Iringa na Mbeya. Aidha, baadhi ya mifugo iliingia katika baadhi ya Mbuga za Wanyamapori na Hifadhi za Taifa. Pia, wafugaji na mifugo yao kutoka nchi jirani walivamia maeneo ya Mikoa ya Arusha, Kagera na Kilimanjaro na kusababisha upungufu mkubwa wa malisho na maji kwenye maeneo husika.

Katika kukabiliana na hali iliyojitokeza, Wizara yangu ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Ilishiriki katika kuandaa Mkakati wa Hifadhi ya Mazingira na Vyanzo vya Maji;

(b) Ilitoa maelekezo kwa wananchi, hususan wafugaji na wafanyabiashara ya mifugo juu ya hatua za kuchukua kukabiliana na janga la ukame; na

(c) Ilitoa chanjo ya Ndigana Kali kwa ndama baada ya ukame ili kupunguza vifo.

Ukame huu uwe ni changamoto kwa wananchi kuchukua hatua za tahadhari mapema ikiwa ni pamoja na kupunguza kwa kuuza mifugo wakati ikiwa na hali nzuri, kulima na kuhifadhi malisho, kuchimba malambo na kuanzisha viwanda vya kusindika nyama ili kupunguza makali ya ukame.

Mheshimiwa Spika, pili ni kuhusu tishio la mafua makali ya ndege. Kwa sasa dunia inakabiliwa na tatizo la kuenea kwa ugonjwa wa mafua makali ya ndege ambao husababisha vifo kwa ndege na binadamu. Kwa mujibu wa taarifa za Shirika la Afya ya Wanyama Duniani *(OIE),* nchi zilizoripoti ugonjwa huo kufikia mwezi Juni, 2006 ni 50 zikiwepo 8 za Bara la Afrika ambazo ni Nigeria, Misri, Niger, Cameroon, Burkina Faso, Sudan, Cot de Voir  na Djibouti .

Pamoja na kwamba taarifa za uchunguzi zinaonyesha kuwa ugonjwa wa mafua makali ya ndege haujaingia nchini, Serikali imechukua hatua zifuatazo kukabiliana na tishio la ugonjwa huo: -

(a) Kupiga marufuku kwa muda uingizaji wa ndege, kuku na mazao yake kutoka nchi zote duniani;

(b) Kufuatilia ugonjwa huo kwenye njia kuu za mapitio ya ndegepori wahamaji ambapo sampuli 1,452 za ndegepori na 190 za kuku zilichukuliwa na kuchunguzwa na zote zimethibitika kutokuwa na virusi vya mafua makali ya ndege. Aidha, sampuli nyingine 4,246 za kuku na bata na 184 za ndege pori zimechukuliwa na uchunguzi unaendelea;

(c) Kutayarisha mpango wa kukabiliana na tishio la ugonjwa huo (*Emergency Preparedness and Response Plan)* na kuuwasilisha kwa wahisani kuombea fedha;

(d) Kutoa elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari kuhusu athari za ugonjwa huu. Jumla ya vipeperushi 4,500 na mabango 500 yamesambazwa katika Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji nchini;

(e) Kuimarisha uwezo wa uchunguzi katika maabara za mifugo kwa kutoa mafunzo kwa wataalam na kununua vifaa muhimu. Kutokana na jitihada hizo, kwa sasa Maabara Kuu ya Mifugo Temeke imeanza kufanya uchunguzi wa ugonjwa huo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, suala la tatu ni kuhusu Mkutano Mkuu wa 74 wa Shirika la Afya ya Wanyama Ulimwenguni *(Office Internationale des Epizooties (OIE).* Mkutano huu ulifanyika Paris, Ufaransa tarehe 21 – 26 Mei, 2006 kuhusu afya ya mifugo hususan tishio la mafua makali ya ndege, usalama wa vyakula vitokanavyo na mifugo na uimarishaji wa upashanaji wa taarifa za magonjwa ya mifugo. Nchi yetu ilishiriki na kupongezwa kwa kuwa miongoni mwa nchi 10 kati ya nchi wanachama 167 duniani kuanza kutumia mfumo mpya wa kutoa taarifa za afya ya wanyama. Mfumo huu unarahisisha utoaji wa taarifa za afya ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, suala la nne ni Mkutano wa Kimataifa kuhusu Udhibiti wa Ugonjwa wa Mdondo wa Kuku *(Newcastle Disease).* Tanzania ilikuwa mwenyeji wa Mkutano wa Kimataifa kuhusu Udhibiti wa Ugonjwa wa Mdondo uliofanyika Dar es Salaam tarehe 5 – 7 Oktoba 2005. Mkutano huo uliandaliwa kwa kushirikiana na Shirika la Msaada la Australia *(AusAid)* lililokuwa linafadhili Mpango wa Kudhibiti Mdondo wa Kuku katika nchi za Malawi, Msumbiji na Tanzania. Mkutano ulihudhuriwa na wajumbe 97 kutoka nchi za *SADC,* Jumuiya ya Afrika Mashariki, Vietnam, Indonesia, Australia, Ghana, Nigeria, Ecuador na Mashirika ya *FAO* na *AU-IBAR.* Mkutano ulijadili mchango wa kuku wa asili katika kupunguza umaskini vijijini na kupendekeza juhudi zaidi zifanyike katika kudhibiti ugonjwa wa mdondo na kukabiliana na janga la mafua makali ya ndege.

Mheshimiwa Spika, suala la tano ni kuhusu Mkutano wa Tisa wa Kimataifa wa Zao la Ngozi wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa *(FAO)* uliofanyika mjini Arusha tarehe 1 – 3 Februari, 2006. Mkutano huo ulijadili hali ya zao la ngozi duniani na kuweka mikakati ya kuendeleza zao hilo ili liongeze mchango wake kwenye uchumi wa mataifa yanayozalisha ngozi. Katika mkutano huo, Tanzania iliwasilisha

mradi wa kukausha ngozi kwa chumvi ili kuongeza ubora ambao kimsingi ulikubalika na unatafutiwa fedha.

Mheshimiwa Spika, suala la sita ni kuhusu Mkutano wa Mwaka wa Wataalam wa Mifugo. Kila mwaka Wizara yangu huandaa mkutano wa wataalam wa Sekta ya Mifugo wa ngazi zote Tanzania Bara ili kubadilishana uzoefu, kujifunza mbinu mpya, kutathmini utekelezaji na kuweka mikakati ya kuboresha utendaji na kuongeza ufanisi. Mkutano huu ulifanyika tarehe 1-2 Desemba, 2005 Mjini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, suala la saba ni, Kongamano la Madaktari wa Mifugo *(Tanzania Veterinary Association (TVA)*. Kila mwaka Wizara yangu hushiriki katika kongamano la Madaktari wa Mifugo, ambalo hukutanisha Madaktari wa Mifugo kutoka nchini kote na nchi za nje. Katika kongamano la 2005/2006, washiriki wa nje walitoka Kenya, Uganda, Uingereza, Sweden, Norway na Marekani kwa madhumuni ya kubadilishana uzoefu na kujifunza mambo mapya yanayojitokeza katika utoaji wa huduma za afya ya mifugo. Kongamano hili lilifanyika tarehe 6 – 8 Desemba, 2005 mjini Arusha. Maudhui ya kongamano hilo yalikuwa "Utoaji huduma za Afya ya Mifugo Tanzania katika Ulimwengu wa Utandawazi" *(Animal Health Services Delivery in Tanzania - Global Implication)*. Kongamano hilo lilishauri uandaliwe Mpango Mkakati wa Kukabiliana na Majanga ya Mifugo. Serikali imezingatia ushauri huo kwa kuandaa Mpango Mkakati wa Kukabiliana na Mafua Makali ya Ndege na ule wa Hifadhi ya Mazingira na Vyanzo vya Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la nane ni Kongamano la Wataalam wa Uzalishaji Mifugo *(Tanzania Society of Animal Production (TSAP)*. Wizara yangu hushiriki katika Kongamano la kila mwaka la Wataalam wa Uzalishaji Mifugo nchini. Katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu ilishiriki kwenye Kongamano la Kimataifa la Uzalishaji Mifugo Afrika lililotayarishwa na *TSAP* na *All African Society of Animal Production.* Kongamano hilo lilifanyika mjini Arusha tarehe 20 – 24 Septemba 2005 na maudhui yake yalikuwa ni: "Nafasi ya Bioteknolojia katika kuendeleza ufugaji katika Afrika: Fursa na Changamoto" *(The Role of Biotechnology in Animal Agriculture in Africa: Opportunities and Challenges)*. Kongamano hilo lilishirikisha washiriki 332 kutoka nchi 26 za Afrika. Aidha, kulikuwa na washiriki kutoka Canada, Uingereza, Marekani, India, Pakistan na Brazil. Katika Kongamano hilo, nchi za Afrika zilikubaliana kushirikiana kuweka mazingira mazuri ya kubadilishana utaalam wa bioteknolojia.

Mheshimiwa Spika, suala la tisa ni Maonyesho ya Nane Nane. Tarehe 8 Agosti kila mwaka Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na *Tanzania Agricultural Society (TASO)* huandaa maadhimisho ya sikukuu ya wakulima na wafugaji nchini – Nane Nane. Madhumuni ya maadhimisho hayo ni kuwawezesha wafugaji na wadau wengine kujifunza mbinu bora za uzalishaji, usindikaji na hifadhi ya mazao yatokanayo na mifugo. Katika mwaka 2005/2006, maadhimisho hayo yalifanyika kitaifa mkoani Mbeya na kufunguliwa na aliyekuwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya, Mbunge wa Rungwe Mashariki na kilele kuhitimishwa na Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mheshimiwa Amani Abeid

Karume. Kauli mbiu ya maonyesho hayo ilikuwa ni: "Kilimo bora ni nyenzo muhimu ya kuondoa aina zote za umaskini".

Napenda kuwashukuru viongozi wote, wadau mbalimbali na wananchi wa Mkoa wa Mbeya kwa kushiriki na kufanikisha maadhimisho hayo. Aidha, nawashukuru wananchi katika Kanda mbalimbali kwa kuadhimisha vivyo hivyo katika maeneo yao.

Katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu itashiriki katika kuandaa maadhimisho hayo ambayo kitaifa yatafanyika katika viwanja vya Themi mkoani Arusha. Kaulimbiu ya maonyesho hayo ni "Tokomeza Njaa na Umaskini kwa Kuzingatia Kilimo, Ufugaji Endelevu na Kuhifadhi Mazingira".

Suala la kumi ni Uhamasishaji Unywaji wa Maziwa. Siku ya uhamasishaji unywaji maziwa duniani huadhimishwa tarehe 1 Juni kila mwaka. Aidha, Wizara yangu huadhimisha Wiki ya Uhamasishaji Unywaji wa Maziwa mwanzoni mwa mwezi Juni kama ilivyo katika Nchi zote za Ushirikiano Kusini mwa Afrika *(SADC)*. Lengo la maadhimisho hayo ni kuhamasisha unywaji wa maziwa na utumiaji wa mazao yatokanayo na maziwa ili kuimarisha na kupanua soko la ndani na kuinua viwango vya ulaji nchini ambavyo viko chini sana ikilinganishwa na viwango vya kimataifa. Unywaji wa maziwa kwa sasa ni wastani wa lita 40 kwa mtu kwa mwaka ikilinganishwa na lita 200, kiwango kinachopendekezwa na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa *(FAO)*. Lengo lingine la maadhimisho hayo ni kuhamasisha unywaji wa maziwa shuleni ili kujenga tabia ya kunywa maziwa. Katika mwaka 2005/2006, Wiki ya Unywaji wa Maziwa iliadhimishwa kitaifa mkoani Morogoro kuanzia tarehe 2-5 Juni, 2006. Kaulimbiu ya maadhimisho haya ilikuwa: "Kunywa Maziwa kwa Afya Yako". Sanjari na maadhimisho hayo, Kongamano na Mkutano wa Mwaka wa Baraza la Wadau wa Maziwa vilifanyika. Pamoja na mambo mengine, wadau walishauri kuwawezesha wazalendo kuzalisha na kusindika maziwa kwa ufanisi ili kukabiliana na ushindani kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, suala la kumi na moja ni kuhusu Siku ya Chakula Duniani. Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, pamoja na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa *(FAO),* tuliandaa na kuadhimisha Siku ya Chakula Duniani iliyofanyika Kitaifa Mombo, Wilayani Korogwe. Maadhimisho hayo hufanyika duniani kote tarehe 16 Oktoba kila mwaka kwa lengo la kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kuzalisha chakula cha kutosha na kuwa na lishe bora. Kaulimbiu ilikuwa: "Mahusiano ya Jamii katika Kuendeleza Kilimo". *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, matukio yote niliyoyaelezea hapo juu yametoa changamoto, msukumo na mchango mkubwa katika kuboresha maendeleo ya Sekta ya Mifugo. Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wengine inaendelea kuyafanyia kazi maazimio yaliyotokana na matukio hayo. Baada ya utangulizi huo, sasa naomba niwasilishe mapitio ya utekelezaji wa mpango wa mwaka 2005/2006 na mpango na malengo kwa mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mifugo ni moja kati ya sekta zilizopewa umuhimu katika Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Nchini (MKUKUTA).

Mifugo huchangia katika kuhakikisha usalama wa chakula, lishe bora, ajira na inatoa mchango mkubwa katika kilimo hususan nguvu kazi na mbolea ambayo ni muhimu katika kilimo endelevu. Vilevile, kwa wafugaji wengi, mifugo ni chanzo cha mapato ya haraka wakati wa dharura na huchangia katika Pato la Taifa. Hivyo, Sekta ya Mifugo ina umuhimu mkubwa katika kumwondolea umaskini mwananchi hasa wa vijijini. Juhudi za Wizara zitaelekezwa katika kuimarisha ufugaji ili kumwongezea mwananchi kipato kutokana na mifugo. Katika Mkakati huo, lengo ni kuongeza ukuaji wa Sekta ya Mifugo kutoka asilimia 5 mwaka 2004 hadi asilimia 9 mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, takwimu zilizopo zinaonyesha kuwa idadi ya mifugo nchini inakadiriwa kuwa ng'ombe milioni 18.5, mbuzi milioni 13.1, kondoo milioni 3.5, kuku wa asili milioni 33 na wa kisasa milioni 17 na nguruwe milioni 1.2. Aidha, viwango vya ulaji wa mazao ya mifugo kwa sasa ni wastani wa kilo 11 za nyama, lita 40 za maziwa na mayai 64 kwa mtu kwa mwaka. Hata hivyo, Sekta hii imeendelea kukabiliwa na matatizo mbalimbali yanayoathiri maendeleo ya Sekta kwa ujumla. Matatizo hayo ni pamoja na:-

(a) Matumizi duni ya ardhi na uhaba wa maji na malisho bora ya mifugo;
(b) Tija ndogo ya uzalishaji kutokana na aina ya mifugo na mifumo ya uzalishaji iliyopo;
(c) Magonjwa ya mifugo hasa magonjwa ya milipuko;
(d) Uhaba wa viwanda vya kusindika mazao ya mifugo, masoko ya mifugo na mazao yatokanayo na mifugo;
(e) Uhaba wa wawekezaji binafsi pamoja na mikopo na
(f) Elimu duni kwa wafugaji.

Mkakati wa kuondokana na matatizo hayo yanayokabili Sekta ya Mifugo uliandaliwa na unaendelea kutekelezwa kupitia Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo Nchini *Agricultural Sector Development Strategy (ASDS).*

Mheshimiwa Spika, mwaka jana Bunge lako Tukufu liliarifiwa kuwa Rasimu ya Sera ya Taifa ya Mifugo iliwasilishwa Serikalini ili ijadiliwe na kupitishwa. Kutokana na muundo wa Serikali ya Awamu ya Nne ya Uongozi, Rasimu ya Sera hiyo imebidi ipitiwe tena na Serikali ili kuiboresha zaidi na taratibu za kuipitisha zinaendelea. Sera hiyo itasambazwa kwa wadau baada ya kupitishwa na Mkakati wa kutekeleza sera utaandaliwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau iliandaa sheria, kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali inayohusu Sekta ya Mifugo kama ifuatavyo:-

(a) Sheria ya Nyama ambapo Muswada wa Sheria umekamilika na kusomwa mara ya kwanza Bungeni mwezi Aprili, 2006; na

(b)Kanuni 7 na miongozo 2 chini ya Sheria ya Veterinari Na. 16 ya mwaka 2003 zimekamilika na nakala 3,000 za kanuni hizo zimesambazwa kwa wadau.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007 sheria zifuatazo zitaandaliwa au kurekebishwa:-

(a)Kurekebisha Sheria za Ulinzi wa Wanyama Wafugwao (*The Animal Protection Ordinance)* Sura ya 153 ya mwaka 1930 na Kuzuia Wanyama Wazururao *(The Animal Pounds Ordinance)* Sura ya 154 ya mwaka 1930;

(b) Kurekebisha Sheria ya Kudhibiti Ndorobo *(The Tsetse fly Control Ordinance)* Sura ya 100 ya mwaka 1943;

(c) Kurekebisha Sheria ya Ngozi Na. 30 Sura ya 120 ya mwaka 1965;

(d) Kuandaa Sheria ya kuanzishwa Taasisi ya Utafiti wa *Mifugo (The National Livestock Research Institute);*

(e) Kuandaa Sheria ya kuanzishwa Maabara Kuu ya Mifugo *(The Central Veterinary Laboratory);*

(f) Kurekebisha Sheria ya Mbolea na Vyakula vya Mifugo *(The Fertilizer and Animal Foodstuff Ordinance)* Sura ya 467 ya mwaka 1962; na

(g) Kuandaa Sheria ya Uendelezaji wa Maeneo ya Malisho.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu ilikusanya, kuchambua na kuhifadhi takwimu mbalimbali za mifugo nchini. Pia, Wizara imeanzisha mtandao wa kompyuta *(Local Area Network)* katika Makao Makuu na Vituo vya Kanda vya Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo. Katika mwaka 2006/2007, Wizara itaendelea kukiimarisha kitengo cha takwimu kwa kukipatia vifaa zaidi, kutoa mafunzo kwa watumishi na kukiunganisha na vituo vingine vya Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, Wizara iliendelea na jitihada za kusambaza mifugo bora nchini ambapo jumla ya mitamba 734 ilizalishwa kutoka kwenye mashamba ya Serikali (LMUs) na kusambazwa kwa wafugaji wadogo katika mikoa ya Dar es Salaam, Iringa, Kagera, Lindi, Mara, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Mwanza, Pwani, Ruvuma, Shinyanga, Singida, Tabora na Tanga). Aidha, Wizara iliendelea kushirikiana na asasi mbalimbali kama vile *Heifer Project Tanzania (HPT), Southern Highlands Livestock Development Association (SHILDA), Caritas, Austro Project Association – Tanzania (APA -T), Land 'O Lakes* na wadau wengine katika kuendeleza ufugaji wa ng'ombe na mbuzi wa maziwa. Jumla ya mitamba 5,120 ya ng'ombe wa maziwa na mbuzi 1,196 wa maziwa walisambazwa kwa wafugaji wadogo chini ya mipango ya "Kopa Ng'ombe Lipa Ng'ombe" na "Kopa Mbuzi Lipa Mbuzi".

Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kuboresha mashamba ya kuzalisha mifugo kwa kuyapatia vitendea kazi na nyenzo mbalimbali ili yaweze kuzalisha kwa ufanisi zaidi. Mashamba ya Kuzalisha Mifugo ya Mabuki na Nangaramo yaliimarishwa kwa kuboresha miundombinu ya maji. Shamba la Kitulo liliimarishwa kwa kutengewa fedha za kununulia mashine ya kukamua maziwa. Pia, ng'ombe wazazi 128 walipelekwa

katika shamba la Sao Hill na 68 Mabuki. Katika mwaka 2006/2007, Wizara itaendelea kuimarisha mashamba ya uzalishaji mitamba ya Nangaramo, Ngerengere, Sao Hill, Mabuki na Kitulo kwa kununua ng'ombe wazazi 310, vitendea kazi na pembejeo za mifugo. Aidha, Wizara itashirikiana na wadau wengine kusambaza ng'ombe 200 ili kuongeza idadi ya ng'ombe wa maziwa katika Mikoa ya Kusini ya Lindi, Mtwara na Ruvuma. Aidha, Wizara yangu kwa kushirikiana na Mkoa wa Rukwa itakamilisha umilikishaji wa shamba la ng'ombe wa maziwa la Malonje kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006 uzalishaji wa maziwa uliongezeka kutoka lita bilioni 1.39 mwaka 2004/2005 hadi lita bilioni 1.41 sawa na ongezeko la asilimia 1.4 Aidha, katika kipindi hicho, unywaji wa maziwa uliongezeka kutoka lita 39 hadi 40 kwa mtu kwa mwaka. Pamoja na uzalishaji huu kuongezeka, kiasi cha lita milioni 7.1 za maziwa ziliingizwa kutoka nje na wafanyabiashara. Katika mwaka 2006/2007, lengo ni kuzalisha lita bilioni 1.43 za maziwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006 Wizara yangu ikishirikiana na wadau wa maziwa imeanzisha Bodi ya Maziwa ili iweze kuendeleza, kuratibu na kusimamia zao la maziwa. Bodi hii ilizinduliwa rasmi tarehe 11 Novemba, 2005. Katika mwaka 2006/2007, Wizara kwa kushirikiana na Bodi ya Maziwa itaendelea kuratibu uzalishaji na usindikaji wa maziwa nchini na kuandaa Wiki ya Uhamasishaji Unywaji wa Maziwa. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Bodi hiyo, Halmashauri na sekta binafsi itaendelea kuhamasisha unywaji wa maziwa hususan mashuleni.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa nyama uliongezeka kwa asilimia 2.6 kutoka tani 378,509 mwaka 2004/2005 hadi tani 388,294 mwaka 2005/2006. Kati ya hizo, nyama ya ng'ombe ni tani 210,370, mbuzi na kondoo tani 78,579, nguruwe tani 29,925 na kuku tani 69,420. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya nyama na kupanuka kwa wigo wa masoko mapya yanayonunua nyama.

Vile vile, kumekuwepo na ongezeko la uzalishaji wa ng'ombe bora kutoka katika Ranchi za Taifa na mashamba ya sekta binafsi. Aidha, ulaji wa nyama uliongezeka kutoka wastani wa kilo 11 hadi 11.4 kwa mtu kwa mwaka. Pamoja na uzalishaji huu kuongezeka, kiasi cha tani 1,139 za nyama kiliagizwa kutoka nje na wafanyabiashara. Katika mwaka wa 2006/2007 kiasi cha tani 403,800 za nyama kitazalishwa sawa na ongezeko la asilimia 3.8. Aidha, Wizara yangu inatarajia kuwa na Sheria ya Nyama baada ya Bunge lako Tukufu kuipitisha ambayo itasimamia zao la nyama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, Kampuni ya Ranchi za Taifa *(NARCO)* imekamilisha kugawa ranchi za Misenyi na Uvinza na kufanya idadi ya ranchi ndogondogo kuwa 125. Ranchi hizo ndogo zimemilikishwa kwa wawekezaji wazalendo ili waweze kufuga kisasa na kibiashara. Ranchi ya West Kilimanjaro bado haijapimwa kutokana na shauri la ardhi ambalo lipo mahakamani.

Mheshimiwa Spika, *NARCO* imebakiwa na eneo lenye ukubwa wa hekta 230,384 kwa ajili ya ranchi za mfano zenye jumla ya ng'ombe 41,711. Katika mwaka 2005/2006, Kampuni ilizalisha ndama wa nyama 10,400 sawa na asilimia 87.2 ya lengo, na mitamba

465 ya maziwa sawa na asilimia 62 ya lengo. Aidha, *NARCO* iliuza ng'ombe 11,000 wa nyama wenye thamani ya Shilingi bilioni 2.4 sawa na asilimia 91.7 ya lengo. Vilevile, kampuni ilinunua ng'ombe wa asili 1,141 wenye thamani ya Shilingi milioni 143.6 na mbuzi na kondoo 121 wenye thamani ya Shilingi milioni 2.7 kwa ajili ya kunenepesha. Pia, *NARCO* ilizalisha mbuzi na kondoo 466 wa nyama katika ranchi za West Kilimanjaro, Kongwa na Mzeri. Katika mwaka 2006/2007, Kampuni itaandaa na kutekeleza Mpango Mkakati wa kuboresha na kuendeleza uzalishaji katika ranchi hizo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, jumla ya ng'ombe 364,453 wenye thamani ya Shilingi bilioni 43.7, mbuzi 312,388 wenye thamani ya Shilingi bilioni 5.6 na kondoo 52,065 wenye thamani ya Shilingi milioni 781 waliuzwa minadani. Aidha, jumla ya ng'ombe 1,706 wenye thamani ya Shilingi milioni 647.9 na mbuzi 800 wenye thamani ya Shilingi milioni 28 waliuzwa nchini Comoro na Burundi. Vilevile, tani 3.5 za nyama ya mbuzi zenye thamani ya Shilingi milioni 6.8 ziliuzwa kwenye Nchi za Falme za Kiarabu. Katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu itaendelea kuhamasisha uzalishaji wa nyama na biashara ya mifugo pamoja na uundwaji wa vyama vya wafanyabiashara ya mifugo ili kuwawezesha kutafuta masoko ya ndani na nje.

Mheshimiwa Spika, katika mfumo wa uchumi wa soko huria, utambuzi, usajili na ufuatiliaji *(Identification, Registration and Traceability)* wa mifugo na mazao yake ni nyenzo muhimu katika kuongeza uzalishaji wenye tija na biashara ya mifugo. Kutokana na umuhimu huo, Wizara yangu imeanzisha Kitengo maalum kitakachohusika na jukumu hilo. Katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu itaimarisha kitengo hicho kwa kutoa mafunzo na vitendea kazi ili kiweze kuandaa mfumo wa kutambua, kusajili na kufuatilia mifugo na mazao yake. *(Makofi)*

Aidha, maandalizi ya kuanzisha Rejista ya Taifa ya kumbukumbu za mifugo kwa ng'ombe wa maziwa na nyama itaanza katika mashamba makubwa 10 ya Serikali na watu binafsi ya Mabuki, Kongwa, Kitulo, Mpwapwa, Nangaramo, Ngerengere, Ruvu, *Sao Hill, Kibebe Farm* na Sumbawanga *Agricultural and Animal Feeds Industries*.

Mheshimiwa Spika, uhamilishaji *(artificial insemination)* unatumika kama njia mojawapo ya kuongeza ubora wa mifugo. Katika mwaka 2005/2006, Kituo cha Taifa cha Uhamilishaji *(NAIC)* cha *Usa River,* Arusha kilizalisha jumla ya dozi 51,230 za mbegu bora ikilinganishwa na dozi 50,000 za mwaka 2004/2005. Aidha, jumla ya ng'ombe 46,530 walihamilishwa katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Iringa, Kagera, Kigoma, Kilimanjaro, Mara, Morogoro, Mbeya, Mwanza na Tanga ikilinganishwa na ng'ombe 41,440 waliohamilishwa mwaka 2004/2005 katika mikoa hiyo. Vilevile, Wizara yangu ilikarabati miundombinu ya Kituo hicho, kutoa mafunzo kwa wahamilishaji 85 na kununua mtambo wa kutengeneza *"liquid nitrogen".* Ili kufikisha huduma ya uhamilishaji karibu zaidi na wafugaji, Wizara imenunua mitungi 28 ya kuhifadhia *"liquid nitrogen"* kwa ajili ya kuanzisha vituo viwili vya uhamilishaji vya Kanda ya Mashariki (Dar es Salaam) na ya Kati (Dodoma). Aidha, vituo vya uhamilishaji vya Mbeya na Mwanza vimeimarishwa kwa kuvinunulia mitungi 16.Katika mwaka 2006/2007, jumla ya dozi 48,950 za mbegu bora za uhamilishaji zitazalishwa ambapo ng'ombe 48,500 watahamilishwa. Aidha, Wizara itaimarisha vituo vyote vya uhamilishaji na kununua

mtambo mpya wa kutengeneza *"liquid nitrogen"* kwa ajili ya Kituo cha Mwanza. Vilevile, matumizi ya teknolojia ya upandikizaji wa mayai yaliyorutubishwa *(Multiple Ovulation and Embryo Transfer)* itaanzishwa katika shamba la mifugo la *Sao Hill.*

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa kuku na mayai nchini umeendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka. Katika mwaka 2005/2006, jumla ya vifaranga milioni 26.8 vya kuku wa biashara vilizalishwa nchini na vifaranga milioni 2.1 viliagizwa kutoka nje. Vilevile, mayai ya kutotoa vifaranga milioni 8.4 yaliagizwa kutoka nje. Aidha, uzalishaji wa mayai uliongezeka kutoka bilioni 1.8 mwaka 2004/2005 hadi mayai bilioni 2.1 mwaka 2005/2006 sawa na ongezeko la asilimia 16.7. Ulaji wa mayai kwa mtu kwa mwaka umeongezeka kwa asilimia 20.7 kutoka 53 hadi 64. Ongezeko hili limetokana na uhamasishaji wa ufugaji bora ikiwa ni pamoja na udhibiti wa magonjwa hususan ugonjwa wa mdondo. Katika mwaka 2006/2007 uzalishaji wa mayai ya kuku unatarajia kufikia bilioni 2.23.

Mheshimiwa Spika, katika zao la ngozi, Wizara yangu imeendelea na jitihada za kuhamasisha uzalishaji wa ngozi bora ili kuongeza thamani yake. Katika mwaka 2005/2006, jumla ya vipande vya ngozi za ng'ombe milioni 1.6, za mbuzi vipande milioni 1.4 na za kondoo vipande 950,000 vilikusanywa. Vipande milioni 1.36 vya ngozi za ng'ombe, milioni 1.2 za mbuzi na 861,770 vya kondoo vyenye thamani ya Shilingi bilioni 7.5 viliuzwa nje ya nchi.

Katika ngozi hizo kwa wastani asilimia 19 ni daraja la kwanza, asilimia 33 daraja la pili, asilimia 33 daraja la tatu na asilimia 15 daraja la nne. Wizara yangu itaendelea kuhamasisha wafugaji na wadau wengine ili kuongeza ubora wa zao la ngozi. Aidha, Wizara yangu ilishirikiana na Chama cha Wafanyabiashara ya Ngozi *(Leather Association of Tanzania)* kuendeleza zao la ngozi na kutoa mafunzo kwa wachinjaji, wachunaji, wawambaji, wachambuzi na wakaguzi wa ngozi 300 kupitia *"Common Fund for Commodities (CFC)".* Katika mwaka 2006/2007, lengo ni kukusanya vipande vya ngozi milioni 4.4. Vipande milioni 3.9 vinatarajiwa kuuzwa nje na kuliingizia Taifa takriban Shilingi bilioni 8.2. Aidha, mafunzo yatatolewa kwa wachinjaji, wachunaji, wakataji nyama *(butchers),* wawambaji na wakaguzi wa ngozi 400 ili kuboresha ubora na ukusanyaji wa ngozi katika maeneo ya vijijini.

Katika mwaka 2005/2006 Wizara yangu imejenga minada ya Lugodalutali (Mufindi) na Ngongo (Lindi Vijijini) na kukarabati mnada wa Mlowa (Iringa Vijijini). Aidha, Wizara inaendelea kukarabati minada ya Mbarali (Mbarali), Mitengo (Manispaa ya Mtwara), Kimande (Iringa Vijijini), Lumecha (Songea Vijijini), Mkongeni (Mvomero) na Malolo (Kilosa), Meserani (Monduli), Igunga (Igunga), Ipuli (Manispaa ya Tabora), Mhunze (Kishapu) na kituo cha kupumzikia mifugo cha Mparange (Rufiji). Vilevile, vituo vya kupakilia mifugo vya Meserani na Karatu, Pugu (Ilala) na Korogwe (Korogwe) vinaendelea kukarabatiwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara itakarabati minada ya Buhigwe (Kasulu), Kasesya (Sumbawanga Vijijini), Lumecha, Mlowa, Mbuyuni (Chunya), Meserani na vituo vya kupakilia mifugo katika minada hiyo. Vilevile, mnada

wa Kizota (Manispaa ya Dodoma) utaboreshwa ili kufikia hadhi ya kituo cha biashara ya mifugo. Pia, mfumo wa kukusanya na kusambaza taarifa za masoko ya mifugo utaanzishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Uongezaji thamani ya Maziwa na Nyama, Wizara yangu imeendelea kuratibu na kuhamasisha usindikaji wa maziwa ili kuongeza thamani ya bidhaa, usalama na muda wa uhifadhi. Kwa sasa kuna jumla ya viwanda 19 vyenye uwezo wa kusindika lita 490,000 ya maziwa kwa siku vikiwemo *Royal Dairies* na *Tan Dairies* (Dar es Salaam), *ASAS* (Iringa), *Tanga Fresh*, na *Azania Dairies (Tanga),* Serengeti na *Arusha Dairies (Arusha).* Katika mwaka 2005/2006 viwanda hivyo vilisindika asilimia 30 ya maziwa yaliyozalishwa nchini. Katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu kwa kushirikiana na Bodi ya Maziwa itabaini maeneo yenye maziwa mengi na kuanzisha mfumo wa kukusanya, kuhifadhi na kusindika maziwa. Aidha, Wizara itahamasisha uundaji wa vikundi vya wasindikaji wa maziwa na mazao yake.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika ujenzi wa viwanda vidogo, vya kati na vikubwa vya uchinjaji na usindikaji nyama. Katika mwaka 2005/2006, ujenzi wa viwanda 2 vya kuchinja na kusindika nyama ya ng'ombe vya *Sumbawanga Agricultural and Animal Feeds Industries Ltd. - SAAFI* (Rukwa) na *Tanzania Pride Meat (Morogoro)* umefikia asilimia 80. Viwanda hivyo vitakapokamilika, kila kimoja kitakuwa na uwezo wa kuchinja kati ya ng'ombe 150 na 200 kwa siku. Aidha, ujenzi wa machinjio ya kisasa ya kuku ya *Mkuza Chicks Limited* (Pwani) yamekamilika na yana uwezo wa kuchinja kuku 16,000 kwa siku. Katika mwaka 2006/2007, Wizara itaendelea kuhamasisha uwekezaji zaidi katika viwanda vya kusindika nyama ili kukidhi mahitaji ya soko.

Mheshimiwa Spika, Uendelezaji wa Mifumo ya Ufugaji wa Asili, ili kuendeleza ufugaji wa asili, katika mwaka 2005/2006, Wizara ilichangia kukamilisha uchimbaji na ukarabati wa malambo 20 katika Wilaya za Babati (2), Bagamoyo (3), Simanjiro (2), Bariadi (2), Hanang (1), Nzega (2), Bukombe (4), Arumeru (1), Manispaa ya Dodoma (1) na Musoma Vijijini (2). Aidha, malambo 15 yalijengwa ama kukarabatiwa chini ya Mpango wa Maendeleo ya Kilimo Wilayani (*DADPs*) katika Wilaya za Bukombe (7), Kongwa (2), Biharamulo (1), Misungwi (1), Morogoro Vijijini (1), Bagamoyo (1), Maswa (1) na Singida Vijijini (2).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri itajenga mabwawa mawili (2) katika Wilaya za Mwanga (1) na Kishapu (1). Aidha, Wizara itachangia ujenzi wa malambo 20 katika maeneo ya Kiwawa na Marendegu (Lindi), Maurowa na Ngereyani (Longido), Mbondo na Matekwa (Nachingwea), Mchakama na Mtandago (Kilwa), Zavuza na Chogo (Handeni), Mwamabiti (Shinyanga Vijijini), Magaji (Chunya), Mwamboka (Misungwi), Tubugwe (Kongwa), Kinamweri (Bariadi), Kambala (Mvomero), Manyoni (1), Urambo (1) na Maswa (2).

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua umuhimu wa matumizi endelevu ya ardhi kwa ajili ya malisho. Katika mwaka 2005/2006, Wizara ilitoa mafunzo kwa

wafugaji 50 na wataalamu 9 kutoka Wilaya za Dodoma Vijijini, Dodoma Mjini, Igunga, Kondoa, Kongwa, Manyoni, Mpwapwa, Nzega na Singida Vijijini ili kukidhi lengo hilo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau itaainisha maeneo yanayofaa kwa ufugaji, itahamasisha kuhusu matumizi endelevu ya ardhi kwa ajili ya malisho na itatoa mafunzo kwa wataalam katika Halmashauri 10 za Wilaya za Bagamoyo, Bukombe, Handeni, Kishapu, Manyoni, Mvomero, Nachingwea, Namtumbo, Nkasi na Urambo kuhusu matumizi bora ya ardhi. Aidha, Wizara itahamasisha uendelezaji wa njia za asili za hifadhi ya malisho, matumizi bora ya mabaki ya mazao ya kilimo, hususan wakati wa kiangazi na kufuatilia hali ya malisho katika maeneo ya malisho ili kutoa tahadhari kwa wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Uzalishaji wa Mbegu za Malisho na Hei katika mwaka 2005/2006 Wizara yangu ilichangia kuzalisha mbegu bora za malisho kwa kuimarisha mashamba ya Langwira (Mbeya) na Vikuge (Pwani). Jumla ya tani 15.7 za mbegu na marobota ya hei 109,000 yalizalishwa kwenye mashamba hayo pamoja na taasisi nyingine za serikali katika vituo vya Buhuri, Kongwa, Mpwapwa, *Sao Hill,* Tanga na Tengeru. Lengo lilikuwa ni kuzalisha tani 10.5 za mbegu za malisho na marobota ya hei 70,000. Aidha, sekta binafsi ilizalisha tani 3.5 za mbegu za malisho na marobota ya hei 69,100.

Katika mwaka 2006/2007 Wizara yangu itaimarisha mashamba ya mfano ya malisho ya Vikuge na Langwira na kuanzisha mashamba mapya Kizota na Kongwa (Dodoma), *Sao Hill* (Iringa), Mivumoni na Buhuri (Tanga), *West Kilimanjaro* na Mabuki (Mwanza) kwa lengo la kuzalisha tani 25 za mbegu za malisho na marobota ya hei 150,000. Sekta binafsi inatarajiwa kuzalisha mbegu tani 5 na marobota ya hei 80,000. Aidha, Wizara itagharamia upimaji wa mashamba ya Vikuge na Langwira na mashamba mapya yatakayoanzishwa. Vilevile, Wizara itahamasisha Halmashauri na Sekta binafsi kuanzisha mashamba ya mbegu za malisho na hei ili kuwa na uhakika wa malisho, hususan wakati wa kiangazi.

Mheshimiwa Spika, Vyakula vya Mifugo, sekta binafsi imeendelea kuzalisha vyakula vya mifugo. Katika mwaka 2005/2006, uzalishaji wa vyakula vya mifugo uliongezeka kwa asilimia 5.6 kutoka tani 529,300 mwaka 2004/2005 hadi tani 559,000. Uzalishaji huu ni sawa na asilimia 86 ya mahitaji ambayo yanakadiriwa kuwa tani 650,000 kwa mwaka. Takriban asilimia 90 ya vyakula hivi ni vya kuku na vilivyobakia ni vya ng'ombe wa maziwa na nguruwe. *(Makofi)*

Wazalishaji wakubwa wa vyakula vya mifugo ni pamoja na *Mkuza Chicks, Kibaha Education Centre* (Pwani), *Twiga Feeds, Igo Feeds, Farmers Center* na *A-Z Company* (Dar es Salaam) na *Burka Feeds* (Arusha). Lengo la uzalishaji wa vyakula vya mifugo halikufikiwa kutokana na ukame uliosababisha upungufu wa nafaka na mgao wa umeme. Katika mwaka 2006/2007, sekta binafsi inatarajiwa kuzalisha tani 574,400 za vyakula vya mifugo na Wizara yangu itaendelea kudhibiti ubora wa vyakula hivyo.

Mheshimiwa Spika, huduma za afya ya mifugo, huduma bora za afya ya mifugo ni muhimu katika kupunguza kuenea kwa magonjwa ya wanyama, vifo vya mifugo na kulinda afya za watumiaji wa mazao ya mifugo. Juhudi za kudhibiti magonjwa mbalimbali ya mifugo nchini zimefanyika kama ifuatavyo:-

Magonjwa ya Milipuko *(Transboundary Diseases)*. Ugonjwa wa Sotoka *(Rinderpest)*

Mheshimiwa Spika, mwaka jana Bunge lako Tukufu liliarifiwa kuwa nchi yetu ilipata cheti cha kutambuliwa rasmi na Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (*OIE*) kuwa huru na ugonjwa wa Sotoka (*free from Rinderpest disease*). Katika mwaka 2005/2006 ufuatiliaji wa Ugonjwa wa Sotoka ulifanyika katika mikoa ya Kanda ya Ziwa na Kanda ya Kaskazini kupata vielelezo vya kuwezesha nchi yetu kutambuliwa kuwa huru na maambukizi ya ugonjwa huo (*free from Rinderpest infection*). Aidha, sampuli 2,890 za damu ya ng'ombe, mbuzi na kondoo na sampuli 24 za damu ya wanyamapori zilikusanywa na kuchunguzwa. Uchunguzi huo ulionyesha kutokuwepo maambukizi ya Sotoka. Katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu itaendelea kufuatilia maambukizi ya Sotoka katika kanda hizo na inatarajia kuwasilisha *OIE* maombi ya nchi yetu kutambuliwa kuwa huru na maambukizi ya Sotoka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ugonjwa wa homa ya mapafu *(Contagious Bovine Pleuropneumonia* (*CBPP*), juhudi za kudhibiti Ugonjwa wa Homa ya Mapafu ziliendelea chini ya mpango wa *Roll Back Vaccination Plan* ambapo ugonjwa unadhibitiwa eneo kwa eneo kuanzia eneo lililopata ugonjwa mwisho, kuelekea eneo ugonjwa ulipoanzia. Mpango huo ulianza mwaka 2004/2005 katika mikoa ya Rukwa, Mbeya na Iringa ambapo hadi sasa jumla ya ng'ombe 3,072,066 wamechanjwa.

Katika mwaka 2005/2006, uchanjaji dhidi ya ugonjwa huo uliendelea pia katika mikoa ya Arusha, Manyara, Dodoma, Kagera, Kigoma, Singida, Tabora, Dar es Salaam na Tanga. Aidha, Wizara ilinunua jumla ya dozi milioni 4 na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (*FAO*) lilitoa dozi milioni 2 za chanjo. Jumla ya ng'ombe 5,494,520 walichanjwa kama inavyoonyeshwa kwenye Kiambatanisho Na. 9 na baadhi ya wilaya zilipata maambukizi ya ugonjwa huu Hatua zilizochukuliwa na Serikali kudhibiti ugonjwa huo zinaonyesha dalili za mafanikio kwa kupunguza kasi ya maambukizi na vifo kwa asilimia 50.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara itanunua dozi milioni 5 na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa *(FAO)* linatarajia kutoa dozi milioni 1 za chanjo ili kuendeleza mpango wa '*Roll Back Vaccination Plan'* utakaotekelezwa na Halmashauri za Wilaya na Manispaa katika mikoa yote nchini isipokuwa Mkoa wa Kilimanjaro ambao hauna ugonjwa. Jumla ya ng`ombe milioni 6 wanatarajiwa kuchanjwa.

Mheshimiwa Spika, Ugonjwa wa Miguu na Midomo (*Foot and Mouth Disease (FMD)* katika mwaka 2005/2006, Ugonjwa wa Miguu na Midomo uliambukiza ng'ombe

2,438 katika mikoa ya Mbeya, Kagera na Ruvuma ambapo ng'ombe 37 walikufa na ng'ombe 18,750 walichanjwa katika wilaya za Bukoba, Muleba, Mbozi na Songea. Ugonjwa wa Miguu na Midomo uliripotiwa katika Wilaya 24 za Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Kagera, Kigoma, Lindi, Mara, Mbeya, Mwanza, Pwani, Rukwa, Ruvuma, Shinyanga, Tabora na Tanga. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu Mheshimiwa Spika kuwa, ujenzi wa ukuta wa Maabara Kuu ya Mifugo Temeke na uwekaji wa baadhi ya vifaa vya maabara kwa ajili ya kuchunguza ugonjwa wa Miguu na Midomo umekamilika kwa asilimia 80. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara itaendelea kushirikiana na sekta binafsi na wafugaji kudhibiti ugonjwa huo. Aidha, Wizara itakamilisha ujenzi wa maabara ya ugonjwa wa Miguu na Midomo, Temeke. Vile vile, Maabara inatarajia kupata vifaa vyenye thamani ya Dola milioni 1.0 kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika kupitia ushirikiano wa Nchi za Jumuiya ya Kusini mwa Afrika, *SADC*.

Mheshimiwa Spika, Ugonjwa wa Homa ya Nguruwe *(African Swine Fever)* Ugonjwa wa Homa ya Nguruwe umeendelea kuwa tishio katika uzalishaji wa nguruwe nchini. Katika mwaka 2005/2006, matukio ya ugonjwa huo yaliripotiwa katika Manispaa ya Mwanza ambapo nguruwe 471 wanaokadiriwa kuwa na thamani ya shilingi milioni 28 walikufa. Aidha, nguruwe 617 waliambukizwa. Ugonjwa huo umedhibitiwa katika maeneo hayo na maeneo yaliyoambukizwa hapo awali ya Arusha, Dar es Salaam, Tabora, Mbeya na Kigoma. Katika mwaka 2006/2007, Wizara itaendelea kushirikiana na Halmashauri na wafugaji kudhibiti ugonjwa huo ambao bado hauna kinga ikiwa ni pamoja na kuzuia usafirishaji holela wa nguruwe na mazao yake.

Mheshimiwa Spika, Magonjwa Yaenezwayo na Wadudu *(Vector-borne Diseases)* Magonjwa Yaenezwayo na Kupe, magonjwa yaenezwayo na kupe, hususan Ndigana Kali (*East Coast Fever – ECF*), ni miongoni mwa magonjwa yanayoathiri uzalishaji wa mifugo na mazao yake nchini. Takwimu za mwaka 2005/2006 zinaonyesha kuwa ng'ombe 1,757 walikufa kwa Ndigana Kali, 754 Ndigana Baridi (*Anaplasmosis*), 322 Maji Moyo (*Heartwater*) na 322 Mkojo Mwekundu (*Babesiosis*). Ili kupunguza athari zitokanazo na magonjwa hayo, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ilianza kukarabati na kujenga majosho chini ya Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo Wilayani (*DADPs*) kuanzia mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, kupitia mpango wa *DADPs*, jumla ya shilingi 341,801,540 zilitolewa kwa ajili ya kukarabati na kujenga majosho 84 katika Halmashauri 36 za Arumeru (2), Kongwa (3), Mufindi (4), Iringa Vijijini (1), Bukoba Vijijini (8), Muleba (3), Karagwe (1), Biharamulo (2), Kasulu (6), Hai (3), Moshi Vijijini (2), Hanang (5), Serengeti (1), Tarime (4), Morogoro Vijijini (1), Kilosa (1), Masasi (2), Geita (2), Kwimba (4), Ukerewe (3), Sengerema (1), Bagamoyo (1), Kibaha (1), Sumbawanga (2), Nkasi (2), Songea Vijijini (1), Namtumbo (2), Mbinga (4), Songea Manispaa (1), Maswa (1), Kishapu (1), Shinyanga Vijijini (1), Iramba (2), Singida Vijijini (1), Igunga (3) na Korogwe (2). Ukarabati na ujenzi wa majosho hayo upo katika hatua mbalimbali. *(Makofi)*

Katika mwaka 2005/2006 uhamasishaji na ufuatiliaji wa chanjo dhidi ya Ndigana Kali *(ECF)* ulifanyika. Jumla ya ng'ombe 30,000 walichanjwa katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Iringa, Kagera, Kilimanjaro, Manyara, Mbeya, Morogoro, Mtwara na Tanga. Matokeo ya chanjo hiyo yameonyesha kupunguza vifo vya ndama vinavyosababishwa na Ndigana Kali kutoka asilimia 50 hadi asilimia 10 kwa ng'ombe waliochanjwa. Katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu itatoa ruzuku ya shilingi milioni 500 kwa ajili ya ununuzi na usambazaji wa madawa ya kuogeshea mifugo. Vilevile, dozi 120,000 za chanjo ya Ndigana Kali zitatolewa na *FAO* kwa ajili ya kuchanja mifugo katika mikoa iliyoathirika zaidi kwa ukame ya Arusha, Dodoma, Iringa, Kilimanjaro, Manyara, Mara, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Pwani, Shinyanga, Singida, Tabora na Tanga. Aidha, Wizara yangu itaendelea kuhamasisha Halmashauri na wafugaji kuhusu udhibiti wa kupe na magonjwa wayaenezayo.

Mheshimiwa Spika, Ugonjwa wa Nagana *(Trypanosomosis)* ugonjwa wa Nagana unaoenezwa na mbung'o uliendelea kuathiri mifugo. Katika mwaka 2005/2006 ugonjwa huo ulitokea katika mikoa 18 ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Kagera, Kigoma, Kilimanjaro, Lindi, Mara, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Mwanza, Pwani, Ruvuma, Shinyanga, Tabora na Tanga ambapo jumla ya ng'ombe 10,019 walipatwa na Nagana na kati ya hao, ng'ombe 299 walikufa. Aidha, uchunguzi wa mbung'o umefanyika katika wilaya za Bariadi, Bukombe, Kahama, Maswa, Meatu na Shinyanga Vijijini ambapo rasimu ya ramani ya usambaaji wa mbung'o imeandaliwa. Vilevile, jumla ya vyambo (targets) 248 vya kuua mbung'o vilitengenezwa na kuwekwa katika mapori ya vijiji vya Mnyamasi, Kasisi na Ugala Wilayani Mpanda. Pia, maandalizi ya mradi wa pamoja wa kutokomeza mbung'o Barani Afrika (*Pan African Tsetse and Trypanosomosis Eradication Campaign – PATTEC*) utakaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)* kwa nchi za Rwanda na Tanzania katika bonde la mto Kagera yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri na wananchi itaendelea kufuatilia na kudhibiti mbung'o na Nagana na kutoa mafunzo kwa wataalam 50 katika mikoa yote yenye tatizo la mbung'o na nagana. Aidha, Wizara itafanya tathmini ya mashamba darasa 10 yaliyo katika mikoa ya Kagera na Tanga.

Magonjwa ya Mifugo Yanayoambukiza Binadamu (*Zoonoses*), katika mwaka 2005/2006 ufuatiliaji na udhibiti wa magonjwa ya mifugo yanayoambukiza binadamu ya Kichaa cha Mbwa, Kimeta, Ugonjwa wa Kutupa Mimba na Kifua Kikuu uliendelea kupewa kipaumbele na Wizara yangu.Kichaa cha Mbwa (*Rabies*), katika mwaka 2005/2006, ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa umeendelea kuwa tishio kwa binadamu na mifugo ambapo jumla ya matukio 72 yalitokea katika wilaya 35 nchini (Kiambatanisho Na. 13). Ili kukabiliana na tatizo hilo, Wizara yangu ilinunua na kusambaza jumla ya dozi 100,000 za chanjo dhidi ya kichaa cha mbwa katika wilaya 70. Katika mwaka 2006/2007, jumla ya dozi 100,000 za chanjo zitanunuliwa na kusambazwa katika wilaya 90. Aidha, Wizara yangu itazihamasisha Halmashauri kutunga sheria ndogo ndogo za kuzuia uzururaji wa mbwa na paka ili kuzuia kuenea kwa ugonjwa huo.

Mheshimiwa Spika, Kimeta (*Anthrax*), katika mwaka 2005/2006 ugonjwa wa Kimeta ulitokea katika wilaya za Monduli, Ngorongoro, Arusha, Arumeru, Rombo, Hai, Mpwapwa na Manispaa ya Kinondoni. Katika wilaya ya Ngorongoro, ugonjwa ulitokea katika hifadhi ya wanyamapori ambapo wanyama mbalimbali 143 walikufa. Ili kudhibiti ugonjwa huo, jumla ya ng'ombe 18,626, mbuzi na kondoo 10,211 na nguruwe 85 walichanjwa katika wilaya za Rombo na Moshi Vijijini. Katika mwaka 2006/2007 Wizara itaendelea kutengeneza chanjo dhidi ya Kimeta katika Maabara Kuu ya Mifugo (*Central Veterinary Laboratory - CVL*) ili chanjo hiyo iweze kupatikana kwa gharama nafuu. Aidha, Halmashauri za wilaya kwa kushirikiana na sekta binafsi zitahimizwa kuchanja mifugo kudhibiti ugonjwa huo.

Mheshimiwa Spika, Ugonjwa wa Kutupa Mimba (*Brucellosis*) katika mwaka 2005/2006, jumla ya ng'ombe 3,911 walifanyiwa uchunguzi wa ugonjwa wa Kutupa Mimba nchini ambapo ng'ombe 244 sawa na asilimia 6.2 waligundulika kuwa na ugonjwa huo. Wafugaji walishauriwa kuchinja ng'ombe waliopatwa na ugonjwa huo ili kupunguza maambukizi mapya. Katika mwaka 2006/2007, jumla ya ng'ombe 10,000 watafanyiwa uchunguzi dhidi ya ugonjwa huo.

Mheshimiwa Spika, Kifua Kikuu cha Ng'ombe *(Bovine Tuberculosis)* katika mwaka 2005/2006, uchunguzi wa ugonjwa wa Kifua Kikuu umefanyika katika ng'ombe 168 katika Kanda ya Ziwa na wote walikutwa hawana ugonjwa. Katika mwaka 2006/2007, ng'ombe 10,000 watafanyiwa uchunguzi kote nchini. Aidha, ukusanyaji wa takwimu za matukio ya ugonjwa huu kutoka katika machinjio utaimarishwa.

Mheshimiwa Spika, Ukaguzi wa Mifugo na Mazao Yake, katika mwaka 2005/2006, ukaguzi wa mifugo na mazao yatokanayo na mifugo uliendelea katika vituo vyote 36 vya mipakani na vituo 381 vya ndani kwa ajili ya kujilinda na magonjwa ya milipuko. Aidha, vituo vya ukaguzi vya mipakani vya Kasesya (Sumbawanga Vijijini), Isongole (Ileje), Sirari (Tarime), Namanga (Longido), Kyaka (Bukoba Vijijini) na Mbamba Bay (Mbinga) viliimarishwa kwa kujenga ofisi na kuvipatia vitendea kazi. Vilevile, huduma za ukaguzi zimeanzishwa katika vituo vya bandari vya Bagamoyo na Pangani. Ujenzi wa kituo cha Karantini cha Marendego (Kilwa) unaendelea. Pia, ukaguzi wa mifugo inayouzwa nje uliendelea ambapo jumla ya ng'ombe 1,706 na mbuzi 800 waliouzwa nchini Comoro na Burundi katika mwaka 2005/2006 walikaguliwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara itaimarisha vituo vya ukaguzi wa mifugo na mazao yake vya Madaba (Songea Vijijini), Sirari (Tarime), Holili (Rombo), Ruvu Darajani (Kibaha) na Kasanga (Sumbawanga Vijijini) pamoja na vituo vya bandarini vya Pangani na Bagamoyo na viwanja vya ndege Kilimanjaro na Dar es Salaam kwa kuvipatia vitendea kazi na vifaa vya mawasiliano. Wizara pia itaimarisha vituo vya Karantini vya Kwala na Mparange (Rufiji), Kirumi (Musoma Vijijini) na Manienga/Ihefu (Mbarali) kwa ajili ya kudhibiti magonjwa ya mifugo na uharibifu wa mazingira. Aidha, Wizara itatoa mafunzo kwa wataalam 60 katika vituo hivyo.

Mheshimiwa Spika, Uimarishaji wa Vituo vya Uchunguzi wa Magonjwa ya Wanyama *(Veterinary Investigation Centres - VICs)*katika mwaka 2005/2006 Wizara

kupitia mradi wa *Pan African Programme for the Control of Epizootics* (*PACE*) unaofadhiliwa na Umoja wa Nchi za Ulaya, imeendelea kuviimarisha Vituo vya Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo (*VICs*) vya Arusha, Iringa, Mpwapwa, Mtwara, Mwanza, Tabora na Maabara Kuu ya Mifugo - Temeke kwa kuvipatia vifaa vya maabara na kuweka mfumo wa uchunguzi wa mienendo ya magonjwa (*Epidemio-surveillance System*) ili kuviwezesha kufanya uchunguzi, kufuatilia mwenendo wa magonjwa, kutoa tahadhari ya milipuko ya magonjwa na kutoa ushauri wa kuyadhibiti. Vilevile, Wizara ilitoa mafunzo kwa watumishi 36 wa vituo hivyo na wa Halmashauri kuhusu magonjwa ya milipuko.

Aidha, Wizara ilinunua na kutoa pikipiki 3 kwa Wilaya za Mvomero, Singida Vijijini na Musoma Vijijini na baiskeli 100 kwa Wilaya 26 za Arusha, Bunda, Handeni, Iringa, Kilindi, Korogwe, Lushoto, Magu, Mbarali, Mbeya, Mbozi, Mbulu, Monduli, Morogoro, Moshi, Muleba, Musoma, Muheza, Nzega, Pangani, Rombo, Rungwe, Same, Simanjiro, Tanga na Temeke kwa ajili ya kufuatilia mwenendo wa magonjwa katika maeneo yao. Katika mwaka 2006/2007, Wizara itaendelea kuviimarisha Vituo vya Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo nchini kwa kuvikarabati na kuvipatia vitendea kazi ili vifanye kazi kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Ukaguzi wa Machinjio, Mabanda ya Ngozi na Nyama, katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ilifanya ukaguzi wa machinjio, mabanda ya ngozi na maghala ya kuhifadhia ngozi. Ukaguzi huo ulibaini kuwa machinjio nyingi zipo katika hali isiyoridhisha kimajengo, usafi na hazina vitendea kazi muhimu. Wizara yangu ilizishauri Halmashauri hizo kuboresha machinjio zake ili kuhakikisha wananchi wanapata nyama safi na salama. Vilevile, wataalam wa mifugo katika Halmashauri walikagua jumla ya ng'ombe 364,091, mbuzi 121,226, kondoo 58,444 na nguruwe 112,190 waliochinjwa. Katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Halmashauri na wadau wengine kufanya ukaguzi wa machinjio, mabanda ya ngozi, maghala ya kuhifadhia ngozi, madawa ya mifugo na pembejeo nyingine. Pia, Wizara yangu itatoa mafunzo kwa wakaguzi wa nyama na ngozi 150 wa Halmashauri mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Usimamizi wa Utoaji Huduma za Mifugo kwa kuzingatia Sheria ya Veterinari Na. 16 ya mwaka 2003, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wengine iliendelea kuratibu na kusimamia utoaji wa huduma za afya ya mifugo. Huduma hizo ni pamoja na utoaji wa kinga na tiba, ukaguzi wa wanyama na mazao yake, uagizaji na usambazaji wa pembejeo yakiwemo madawa ya mifugo. Katika mwaka 2005/2006 ili kusimamia kikamilifu utoaji wa huduma hizo, Baraza la Veterinari lilisajili madaktari wa mifugo 24 na kufanya idadi ya madaktari wa mifugo waliosajiliwa kufikia 530. Kati ya hao, asilimia 53 wameajiriwa na Serikali na Taasisi za Umma, na asilimia 47 wako kwenye sekta binafsi. Pia, wataalamu wasaidizi 180 waliorodheshwa na 150 kuandikishwa, hivyo kufanya idadi ya wataalam hao kufikia 461. Aidha, taratibu za usajili wa wataalamu kutoka nje wanaotaka kutoa huduma za afya ya mifugo nchini zimeandaliwa na zimeanza kutumika. Vilevile, vituo 29 vya huduma ya afya ya mifugo vilisajiliwa na kufanya idadi ya vituo vilivyosajiliwa nchini kufikia 107. Asilimia 70 ya vituo hivyo vipo katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Morogoro na Mwanza.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, wakaguzi 77 wa huduma za mifugo katika Halmashauri waliteuliwa. Katika ukaguzi uliofanyika, wataalamu 4 walibainika kukiuka maadili katika mikoa ya Arusha na Dar es Salaam na waliadhibiwa kwa mujibu wa sheria. Wataalamu wasaidizi wa mifugo waliwezeshwa kuunda umoja wao ujulikanao kama *Tanzania Veterinary Paraprofessionals Association – (TAVEPA).*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu itaendelea kuimarisha Baraza la Veterinari ili liweze kusimamia utekelezaji wa miongozo, kusajili madaktari wapya, kuandikisha, kuorodhesha na kujenga uwezo wa wataalamu wasaidizi 300 wa afya ya mifugo; kusajili na kukagua vituo 140; kutoa mafunzo ya kitaaluma kwa wajumbe 9, watendaji 65 wa Baraza la Taaluma ya Veterinari na wakaguzi 77 na kuhamasisha Halmashauri kuhusu ushirikishwaji wa sekta binafsi katika kutoa huduma za mifugo.

Mheshimiwa Spika, utafiti wa mifugo ni kati ya majukumu yanayotekelezwa na Wizara yangu kwa lengo la kuzalisha na kusambaza teknolojia zinazoongeza uzalishaji wa mifugo na mazao ya mifugo, pamoja na kutambua na kudhibiti magonjwa ya mifugo. Utafiti huu uliendelea kufanyika kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tume ya Sayansi na Teknolojia (*COSTECH*) na Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mifugo *(International Livestock Research Institute)* Nairobi, Kenya.

Mheshimiwa Spika, Utafiti wa Ng'ombe wa Nyama, Wizara imeendelea kuratibu utafiti pamoja na uendelezaji wa ng'ombe aina ya Mpwapwa na Ankole. Katika mwaka 2005/2006, idadi ya ng'ombe aina ya Mpwapwa katika Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Mpwapwa imeongezeka kutoka ng'ombe 833 hadi 979. Lengo ni kufikia ng'ombe zaidi ya 1,000 katika taasisi hiyo ili ng'ombe hao waweze kutambulika kama koo kamili *(stable breed).* Aidha, madume 146 aina ya Mpwapwa yalitengwa kwa ajili ya vikundi vya wafugaji. Kati ya hayo, madume 104 yameuzwa kwa vikundi vya wafugaji katika Wilaya za Iramba (28), Simanjiro (20), Mpwapwa (4), Dodoma Mjini (11), Kongwa (4), Singida Vijijini (11) Chunya (9) na Manyoni (17). Madume 42 yaliyobaki yametengwa kwa ajili ya wilaya za Ngorongoro, Sumbawanga Vijijini na Longido. Utafiti kuhusu ng'ombe aina ya Ankole na utafiti juu ya kosaafu za ng'ombe wa asili kama vile *Singida White, Iringa Red, Masai Red, Masai Black* na *Tarime* uliendelea. Katika mwaka 2006/2007, Wizara itaendelea kufanya utafiti wa ng'ombe hao pamoja na kuongeza idadi yao ili waweze kusambazwa kwa wingi kwa wafugaji nchini.

Mheshimiwa Spika, utafiti wa ng'ombe wa maziwa, Wizara imeendelea kufanya utafiti wa ng'ombe wa maziwa katika vituo vya Utafiti wa Mifugo Tanga, Mpwapwa na Uyole. Katika mwaka 2005/2006, tafiti zilizofanyika zilihusu mifumo ya lishe ya ng'ombe wa maziwa; ubora wa ngo'mbe wa asili (TSZ) na chotara (*cross breeds*) wanaokusudiwa kutoa maziwa katika mazingira ya wafugaji wadogo; koosafu za ng'ombe wa asili waliopo nchini; uboreshaji wa lishe na vyakula vya nyongeza (*supplementary feeds*), utambuzi na utumiaji wa mifumo ya masoko ya maziwa na mazao yake. Kutokana na tafiti hizo zilizofanyika katika vijiji vya Lugoba (Bagamoyo),

Languseto na Kwenjugo (Handeni), jumla ya ndama chotara 328 wamezaliwa na kuonyesha kasi ya ukuaji kwa siku wa wastani wa gramu 268 ikilinganishwa na gramu 100 wa ndama wa asili. Vilevile, ng'ombe chotara walionekana kupunguza kipindi cha mzao mmoja hadi mwingine (*calving interval*) kufikia wastani wa siku 461 ikilinganishwa na siku 535 kwa ng'ombe wa asili. Aidha, ng'ombe chotara wameonyesha kuongeza uzalishaji wa maziwa kutoka lita 6 hadi 8 ikilinganishwa na lita 1 hadi 2 kwa siku kwa ng'ombe wa asili.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu itaendelea kufanya utafiti wa ng'ombe wa maziwa kwa kuzalisha na kusambaza teknolojia zitakazolenga kuongeza kiwango cha kuzaa (*calving rate*) kutoka wastani wa asilimia 40 hadi 70, kupunguza muda wa mzao *(calving interval)* kutoka wastani wa miezi 24 hadi miezi 15, kupunguza vifo vya ndama (*mortality rate*) kutoka asilimia 40 hadi 10, kuongeza uzalishaji wa maziwa ya ng'ombe wa asili kutoka wastani wa nusu lita hadi lita 4 kwa siku, na kuongeza uzito wa ng'ombe wa nyama wa asili wakati wa kuchinja kutoka kilo 250 hadi kilo 450 katika umri wa miaka 4.

Mheshimiwa Spika, utafiti wa uzalishaji wa mbuzi na kondoo utafiti wa mbuzi na kondoo unalenga kuboresha viwango vya uzalishaji wa mbuzi na kondoo wa asili na kuongeza uwezo wa mbuzi kuzaa mapacha. Katika mwaka 2005/2006, utafiti wa mbuzi aina ya *Malya Blended Goats)* 585 uliendelea katika vituo vya Mpwapwa, Kongwa, Tanga na West Kilimanjaro na kuhusu mbuzi jamii ya *Newala* katika Kituo cha Mnima wilayani Newala.

Utafiti kuhusu mbuzi aina ya *Ujiji* nao uliendelea. Tathmini ya mbuzi 740 aina ya Malya waliosambazwa na 1,472 chotara waliozaliwa katika wilaya za Kondoa, Muheza, Kilosa, Bagamoyo na Handeni kuanzia mwaka 2001/2002 iliendelea. Utafiti huo umeonyesha kuwa mbuzi chotara wana uwezo wa kustahimili mfumo wa ufugaji wa asili ambapo vifo vyao ni chini ya asilimia 5 sawa na mbuzi wa asili. Aidha, mbuzi hao huzalisha maziwa kati ya lita 1.2 hadi 1.5 kwa siku. Katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu itaendelea kufanya utafiti wa mbuzi na kondoo kwa kuzalisha na kusambaza teknolojia zitakazolenga kupunguza vifo vya vitoto vya mbuzi na kondoo kutoka wastani wa asilimia 50 hadi 20 na kuongeza uzito wa mbuzi na kondoo kutoka kilo 25 hadi kilo 45 kwa umri wa miaka 2.

Mheshimiwa Spika, utafiti wa kuku, katika mwaka 2005/2006, utafiti wa kuku ulilenga katika kutathmini ubora wa kuku chotara wanaoweza kukua haraka na kuzalisha mayai kwa wingi katika mazingira ya wafugaji wadogo. Utafiti huo unaendelea katika vijiji 36 vya wilaya za Bagamoyo, Kilosa, Korogwe, Mbozi, Muheza, Pangani na Tanga na jumla ya kuku chotara 3,200 wanahusika. Matokeo ya awali yanaonyesha kuwa uzito wa kuku chotara unaweza kufikia wastani wa kilo 2 ukilinganisha na kilo 0.75 kwa kuku wa asili katika umri wa mwaka mmoja, uzito wa yai kutoka wastani wa gramu 25 kufikia gramu 50 na wingi wa mayai kutoka 40 hadi 100 kwa mwaka. Katika mwaka 2006/2007, utafiti huu utaendelea.

Mheshimiwa Spika, Utafiti wa Nguruwe katika mwaka 2005/2006, utafiti wa nguruwe ulilenga kuboresha nguruwe wa asili na ulifanyika katika Wilaya za Rungwe na

Mbozi ambapo kaya 50 zinazofuga zilihusishwa. Madume bora aina ya *Landrace* na *Large White* yalitumika kupandisha nguruwe wa asili ili kupata nguruwe chotara. Utafiti huo umeonyesha kuwa nguruwe wa asili huzaa watoto wachache kati ya 3 hadi 5 ikilinganishwa na nguruwe chotara wanaozaa kati ya watoto 8 hadi 15. Katika mwaka 2006/2007 utafiti huo utaendelezwa katika maeneo mengine ya mikoa ya Mbeya, Iringa na Rukwa.

Mheshimiwa Spika, Utafiti wa Malisho ya Mifugo katika mwaka 2005/2006 utafiti wa malisho ya mifugo ulifanyika katika Vituo vya Utafiti wa Mifugo vya Kongwa, Mpwapwa, Tanga na Uyole. Utafiti huo ulilenga katika kuongeza wingi, ubora, matumizi na hifadhi endelevu ya malisho ili kuhakikisha kunakuwepo na malisho ya kutosha, hususan wakati wa kiangazi. Jumla ya hekta 625 za malisho zilifanyiwa majaribio ya utafiti kwa kusia mbegu bora aina ya nyasi na mikunde na kuweka utaratibu wa matumizi bora ya malisho hayo katika wilaya za Chunya, Kilindi, Kilombero, Mbarali, Mbeya Vijijini, Mbozi, Mufindi, Muheza, Mvomero, Njombe, Rungwe na Sumbawanga. Utafiti huo ulionyesha ongezeko la malisho kutoka tani 1 hadi 2.5 kwa hekta. Katika mwaka 2006/2007 tafiti hizi zitaendelezwa katika mikoa yenye mifugo mingi na maeneo kame ya Arusha, Dodoma, Iringa, Kilimanjaro, Manyara, Mara, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Pwani, Rukwa, Shinyanga, Singida, Tabora na Tanga.

Mheshimiwa Spika, utafiti wa maradhi ya Mifugo, katika mwaka 2005/2006, utafiti wa maradhi ya mifugo uliendelea kufanyika katika Maabara Kuu ya Mifugo Temeke na Taasisi ya Utafiti wa Ndorobo na Malale (*Tsetse and Trypanosomosis Research Institute (TTRI*), Tanga. Utafiti ulilenga katika kupata mbinu bora za kutambua maradhi haraka, kushauri juu ya tiba na kinga na kutengeneza chanjo bora za bakteria na virusi vinavyoathiri mifugo. Katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu itaendelea na utafiti huo.

Mheshimiwa Spika, utafiti wa chanjo ya ugonjwa wa mdondo wa kuku ya I-2 umeendelea kufanyika katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Iringa, Mbeya, Mtwara na Kanda ya Ziwa. Chanjo hii inastahimili joto na matumizi yake huhitaji teknolojia rahisi kwa ajili ya kuku wa asili vijijini ambako hakuna majokofu. Katika mwaka 2005/2006, jumla ya dozi 6,795,200 zilizalishwa na kusambazwa kwa wafugaji takriban mikoa yote nchini na imeonyesha mafanikio makubwa ambapo imepunguza vifo vya kuku kutoka asilimia 90 hadi 5 pale ilipotumika. Katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu itaendelea na utafiti huo pamoja na kuzalisha na kusambaza dozi milioni 12 za chanjo hiyo.

Mheshimiwa Spika, utafiti wa mbung'o na Nagana, katika mwaka 2005/2006 utafiti wa namna ya kuangamiza mbun'go aina ya *Glossina swynnertoni* uliendelea katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Kilimanjaro, Manyara, Mara na Shinyanga. Vilevile, uchunguzi wa awali wa kubaini mtawanyiko wa aina mbalimbali za Mbung'o ulifanyika katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Kilimanjaro, Manyara, Mara, Shinyanga, Singida na Tanga. Uchunguzi umeonyesha kuwa mbung'o wamepungua katika maeneo mengi ya makazi kuliko ilivyokuwa miaka ya nyuma. Pia, Taasisi ya Utafiti wa Mbung'o na Nagana *(TTRI)* Tanga ilipatiwa vifaa maalum vya kutengeneza ramani kwa kutumia

*satellite (GIS)* kutoka Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki -*International Atomic Energy Agency* (*IAEA*).

Mheshimiwa Spika, utafiti wa kutokomeza mbung'o aina ya *Glossina brevipalpis* umeendelea kufanyika katika Wilaya ya Mafia kwa kutumia mbung'o 3,500 wanaokuzwa kwenye maabara ya Tanga. Vilevile, Taasisi inaendelea kuzalisha na kutunza mbung'o 80,000 aina ya *Glossinna austeni* kwa ajili ya matumizi ya utafiti nchini Afrika ya Kusini na mbung'o 5,500 aina ya *Glossina morstans* kwa ajili ya Botswana, Ethiopia na Afrika Kusini. Aidha, majaribio ya matumizi ya dawa ya *acetone* na mkojo wa ng'ombe kama chambo katika aina 7 za mitego yalifanyika katika maeneo ya ukanda wa Pwani na Kaskazini mwa Tanzania. Matokeo ya majaribio hayo yameonyesha kuwa matumizi ya chambo kwa mbung'o yaliongeza uwezo wa mitego katika kunasa mbung'o kwa asilimia 4 hadi 11.

Mheshimiwa Spika katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu itaimarisha Taasisi ya Mbung'o na Nagana kwa kukarabati majengo na kununua vitendea kazi. Aidha, Wizara itakamilisha ramani inayoonyesha mtawanyiko wa mbung'o nchini na itahamasisha wafugaji kutumia mitego inayohamishika ili kuweza kunasa mbung'o kwa wingi.

Mheshimiwa Spika, Huduma za Ugani Wizara imeendelea kuimarisha huduma za ushauri kwa wafugaji ili kuwawezesha kuongeza uzalishaji wa mifugo na mazao yake. Katika mwaka 2005/2006, Wizara iliandaa na kusambaza nakala 2,000 za vijitabu na 16,000 za vipeperushi vya ufugaji bora wa ng'ombe wa nyama na maziwa, mbuzi, kuku na nguruwe pamoja na vipeperushi kuhusu usalama na ubora wa vyakula vitokanavyo na mifugo. Aidha, Wizara iliandaa na kurusha hewani vipindi 52 vya redio na 12 vya televisheni. Vilevile, Wizara ilihamasisha na kuwezesha kuanzishwa kwa Chama cha Kitaifa cha Wafanyabiashara ya Mifugo na Nyama (*Tanzania Livestock and Meat Traders Association (TALMETA*) ambacho kitashughulikia maslahi ya wadau wake.

Mheshimiwa Spika, jumla ya wafugaji 1,637 walipata mafunzo ya muda mfupi katika fani za ufugaji bora wa ng'ombe na mbuzi wa maziwa, usindikaji maziwa, ufugaji wa nyuki na uvunaji wa maji ya mvua (Kiambatanisho Na 14). Mafunzo hayo yalifadhiliwa na serikali kwa kushirikiana na Asasi zisizokuwa za kiserikali za *Heifer Project Tanzania (HPT),* Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Tanga Dairy Trust (*TADAT*), *Small Holder Dairy Support Program (SDSP), Land O' Lakes, Caritas Tanzania, World Vision* na *Farm Africa*. Aidha, wafugaji 70 kutoka mikoa ya Kagera, Mara, Mwanza na Shinyanga walifundishwa juu ya uendeshaji wa ranchi kibiashara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu itatayarisha na kusambaza mwongozo wa utoaji wa huduma za ugani na kuratibu utoaji wa huduma hizo katika Halmashauri na sekta binafsi. Aidha, kwa kushirikiana na Halmashauri na wadau wengine itawaelimisha wafugaji 20,000 juu ya umuhimu wa ufugaji bora ikiwa ni pamoja na matumizi na hifadhi bora ya mabaki yatokanayo na mazao ya kilimo ili kuongeza chakula cha mifugo wakati wa kiangazi. Mafunzo hayo yatatolewa katika vituo vya Babati, Buhemba (Musoma Vijijini), Kahama, Kikulula (Karagwe), Kihinga (Kigoma),

Kibaha, Mabuki (Misungwi), Mpwapwa, Mogabiri (Tarime), Monduli, Nachingwea, Newala, Njombe, Nzega, Nkundi (Sumbawanga), Shinyanga, Simanjiro na Singida. Vilevile, Wizara itashirikiana na Halmashauri kuanzisha mashamba darasa 10 katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Morogoro, Mwanza na Shinyanga na kuimarisha 10 katika wilaya za Bukoba Vijijini (2), Karagwe (2), Tanga Vijijini (1), Pangani (3) na Handeni (2). Pia, Wizara itaandaa na kusambaza vipeperushi 24,000 vya ufugaji bora, kuandaa na kurusha hewani vipindi 64 vya redio na televisheni kuhusu ufugaji bora. Aidha, Wizara yangu itashirikiana na *TALMETA* na Halmashauri kukamilisha uundaji wa vikundi vya wafanyabiashara ya mifugo katika mikoa ya Manyara, Singida na Tabora.

Mheshimiwa Spika, Masuala ya Jumla, Mafunzo ya Watumishi na Wataalam wa Mifugo, Wizara yangu iliendelea na jukumu la kuandaa na kuratibu mafunzo kwa wataalam wa Sekta ya Mifugo, kukuza na kuendeleza mitaala. Katika mwaka 2005/2006, jumla ya wanafunzi 748 waliendelea na mafunzo ya stashahada na astashahada katika vyuo vya mafunzo ya mifugo vya Morogoro, Mpwapwa, Madaba, Temeke na Tengeru (Kiambatanisho Na. 15). Kati ya hao, 225 walifadhiliwa na Serikali na 523 walijigharamia. Aidha, jumla ya wataalamu 363 walihitimu mafunzo katika vyuo hivyo. Pia, mafunzo ya uzamili yalitolewa kwa watumishi 6 na mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa watumishi 66. Vilevile, Wizara ilikarabati miundombinu ya Vyuo vyote 6 vya Mafunzo ya Mifugo na kuvipatia vitendea kazi pamoja na kutoa mafunzo kuhusu uandaaji wa mihutasari ya kozi za astashahada na stashahada katika mfumo wa moduli kwa ajili ya kutambuliwa rasmi na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (*NACTE*).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu itaongeza idadi ya wanafunzi katika Vyuo vya Mafunzo kutoka 748 waliopo kwa sasa hadi 800 kwa lengo la kutumia kikamilifu uwezo wa vyuo hivyo. Aidha, Wizara itagharamia mafunzo kwa wataalam 250 katika ngazi ya astashahada (80) na stashahada (170). Vilevile, Wizara itaendelea kuandaa na kusimamia utekelezaji wa mitaala na mitihani katika vyuo vya mafunzo ya mifugo. Pia, kozi ya ufugaji kibiashara itaanzishwa ili kuboresha mbinu za ufugaji wa kibiashara. Aidha, Wizara yangu itakarabati majengo, miundombinu na kununua vifaa kwa ajili ya vyuo 6 vya mafunzo ya mifugo na itaendelea kugharamia mafunzo ya uzamili kwa watumishi wake 6.

Mheshimiwa Spika, Utawala na Maendeleo ya Watumishi,Wizara yangu imeendelea kutoa huduma kwa wateja kwa kuzingatia Mkataba wa Huduma kwa Mteja (Client Service Charter) uliozinduliwa mwaka 2002. Wizara ina jumla ya watumishi 1,207 wa kada mbalimbali ambapo watumishi 254 ni wanawake na 953 ni wanaume.

Katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu iliajiri jumla ya watumishi 22 katika fani mbalimbali, iliwapandisha vyeo watumishi 217 na kuwathibitisha kazini watumishi 26. Katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu itaajiri watumishi 113 ili kuimarisha utendaji na kutoa motisha kwa watumishi ikiwa ni pamoja na kuwapatia vitendea kazi na mafunzo.

Mheshimiwa Spika, Vita dhidi ya Rushwa,katika mwaka 2005/2006 Wizara yangu iliendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kupambana na Rushwa katika maeneo

ya ununuzi, ajira na utoaji huduma. Katika juhudi hizo Wizara ilizingatia Sheria ya Ununuzi ya mwaka 2004, kwa kuunda Bodi ya Zabuni ya Wizara na Kamati ya Ununuzi.

Aidha, Kamati Maalum ya Ajira iliundwa kwa mujibu wa Waraka wa Utumishi wa Umma Na. 1 wa 2004. Vilevile, nafasi za kazi zilitangazwa na kujazwa kwa ushindani ulio wazi kwa kuzingatia Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002. Katika mwaka 2006/2007 Wizara yangu itaendelea kutoa elimu kwa watumishi wake na wadau wa Sekta ya Mifugo kuhusu taratibu, kanuni, na maadili ya utendaji katika utumishi wa umma. Aidha, Wizara yangu itaendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kupambana na Rushwa.

Mheshimiwa Spika, Masuala ya Jinsia, katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu ilianzisha na kuimarisha dawati la jinsia pamoja na kuainisha masuala ya jinsia katika sera, mipango, programu na katika utendaji wa kila siku. Aidha, Wizara ilizingatia usawa kijinsia katika ajira, upandishaji vyeo, mafunzo kama ilivyoelekezwa kwenye taratibu za ajira Serikalini. Pia, watumishi 2 wa Wizara walihudhuria mafunzo kuhusu jinsia. Katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu itaendelea kuimarisha mahusiano ya jinsia katika vitengo vyake. Aidha, Wizara itaendesha mafunzo yahusuyo masuala ya jinsia na kuandaa viashiria muhimu vya kuweza kufuatilia na kupima mafanikio ya jinsia ndani ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, Mapambano Dhidi ya UKIMWI katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu iliendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa Kudhibiti UKIMWI sehemu ya kazi kwa kusambaza kondomu, vipeperushi na kuendesha semina juu ya mbinu za kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huo. Katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI (*TACAIDS*), itafanya tathmini ya athari za UKIMWI kijamii na kiuchumi katika Wizara na Taasisi zake na kuchukua hatua za kuzuia athari hizo. Pia, katika kipindi hicho, Wizara itaendesha mafunzo kwa watumishi wa ngazi zote kwa lengo la kupambana na kupunguza athari zitokanazo na ugonjwa huu hatari wa UKIMWI. Vilevile, Wizara itapitia na kuboresha mkakati wake wa kupambana na kuenea kwa UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, Habari, Mawasiliano na Elimu,katika mwaka 2005/2006, Wizara yangu ilianzisha kitengo cha habari, mawasiliano na elimu kwa madhumuni ya kuboresha mawasiliano na wadau. Aidha, Wizara yangu imeanzisha tovuti yake *(http://www.mifugo.go.tz)* kwa lengo la kuimarisha mawasiliano. Katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wa sekta itakamilisha maandalizi ya Mkakati wa Mawasiliano wa Wizara. Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha kitengo cha habari, mawasiliano na elimu kwa kutoa mafunzo kwa watumishi na kukipatia vifaa na vitendea kazi muhimu ili kiweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi

Mheshimiwa Spika, shukurani, kabla ya kumaliza hotuba yangu, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyingine katika kuiwezesha Wizara yangu kufanikisha majukumu yake. Mafanikio yaliyopatikana katika mwaka uliopita yametokana na ushirikiano na misaada mikubwa ya kifedha na kiufundi toka kwa nchi wahisani, mashirika mbalimbali, taasisi za hiari zisizokuwa za

Kiserikali, Mashirika ya Kidini na taasisi za fedha, bila kusahau hamasa na ushiriki wa wananchi wakiongozwa na wawakilishi wao Waheshimiwa Wabunge na Madiwani.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzishukuru Serikali za nchi mbalimbli zikiwemo, Australia, Austria, Denmark, Japan, Jamhuri ya Afrika ya Kusini, Jamhuri ya Watu wa China, Ireland, Marekani (*USAID)*, Misri, Sweden, Ubelgiji, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani na Uswisi. Aidha, napenda kutoa shukurani kwa taasisi za fedha za kimataifa, ikiwa ni pamoja na Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)* pamoja na Jumuiya ya Nchi za Ulaya *(EU),* Mashirika ya Umoja wa Mataifa ya *UNDP*, Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki *(IAEA),* Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa *(FAO)* pamoja na Mfuko wa Kimataifa wa Kuendeleza Kilimo *(IFAD),* Mfuko wa Maendeleo wa Mazao ya Kilimo na Mifugo *(CFC),* Shirika la Afya ya Wanyama Duniani *(OIE)* na Taasisi ya Raslimali za Wanyama ya Umoja wa Afrika (*AU/IBAR)* kwa misaada na michango yao katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu na malengo ya Wizara yangu. Aidha, nachukua nafasi hii kuyashukuru Mashirika ya kidini ikiwa ni pamoja na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania *(KKKT)* na Kanisa Katoliki Tanzania *(TEC),* pamoja na Taasisi nyingine za hiari za *Vet Aid, OXFAM* na *Wellcome Trust* za Uingereza, *Austro-Project, Heifer Project Tanzania (HPT)*, *World Vision, FARM Africa, Land O' Lakes* na *ASARECA* na wote wale ambao kwa njia moja au nyingine wanaendelea kuisaidia Wizara yangu. Naomba kupitia kwako

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwashukuru wote hawa kwa dhati kabisa na kuwaomba waendelee kushirikiana nasi katika kuendeleza Sekta ya Mifugo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa shukurani zangu za pekee kwa wananchi wote hususan wafugaji na wadau wengine kwa michango yao ya mawazo katika kuendeleza Sekta ya Mifugo nchini. Naomba waendelee na moyo huu ili kuimarisha huduma zitolewazo na Wizara yangu. Wizara yangu itaendelea kushirikiana nao kwa lengo la kuboresha hali ya maisha yao na uchumi wa Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mhe. Dr. Charles Ogesa Mlingwa, Mbunge Shinyanga Mjini, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo kwa msaada wake wa karibu katika kusimamia kazi za wizara yangu. Aidha, napenda pia nitoe shukurani zangu kwa Katibu Mkuu wa Wizara yangu, Dr. Charles Nyamrunda na Naibu Katibu Mkuu Dr. Jonas Melewas, Wakuu wa Idara na watumishi wote kwa kutekeleza majukumu tuliyopewa na Taifa na kufanikisha maandalizi mazuri ya Bajeti ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, maombi ya fedha kwa mwaka 2006/2007, baada ya maelekezo hayo, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 22,551,409,000 ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu na malengo yake kwa mwaka 2006/2007. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida ni shilingi 12,636,749,000 ambapo shilingi 4,300,869,000 ni Mishahara (PE) na shilingi 8,335,880,000 ni Matumizi mengine (OC). Bajeti ya maendeleo shilingi 9,914,66,000 ambapo kati ya hizo shilingi 1,699,998,000 ni fedha za ndani na shilingi 8,214,662,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe shukurani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamuita Mwenyekiti wa Kamati, ili kutoa taarifa yake nilikuwa napenda kusema kutokana na tangazo langu kuhusu ile sikukuu ya kuzaliwa, mkewe Dr. David Mathayo David Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara amemkumbushe kwamba Dr. David leo ni sikukuu yake ya kuzaliwa. Lakini haiishii hapo, nimepata ujumbe sasa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Uraia Mheshimiwa Bakari Mwapachu kwamba kesho ni sikukuu yake ya kuzaliwa. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. JOYCE N. MACHIMU (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO NA ARDHI)** Mheshimiwa Spika, kabla sijawasilisha Taarifa ya Kamati ya Kilimo na Ardhi naomba masahihisho ukurasa wa pili aya ya mwisho ongeza maneno yafuatayo: Bunge ya Kilimo na Ardhi ambao ndiyo waliochambua na. Sahihisho la pili, ukurasa namba 17 kile kifungu namba 5.2 fedha zinazoombwa na Wizara kifungu namba 99 ni shilingi bilioni 22,551,409,000/=

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi naomba nitoe taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo na Ardhi juu ya utekelezaji ya malengo ya bajeti ya Wizara ya Maendeleo na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2005/2006 pamoja na maoni ya kamati juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, utangulizi awali ya yote, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kilimo na Ardhi, juu ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo kwa mwaka uliopita pamoja na maoni ya kamati juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, naomba kabla sijaanza kutekeleza Kanuni namba 81 (1) ya Kanuni za Bunge toleo la mwaka 2004 nitumie nafasi hii kuwapongeza wafuatao; kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti, wa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Amani Abeid Karume kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili napenda nikupongeze wewe kwa kuchaguliwa kuliongoza Bunge hili tukufu kwa kipindi cha miaka mitano. Aidha nampongeza Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, kwa kuchaguliwa kukusaidia kuliongoza Bunge letu tukufu. Tunawatakia kila la heri katika kutuongoza kwa viwango na kasi mpya.

Tatu, napenda kumpongeza Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais na kuthibitishwa na Bunge, kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri, wote kwa kuteuliwa kushika nyadhifa walizonazo. Wote wameanza kazi zao vizuri nawatakia mafanikio tuko pamoja.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe pongezi za pekee kwa wapiga kura wa Mkoa wa Shinyanga hasa wanawake na wanachama wa Chama cha Mapinduzi wa Kata ya Rugurwa ambao walinijengea mazingira mazuri hadi kunifikisha hapa nilipo leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho napongeza Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kuchaguliwa na wananchi au kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuingia katika Bunge hili tukufu wote nawatakia uwakilishi mwema.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi na shukurani hizo napenda kuwatambua wajumbe wa Kamati ya Kudumu na Ardhi ambao ndiyo walichambua na kutoa maoni, ushauri na mapendekezo kuhusu bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo nao ni hawa wafuatao; Mheshimiwa Gideon A. Cheyo Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Kidawa Salehe Makamu wa Mwenyekiti, Mheshimiwa Maida Abdallah Mjumbe, Mheshimiwa Kheri Ameir, Mheshimiwa Idd Azzan, Mheshimiwa Mwadini Jecha, Mheshimiwa Salum Khamis, Mheshimiwa Castor Ligalama, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe, Mheshimiwa Joyce Machimu, ndiyo mimi mwenyewe ninayewakilisha, Mheshimiwa Manju Msambya, Mheshimiwa Cynthia Ngoye, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Juma Omar, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Fred Mpendazoe na Samson Mpanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utekelezaji na ushauri wa Kamati kwa mwaka 2005/2006. Katika mwaka uliopita kamati yangu ilitoa ushauri na maagizo katika maeneo kadhaa nafurahi kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa Wizara kwa kiasi kikubwa imeyafanyia kazi maeneo husika na hatua za utekelezaji zinaridhisha. Hata hivyo, katika maeneo ambayo yameonekana kuhitaji juhudi na kuboreshwa zaidi kamati imeshauri ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, mafanikio na changamoto katika utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2005/2006. Mafanikio, Kamati yangu ilifahamishwa mafanikio mbalimbali yaliyopatikana katika utekelezaji wa malengo na majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo, kwa mwaka wa fedha uliopita. Baadhi ya mafanikio hayo ni pamoja na kuandaa Sera ya Taifa ya Mifugo, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imekamilisha rasimu ya mwisho ya sera ya mifugo. Utayarishaji wa uanzishaji wa mfuko wa programu ya sekta ya kilimo *ASDP Basket Fund* umekamilika kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa utekelezaji wake unasubiliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Wilaya *DADPs* umefanyika kwa pamoja kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za

Mikoa TAMISEMI na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Waraka wa kubinafsisha machinjio ya Dodoma umeandaliwa na kuwasilishwa kwa Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri kwa hatua zaidi. Takwimu mbalimbali za mifugo kutoka ngazi za chini zimeendelea kukusanywa, kuhifadhiwa na kusambazwa kwa wadau mbalimbali katika sekta mbalimbali, kwa matumizi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Muswada wa Sheria ya Nyama umekamilika na umesomwa kwa mara ya kwanza Bungeni mwezi Aprili, 2006 maandalizi yanafanyika ili uweze kusomwa Bungeni kwa mara ya pili. Matayarisho ya Kanuni chini ya *Animal Disease Act* namba 17 ya mwaka 2003 yamekamilika. Kanuni mbalimbali zimetayarishwa na tayari zinatumika chini ya *veterinary act* namba 16 ya mwaka 2003. Miongozo chini ya *veterinary* namba 17 ya mwaka 2003 imekamilika na kuanza kutumika. Nakala 3,000 za Kanuni ya *veterinary* namba 17 ya mwaka 2003 zilichapishwa na kusambazwa kwa wadau. Aidha wadau katika Halmashauri na Watalaam katika vyuo vya mifugo waliemishwa na kuhamasishwa kuhusu usimamizi na utekelezaji wa kanuni hizo.

Mheshimiwa Spika, changamoto, pamoja na mafanikio hayo kamati pia ilibaini changamoto kadhaa zinazoikabili Wizara ambazo baadhi ni kama ifuatavyo; mabadiliko ya majukumu ya Wizara kulingana na mpango wa marekebisho ya sekta ya umma *PSRP* yamepeleka majukumu ya utekelezaji kwenye Halmashauri ambazo kwa sasa hazijawa na uwezo wa kutosha kiutendaji hususan upungufu wa watalaam.

Katika bajeti ya Wizara kwa mwaka 2005/2006 kiasi cha fedha za nje kilichoidhinishwa na Bunge hakikutolewa chote kutokana na baadhi ya wahisani kushindwa kutoa fedha zote kama walivyoahidi. Uwezo mdogo wa Serikali kukabiliana na magonjwa mbalimbali hususan ya mlipuko kunaathiri kwa kiasi kikubw uendelevu wa sekta ya mifugo nchini.

Mheshimiwa Spika, tija ndogo katika uzalishaji wa mifugo hasa kwa wafugaji wa sekta asili *(traditional sector)* umefanya sekta hii ishindwe kuchangia kikamilifu katika pato la taifa. Hali hii imesababishwa na mazoea ya baadhi ya wafugaji kufuga mifugo mingi kama ishara ya ufahari na utajiri. Aidha mifugo mingi ya asili ina ukosefu mdogo na hivyo kuwa na viwango vidogo vya uzalishaji. Sekta ya mifugo nchini bado inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa viwanda vya kusindika mazao yatokanayo na mifugo, masoko ya uhakika na kukosekana kwa miundombinu ya kuweza kuuza bidhaa za mifugo katika soko la kimataifa.

Gharama za pembejeo mfano madawa ya mifugo zimepanda mno na kuwafanya wafugaji kushindwa kununua na hivyo kupunguza uzalishaji tija na hatimaye mapato. Ukame umesababisha vifo vingi vya mifugo kutokana na kukauka kwa mito na mabwawa ya maji na kukosekana kwa malisho. Wafugaji wengi hawana uwezo wa kupata mikopo kutoka vyombo vya fedha kutokana na masharti magumu yaliyowekwa na vyombo husika. Kutotenga maeneo maalum ya ufugaji kumesababisha wafugaji kuhama hama na hivyo kuleta uharibifu wa mazingira, kusambaza magonjwa ya mifugo na kusababisha migogoro na wakulima.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa kamati, kutenganisha Maafisa Kilimo na Mifugo katika Halmashauri za Wilaya. Moja ya vikwazo vilivyosababisha kutokuwepo ufanisi na na uwajibikaji katika ngazi ya Halmashauri ni kutotenganishwa kwa majukumu ya bwana shamba na bwana mifugo. Bwana shamba anafanyakazi za bwana mifugo na kinyume chake. Ili kuleta ufanisi uwajibikaji na motisha kwa maafisa hao kamati inashauri wataalam warudi kwenye fani zao kwa mujibu wa masharti ya ajira zao. Sambamba na hilo Serikali ifanye juhudi za makusudi ili kuwa na watalaam wa kutosha wa sekta ya mifugo kwenye Halmashauri za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Uwezekezaji katika malisho ya mifugo. Katika hotuba ya ufunguzi wa Bunge lako tukufu mnamo tarehe 30 Desemba 2005 Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alibaini kuwa mfumo wa sasa wa ufugaji wa kuhamahama kutafuta marisho hauna tija na unasababisha mchungaji kukonda hali kadhalika mifugo yake nayo kukonda. Kauli hiyo ya Mheshimiwa Rais, inadhihirisha kuwa bado hatujawekeza ipasavyo ili kujihakikisha malisho bora ya mifugo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kamati ilipata fursa ya kutembelea shamba la mbegu za malisho ya mifugo huko Vikuge Mkoani Pwani mwezi Machi, 2006. Ziara hiyo ilidhihirisha kuwa bado tuna safari ndefu ya kujihakikishia malisho bora ya mifugo hasa ukizingatia uwingi wa mifugo katika nchi yetu na ukubwa wake kijiografia iwapo hatua za haraka hazitachukuliwa.

Mheshimiwa Spika, ili kufikia azma hiyo kamati inashauri Wizara kuhamasisha watu binafsi na makampuni kuwekeza katika malisho ya mifugo kwani soko ni la uhakika. Aidha msisitizo uwekwe katika uanzishaji wa mashamba ya malisho ya mifugo katika sehemu mbalimbali za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji katika sekta ya usindikaji wa mazao ya mifugo. Juhudi za kuleta maendeleo katika sekta ya mifugo lazima ziende sambamba na upatikanaji wa masoko ya mazao ya mifugo kama vile nyama, maziwa, ngozi na kadhalika. Hata hivyo upatikanaji wa masoko ya mazao ya mifugo hapa nchini si wa uhakika. Hali hii inasababishwa kwa kiasi kikubwa na uwekezaji mdogo katika sekta ya usindikaji wa mazao ya mifugo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kuwa sekta binafsi ndiyo muhimu wa maendeleo ya kiuchumi kamati inaishauri Wizara iwahamasishe wadau mbalimbali wenye uwezo wawekeze katika aina hii ya viwanda. Aidha Serikali isijitoe kabisa bali iangalie ni jinsi gani itawasaidia wawekezaji hawa kwa kuweka miundombinu inayohitajika na mazingira ya kuwavutia kuwekeza katika sekta hii.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine iangalie uwezekano wa kuanzisha miradi ya ujenzi wa viwanda vya kusindika mazao ya mifugo kama vile nyama, maziwa na ngozi. Aidha juhudi za makusudi zichukuliwe ili kufufua viwanda vya nyama vilivyokufa vya Mbeya na Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, magonjwa ya mifugo. Wizara imefanya jitihada kubwa kukabiliana na magonjwa ya mifugo yanayosababishwa na kupe, ndorobo na minyoo. Aidha ugonjwa wa kichaa cha mbwa ambao siku za nyuma ulikuwa tishio umepungua. Pamoja na juhudi hizo bado baadhi ya Halmashauri haziwajibiki ipasavyo katika suala hili. Hivyo kamati inaishauri Serikali kuimarisha usimamizi wa utekelezaji kwa kuihusisha TAMISEMI na hivyo kuleta ufanisi. Aidha, Wizara iendelee na juhudi za kusambaza madawa hususan katika maeneo yanayopakana na mbuga za wanyama.

Mheshimiwa Spika, kadhalika hali ya majosho nchini bado si nzuri kamati inaishauri Wizara iwe na utaratibu maalum wa kushughulikia majosho katika Halmashauri zote ili kuboresha ufugaji. Aidha jitihada za ukarabati wa majosho yaliyopo ziende sambamba na ujenzi wa majosho mapya.

Mheshimiwa Spika, kutenga maeneo maalum ya wafugaji. Migogoro baina ya wafugaji na wakulima katika maeneo mengi ya nchi yetu, inasababishwa na kutokuwepo na utaratibu wa kutenga maeneo kwa ajili ya wafugaji. Ili kuepusha migogoro hiyo na kuleta tija katika ufugaji, kamati inaishauri Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, kutenga na kuaininisha maeneo ya wafugaji kwa mujibu wa sheria ya ardhi ya vijiji namba 5 ya mwaka 1999.

Wafugaji wa asili ni kundi muhimu hivyo ni lazima tuanze kutenga na kuanisha maeneo na kuwamilikisha wafugaji wa asili kwa mujibu wa sheria ya ardhi ya namba 5 mwaka 1999. Katika maeneo hayo kuwe na huduma muhimu kama mabwawa na majosho. Aidha utaratibu huo uzingatie kuwa wafugaji wanahitaji maeneo yenye ardhi nzuri yatakayosaidia kuongeza tija.

Gharama kubwa za pembejeo za uzalishaji ya mazao yatokanayo na mifugo. Gharama za pembejeo za uzalishaji yatokanayo na mifugo yakiwemo madawa zimepanda mno na kuwafanya wafugaji kushindwa kununua na hivyo kupunguza uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, tija na mapato, ili kupunguza gharama za pembejeo hizo kamati inaishauri Serikali iangalie uwezekano wa kutoa ruzuku katika sekta ya mifugo kama inavyofanya katika sekta ya kilimo.

Utafiti katika sekta ya mifugo. Utafiti ni nyenzo muhimu katika kuhakikisha kuwa sekta ya mifugo, inachangia ipasavyo katika maendeleo ya uchumi wa nchi. Kamati yangu ilitembelea taasisi ya utafiti wa ndoroto Mkoani Tanga mwezi Mei 2006. Ziara hiyo ilibaini kuwa bado hatujalipa uzito unaostahili suala la kuimarisha vyuo na taasisi za utafiti ili zitekeleze majukumu yao ipasavyo. Hivyo kamati inaishauri Serikali kuzitengea taasisi za utafiti fedha za kutosha na kuzipatia nyenzo za kisasa ili zilete ufanisi katika shughuli zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha kamati inaishauri Serikali kuboresha mazingira ya kazi katika taasisi hizo ili kulinda afya za wafanyakazi. Sambamba na hilo juhudi zifanywe kusambaza matokeo ya tafiti kwa wadau mbalimbali ili waweze kunufaika na tafiti hizo.

Mheshimiwa Spika, athari za ukame kwa mifugo. Ukame ulioikumba sehemu kubwa ya nchi yetu katika msimu uliopita umesababisha vifo vya mifugo kutokana na kukauka kwa mabwawa ya maji na kukosekana kwa malisho. Ili kupunguza athari zinazosababishwa na ukame kwa mifugo kamati inaishauri Serikali iongeze kasi ya uchimbaji wa mabwawa na malambo katika maeneo kame na kuhamasisha uanzishaji wa malisho ya mifugo nchini kote.

Mheshimiwa Spika, wafugaji wengi kukosa uwezo wa kukosa mikopo. Masharti ya mikopo yanayowekwa na taasisi za fedha katika mabenki ni kikwazo kwa wafugaji walio wengi kupata mikopo, hii ni kutokana na ukweli kwamba wafugaji wengi hawana dhamana zinazohitajika katika hati za kumiliki ardhi. Hivyo ili kuwawezesha wafugaji kupata mikopo, kamati inaishauri Serikali kutenga maeneo na kuwamilikisha wafugaji ili waweze kuwa na hati miliki na hiyo kuwa na dhamana ya kupata mikopo toka taasisi za fedha.

Mheshimiwa Spika, kiwango kidogo cha unywaji wa maziwa na ulaji wa nyama miongoni mwa Watanzania bado ni kidogo sana. Unywaji wa maziwa hapa nchini unakadiriwa kuwa lita 39 kwa mtu kwa mwaka na ulaji wa nyama kilo 10.3 kwa mtu kwa mwaka. Kwa mujibu wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa *FAO*, kiwango kinachopendekezwa ni lita 200 za maziwa na kilo 50 mpaka 60 za nyama kwa mtu kwa mwaka.

Kiwango hiki kidogo cha utumiaji wa mazao ya mifugo nchini hakisababishwi na ukosefu wa nyama au maziwa bali kwa kiasi kikubwa ni kutokana Watanzania wengi kutokuwa na utamaduni wa kunywa maziwa na kula nyama kwa wingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuinua kiwango cha umiaji wa nyama na maziwa miongoni mwa Watanzania kamati inaishauri Wizara na wadau mbalimbali wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, kuelimisha umuhimu wa kula nyama kunywa maziwa kwa ajili ya afya zao na kuhamasisha wananchi kuongeza kiwango cha matumizi ya mazao hayo yatokana na mifugo.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa machinjio ya kisasa. Kamati inapongeza Wizara kwa hatua ilizochukua za ujenzi wa machinjio ya kisasa katika Mji wa Dodoma. Hatua hiyo, siyo tu si tu inapunguza gharama za usafirishaji wa mifugo kutoka Mkoa hadi na pia kwenda Dar es Salaam bali inaongeza thamani na ubora wa nyama.

Mheshimiwa Spika, ili juhudi hizo zilete mafanikio zaidi kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya kuhamasisha ujenzi wa machinjio kama hayo katika Mikoa yenye mifugo mingi. Aidha Serikali isimamie ipasavyo ubora wa mabucha ya nyama nchini kote ili kulinda afya za walaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maombi ya fedha kwa mwaka 2006/2007. Wizara kutengewa kiasi kidogo cha fedha za maendeleo. Kwa mwaka 2006/2007 Wizara ya Maendeleo ya

Mifugo, imetengewa kiasi cha shilingi bilioni 9,914,660,000 fedha za maendeleo ambazo fedha za ndani ni shilingi bilioni 1,669,998,000 tu.

Kiasi hiki cha fedha ni kidogo sana ukilinganisha na majukumu ya Wizara hii ya kuifanya sekta ya mifugo kuwa ya kisasa na yenye tija. Hivyo kamati inaishauri Serikali kuitengea sekta hii fedha za kutosha za maendeleo ya ndani katika mwaka ujao wa fedha ili iweze kutekeleza majukumu yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilikutana Jijini Dar es Salaam tarehe 29 Mei, 2006 na kupitia na kuchambua Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo. Kiasi cha fedha kinachoombwa katika Fungu 99 ni shilingi 22,551,409,000. Kati ya fedha hizo shilingi 12,636,749,000 ni kwa ajili ya matumizi ya Kawaida na shilingi 9,914,660,000 ni fedha za Maendeleo, ambapo fedha za ndani ni shilingi 1,699,998,000 na fedha za nje ni shilingi 8,214,662,000.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, napenda kutumia nafasi hii, kuwapongeza Waziri wa Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Dr. Shukuru J. Kawambwa, Naibu Waziri wake na Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, kwa kazi nzuri na ushirikiano mkubwa wanaoipa Kamati. *(Makofi)*

Nawapongeza pia Katibu Mkuu wa Wizara, Bwana Charles Nyamurunda, Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Jonas Melewas, pamoja na Wataalam wote wa Wizara hii, kwa jinsi walivyoweza kufafanua hoja mbalimbali zilizotolewa na Wajumbe wa Kamati wakati wa kuchambua Bajeti hii. Aidha, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati hii kwa michango yao, ushirikiano na ustahimilivu katika kufanikisha kazi hii.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, napenda nikushukuru wewe binafsi, pamoja na Ofisi yako, hasa Katibu wa Bunge, Ndugu Damian S.L. Foka na Wasaidizi wake, Makatibu wa Kamati Ndugu Frank Mbumi, Ndugu Daniel Eliufoo, wakisaidiwa na Bi. Mariam Mwakasege, kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi Taarifa hii kukamilika.

Nakushukuru Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

Baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kamati napenda kutamka kuwa naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE MWADINI ABBAS JECHA – MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, maoni ya Kambi ya Upinzani, kuhusu Wizara ya Maendeleo ya Mifugo katika mwaka wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwenye kupasa kushukuriwa, ambaye ni Rahimu, mwenye nguvu, mwenye

ukarimu na mwingi wa hekima, ambaye ni vyake vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini. Yeye ndiye aliye juu, mkuu na mwenye uwezo wa kuweka Serikali za wanadamu na Mabunge ya Mataifa, kwa kutupa uhai na afya njema siku ya leo tukaweza kukutana ndani ya jengo hili jipya, zuri na lenye haiba ya aina yake, kutekeleza wajibu wetu tuliokabidhiwa na wananchi kwa manufaa yao na kwa manufa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kadhalika nakupongeza wewe binafsi, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuliongoza Bunge hili Tukufu, tunakuahidi ushirikiano wetu makubwa. Aidha, nakushukuru kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu, kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani, kuhusu Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo kwa mwaka wa fedha 2006/2007, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 43(5)(b) na (c), Toleo la 2004.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua nafasi hii adhimu, kuwapongeza Naibu Spika, Mheshimiwa Anne S. Makinda na Wenyeviti, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama na Mheshimiwa Job Y. Ndugai, kwa kuchaguliwa kwao, kusaidiana nawe kuliongoza Bunge hili Tukufu. Tunaahidi nao kuwapa ushirikiano wetu wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchache wa fadhila, kama sikuchukua nafasi hii kuwapongeza wananchi wa Jimbo langu la Wete, kwa kunichagua kwa kura nyingi sana katika Uchaguzi Mkuu uliopita na kuniwezesha kuwa Mbunge wao. Nasema nawapa ahsante kubwa kwa uamuzi wao huo, kwani wamenipa heshima kubwa, nikijua kuwa hii ni dhamana nzito. Nawaahidi kuwatumikia vyema na kwa juhudi zangu zote, kwa manufaa yao na kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, tumejaaliwa rasilimali kubwa ya mifugo. Kwa mujibu wa takwimu za hivi karibuni, nchi yetu ina jumla ya mifugo milioni 66.3, kati ya hiyo ng'ombe milioni 18.5, mbuzi milioni 13.1, kondoo milioni 3.5, kuku wa kienyeji milioni 30 na nguruwe milioni 1.2. Aidha, mchango wa Sekta ya Mifugo katika Kilimo kwa ujumla wake inachangia asilimia 30 ama katika Pato la Taifa, sekta hii inachangia asilimia 6.1 na kwa kulingana na mchango huo, asilimia 40 inatokana na uzalishaji wa nyama, asilimia 30 maziwa na asilimia 30 kuku. Kiwango hicho katika kuchangia Pato la Taifa ni kidogo sana, hasa tukijilinganisha na ndugu zetu wa Kenya, ambao wana wastani wa jumla ya mifugo milioni 58.4 lakini mchango wa sekta ya Mifugo katika Pato lao la Taifa ni asilimia 12.

Mheshimiwa Spika karibu asilimia 99 ya mifugo hapa nchini inamilikiwa na kutunzwa kienyeji na asilimia moja iliyosalia ni mifugo inayofugwa katika mashamba makubwa kwa ajili ya uzalishaji wa nyama na maziwa. Pamoja na rasilimali kubwa ya mifugo tuliyonayo, takriban zaidi ya asilimia 63 ya wafugaji wetu ni maskini. Hii ni changamoto kubwa, inatupasa tukae na kutafakari nini la kufanya kuondokana na hali hii.

Mheshimiwa Spika, miaka iliyopita nilisema na leo nasema na Kamati imesema kwamba, utumiaji wa mazao ya mifugo kwa chakula hapa nchini ni mdogo mno. Kwa wastani Mtanzania anakula kilogramu 12 za nyama, anakunywa maziwa lita 39 na anakula mayai 54 kwa mwaka. Tukiangalia ndugu zetu wa Kenya, mtu mmoja kwa

wastani anakula nyama kilogramu 20 na anakunywa maziwa lita 70. Viwango hivi bado havijafikia vile vilivyowekwa Kimataifa, ambavyo Kamati imevizungumzia hapa. Ni dhahiri utaona ni jinsi gani sisi Watanzania tulivyo nyuma katika matumizi ya rasilimali zetu za mifugo, lakini pia tunavyoshusha uwezo wa soko la bidhaa hizo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanzisha Wiki Maalum ya Kuhimiza Unywaji wa Maziwa. Lakini kwa kuwa si matumizi ya maziwa pekee ambayo yanahitaji kutiliwa mkazo, bali hata ulaji wa nyama na mayai unahitaji mkazo huo huo, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ilieleze Bunge hili ni lini basi itajumuisha uhimizaji wa kula nyama na mayai, sambamba na unywaji wa maziwa.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na malalamiko mengi kuhusu uharibifu wa mazingira na hasa sehemu zenye vyanzo vya maji, lawama ambazo pia zinagusa wafugaji. Suala la uharibifu wa mazingira katika mantiki yake, linamgusa kila mtu kwa sababu kama hukufanya hili, basi utafanya lile, ili mradi shughuli za kila siku za mwanadamu zinapelekea kwa namna moja au nyingine kuharibu au kuchangia kuharibu mazingira. Sisi kama binadamu ni lazima tukumbuke kwamba, mifugo nayo inahitaji malisho, maji, pamoja na mambo mengine, ili iweze kuishi na kuweza kuzalisha mazao.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imejaliwa rasilimali nyingi za kuweza kustawisha mifugo ikiwemo ardhi, maji na nyanda za malisho. Tanzania ina jumla ya ekta 88.6 milioni, kati hizo milioni 60 ni nyanda za malisho. Lakini kutokana na tatizo la kuwepo kwa mbung'o *(tse tse flies),* kumesababisha maeneo halisi yanayofaa kwa kuchunga kuwa ekta 24 milioni (sawa na asilimia 40 ya hekta 60 milioni). Ni dhahiri kwamba, eneo kubwa tu lipo kupanua shughuli za ufugaji na kuinua kipato cha mfugaji.

Mheshimiwa Spika, dunia sasa inakabiliwa na mabadiliko ya hali ya hewa, inayosababisha mabadiliko katika mienendo ya upepo, mvua, joto na kadhalika. Nchi yetu kama zilivyo nchi nyingine, inakabiliwa na tatizo la ukosefu wa mvua. Hali hii imesababisha kushuka kwa uzalishaji wa mazao ya chakula. Aidha, nyanda za malisho nazo zimeathirika, hali inayotishia upatikanaji wa malisho bora ya kutosha na maji. Hali kama hiyo ni ukweli kwamba, malisho katika nyanda huwa ni ya msimu kulingana na hali ya hewa ilivyo, lakini pia uzalishaji huwa mdogo na thamani nayo kupungua *(Poor Quantity and Quality).*

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa maji kwenye malisho nao unaathiri hali nzima ya ufugaji hapa nchini. Idadi ya mabwawa na malambo yamekuwa hayatoshelezi kutokana na uchache wake, lakini pia kutokana na athari ya ukame ulioikumba nchi yetu. Kutokana na hali hii wafugaji wanalazimika kuhama kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine kufuata malisho na maji pale yanapopatikana.

Mheshimiwa Spika, tabia hii ya kuhama hama, haiko tu kwa wafugaji pekee, bali hata mwanadamu mwenye hisia za kawaida, hawezi kuendelea kuishi sehemu ambayo anashindwa kupata mahitaji yake ya kila siku na ndiyo maana kumekuwa na tabia na hasa kwa vijana, kuhama vijijini na kuhamia mijini ili kufuatia maendeleo wakiamini kwamba, huko ndiko yaliko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wafugaji wanapohama sehemu moja kwenda nyingine ni dhahiri kwamba, wanafanya hivyo kwa nia njema kabisa ya kunusuru maisha yao na mifugo yao. Lakini kwa sababu hapakuwa na maandalizi muhimu yaliyofanywa kufuatilia uhamaji huo, hali hii ilisababisha mtafaruku baina ya wafugaji na wakulima na hali ya mazingira kwa ujumla.

Kambi ya Upinzani inaona kwamba, ni lazima tufanye mabadiliko makubwa katika mazoea tuliyonayo ya kuchunga na sasa tuanze kufuga. Ili tufikie huko, taaluma ya kutosha ni lazima itolewe, kuwahamasisha wachungaji wabadilike ili wajiandae kuingia katika hatua nyingine ya ufugaji wa kisasa. Hili nalo linahitaji maandalizi, yakiwemo upatikanaji wa maeneo ya ardhi nzuri na ya kutosha, mbegu bora za malisho, maji ya kutosha, kwa kujenga mabwawa yenye uwezo mkubwa wa kuhifadhi maji, kuboresha ukosaafu wa mifugo yetu ya asili, kudhibiti magonjwa ya mifugo, kuimarisha masoko na viwanda vya kusindika mazao ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa nia njema kabisa, imepitisha uamuzi wa kuyagawa baadhi ya mashamba yake makubwa ya mifugo, kuwamilikisha wafugaji wadogo ili kuendeleza shughuli binafsi za ufugaji. Nachukua nafasi hii, kuipongeza Serikali kwa uamuzi wake huu. Kwa mujibu wa utaratibu huu, wafugaji wanaopatiwa mashamba haya, wanatakiwa kufuata kanuni bora za ufugaji ili waweze kuongeza tija.

Taarifa tuliyonayo ni kwamba, hadi hivi sasa Mashamba ya Iwabi (Mbeya), Malonje na Kalambo (Rukwa), utaifishaji bado unasuasua. Sababu za msingi zimekuwa hazijulikani na kwamba, wananchi walioomba kupatiwa mashamba hayo na ambao tayari taratibu zote wameshazikamilisha, hawajui hatma yao. Ni vyema basi Serikali sasa ikatoa tamko rasmi kuhusu hatma ya mashamba hayo na kuwaeleza wananchi ni lini watapatiwa maeneo hayo ili waanze shughuli za uzalishaji. Aidha, kwa yale mashamba ambayo tayari yamegawiwa, sisi Kambi ya Upinzani tunapata wasiwasi kujua iwapo Serikali inafuatilia ipasavyo kuona kwamba, waliopewa mashamba haya wanafuga kwa mujibu wa makubaliano na madhumuni ya kutaifisha mashamba haya.

Mheshimiwa Spika, tunaitaka Serikali itueleze ni vipi na ni kwa namna gain, wameandaa mikakati ya kujiridhisha kuona kwamba, wafugaji waliopewa mashamba haya wanafuata taratibu zilizowekwa katika kuendesha shughuli za ufugaji wa kisasa.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imekuwa inazalisha wataalamu wengi wa Mifugo. Wataalamu hawa mara nyingi huwa wanasubiri kuajiriwa na Serikali. Wakati mwingine huchukua muda mrefu kabla ya kupata ajira na hivyo, kupoteza muda mwingi wakizurura. Wakati umefika sasa, nasi kuiga nchi za wenzetu ambapo wahitimu wa Vyuo Vikuu katika fani za kilimo hupewa ardhi ya kutosha, zana za kilimo na vifaa vinginevyo kwa njia ya mkopo ili kuzalisha. Kwa kufuata utaratibu huu, kwanza wataalamu hawa huwa wanaitumia kivitendo elimu yao, wanakuwa wakulima bora ambapo wengine hujifunza kutoka kwao. Lakini la msingi zaidi ni kuwa, wanajiajiri wenyewe. Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali, kuanzisha utaratibu wa kuwapatia

wasomi wetu ardhi, zana, mifugo na mitaji, kwa njia ya mkopo ili waweze kujiajiri wenyewe, lakini pia iwe ni fursa kwa wafugaji kujifunza kutoka kwao.

Mheshimiwa Spika, hili ni eneo moja ambalo kama litatumika ipasavyo, linaweza kusukuma mbele maendeleo ya wafugaji hapa nchini. Kwa muda mrefu, tumekuwa tunafanya tafiti mbalimbali kuhusu mifugo. Kwa bahati mbaya, nyingi ya tafiti zinazofanywa, bado hazijaelekezwa kutatua matatizo halisi ya mfugaji. Aidha, ugani nao kutokana na udhaifu wake, umeshindwa kubadilisha hali ya ufugaji nchini na hatimaye tumeendelea kufuga kwa mtindo ule ule wa kale, jambo ambalo linasababisha kushuka kwa viwango vya uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, uhusiano baina ya utafiti na ugani, umekuwa ni mdogo mno kiasi ambacho, kumetokea matokeo ya tafiti ambazo zinalenga kuwakomboa wafugaji, hayawafikii wahusika. Mahusiano ya tafiti na ugani ni muhimu sana ili pawepo na mwingiliano wa taarifa toka kwa watafiti kwenda kwa wafugaji na kinyume chake. Haya yote hayataweza kufanyika ikiwa wataalam wa ugani ni wachache, wenye maarifa duni, wasio na vitendea kazi, wanaolipwa mishahara midogo, palipo na uchache wa mawasiliano baina yao, watafiti na kadhalika.

Katika kulikabili tatizo hilo, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ichukue hatua madhubuti kuhakikisha kuwa shughuli za utafiti na za ugani, zinatekelezwa ipasavyo. Miongoni mwa hatua muhimu ambazo tunashauri kuchukuliwa ni pamoja na Kuunganisha na kuimarisha shughuli za ugani ikiwa ni pamoja na wagani wenyewe; Kuunganisha na kuimarisha mahusiano baina ya utafiti, mafunzo, ugani na mfugaji; Kuimarisha miundombinu na vifaa kwa ajili ya shughuli za ugani; Kuendeleza na kuimarisha ushirikishwaji katika shughuli za ugani; na kuimarisha elimu na huduma za kitaalam, kwa watafiti na wagani wa mifugo.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi kirefu sasa, Serikali imekuwa inatoa mafunzo ya ufugaji kwa wafugaji katika vyuo vyetu vya mifugo. Mwaka 2003/2004, wafugaji 1,434 walipatiwa mafunzo. Mwaka 2004/2005 wafugaji 1,153 na mwaka 2005/2006 wafugaji 1,637. Hii ni idadi ndogo sana, ukilinganisha na idadi ya wafugaji tulionao nchini. Aidha, elimu inayotolewa bado haijaweza kuleta mabadiliko makubwa ya kumkomboa mfugaji ipasavyo. Sisi tunaona ipo haja ya kuvipanua vyuo hivi ili kwanza, kuongeza idadi ya wafugaji wanaopata mafunzo, lakini pia kuimarisha mitaala ili iweze kuleta mapinduzi makubwa katika uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwelekeo tunaouona katika utoaji wa taaluma hiyo ni kuwa, unalenga zaidi wafugaji wanaomiliki ng'ombe wachache wa maziwa. Lakini wafugaji wenye mifugo mingi, ambao ingelikuwa ndio lengo hasa la Serikali kuwapatia mwanga wa ufugaji bora, hawaipati nafasi hiyo. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kueleza ni hatua gani madhubuti, itazichukua kuhakikisha kwamba, wachungaji nao pia wanashirikishwa katika mafunzo haya ili waweze hatimaye kubadilika kutoka katika hali ya uchungaji waliyonayo na kuwa wafugaji wanaofuata mbinu za kisasa za kukuza uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali, *NGOs,* pamoja na wadau wengine, wanaonesha nia nzuri na azma ya kuendeleza mifugo nchini. Hii ni dhana pana na kwamba, kila mmoja ana mbinu na utaratibu wake wa kutekeleza azma hii. Kadhalika ni lazima tujue kwamba, jambo lolote na hasa lenye kuleta maendeleo, ni lazima liwe na pa kuanzia *(Bench Mark).* Kutokana na chanzo hicho, ndipo unapata mwanga wa kutosha kuweza kutambua changamoto zinazokukabili na hatimaye kutandika mbinu zitakazotuwezesha kutimiza malengo yanayokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, ili tuweze kuleta maendeleo ya mifugo nchini, hapana budi kwanza, tuwe na taarifa muhimu ambazo zitatupa njia sahihi katika kupanga mbinu za utekelezaji. Kwa hiyo ni lazima tujue idadi kamili ya mifugo tuliyonayo na mtawanyiko wake hapa nchini *(distribution);* taarifa za uzalishaji; masoko na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kutokana taarifa hizo tunaweza pia kujua ni namna gani rasilimali hii inawasaidia wananchi na Taifa kwa ujumla; kiwango cha uharibifu wa mazingira kinachosababishwa na rasilimali hiyo na namna ya kuukabili uharibifu huo; iwapo rasilimali ya mifugo tuliyonayo, inaweza kuhimili soko la ndani na nje; kujua na kubuni mbinu mbalimbali za kuweza kulinda rasilimali hizo; na pia kuweza kukadiria kwa umakini zaidi na kuweza kupima mafanikio ya Sekta hii kwa miaka ya mbele.

Mheshimiwa Spika, ili tuweze kufanikiwa katika hayo ni lazima Taifa lifanye sensa kamili *(Complete Enumaration*) ya mifugo iliyopo hapa nchini. Kwa muda mrefu sasa tumekuwa tunapewa takwimu za mifugo kutokana na makadirio *(Extrapulated Information Based on Sample Census).* Sensa ya mwisho ilifanywa mwaka 1984, wakati huo takwimu zilionesha kwamba, Taifa lina ng'ombe milioni 12.5, mbuzi milioni 6.4, kondoo milioni 3.1 na nguruwe 280,000. Aidha, kwenye miaka ya 1961 na 1964, Sensa kamili ya mifugo pia ilifanyika. Mwaka 1971/72 kulifanyika *Survey* ya kilimo ambapo pia mifugo ilijumuishwa. *Survey*s nyingine za kilimo ambazo pia zilijumuisha mifugo ni kama ifuatavyo: *National Sample Census of Agriculture 1993/94; National Sample Census of Agriculture 1994/95; Expanded Survey of Agriculture 1996/97; District Integrated Agricultural Survey 1998/99* na *Agricultural Sample Census 2002/03.*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kuwa Sensa kamili ya mifugo ya mwisho ilifanywa mwaka 1984, ambapo ni zaidi ya miaka 20 sasa, haingekuwa busara kabisa kutumia takwimu zinazotokana na makadirio ya Sensa iliyofanyika miaka ishirini iliyopita *(are not justifiable)* na takwimu zinazotokana na *surveys* nilizozitaja awali. Kwa kuwa Shirika la Chakula na Kilimo Duniani *(FAO)*, linapendekeza kwamba, Sensa ya Mifugo iwe inafanywa kila baada ya miaka kumi, ni dhahiri kwamba, tunahitaji takwimu sahihi na zilizo bora ili kupanga mikakati madhubuti ya kuleta maendeleo ya mifugo nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kulieleza Bunge lako Tukufu, iwapo inaona upo umuhimu wa kufanya Sensa kamili *(Complete Enumaration)* na ni lini Sensa hiyo itafanywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nilitangulia kusema awali kuwa, Tanzania tumejaliwa rasilimali kubwa ya mifugo, takwimu za uzalishaji zinaonesha kuongezeka mwaka hadi mwaka. Lakini kuongezeka kwa uzalishaji huu, kamwe kwa kiasi kikubwa hakutokani na kuongezeka kwa wastani wa uzalishaji kwa mnyama, bali inatokana na kuongezeka kwa idadi ya mifugo yenyewe.

Mheshimiwa Spika, ili tuweze kupiga hatua katika kuongeza uzalishaji ni lazima sasa Serikali na sote kwa ujumla, tuangalie nyuma, tutazame wapi tumejikwaa na ni zipi changamoto, ambazo zimetukabili na ambazo zikishughulikiwa ipasavyo, tunaweza kusonga mbele. Kambi ya Upinzani ina imani kuwa, kama tutaangalia maeneo yafuatayo kwa minajili ya kubaini kasoro zilizopo na hatimaye Serikali kwa kushirikiana na wadau wote, tunaweza kuleta maendeleo makubwa ya mifugo hapa nchini. Eneo la kwanza ni la kukosa afya.

Mheshimiwa Spika pamoja na kwamba, tuna ng'ombe wengi hapa nchini lakini asilimia kubwa ni wenye asili ya kienyeji, ambao ukuaji wao ni mdogo na maumbile yao ni madogo, uzalishaji pia ni mdogo, ng'ombe mmoja anatoa lita 1.5 kwa siku, lakini wanyama hawa wana sifa ya kuhimili maradhi na sulubu.

Mheshimiwa Spika, ili tuweze kuongeza ukuaji wao na hatimaye kuongeza uzalishaji wa ngombe hao, jambo la msingi ni kuboresha kwa kiwango Fulani, ukosaafu *(Genetic Makeup)* wa mifugo yetu. Kwa kubaini hili, Serikali imechukua hatua kadhaa kuimarisha shughuli za uhamilishaji nchini *(Artificial Insemination).* Madume na mbegu bora zimekuwa zinaagizwa kutoka nje ya nchi, lakini kadhalika kilianzishwa kituo maalum cha kitaifa cha kuendeleza shughuli za ukosaafu *(National Artificial Insemination Center).* Juhudi hii imeonekana na kwa kweli tunaipongeza. Kwa muda mrefu sasa, hiyo ndiyo imekuwa njia pekee inayotumika Tanzania kuboresha ukosaafu wa ng'ombe wetu wa kienyeji, yaani kupandisha kwa kutumia madume au mbegu za kigeni, ambapo kizazi kinachopatikana kina sifa ya ukuaji bora na uzalishaji mzuri. Lakini ni lazima tukiri kwamba, njia hii pamoja na kwamba ni rahisi kulinganisha na nyingine, inachukua muda mrefu sana kufikia malengo. Aidha, huduma hii haiwafikii wafugaji wengi kutokana na matatizo ya usafiri, zana na vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi teknolojia hii itatucheleweshaa sana katika kumkomboa Mtanzania. Hivi sasa dunia inasonga mbele, teknolojia mpya zinavumbuliwa, Tanzania nasi kama walimwengu wengine, ni lazima tubadilike pia. Ili kuweza kuleta mabadiliko ya haraka ni lazima sasa Serikali iwekeze na kutoa kipaumbele matumizi ya teknolojia za kisasa katika uzalishaji kama hii ya *Multiple Ovulation Embryo Transfer (MOET). (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ni njia moja nyepesi na ya haraka katika kuongeza idadi ya ng'ombe wenye ubora wa uzalishaji. Sisi tunachelewa kuipokea, baadhi ya wenzetu wa nchi zinazoendelea, wameipokea teknolojia hii mapema na sasa wamepiga hatua kubwa. Ni dhahiri kwamba, sasa wakati umefika na sisi tuitumie teknolojia hii na hasa ukizingatia tuna rasilimali ya kutosha kutusaidia. Jambo la muhimu hapa ni kuona

tunawekeza ipasavyo na kwa hiyo, tutumie fursa hii kukuza uhusiano wa kitaalamu *(Technical Cooperation)* na nchi zilizotutangulia ili kuchota uzoefu wao. Sasa basi hatuna sababu ya kuchelewa zaidi.

Mheshimiwa Spika, Tanzania tumeanzisha *Mpwapwa Breed,* kwa bahati mbaya ng'ombe hawa pamoja na kwamba, wana uwezo mkubwa wa kuzalisha nyama na maziwa, wamekuwa hawazalishwi kwa wingi kuenea nchi nzima ili kuweza kuwanufaisha wafugaji. Kadhalika ng'ombe aina ya *Ankole,* nao hawaongezeki, ni ng'ombe wazuri wakiweza kuzalishwa kwa wingi na kusambazwa kwa wafugaji, tunaweza kupiga hatua kubwa katika uzalishaji.

Njia pekee inayoweza kutufikisha mahali pazuri ni kutumia teknolojia hii ya *MOET*, ambapo vizazi bora vinaweza kuzalishwa vingi na kwa muda mfupi ili kuweza kukidhi mahitaji yetu. Serikali haina budi ni lazima iwekeze fedha za kutosha, kuwafundisha wataalamu wetu, kununua vifaa na zana na kuimarisha maabara zetu ili tuweze kumudu mabadiliko hayo ya teknolojia duniani. Sambamba na hilo, mashamba yetu ya mifugo yaimarishwe, idadi ya mifugo izalishwe kwa wingi hatimaye mifugo hiyo iwafikie wafugaji katika sehemu zote za nchi hii.

Mheshimiwa Spika, hatua inayochukuliwa hivi sasa ya kuboresha ukosaafu wa mbuzi nayo pia ni nzuri, isipokuwa kwa sababu tunatumia upandishaji wa kawaida *(Natural Mating),* matokeo yatachukua muda mrefu na kwa hiyo, hatuna budi kubadili mbinu ya kutuwezesha kuongeza idadi ya mbuzi wa kisasa kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Spika, mifugo yetu inakabiliwa na maradhi mbalimbali, lakini zaidi ni yale yanayosambazwa na kupe na ndorobo. Maradhi kama ndigana, ndiganabaridi, malale, miguu, midomo na kadhalika, yamekuwa ni kikwazo katika kukuza uzalishaji wa mifugo nchini. Inatupasa sasa tujiulize hivi ni kwa nini miaka mingi tumekuwa tukijitahidi kudhibiti magonjwa ya mifugo bila ya mafanikio ya kutosha, japokuwa kila mwaka chanjo na madawa kadhaa, yananunuliwa tena kwa gharama nyingi kutoka nje. Huo ni mwanzo mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inashauri ili kukabiliana na changamoto hii, tunaona ipo haja sasa kwa Serikali kuchukua hatua zifuatazo:-

- Wadau wanaoagiza madawa ya mifugo kutoka nje, wasamehewe ushuru ili kuwezesha madawa hayo kuingia kwa wingi nchini na hatimaye bei itashuka ili wafugaji wamudu kuyanunua. Ushuru huu unaweza kujirudia *(recovered)* kwenye masoko ya bidhaa za mifugo. *(Makofi)*
- Serikali ihakikishe kwamba, madawa yanayoagizwa yana ubora unaostahili lakini pia maduka yanayouza madawa, yawe yanakaguliwa mara kwa mara kuhakikisha hakuna madawa yanayouzwa ambayo yamepitwa na wakati au yenye viwango duni.

- Ruzuku itolewe kwa madawa hasa ya kukogeshea na chanjo muhimu za kudhibiti magonjwa ya mlipuko.

- Serikali iache kila wakati kuitangazia dunia kuwa mifugo yetu ina maradhi. Hali hii inaongeza hofu kwa jamii za Kimataifa na hatimaye tunaharibu soko letu wenyewe la mazao ya mifugo na kwamba, fursa hii kuchukuliwa na nchi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunafahamu wazi kwamba, nchi za wenzetu pia zina matatizo makubwa ya maradhi ya mifugo, pengine zaidi kuliko sisi lakini wao hawapigi makelele na kwa hiyo, biashara yao inaimarika siku hadi siku. Waswahili wanasema "usiumwe na mbwa ukatangaza kidonda." La msingi pia hapa ni kuhakikisha kwamba, hatua madhubuti zinachukuliwa kudhibiti maradhi hayo.

Mheshimiwa Spika, mnyama kama alivyo binadamu, anahitaji chakula kilicho bora na maji safi na salama. Ni makosa makubwa kudhania kwamba, wanyama wanaweza kuishi vizuri na kuzalisha katika viwango vilivyo bora, kwa kuokota okota malisho na kukosa maji yaliyo bora na salama. Nimetangulia kusema awali kwamba, nchi yetu ina maeneo makubwa ya nyanda za malisho. Nyanda hizi ndizo ambazo zinatoa malisho ya takriban asilimia 90 ya mifugo nchini. Aidha, malisho yaliyomo katika nyanda hizo, hayana ubora unaostahili, yanapatikana kwa msimu kutegemea unyeshaji wa mvua. Katika hali kama hii ya kutegemea nyanda hizi, hatuwezi kamwe kuongeza tija katika mifugo katika nchi hii. Tija ya mifugo inatokana, pamoja na mambo mengine, malisho yaliyo bora na maji ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inayo mashamba mawili ya kuzalisha mbegu za malisho; Vikuge (Pwani) na Langwira (Mbeya). Mashamba haya yanafanya kazi nzuri na kwa kweli yanastahili pongezi. Mbegu mbalimbali zinazalishwa kwa ajili ya malisho ambayo huuzwa kuongeza mapato ya shamba. Tunachojifunza hapa ni kwamba, kuna mwamko unaoonekana kwa wafugaji kuona umuhimu wa kuwapatia mifugo yao chakula kilicho bora. Chakula bora ni pamoja na mchanganyo wa malisho ya aina ya majani na mikunde kunde. Tukitathmini wafugaji wenye mwamko huu, tutaona ni wale tu ambao wanamiliki ardhi na ambao wanapanda malisho kwa ajili ya mifugo yao, hawa ni wachache sana.

Mheshimiwa Spika, malisho ya mifugo kwenye nyanda na mbuga, yanategemea sana mvua na hali ya hewa iliyopo na hivyo uzalishaji unaathirika kulingana na hali ya hewa. Kipindi kilichopita, tumeona jinsi gani ukosefu wa mvua ulivyoathiri upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo. Kama ulivyo uzalishaji wa mazao ya chakula kwa binadamu, kuna baadhi ya maeneo yalikuwa na uhaba mkubwa wa chakula na maeneo mengine yalikuwa na ziada. Serikali ilichukua hatua ama ya kuagiza chakula kutoka nje ya nchi au kuhamisha chakula sehemu moja ya nchi kwenda sehemu nyingine. Hatua hii ilifanywa ili kunusuru uhai wa binadamu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa wafugaji, hali haikuwa hivyo, wafugaji walilazimika kuinusuru mifugo yao kwa kuihamishia maeneo ambayo maji na malisho ya kutosha yanapatikana. Aidha, Serikali ilitangaza hatua ya dharura ya kuruhusu mifugo kuchungwa katika maeneo ya hifadhi ya wanyamapori. Hatua hii ina athari zake hasa katika maambukizi ya maradhi ya mifugo. *(Makofi)*

Ni lazima tukubali kwamba, njaa inaleta fadhaa, kila mtu aliyepatwa na janga hili alifadhaika. Kadhalika na wafugaji nao walifadhaika kutokana na janga la ukame lililoikumba nchi yetu. Wafugaji walichukua hatua, pengine kwa fadhaa hiyo hiyo, wakalazimika kuhamisha mifugo yao na kuipeleka sehemu zenye malisho na maji. Kitendo hiki kimelaumiwa sana na baadhi ya watu na hasa wakulima wa mazao na wanamazingira.

Mheshimiwa Spika, ili kujiepusha na tatizo hili hapo baadae, Kambi ya Upinzani inashauri mambo yafutayo:-

- Wafugaji wamilikishwe maeneo ya ardhi iliyo nzuri kulingana na uwezo wao wa kuyahudumia.

- Maeneo ambayo mifugo ipo mingi ni lazima miundombinu kama malambo na mabwawa kwa ajili ya upatikanaji wa maji, yajengwe na kuimarishwa ili kuondoa kabisa matatizo ya upatikanaji wa maji.

- Majosho mapya yajengwe sehemu ambazo hakuna na kufanyiwa ukarabati yale ambayo hayafanyi kazi.
- Utaratibu wa kuwapatia wafugaji mikopo nafuu uandaliwe.

- Huduma za masoko na viwanda vya kusindika mazao ya mifugo ziimarishwe.

- Upatikanaji wa mbegu za malisho bora na taaluma ya uvunaji na hifadhi ya malisho kwa matumizi ya baadae uimarishwe na kuendelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Mheshimiwa Waziri Mkuu, alikutana na wakulima wa mazao mbalimbali ya biashara, pamoja na Waheshimiwa Wabunge wanaotoka maeneo ambayo mazao hayo yanazalishwa. Madhumuni makubwa ya vikao hivyo ilikuwa ni kutambua changamoto wanazozikabili wakulima hao ili hatimaye kuandaa mikakati ya pamoja kuboresha na kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, wafugaji nao wakiwa pia ni wenye kuchangia Pato la Taifa, kadhalika wanakabiliwa na changamoto nyingi, zinazowakwaza katika uzalishaji. Ni dhahiri na wao wangependa kukutana na Waziri Mkuu wao, ili kubadilishana nae mawazo juu ya suala zima la ufugaji nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii tena, kwa heshima na taadhima kubwa, kupitia kwako, kumwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, akutane na wafugaji, Waheshimiwa Wabunge wanaotoka katika maeneo ya wafugaji pamoja na wadau wengine, ili kwa pamoja watafakari jinsi ya kupambana na changamoto zinazoikabili sekta ya mifugo nchini na kuaandaa mikakati madhubuti ya kusukuma mbele maendeleo ya mifugo kwa ujumla.

Mwisho, lakini sio kwa umuhimu, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Waziri wa Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Dr. Shukuru Jumanne Kawambwa na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Charles Ogesa Mlingwa, kwa mashirikiano makubwa wanayonipa. Aidha, nampongeza Katibu Mkuu, Dr. Charles Nyamurunda, Naibu Katibu Mkuu, Dr. Jonas Malewas, pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kusukuma mbele Maendeleo ya Mifugo nchini, pamoja na maandalizi mazuri ya hotuba hii, ambayo hatimaye imeweza kuwasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu. Kadhalika naomba niwapongeze na kuwatakia afya njema na maisha marefu, wale wote ambao kwa siku ya leo wanaadhimisha siku ya kuzaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika baada ya maelezo hayo na kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Msemaji Mkuu wa Upinzani. Waheshimiwa Wabunge, katika orodha yangu, ninao wachangiaji 18, lakini tunaoweza kumudu ni tisa tu. Sasa nitoe maelezo ili walioachwa wajaribu kuelewa. Kwanza, kama kawaida tunatoa kipaumbele kwa Waheshimiwa Wabunge, ambao hawajachangia hata mara moja na wako wawili, nao ni Mheshimiwa Maria I. Hewa na Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami. Baada ya hapo, nimechekecha upya majina ili niweze kupata mchango wa Waheshimiwa Wabunge wanaotoka katika maeneo ya ufugaji. Kwa hiyo, hata kama umechangia mara moja au mara mbili, lakini ndani ya orodha ile nitateua wale ambao wanatoka maeneo halisi ya ufugaji, ili Serikali iweze kupata mchango halisi wa matatizo halisi yalivyo. Kwa hiyo, orodha hiyo sasa inakamilishwa, lakini tutaanza na Mheshimiwa Maria I. Hewa, ajiandaye Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami. *(Makofi)*

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia walau katika Bunge hili la bajeti, kwa mara yangu ya kwanza, baada ya kuwa na shughuli nyingine ambazo ni za kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, napenda pia na mimi kuwapongeza wale wote, ambao umekuwa nao katika kuwapongeza kufikisha miaka yao ambayo haikutajwa hapa, kwa maana *birthdays* zao na wale wengine ambao wanatarajia kufikisha miaka ambayo najua haitajulikana, katika mwaka huu nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kingine ambacho nazidi kukipongeza ni kile cha Wizara hii, sasa hivi kujitegemea. Wizara hii ya Maendeleo ya Mifugo, ilikuwa ikiunganishwa kila wakati na Wizara nyingine, kiasi cha kwamba, nadhani Wizara yenyewe ilikuwa ikionekana kuyumbayumba tu, ndio maana hata mambo yake yalikuwa hayaeleweki vizuri. Lakini kwa sasa, kwa vile ni Wizara inayojitegemea kabisa, naamini itafanya makuu na itawatendea haki wafugaji. Kwa kweli naipongeza sana Serikali hii ya Awamu ya Nne, kwa kuona umuhimu wa wafugaji kuwa na Wizara yao inayojitegemea kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mtovu pia wa fadhila kama sitawakumbuka na kuwashukuru sana sana wanawake wa kutoka Mkoa wa Mwanza. Kuniwezesha na mimi walau leo nizungumze, ndani ya Bunge lako Tukufu baada ya kunikubalia kwamba niwe

Mbunge wao kuwawakilisha, kwa kweli ninawashukuru wanawake wa Mwanza nasema asante sana kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mama Hewa huwa ni msemaji wa mambo mafupi tu, mimi huwa sio msemaji sana. Ninachotaka kuanza kuzungumza katika hotuba hii au msahafu uliotolewa leo na Waziri wa Maendeleo ya Mifugo mbele yetu katika Bunge lako Tukufu, ni kwamba, hotuba yenyewe kwa kweli ni nzuri na inatupa mweleko mzuri wafugaji wa nchi hii yetu ya Tanzania, ambayo kwa kweli nadhani inategemea pia ufugaji ulio bora ili kuinua uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya nchi katika Afrika, ambazo wanategemea kabisa mifugo kwa maana ya kuinua uchumi wao. Sitaki kuzungumzia kwa undani sana ni nchi zipi, lakini zipo. Kwa wale ambao wanafuatilia sana mambo ya wafugaji, zipo nchi kwa mfano, Botswana na nchi nyingine ambazo zinategemea kabisa ufugaji, kwa maana ya kuinua uchumi wa nchi zao. Lakini Tanzania na sisi tu wafugaji na tuna mifugo mingi tu, kama ilivyotolewa katika hotuba, lakini je, swali la kujiuliza, sisi ni wafugaji bora au ni bora wafugaji? Hili ndilo swali la kujiuliza ili tutoke mahali tulipo. Tukitaka kusema ule ukweli, Tanzania kama hatutaamua kubadilika, tutaendelea kuwa bora wafugaji na ndio maana kuna kutangatanga, kwa sababu hatulitilii maanani ufugaji wa mifugo yetu katika hali halisi ya ufugaji bora.

Mheshimiwa Spika, wafugaji wa Tanzania wanachokikosa hapa niseme kwa uwazi, hawana elimu ya jinsi gani waweze kufuga mifugo yao katika ufugaji bora. Tunahitaji kuwaelimisha kabisa wafugaji hawa, maana nacho ni kitengo muhimu ambacho tunacho nchini. Tunapozungumzia mara nyingi suala zima la umaskini, ninaamini na kikundi hiki cha wafugaji, nao huwa tunawajumuisha humo kwamba ni maskini. Lakini kwa nini tunawasema maskini na pindi wanazungukwa na utajiri mkubwa tu mahali wanapoishi. Unaweza ukakuta mfugaji mmoja ana ng’ombe 100 mpaka 1,000, lakini ukimjulisha kwa haraka haraka ukiulizwa huyu ni maskini au ni mtu wa kawaida au ni tajiri, utasema ni maskini, lakini kazungukwa na utajiri wa hali ya juu sana. Yote hii ni kwa sababu mfugaji huyu, hana elimu ya ufugaji bora wa mifugo yake. Angeliweza kuwaeleimisha tena, suala la umaskini kwa mfugaji lisingekuwepo kabisa, lakini unamkuta huyo huyo anafuga ng’ombe, analala chini, mtoto hapelekwi shule, hayo maziwa mnayosema kunywa yeye hanywi, kukicha asubuhi anafungasha kwenye baiskeli, kama ndio wafugaji wangu wa Mkoa wa Mwanza, maziwa yote anakusanya anafuata na ya wengine, anawapelekea watu wa mjini. Sasa leo tunaambiwa mtu mmoja anapaswa kunywa lita 20, kitu kama hicho nimeona kwenye ratiba, kula mayai 64.

Mheshimiwa Spika, yote hayo yanayosemwa, tunawapelekea wengine, lakini mfugaji yule yuko palepale, hali na wala hanywi, yaani anapeleka tu kuuza, kuna mtoto hamsomeshi, kuvaa havai na kulala analala chini, nyumba yake ni duni tu. Sasa naomba Wizara hii ya Maendeleo ya Mifugo, wachukue kabisa mikakati ya lazima ya kuwaelimisha wafugaji hawa, kwa nini wanafuga na wanapaswa wafuge namna gain, kwa manufaa yao na kwa manufaa ya Taifa zima. Katika kuwaelimisha, si katika vituo hivi tulivyotajiwa hapa, wametaja wafugaji wanaenda kuelimishwa katika vituo. Mimi ningelishauri Wizara ichukue makusudi mazima, kuwafuata wafugaji mahali waliko,

wawafuate katika ngazi za vijiji, kata au katika ngazi za mkoa, huko huko waliko, ndiko waliko wafugaji.

Vinginevyo kama mtachagua *center* mbalimbali za kuwapa elimu, watu hawa ni kazi bure, kwanza mfugaji haachani na ng'ombe wake. Unapomwambia nenda ukafundishwe mahali fulani, anasema tangu nizaliwe nafuga, naenda kupata elimu gani? Kwa hiyo, utakapoamua kumfuata mahali aliko na kuwagawa katika mafungu madogo madogo, elimu hii itawapata. Wataweza kuelewa wanapaswa kufuga ng'ombe, kuku, mbwa au bata na kwa namna gani ataweza kupata elimu ya kumwezesha kuwa na maisha bora, asomeshe watoto, alale pazuri, ale vizuri na hayo mayai tunayoyataja kwenye vitabu ale vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuongelea suala la hiyo hiyo mifugo. Tunapoongea kwa mfano, ng'ombe ana hatua kama nne kumwezesha aweze kuishi katika maisha ambayo hahitaji mambo mengine zaidi. Ng'ombe huyu au mifugo hii inahitaji kwanza chakula, sasa chakula hiki kwa ng'ombe walio wengi huwa wanadhani kila jani linalika. Ng'ombe hali kila jani, ng'ombe ana uchaguzi na yeye wa majani anayokula, kama unavyochagua wewe binadamu chakula unachokitaka. Lakini unakuta mnatenga maeneo ya malisho, ambayo mnadhani huko ndiko maeneo ya kuwafugia hawa ng'ombe, hata kidogo, muelewe kabisa kwamba, kila jani si chakula cha mifugo hii. Sasa naomba katika hili, kuwepo na maeneo ambayo tutayatenga vizuri tu kwa ajili ya chakula, lakini kwenye majani ambayo yanalika na mifugo hii.

Chanjo ni muhimu, tuwe na *centres* mbalimbali huko tuliko. Katika hotuba hii mimi sijaona kwamba kuna mahali ambapo wamejenga *veterinary centres,* ambazo zitawahudumia wafugaji hawa kwa urahisi. Nimeona kwenye hotuba hii, majosho yametajwa mwaka 2005/2006; mwaka 2006/2007 yako wapi mapya? Tuongeze ujenzi wa majosho, ambapo wananchi hawa wafugaji wataenda kuosha mifugo yao, pamoja na kwamba, hawana uzito mkubwa kama yanavyosema maandishi mengine, lakini ile tu kumwosha ng'ombe kila wakati anapohitajika kuoshwa, unakinga magonjwa mengi sana ya kupe. Kwa hiyo, tutaendelea kupata mifugo iliyo bora tu na mwisho ndio hayo matibabu. *(Makofi)*

*Clinics* zetu hazipo zimekufa, sasa kila mfugaji ni mganga, waganga wako wapi? Zamani tulikuwa tukiwaona waganga wa mifugo hawa, anakuvalia koti, amekuvalia buti na pikipiki walikuwa nazo. Wako wapi sasa hivi? Hawapo tusidanganyane hapa, tuwatafute mabwana mifugo hawa, wawezeshwe hata kupatiwa pikipiki ikibidi na *kits* zao, waweze kutembelea wafugaji, ndipo hapo tunaweza tukafika mahali kweli Wizara hii tukaipenda na wafugaji wabadilike. Kwa kujua kwamba, sasa tunajitegemea na lazima tufanye kazi usiku na mchana, kurudisha heshima na hadhi ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, sipendi kupigiwa kengele ya pili, lakini napenda kusema kuwa, tutenge maeneo ya malisho yaliyo na chakula cha mifugo, tuwe na maeneo ya chanjo yanayoeleweka, majosho yaongezwe na *clinic centres* za matibabu zieleweke na mabwana mifugo waweze kututembelea katika maeneo ya mifugo, ambako mifugo inapatikana.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Asante. *(Makofi)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa fursa uliyonipatia ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo.

Naanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba nzuri aliyoitoa na kwa jinsi hiyo, nasema kuwa naunga mkono moja kwa moja. *(Makofi)*

Kabla sijaanza, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kongwa, nasema *Happy Birthday* kwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu. *(Makofi)*

Katika kuanza kuchangia hotuba hii, nimkumbushe tu Mheshimiwa Waziri mambo muhimu ambayo tumekuwa tukizungumza naye tangu ameteuliwa, ambayo nimeyasisitiza sana, sitapata muda wa kuyaongelea hapa, lakini nimemwandikia kwa kumkumbusha tu, najua anajua lakini nimeandika kwa kumkumbusha, naomba yazingatiwe.

Mheshimiwa Spika, ufugaji wa nchi yetu unaweza ukaugawanya katika sehemu mbili, yaani kuna wafugaji wakubwa kupitia *ranch*, mashamba ya Ushirika na kadhalika na kuna ufugaji mdogo. Huo ufugaji mdogo ndiyo sehemu kubwa ya wafugaji wa nchi yetu, wanaangukia kwenye *category* hiyo. Ufugaji huu ni wa kifamilia, inaweza kuwa ni familia yenye mifugo michache sana, ng'ombe mmoja au wawili, mbuzi wawili au watatu, kondoo na kadhalika, inaweza ikawa familia yenye ng'ombe wengi kwa maelfu. Lakini kwa kiwango kikubwa, ufugaji wetu uko kwenye familia moja moja na ndogo ndogo.

Kwa hiyo, hata tunaposhughulikia masuala ya mifugo, ni vema tukalenga hiyo hali halisi kwamba, mifugo iliyo mingi iko kwenye familia za Watanzania ndogo ndogo. Wananchi hawa wanafuga katika utaratibu ambao wataalam wenyewe wanauita *open access,* ambao kama kuna mbuga ya malisho, kila mmoja anapeleka ng'ombe wake pale bila kizuizi chochote. Hakuna ubinafsishaji wa maeneo ya malisho na kwa jinsi hiyo, wanahamahama wafugaji walio wengi ama hawahami wenyewe ila wanahamisha mifugo, lakini ile *element* ya kuhamahama ipo ama katika maeneo kidogo ama maeneo marefu. Hali hiyo ipo hivyo kwa miaka mingi, kwa sababu ya kuyatumia yale maeneo vizuri zaidi siyo kwamba wanapenda, ni kitu ambacho kimetokana na uzoefu wa maelfu ya miaka, huwezi kubadili hiyo kwa hotuba moja. *(Makofi)*

Kwa eneo kame kama Dodoma na Kongwa, tunakuwa na ufugaji ambao tunachanganya na kilimo kidogo, kwa wafugaji walio wengi na katika maeneo makame ukitazama familia yenye ng'ombe wawili au watatu, ambao wanafuga mifugo na mbuzi na kondoo na familia ambayo inalima tu kiasi, utakuta kwamba familia yenye mifugo ina unafuu mkubwa zaidi, kuliko familia inayolima ekari moja, mbili, tatu au nne. Ikitokea *shock,* ukame au janga lolote, ikalipata familia hizi mbili, utakuta familia yenye mifugo

ina unafuu zaidi kuliko familia ya mkulima wa kawaida wa ekari mbili au tatu. Mtoto akifaulu kwenda sekondari wa familia ya mfugaji na mtoto wa familia ya mkulima wa ekari moja, mbili au tatu, akienda kidato cha kwanza, mtoto wa familia ya mfugaji ana uwezekano mkubwa zaidi wa kwenda sekondari na kumudu zile gharama kuliko familia ya huyu mkulima wa ekari moja, mbili au tatu.

Lakini nini kinatokea, msisitizo ni kilimo. Ni kweli yapo maeneo ambayo msisitizo uwe ni kilimo, lakini yapo maeneo ambayo ni kame, hali ya hewa hairuhusu kilimo kikubwa, ni kilimo cha ku–*subsidise* mapato kutokana na ufugaji. Sisi Wagogo hapa katika mazungumzo ya kawaida, mtu akikwambia fulani ni tajiri sana, huwezi kuwaza kwamba ana nyumba kama hii ya Ofisi ya Bunge au huwezi kuwazia kama ni Mkurugenzi au ana hela nyingi sana.

Ukisikia fulani ni tajiri, unachojua ana ng'ombe, kwa lugha yetu tunaita *mgoli* na huyo mtu anaheshimika sana, ni mtu ambaye ukibanwa na matatizo mengi, unamkimbilia, ni kimbilio la watu wa kijijini pale. Pakiwa na mchango wa shule, wale wa ekari moja au mbili wataweza kuchangia? *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Hawawezi!

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Wanaitwa wafugaji wanachangia siku moja tu. Nina vijiji vyangu vingi, tuna miradi kwa mfano ya maji. Nina Kijiji kule Leganga, ambapo walitakiwa wachangie asilimia tano ya fedha zilizotolewa na Serikali kupitia *World Bank,* kwenye huu Mradi wa Maji unaosemwa kila wakati, mchango wa kijiji ni shilingi milioni sita. Waliitwa wafugaji walichangia shilingi milioni sita kwa siku moja katika kikao kimoja. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Safi sana hiyo!

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Kwa hiyo, ndugu zangu ufugaji ni chanzo cha kipato cha hakika, tukifika mahali kila anayesimama analaani ufugaji tunafanya kosa moja kubwa la msingi. Hali ya hewa ya maeneo kame, ufugaji unalipa zaidi *per area* kuliko kilimo lakini kinachotokea ni kwamba, maeneo yamezidi kuwa yanachukuliwa na jembe wanalima mwaka mmoja wanahama, yanachukuliwa na jembe, mifugo haina tena mahali pa kukaa hata njia za kwenda kwenye malisho sasa tabu, hata njia za kwenda kwenye maji tabu, wafugaji wamebanwa hawawezi kupumua tena.

Kwa hiyo, ushauri wangu wa kwanza ni kumwomba sana Mheshimiwa Waziri, ipo Sheria ambayo mnaitengeneza tengeneza, ije kwa ajili ya kutenga maeneo maalumu ya wafugaji ili yapate *Legal Status,* yasiingiliwe kama ambavyo Sekta ya Wanyamapori imefanya. Sekta ya wanyamapori imetenga hifadhi zinazoeleweka, haziingiliwi ovyo ovyo. Tutenge kabisa maeneo katika nchi yetu ambayo ni ya mifugo.

Ukitoka hapa Dodoma kwenda Dar es Salaam, angalia njiani kushoto na kulia kwa mfano, unataka uanzishe *ranch* ndogo ya ekta hata 10,000 tu utapata wapi? Toka hapa mpaka Dar es Salaam, tembea angalia kushoto na kulia ni wapi utakuta eneo zuri, limekaa sawasawa, ambalo unaweza ukasema hebu hili eneo tulizuie liwe la mifugo. Ni

mashamba matupu na mashamba yenyewe hebu tazama *critically* kilichopo huko ni nini, alicholima huyu mtu na alichovuna ni kitu gain. Utakuta hakuna cha mahindi wala kitu chochote cha maana, kumbe wale wananchi wangeweza kufuga ng'ombe angalau wawili au watatu, kwa kila familia, tena ng'ombe bora, kipato cha familia hizi kingeliongezeka sana, kuliko kilimo hiki cha jembe la mkono cha ovyo ovyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru Wizara, imekuwa ikitoa fedha kwenye Halmashauri zetu, kukarabati majosho na baadhi ya majosho yamekarabatiwa japo machache sana lakini mengi yaliyokarabatiwa, hayafanyi kazi kwa sababu tatizo siyo majosho. Kukosekana kwa majosho ni tatizo, lakini ukijengewa majosho yakakaa pale, bado hatujafumbua chochote. Kinachotakiwa ni yale madawa yanayohitajika kwa ajili ya kuwaogesha mifugo, madawa yale ni ghali hayapatikani. Kinachotakiwa ni chanjo kwa mifugo. Chanjo kwa mifugo ni tabu, binadamu hasa watoto wetu na kadhalika, tunawachanja bure, ni vema na sera hii ni sahihi. Nilikuwa nasema hali ikiruhusu basi na mifugo nayo upande wa chanjo, tuangalie uwezekano wa *subsidy.*

Mheshimiwa Spika, kuna jambo la moto huwa linaongelewa mara kwa mara, usionekane mahali popote. Mimi ni mtaalamu wa wanyamapori, katika hifadhi za wanyamapori, huwezi ku-*maintain* hifadhi ya wanyamapori bila moto, lakini sisi tunaita *Management Fire,* ule moto kichaa, ule kila mmoja anaupiga vita. Lakini tunapoweka *total burn,* moto usionekane mahali popote, tunafanya kosa moja kubwa la kimsingi na la kitalaamu. Mbuga yoyote ambayo haijapata moto hata kidogo kwa miaka 20, ukeleta ngombe wako 1,000 katika muda wa miezi mitatu, hao ng'ombe wanabaki 50, kwa sababu kuna wadudu wa aina mbalimbali, ambao sasa wameshaaza na imeshakuwa tatizo, wadudu kama Kupe na wengine.

Kwa hiyo, *Management Fire* ni muhimu sana, wananchi wetu waelimishwe moto unaohitajika wakati majani hayajakauka sana, bado ni ya kijani kidogo, unapitisha moto wa taratibu asubuhi au jioni. Moto wenyewe uwe wa taratibu na wa juu juu, unasaidia sana kutengeneza malisho yawezekane kwa wafugaji. Lakini ikiwa ni marufuku ya moja kwa moja, asilimia 100, *unless* hatutaki ufugaji. Sisi kwenye hifadhi tunachoma, lakini kama nilivyosema ni *Management Fire*. Kwa hiyo, hili nalo litazamwe, vinginevyo mifugo haiwezi kubaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja kwamba, mifugo inaongezeka sana, ng'ombe wanaongezeka wanaharibu mazingira. Mimi ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Mazingira ya Bunge, ni kweli ng'ombe wameongezeka kwa idadi, ingawa mpaka sasa sensa yetu ya mwisho ni ya mwaka 1984, kwa sensa ya 2004 tuna mifugo kwa maana ya ng'ombe, kondoo, mbuzi na nguruwe, wanaweza kufikia kwenye milioni 36 hivi kwa ujumla wao.

Ni kweli mifugo inaongezeka, lakini tukumbuke na idadi ya watu inaongezeka kwa hiyo, kinachotokea ni nini? Ile familia ambayo ilikuwa inategemea mifugo kiasi cha idadi fulani, familia imekua kubwa sasa haiwezekani kutegemea ng'ombe wale wachache waliopo kutokana na kukosekana kwa *balance* hiyo, mnaona vijana wa Kimasai wamejaa kule Dar es Salaam mitaani na wa makabila mengine ya wafugaji wamejaa kule mitaani.

Kama ng'ombe wangekuwa wameongezeka, wale vijana wangefuata nini mjini? Tunaamini kuwa wanafuata ule umeme? Siyo kweli hata kidogo, ni kwa sababu sasa hivi ile *balance* haipo tena, kati ya idadi ya watu katika utegemezi wao kwa rasilimali ya mifugo iliyopo, mifugo imeongezeka lakini watu wameongezeka zaidi, kwa hiyo, ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, Masoko ya Mifugo bado si ya uhakika, ukichukua Mkoa wa Mwanza, Manyara, Arusha, Kilimanjaro hata mpaka Tanga, karibu ng'ombe wao wengi wanawauza Kenya; kwa nini? Sisi tuliobaki wote au mikoa iliyobaki yote, soko letu kubwa ni Dar es Salaam na Dar es Salaam wana uwezo sana sana wa kula ng'ombe 1,000 kwa siku. Kwa hiyo, kama utapeleka ng'ombe 1,000 kila siku, maana yake kwa mwaka ni kama ng'ombe 400,000 tu, ambayo ni *off take* ndogo sana. Watu wa Dar es Salaam, kuleni nyama na watu wa mijini kuleni nyama, kunyweni maziwa. Mpaka sasa hivi Watanzania wanaokula nyama na kunywa maziwa kila siku ni wachache sana na matokeo yake nyama ni ghali sana. Tunatoa wito maalumu, inakuwa bei ghali kwa vile walaji ni wachache, moja ya sababu na sababu nyingine, ili tuweze kupunguza mifugo yetu na wafugaji wapate fedha za kutosha kwa maana ya kuuza mifugo yao vizuri, tunaomba hilo soko likae sawa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliwahi kutembelea Kenya mwaka 2004, nikafika katika kiwanda kimoja kinaitwa *Group Side Dairy,* kinashughulikia eneo la Mlima Kenya lote, *actually* ni kiwanda cha Bwana Uhuru Kenyatta. Tunataka kiwanda hapa Dodoma, kila familia huko vijijini imepewa ng'ombe mmoja au wawili wa maziwa, wanauza katika *center* zinazoeleweka, maziwa yanakusanywa, baada ya kupoozwa, yanapelekwa kwenye kiwanda yanasindikwa, yanauzwa kokote ndani na nje ya nchi.

Waheshimiwa Wabunge, ni wapi utaenda uweze kuagiza hapa nchini kwetu, hebu naomba *packet* ya maziwa ya mgando? Kila mtu anakunywa fanta na cocacola, vinywaji ambavyo vimejaa sukari nyingi sana, matokeo watu tuna matatizo ya sukari, *pressure* na mengineyo, kwa sababu asubuhi mpaka jioni ni cocacola na fanta na wakati mwingine bia, ambayo matokeo yake si mazuri. Maziwa yako wapi? Kwa hiyo, tuna maeneo muhimu sana ya kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, nimezungumza baada ya Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami kuzungumza, sijui yanayoendelea Rukwa, lakini nilikuwa nimepanga hapa kumpongeza sana Mheshimwia Dr. Chrisant M. Mzindakaya, kwa sababu anajenga kiwanda cha kisasa cha kusindika nyama ili kuuza nje ya nchi na ndani ya nchi. Ni Mbunge mwenzetu ameweza kufanya. Mheshimiwa Waziri, tuwezesheni na sisi tufanye, tunaweza kabisa. Mbunge huyu ameonesha mfano na ni mfano wa kuigwa, kwa kuweka kiwanda cha kisasa, sijakiona lakini nina hamu ya kukiona na baada ya Bunge hili, nitakwenda Sumbawanga kuona nini kinaendelea. Kwa sababu hiyo ndiyo njia sahihi ya kuendeleza mifugo yetu ili na sisi tufanane na Botswana na nchi nyingine, ambazo mifugo inawalipa vizuri sana. *(Makofi)*

Yapo mengi ya uendelezaji wa Mifugo, lakini Mheshimiwa Waziri ameyaeleza yaliyo mengi, nitaje machache tu. Kwanza, wafugaji wanahitaji mafunzo ili waweze

kushughulikia magonjwa madogomadogo ya mifugo yao wenyewe au kuchukua vijana wawili au watatu kijijini kwenda kwenye vyuo vyenu vya mafunzo ya tiba ya mifugo, wakapate kozi ndogo ya miezi mitatu au mine, ili kushughulikia matatizo madogo madogo vijijini, hawahitaji kuajiriwa na mtu hawa. Wakipewa uwezo huo, wanaweza kufanya hivyo kwa sababu madaktari wetu wa mifugo ni wachache. Naomba sana minada iliyopo na ikiwezekana tu-*introduce* mizani tena.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kueneza madume bora ni muhimu sana kwa mfano, sisi wa Kongwa kule, tunayo *ranch*, ambayo nimesimama mara kadhaa kuelezea hapa. Nimesema leo sitazungumzia masuala ya *ranch*, lakini niseme tu inawezekana mpango wa madume bora unawezekana kwa Kongwa na Kongwa ikawa ni mfano wa ufugaji bora. Kupeleka watu kila siku kushangaa ng'ombe wa *ranch* wakati vijiji jirani vyote 13, vina ng'ombe wa kizamani, waliopitwa na wakati, haisaidii kwetu sisi wala hatufurahii chochote pale. Ndiyo maana mara kwa mara husema ile ranch sisi kwetu ni mzigo tu. Tunataka kuwepo kwa *ranch* ile kuwe na maana kwa wananchi wa Kongwa na wananchi wa Mkoa wa Dodoma. Kuhusiana na *ranch* nimesema nimekuandikia, sitazungumzia hapa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kusema kuwa, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Job Y. Ndugai. Wakati huohuo nimepokea ombi kutoka kwa Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mbunge wa Karagwe na nikagundua kwamba, kijiografia ilikuwa hakuna Mbunge yeyote wa kutoka Maeneo ya Kagera. Kwa hiyo, nimemwomba Mheshimiwa George M. Lubeleje, ambaye namshukuru sana amekubali achangie kwa dakika saba na nusu, halafu nitamwita Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mbunge wa Karagwe, achangie kwa dakika saba na nusu ili zile dakika zitimie na tupate ladha ya sehemu zote mbili, halafu tutaendelea kama kawaida. *(Makofi)*

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika na mimi naomba nitumie fursa hii, kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo.

Kwanza, napenda nikupongeze wewe, kama Mume wa *Mama Birthday* au *Birthday Woman,* ambaye leo hii anasherehekea siku ya kuzaliwa kwake, kwa kweli mafanikio yote ya Mwanaume huwa yanakuwa *backed-up* na Mwanamke. Nina imani kwamba, sherehe hii tutasherehekea wote, hata kama kuna keki nadhani Waheshimiwa Wabunge, watapata nafasi ya kuweza kuionja.

Mheshimiwa Spika, nijielekeze katika hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo. Mimi namshangaa mtu yeyote anayesema kwamba, watu wapunguze mifugo, nadhani huyu mtu haelewi mifugo maana yake ni nini. Mifugo si suala la kupunguza, kama hawana ni vema tukawaelewesha kwamba, mifugo iko namna gani na faida ya mifugo ni nini.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri, ametaja kabisa kwamba, kama sehemu ya MKUKUTA, mifugo inachangia asilimia tano na inategemea

kuchangia mpaka asilimia tisa katika Pato la Taifa. Sasa mtu anayesema kwamba, punguza mifugo, wengine hawajui maana ya mifugo, cha msingi hapa ni namna gani tuweze kuboresha mifugo yetu, si suala la kupunguza mifugo. Sisi tunaotoka katika familia za wafugaji, mifugo ndiyo imetufikisha hapa tulipo sasa hivi. Mimi nilipokwenda sekondari kwa mara ya kwanza, Baba yangu aliuza ng'ombe ndiyo nikaenda sekondari, sasa leo ukisema kwamba, tupunguze mifugo sitaelewa suala hili.

Lakini ni vema Serikali ikajaribu kuweka mipango mahususi, unapozungumzia mifugo weka sambamba na kilimo, ili yote yaweze kwenda kwa pamoja, kwa sababu mtu wa mazingira atasema mifugo inaharibu mazingira, kitu ambacho ni kujaribu kufanya *coordination.* Tushughulikie mazingira na tushughulikie kuboresha mifugo ili iweze kuongeza mchango wake katika maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, nasikitika kuona kwamba, mfugaji hapa nchini anakuwa kama mkimbizi, akienda mahali anakuwa kama mvamizi na mkimbizi, kwa nini huyu mfugaji anaanza kuhukumiwa kwa kosa ambalo Serikali haijamuwekea mazingira mazuri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana kwa sababu ukiangalia hata katika bajeti hii, sioni namna gani mfugaji mdogo, ambaye ndiyo msingi sana, ameweza kufikiriwa katika bajeti hii. Tunaongea kuhusu kuweka ruzuku au kuongeza ruzuku katika suala la kilimo, lakini hakuna ruzuku ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, leo hii mifugo hii hii, kunapotokea matatizo, Mheshimiwa Job Y. Ndugai, amezungumza vizuri sana, ukiwa na shida ya harakaharaka mtu ambaye ni mfugaji, ndiye anakuwa mtu wa kwanza kuchangia na kuweza kuokoa tatizo hilo la dharura, lakini leo hapewi kipaumbele na Serikali.

Mheshimiwa Spika, ningeomba sana suala hili, tujaribu kulipa mtazamo tofauti na vile ambavyo watu tulikuwa tukiliangalia. Ninapenda kuona mfugaji sasa anathaminiwa, anaheshimiwa na anapewa hata msaada na Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingi na hasa Usukumani, pengine mifugo ya Usukumani ni mizuri sana, maana Wamasai walikuwa wanakuja kuiba kuipeleka Arusha. Wamasai walikuwa wanakuja kuiba mifugo ya Wasukuma lakini tukawadhibiti siku hizi hawaibi. Leo hii hebu mtazame kwanza mfugaji ambaye ana ng'ombe wake kati ya kumi hadi 100; kwanza, anatunza familia; pili, anachangia huduma za maendeleo katika eneo husika; na tatu, anaielimisha familia yake. Anasomesha watoto, ahadumia familia yake na mke wake vilevile au wake zake.

Mheshimiwa Spika, huyu mfugaji hana huduma ya ugani, kuna wakati Serikali ilisaidia kukarabati baadhi ya majosho, lakini ukarabati wa majosho hauna maana yoyote, kama hauna huduma zinazoendana na josho lenyewe liweze kufanya kazi kumhudumia huyu mfugaji, hakuna madawa ya kuogeshea wanyama, hakuna dawa za kutibu magonjwa ambayo wanyama hawa yanawakumba. Sasa ni vyema Serikali ikajaribu kuliangalia hili suala kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, hakuna mpango wowote kwa mfugaji katika kuona kwamba, anaelimishwa namna ya kuongeza thamani ya mazao yake. Sasa hivi ukipita katika *Super Markets* nyingi hapa nchini na hasa mijini, unakuta hata nyama inaagizwa kutoka nje ya nchi, tatizo ni kwamba, eti ng'ombe wetu hawana kiwango cha ubora wa kuliwa hapa. Wawekezaji wengi wanakula mazao ya mifugo kutoka nje ya nchi, eti mifugo yetu haina ubora wa kiwango. Lakini sisi wenyewe Watanzania, tunashindwa kuuza *our own products,* Wizara inashindwa kuwa na mkakati kwamba, basi kama ni ng'ombe wanaboreshwa waweze kutoa mazao ambayo yanakidhi haja na viwango vinavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, inatia aibu nchi kama Botswana, ambayo inaishi kwa sehemu kubwa sana, kutegemea pato kubwa la nchi kutokana na mifugo, sisi hapa tuna wanyama wengi sana au tuna mifugo mingi sana, lakini kwa bahati mbaya sana eti haina kiwango cha ubora. Ni nani atakayemsaidia mkulima na mfugaji, kupandisha kiwango cha ubora wa mifugo yetu kama siyo Serikali?

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana suala hili, tuliwekee mkakati maalumu na ningependa katika maelezo yake, Mheshimiwa Waziri, aweze kutueleza kwamba, ana mkakati gani wa kupandisha ubora wa mazao ya mifugo hapa Tanzania? Ni lazima tuwe na mkakati.

Kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, inasema kwamba, tutaboresha ufugaji, tutafanya ufugaji wa kisasa na kadhalika, sasa ufugaji huu ni lazima tuwe na mkakati na mpango mkakati kwamba, tuweze kupima kwamba mwaka huu tumekwenda kwa kiwango gani isije ikawa ni hadithi mpaka miaka mitano ikiisha tunasema kwamba Ilani ya Uchaguzi inasema kuboresha mifugo yetu hapa nchini. Mimi ningeshukuru sana kama Mheshimiwa Waziri, atalizingatia hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini pili, tatizo kubwa la wafugaji ni malisho. Mimi Jimbo langu linapakana na hifadhi ya Serengeti, wakati wa kiangazi kuna wakati wanyama wa Serengeti wanakuja kwenye makazi ya wananchi, wanatafuta maji na malisho, lakini haturuhusiwi kuwawinda, ni lazima tuwaheshimu na warudi salama baada ya kuwa wamekula na kushiba. Lakini sisi mifugo inapokuwa imeathirika kwa sababu ya kiangazi, ikikanyaga tu ndani ya Hifadhi namna hii, wananchi wanamakatwa na mifugo inakamatwa, tatizo ni kwamba, hakuna sera, wala mpango mkakati wa kuhakikisha kwamba, wafugaji wanapewa huduma zinazolingana na ufugaji wao, walau kuchimbiwa mabwawa ambayo yatawasaidia kuweza kupata maji na malisho safi kwa mifugo.

Sasa mwaka 2005 kulitokea janga kubwa sana, kuna baadhi ya maeneo Serikali ilitoa tamko la papo kwa papo kwamba, wafugaji waruhusiwe kuchunga ndani ya Hifadhi ya Serengeti na kuna baadhi ya maeneo na hasa katika Jimbo langu, wafugaji hawakuruhusiwa, walikamatwa na kutozwa faini kubwa sana, sasa hii inakuwa ni *double standard*. Watu wa Bariadi na Maswa, wanaruhusiwa kuchunga kwenye Hifadhi. Waziri alitoa tamko wakati akiwa Waziri kwamba, watu wachunge kwenye hifadhi, sasa kuna maeneo mengine haikuruhusiwa, kwa hiyo, tungeomba kuwe na utaratibu maalumu au mwongozo maalumu, inapotokea janga basi tuangalie, tuweze kulikabili sambamba na sawia.

Mheshimiwa Spika, lingine ni tatizo la ughali wa pembejeo za mifugo, kwa kweli ng'ombe mmoja kuendelea kumtunza ni aghali sana. Sasa hivi watu wanaoshughulika na biashara ya mifugo wanachofanya, wananunua ng'ombe, wanawanenepesha na kuwapakia kwenye malori kwenda kuwauza Kenya na Dar es Salaam, baadhi yao. Lakini sisi watu wa Mkoa wa Mwanza, kwetu ni karibu na soko la Kenya, ni zuri *alhamdulillah,* ukipeleka ng'ombe mmoja si chini ya shilingi 400,000 au shilingi 500,000 unakula.

Lakini ni kwa sababu gani tungeweza kuwa na mpango ambao huyu mfugaji tukimsaidia akajaribu kuboresha zaidi mifugo yake ataweza kutoa mazao ambayo yanalingana na kiwango kinachotakiwa? Bado hii Sheria Namba 5 ya mwaka 1999, haijafanyiwa kazi na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo, isaidie wananchi na wafugaji kutenga maeneo ya kuchungia, ambayo kweli yatawasaidia sana kuweza kupata malisho na kuweza kuhakikisha kwamba, mifugo hii inaweza kuwa bora zaidi.

Mheshimiwa Spika, watu wa mazingira wanasema kwamba, tutunze mazingira na tusiharibu mazingira. Lakini ukiangalia utitiri, Mheshimiwa Job Y. Ndugai, alizungumza hapa sasa hivi, kila mahali kandokando ya barabara kulia na kushoto, watu wanajenga nyumba, wanaweka vijiji na kadhalika, huu utaratibu unaathiri mazingira kwa kiwango kikubwa sana, kuliko mfugaji anapokuwa anatafuta malisho ya ng'ombe wake. Kwanza, akipeleka ng'ombe kwenye malisho, yule ng'ombe anapokuwa anajisaidia ile ni mbolea, inarutubisha ardhi lakini huyu mkulima mdogo yeye atakata miti na kuweka makazi. Ni vyema basi hii Sheria tujaribu kuiangalia vizuri zaidi, tutenge maeneo mahususi ya kuwasaidia wakulima, waweze kupata malisho bora na maji bora, kwa ajili ya mifugo yao.

Mheshimiwa Spika, mimi bado sijapata mantiki, napenda kupata maelezo, kuna Chuo cha Machinjio hapa Dodoma na mimi sijui Serikali ilitumia kigezo gani kukiweka hapa nyuma tu ya hili Jengo la Bunge, kuna chuo cha kujifunzia mambo ya machinjio. Nilidhani chuo kama hiki, kingewekwa mahali ambapo ni karibu na mifugo na siyo hapa, kisaidie zaidi kazi ya kuboresha suala la machinjio ya mifugo.

Sasa sijui, labda Mheshimiwa Waziri anipe maelezo, hiki chuo kinafanya nini?

Toka nimekaa hapa sioni ng'ombe wakipelekwa pale, kimekaa tu, sioni nyama inayotoka pale, sioni wanafunzi wanaofundishwa pale, sasa dhamira ya kuweka chuo hiki hapa ilikuwa ni nini?

Ninaomba Mheshimiwa Waziri, anipe maelezo juu ya suala hilo.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni suala zima la wafugaji. Mimi naomba Watanzania wote tuelewane, ukiona Msukuma amekwenda Rukwa kutafuta malisho, basi aheshimiwe, asionekane kama ni mkimbizi. Hali ya kuwa tunafukuzana fukuzana, hii ni nchi yetu, hakuna mtu ambaye ana hati miliki ya nchi hii, hati miliki ni ya Watanzania wote. Katiba inasema kwamba, Mtanzania aende mahali popote na aishi mahali popote,

ilimradi havunji sheria.  Sasa hii sheria ya kusema kwamba, mtu anatoka Mwanza au Shinyanga kwenda Rukwa, anaonekana ni mkimbizi, eti amekuja na kundi kubwa la ng'ombe, hii tuachane nayo.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali iweke utaratibu mahsusi wa kutuongoza sote. Nina imani kwamba, Watanzania wote tunapendana, suala la kubaguana kwamba, huyu ni mfugaji na huyu ni mkulima, hii biashara iishe.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda basi niunge mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo. Lakini napenda nipate maelezo ambayo nimetaka kuyapata. Katika majumuisho yake Mheshimiwa Waziri ni vyema nikasikia kauli yake inasemaje.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na ninampongeza Mheshimiwa Margareth S. Sitta, kwa kuwa na *birthday* leo.  Ahsante sana.  *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge ahsante na pia tunashukuru kwa pongezi hizo, tunazipokea.  Sasa ni ule muda wa ubia, zile dakika 15, kati ya Mheshimiwa George M. Lubeleje na Mheshimiwa Gosbert B. Blandes.  Tunaanza na Mheshimiwa George M. Lubeleje.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie machache, kuhusu Wizara ya hii ya Maendeleo ya Mifugo. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, watumishi wote na wataalam wa Wizara hii, wanafanya kazi nzuri katika mazingira magumu sana. Nimeona bajeti yao ya mwaka 2006/2007, ni shilingi bilioni 22.2, fedha ambazo kwa kweli ni kidogo. Naomba kwenye bajeti ijayo, Wizara hii iongezewe fedha.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda nimjibu Mheshimiwa Mbunge, pamoja na kwamba, mimi sitakiwi kumjibu, lakini kujenga machinjio ya kisasa Dodoma ni muhimu, kujenga Chuo Kikuu Dodoma ni muhimu.  Kwa hiyo, watani zangu Wasukuma, naona mngetuunga mkono tu.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nimesimama kuzungumzia mambo mawili au matatu. La kwanza, ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa jibu zuri alilojibu wiki iliyopita.  Jibu la swali namba 253 la kuomba Serikali ipandishe hadhi Kituo cha Utafiti wa Mifugo  Mpwapwa na kuwa Taasisi ya Kitaifa.  Kwa hiyo, hili nampongeza sana Mheshimiwa Waziri.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema siku ile, wakati nauliza  swali la nyongeza, ni kwamba, Kituo hiki kina historia ndefu na mwaka 2005 kulikuwa na sherehe kubwa sana ya kutimiza miaka 100 ya Huduma za Kituo cha Mifugo Mpwapwa.  Kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, lakini Kituo hiki kinakabiliwa na matatizo makubwa; kwanza, kama nilivyosema, ni Kituo cha miaka mingi, tangu mwaka 1905. Kwa hiyo, kinatakiwa kiboreshwe, kinatakiwa ukarabati wa majengo, tuna *dairies* kwa ajili ya kukamua, kwa hiyo, zinatakiwa zifanyiwe ukarabati, lakini vilevile kuongeza idadi ya mifugo. Mifugo iliyopo sasa ni michache, kwa suala zima la utafiti kwa sababu kituo hicho kitakuwa ni taasisi ya utafiti. Mimi nina uhakika tukiongeza idadi ya mifugo, utafiti utafanyika vizuri zaidi.

Lakini vilevile tuna tatizo la vitendea kazi kama vile magari, yaliyoko pale yamechakaa ni ya Mradi wa *TAPR II* mwaka 1996, kwa hiyo yamechakaa. Naomba mhakikishe kwamba, tunapata vitendea kazi kama magari ya kutosha. Pia wataalamu hasa watafiti, kwa kuwa sasa hivi inakuwa ni Taasisi, kwa hiyo, wanatakiwa watafiti wa kutosha ambao wamebobea katika mambo ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, niingie kwenye suala la kudhibiti magonjwa ya mifugo. Yapo magonjwa ambayo yanaweza kuzuilika, tunayaita *vector born diseases* kwa mfano, magonjwa ya kupe. Ng’ombe anakufa eti kwa sababu ya kutoogeshwa ni aibu kubwa sana. Kwa hiyo, naomba kama walivyoshauri Waheshimiwa Wabunge wenzangu, lazima tuhakikishe kwamba, tunakarabati majosho.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya kazi nzuri sana, kuhusu Mpango wa MMEM, imetafuta fedha tumekarabati shule na kujenga madarasa karibu katika Vijiji vyote. Serikali inashindwaje kutafuta fedha ili kukarabati majosho yote katika nchi nzima? Hakuna haja ya kutupiana mpira, ni Halmashauri. Halmashauri zote ziko chini ya TAMISEMI na TAMISEMI ni Serikali, sasa kwa nini tusikarabati majosho? Kwa hiyo, naomba majosho yakarabatiwe yote, halafu yakabidhiwe kwenye Halmashauri na wananchi waweze kuyaendesha. *(Makofi)*

Lakini vilevile bei ya madawa ya mifugo ni gharama kubwa sana. Dawa ya kuogeshea ng’ombe ni fedha nyingi sana na madawa ya chanjo. Kwa hiyo, wafugaji wa kawaida, hawana uwezo wa kununua madawa hayo. Kwa hiyo, vilevile Serikali iangalie jinsi ya kupunguza bei ya madawa ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, lingine kuhusu mabwawa na malambo. Huwezi kuboresha mifugo kama hakuna mabwawa na malambo, hiyo mifugo itapata wapi maji. Kwa hiyo, naishauri Serikali, iweke mikakati kuhakikisha kwamba, maeneo yote kame na maeneo yote ya wafugaji, mabwawa pamoja na malambo yachimbwe ili kuhudumia. Mabwawa na malambo yatasaidia mifugo pamoja na binadamu.

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru sana Serikali kwa kujenga machinjio ya kisasa Dodoma, maana sasa hivi Vijijini watu wanakula nyama bila ya kukaguliwa. Lazima tuwe na wataalamu wa mifugo katika kila kijiji, tuongeze idadi ya wanafunzi katika Vyuo vya Mifugo. Nyama ni hatari, kuna magonjwa yanaua sana kwa mfano, *anthrax*, ni ugonjwa mbaya sana. Ukishapata *anthrax* kwa mfano, maana yale magonjwa yako kwenye kundi la *communicable diseases,* ambayo yanaweza kuwa *transmitted* kutoka kwa mnyama kwenda kwa binadamu, unapata kimeta kwa kula nyama au kwa kulala

kwenye ngozi. Kwa sababu *conservative agents,* ambayo tunaita *bacillus anthracis,* hata ukilalia ngozi, unapata ugonjwa. Kwa hiyo, nashauri, chanjo iendelee kwa hayo magonjwa ambayo yanaweza kuzuilika. Lakini vilevile tuwe na wataalam wa mifugo katika kila kijiji.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya kutenganishwa Bwana Shamba na Bwana Mifugo, lakini mimi ninavyojua, huwezi kujifunza *Agriculture* bila kujifunza *Livestock*. Unapojifunza mifugo, lazima ujifunze na mambo ya kilimo vilevile, maana kuna mambo ya malisho ya mifugo na unapojifunza *Livestock* lazima ujifunze na kilimo kidogo. Kwa hiyo, kwa mfano, Afisa wa Kilimo na Mifugo wa Wilaya ya Mpwapwa, yeye ni mtaalamu wa mifugo, lakini kwa sababu yote yanakwenda pamoja, kuyatenganisha itakuwa ni kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni kwamba, vituo vyetu vya utafiti, vitumike vizuri ili kuhakikisha kwamba, tunaboresha hali ya ufugaji katika nchi hii. Hali ya ufugaji wetu bado ni ya kizamani, tunataka tuwe na makundi mengi, lakini ng'ombe sio bora, watu waelezwe wale nyama, nyama ni aina mojawapo ya *animal protein*, kwa hiyo inajenga mwili. Tuwaelimishe wananchi wale nyama, maana sisi zamani hata ukimwambia mzee tunaomba mbuzi tule, anasema haiwezekani, mpaka ng'ombe afe au mpaka mbuzi afie kwenye zizi ndiyo watu wanakula. Lakini tuwashauri watu wale nyama na wanywe maziwa, wakishakunywa maziwa mwili utajengeka na utakuwa na afya nzuri.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, naishukuru Wizara, ilikuwa na matatizo makubwa sana hasa ya kupandisha vyeo watumishi. Kituo cha Utafiti Mpwapwa, Kituo cha Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo pale Mpwapwa, watumishi walikuwa wanalalamika sana juu ya upandishwaji wa vyeo, pamoja na marekebisho ya mishahara. Hivi sasa mambo hayo Serikali imejitahidi, wamebakia watumishi wachache sana kupandishwa vyeo na marekebisho ya mishahara ni haki ya kila mtumishi. Kwa hiyo, nilikuwa naishauri Serikali, iendelee kuwapandisha vyeo watumishi wa Wizara hii, ili waweze kuboresha hali ya utendaji kazi katika Sekta hii ya Mifugo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunipa nafasi na ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa George M. Lubeleje, nami nakushukuru sana kwa ustaarabu ulioonesha kumpa nafasi mwenzio. Sasa namwita Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mbunge wa Karagwe, ni dakika nane. Dakika sita kengele italia, utamalizia dakika mbili.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya dakika nane na mimi nitajitahidi kuzitumia vizuri. Kama wenzangu waliotangulia, nami nampongeza Mheshimiwa Margareth S. Sitta, kwa siku yake ya kuzaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, kabla sijaendelea, naunga mkono hotuba hii ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo. Vilevile naipongeza Serikali kwa kazi kubwa sana waliyoifanya ya kurudisha wafugaji haramu kutoka Uganda na Rwanda, ambao walikuwa wanakalia ardhi ya Karagwe kwa mabavu. Vilevile naiomba Serikali, kwa wale ambao bado wanang'ang'ania kubaki kwenye ardhi ya Karagwe, ijitahidi sana kuwaondoa wote na kuwamaliza.

Mheshimiwa Spika, wakati wananchi wa Karagwe wanasherekea na kufurahia kwa kuondoka wahamiaji na wafugaji haramu katika ardhi ya Karagwe, limejitokeza tatizo kubwa sana, nalo ni kwamba, hao ndugu zetu kutoka Uganda pamoja na Rwanda, ambao wameondolewa Karagwe, wamerudi kwa njia nyingine ya kulipiza kisasi. Hao watu sasa hivi wanakuja na silaha za kisasa na wanakuja wanavamia na kuiba mifugo yetu. Wanakuja wakati wa usiku, wanaingia kwenye sehemu ambazo mifugo imetunzwa, wanaswaga zizi zima. Wakati mwingine wanakuja mchana kwa sababu kinakuja kikosi kizima, kina silaha za kisasa, kinavamia wachugaji, wanawanyang'anya mifugo yao, wanakimbia nayo kuipeleka Rwanda.

Mheshimiwa Spika, ninavyozungumza hivi sasa, usiku wa kuamkia leo, ng'ombe zaidi ya 300 wameibiwa kule Karagwe. Hivi ninavyozungumza ni kwamba, wananchi wa Karagwe wako porini wakipambana na hayo majambazi kutoka nchi ya Rwanda. La kusikitisha ni kwamba, leo wamenitumia ujumbe kwa njia ya simu wakiwa porini, wanasema kwamba, tayari wameshazingira hao wezi, lakini wanasema wana silaha kali mno na Askari wetu kutoka pale Wilayani Karagwe Kayanga, hawatoshi na hakuna Askari wa kuweza kuwasaidia. Sasa wamenitumia ujumbe, wakiniomba mimi kama Mbunge wao, niweze kutafuta njia ya kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi njia yangu ni kumwomba Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana na hasa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo, ashirikiane na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Waziri wa Usalama wa Raia. Kwa kuwa tunafahamu kwamba, ni wajibu wa Serikali kulinda wananchi na mali zao, ninaomba sana sana kwamba, Serikali iweze kulifanyia kazi suala hili haraka sana na ikiwezekana watume kikosi cha Askari kuanzia leo, kiende kuwasaidia wananchi wa Karagwe, ambao wako porini wanatafuta mifugo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo la wizi wa mifugo katika Wilaya ya Karagwe, limekuwa ni la muda mrefu na sugu. Serikali imekuwa ikikwepa sana jukumu hili, kwa sababu mifugo yote ya Wilaya ya Karagwe, imehamia Rwanda kwa njia ya wizi. Sasa mimi nafikia mahali nashindwa kuelewa kwamba, hii Serikali yetu ya Tanzania, kila mara tunaipiga kelele jamani mifugo ya Karagwe inaishia Rwanda, hizo takwimu wanazo na hizo kelele wanazisikia, lakini nashindwa kuelewa ni kwa nini Serikali inapata kigugumizi cha kuweka mikakati imara na ya kudumu ya kuweza kusimamia na kupambana na wimbi la wezi wa mifugo kutoka Rwanda?

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine nashawishika kusema kwamba, sijui Serikali inaogopa Wanyarwanda, ndiyo maana wanashindwa kupambana nao huko porini. Sasa wananchi wa Karagwe wamenituma na wameniomba kwamba, kama

Serikali inapata kigugumizi, basi iwape silaha za kutosha wananchi wa Karagwe ili wao wenyewe, waweze kupambana na kulinda mifugo yao. Kwa sababu wale wenzetu wa Rwanda, wanakuja na silaha za kisasa na tunapata shida ya kupambana nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wiki iliyopita, kuna bwana mmoja anaitwa Telesphory Batulumayo, aliibiwa ng'ombe 70 mpaka sasa hivi hawajapatikana. Bwana mwingine anaitwa Mathias Paulo Tinkasimile, aliibiwa ng'ombe 65, bwana mwingine anaitwa Andrew Kazimoto, aliibiwa ng'ombe 90 na wengine wengi wameibiwa ng'ombe wao.

Mheshimiwa Spika, sasa naiomba sana Serikali, namwomba sana Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana, kwa sababu Wizara yake ni ya Maendeleo ya Mifugo, asije akaishia kuwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo, ambapo mifugo imehamia katika nchi jirani, mwisho atabakia kuwa Waziri ambaye hana mfugo hata mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mapendekezo yangu na maombi yangu kwa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo, kwa kushirikiana na Wizara ya Usalama wa Raia, naomba kwa haraka sana, watume kikosi cha kuokoa mifugo yetu ambayo iko porini na karibu inavushwa kuelekea nchi ya Rwanda.

Lakini vilevile Askari wetu wa Karagwe, waongezewe nguvu, waweze kufukuza hata ile mifugo ambayo tayari imeshaingia katika nchi ya Rwanda. Kwa kuwa Sheria inaruhusu kama mtu amekuibia mifugo yako au mali yako kumfukuza mpaka nje ya mipaka ya nchi yako, mpaka uingie ndani ukatafute mali yako.

Mheshimiwa Spika, vilevile naiomba Serikali, wakati umefika wa kuweka kikosi imara sana, ambacho kitakaa kwenye Pori la Kimisi ambayo ni hifadhi ya wanyamapori, ambayo ndiyo njia ya wezi wanakopitia na hakuna watu wanaokaa katika hilo Pori. Sasa Serikali iweke kikosi imara, kitakacho-*patrol* kwa saa 24 na kwa muda wa mwaka mzima, sio wakati wizi unapotokea na Askari wetu waweze kuwa na vifaa vya kutosha na kulinda mifugo ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, ninaomba nikumbushe kwamba, kuna majosho mengi sana pale Wilayani Karagwe, yalishaharibika zaidi ya miaka 10 au 15, hayafanyi kazi, sana sana tumebaki na mapaa tu, ambapo na mabati yake yamechakaa. Naiomba sana Serikali, ije ifufue majosho hayo na tuweze kuyatumia kuogeshea mifugo yetu. Vilevile tunayo maziwa ya kutosha, lakini hatuna soko hata kiwanda kidogo. Tunaiomba sana Wizara ya Maendeleo ya Mifugo, itusaidie kujenga viwanda vidogo vidogo kwa ajili ya kuuza maziwa yetu.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, ng'ombe wa Karagwe wanazidi kuongezeka, lakini tunahitaji sana mbegu ya ng'ombe wa kisasa, kwani hatuna kituo cha mbegu za ng'ombe wa kisasa, cha kuweza kuzalisha ng'ombe wazuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, narudia tena kusema kwamba, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya mwisho mchana huu, niweze kuchangia hoja ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo.

Mheshimiwa Spika, kwanza na mimi napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa kweli kwa kuifanya hii Wizara iwe ni Wizara kamili inayojitegemea. Huko nyuma ilikuwa imewekwa kwenye Kilimo na halafu ikawekwa kwenye Maji, kwa hiyo ikawa imekosa msimamo mzuri. Lakini nadhani sasa itapata msimamo kwa sababu inajitegemea.

Mheshimiwa Spika, lakini pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Charles O. Mlingwa, Katibu Mkuu na Wataalamu wote wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo.

Mheshimiwa Spika, inaonekana sasa Mheshimiwa Rais, katika kuipa uzito Wizara hii, inaongozwa na wasomi, kwa kweli wote wale ni Madaktari. Nafikiri Mheshimiwa Rais, amefanya makusudi mazima kwamba, baada ya Wizara hii kuyumba yumba kwa muda mrefu kidogo, sasa ikafanywa kuwa Wizara kamili na kuwapa wasomi waliobobea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina hakika sana kama mifugo ni fani waliyoisomea, lakini ni wasomi waliobobea. Zaidi ya hayo ni kwamba, watu wenyewe ninavyowaona mimi na kwa *assessment* yangu, kwa kweli ni wapole na watu wanyenyekevu sana. Sasa nakuwa na matumaini makubwa kwamba, watasikiliza wafugaji na watajaribu kutatua matatizo yao. Kwa sababu wafugaji kwa kweli hawana elimu kubwa kama wao, kwa maana ya *formal education*, lakini wana uzoefu mkubwa wa mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina mashaka na nilivyo wa-*assessment* kwamba ni wanyenyekevu na wapole, nina hakika watatusaidia kupitia pia kwa viongozi mbalimbali, hasa Waheshimiwa Wabunge na viongozi wa wafugaji wa ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, wafugaji kwa kweli kama walivyo makundi mengine katika nchi yetu, wana matatizo mengi. Moja, ni ukosefu wa maji katika maeneo ya wafugaji. Hili limeshazungumzwa sana na sina haja ya kulirudia. Nataka kuendelea tu kulitilia mkazo kwamba, katika maeneo ya wafugaji, kwa kweli suala la maji lina matatizo makubwa sana. Tunaweza tukawa na malisho mazuri, lakini maji yakawa ni tatizo. Kwa mfano, kule Ngorongoro, kulikuwa na utafiti fulani ulioendeshwa kuhusu majani ya aina fulani, sisi tunayaita makutiani. Ni majani magumu sana yamemaliza meno ya ng'ombe, kwa hiyo, ng'ombe wamekuwa vibogoyo kabisa. Lakini sasa utafiti unaendelea kufanywa na *Sokoine Univeristy of Agriculture*, lakini matokeo bado hatujapata kwamba, sasa *alternative* itakuwa ni nini.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka niliseme ni kwamba, kule kwangu Ngorongoro maeneo ya mbugani, sehemu tambarare, sehemu kama za Olebalubalu, Kiloki, Engejumiro, Osere, Kakesyo, Osinoni, Masusu, maeneo mbali mbali, ni tambarare, lakini ni makame sana. Nasikitika ya kwamba, katika kitabu cha

hotuba ya Waziri, sioni hata lambo moja limewekwa katika maeneo yale. Mimi ombi langu ni kwamba, mtukumbuke kwenye ufalme wenu wa kutusaidia malambo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, mkitaka wafugaji wasiendelee kuhama hama, jamani wekeni maji kila mahali. Tuna malisho lakini tuna matatizo ya maji, wekeni maji kila mahali na tunawaahidi kwamba, hatuwezi kuhamahama. Mifugo yetu itakula majani hapo, itaondoka itakwenda sehemu nyingine, lakini ni marufuku mifugo kuja kula majani ambapo mifugo imeondoka. Kwa hiyo, *by the time* tunamaliza eneo letu kubwa la malisho, huku kwingine kunakuwa kumeshaota majani, kwa hiyo tunarudi. Kwa hiyo, ni mambo ya *zone* na ni utaalamu sana. Mimi nawashangaa watu wanaosema tunahama hama na tunaharibu mazingira, si kweli.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kulisemea ni yale maeneo yenye ukame, tukishajengewa mabwawa na tukichimbiwa visima virefu na vifupi, kwa ajili ya maji ya binadamu, kwa kweli tutakaa kwenye maeneo na tutatumia maeneo yetu vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, lingine nije kwenye magonjwa ya mifugo. Nashukuru kwamba, suala la magonjwa ya mifugo limezungumzwa sana, lakini mdudu kupe ndiyo kwa kweli anasababisha magonjwa mengi ya mifugo. Tukiweza kumdhibiti kupe, kwa kuweka majosho katika maeneo ya mifugo na yawe majosho ya kutumbukiza mifugo ili iogeshwe kikamilifu, mifugo inaweza ikaongezeka, baadaye na sisi tutaiboresha mifugo yetu katika hali ya kisasa ambayo inatakiwa.

Mheshimiwa Spika, kule Ngorongoro napenda pia niwashukuru, kuna Mradi mmoja unaitwa *ERETO,* lakini kwa Kiingereza wanauita *Ngorongoro Pastoral Project*. Hawa wametusaidia katika sehemu tatu; wamesaidia *veterinary services*, wamesaidia *livestocking* kwa upande wa mifugo na wamesaidia mambo ya maji *(water services).* Lakini bahati mbaya sana, miradi ya namna hii inakuwa ya muda, inafika mahali basi wanamaliza muda wao wanaondoka.

Mheshimiwa Spika, lakini nashukuru kwamba, wameingia *Joint Venture* na Serikali ya Tanzania kwamba, kuna kiasi fulani cha fedha, Serikali ya Tanzania inatoa na hii Serikali ya Denmark inatoa kwa ajili ya kuwasaidia watu hawa.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro, wanashughulikia zaidi magonjwa ya mlipuko. Lakini nilikuwa nataka kuuliza kwa sababu kule Serengeti kuna *Research Instutite* moja, inayoshughulikia wanyamapori inaitwa *TAWIRI.* Sasa kwa sababu nilishasema wanyamapori na mifugo kwa kiasi fulani wanategemeana, hiyo *Research Centre,* ambayo ni kubwa, nzuri na ina zana mbalimbali, kwa nini nayo isitafiti magonjwa ya mifugo?

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni huduma za mifugo. Kama nilivyosema, mifugo ni kila kitu kwa mfugaji; ni chakula kwa sababu inatengeneza mahitaji mengine yote muhimu ya binadamu, ni elimu kwa maana ya wanauza mifugo yao wanawapeleka watoto shule, ni mtaji na ni kitu cha thamani, kwa

hiyo ni maisha kwa ujumla. Kama kilivyo kilimo kwa mkulima na kama ilivyo biashara kwa mfanyabiashara, kama ilivyo mshahara kwa mtumishi wa Serikali na kama ilivyo uvuvi kwa mvuvi, ni maisha. Kwa hiyo, ufugaji ni maisha ya hao wanaofuga. Kwa hiyo, naomba huduma hizi ziendelee kutolewa na zifike mpaka vijijini waliko wafugaji wenyewe kama Mheshimiwa Mbunge mmoja alivyosema. Huduma za ugani, waganga wa mifugo na madaktari wa mifugo, wawepo katika maeneo ya wafugaji ili waweze kutoa misaada mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka nilisemee ni maeneo ya wafugaji kutengwa bayana na kwa sheria na yakishatengwa yawekewe sheria kama ilivyo sheria isimamiwe na sisi tunaotoka katika maeneo yale tutasaidia kusimamia sheria hizi. Lakini kamwe maeneo haya yakishatengwa, yasitolewe tena kwa wawekezaji, yabakie ni maeneo ya wafugaji, yasitolewe tena kwa wakulima wala wawekezaji wa aina yoyote ile na wala yasifanywe tena maeneo ya wanyamapori au vitalu tena vya wawindaji, yabakie ni maeneo maalum kwa ajili ya wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika maeneo hayo, nitaomba yakishatengwa hivyo, miundombinu mbalimbali iweze kuwekwa katika maeneo yale kama vile maji, *veterinary services,* majosho na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie habari ya minada. Mimi ninaomba sana Mheshimiwa Waziri, nina kijiji changu kinaitwa Ngarisero, uanzishwe mnada kubwa kabisa wa Kimataifa katika eneo lile. Huko nyuma wakati wa ukoloni, kulikuwa na Mradi mmoja mkubwa kule Holala, ulikuwa unazuia mifugo yote kutoka Tanzania isiende Kenya. Kwa sababu bei ni nzuri na kuna kila aina ya miundombinu. Sasa hiyo imekufa, miaka yote hiyo hakuna tena kitu chochote pale. Kwa sababu Holala na hapo Ngarisero si mbali, naomba mnada mkubwa uanzishwe pale ili tuweze kukamata hilo soko la mifugo na kuzuia mifugo yetu isiendelee kwenda Kenya.

Mheshimiwa Spika, kuna utafiti mdogo ulifanyika pale Arusha, katika mabucha 120 yaliyofanyiwa utafiti, kila siku kwa muda wa wiki mbili, walikuja kugundua kwamba, wanauza nyama ya ng'ombe, mbuzi na kondoo asilimia 97. 5, hii ni nyama nyingi sana kwa Mji wa Arusha pekee. Sasa na hii nyama yote inatoka kwa wafugaji hao wadogo wadogo, ambao ninyi mnataka waendelee kuhangaika tu. Sasa naomba sana, kiwanda kijengwe kwa ajili ya kusindika nyama na mazao ya mifugo kule au kukata nyama ili tuweze kupata soko la ndani na hatimaye kuweza kujitosheleza kwa nyama kwa upande wa soko la ndani.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nizungumzie kidogo ulinganisho kati ya uharibifu wa mazingira, unaotokana na kilimo na unatokana na mifugo. Kwanza, wafugaji hawakati miti, katika kutengeneza maboma yao yale wanakata matawi. Kwa hiyo, ule mti mkubwa unaendelea kukua tu kwenda juu. Wanakata matawi yale ili kutengeneza maboma yao, kwa hiyo sio uharibifu wa mazingira hata kidogo. Wanakata hayo matawi kutengenezea nyumba hizo za muda, maana leo wapo hapo, kesho wanaondoka, lakini kwa nia njema kabisa. Pia hawafyeki misitu, kama kilimo ambavyo kifanyika. Mkitaka kufungua mashamba, mnafyeka miti mikubwa na midogo, *you clear the earth* yote hiyo.

Kwa hiyo, hawa hawafanyi hivyo, wafugaji pia hawachomi mkaa na katika kuhama hama huku, wanajaribu kutoa nafasi kwa ardhi ku-*regenerate* tena. Sasa ni kama unavyoacha kulima shamba lako kwa muda wa mwaka mmoja au miaka miwili, ardhi inapata rutuba tena wakati mwingine ukija kulima. Ndivyo hivyo tunavyofanya sisi wafugaji. Kwa hiyo, naomba msiendelee kutuhukumu kwa jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda niseme mpaka sasa kwa kweli hakuna utafiti wa kisayansi, uliofanyika wa kuthibitisha kwamba, huu uchungaji au huu ufugaji tunaofanya sisi, unaharibu mazingira. Badala yake hao ng'ombe wanapopita, wanaacha vinyesi ambavyo ni mbolea, inasaidia ardhi tena kurutubika. Kwa hiyo, naomba suala hili kwa kweli litazamwe upya kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninachosema kuendelea kuwalaumu wafugaji hawa kwamba, wanaharibu mazingira kwa kweli siyo sawasawa. Naomba pia Mheshimiwa Waziri, atekeleze mambo ambayo yamezungumzwa katika Ilani ya Uchaguzi ukurasa wa 29 mpaka 31 kuhusiana na mifugo, tukifanya hivyo kwa kweli hii Sekta ya Mifugo itaboreka zaidi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa kusitisha Shughuli za Bunge kwa mchana huu umewadia. Nakumbusha tu kwamba, saa 11.00 jioni nitamwita Mheshimiwa Michael L. Laizer, saa 11.15 nitamwita Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya na saa 11.30 msemaji wa mwisho atakuwa ni Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka. Baada ya hapo saa kumi na mbili kasorobo, nitamwita Naibu Waziri kwa robo saa tu. Halafu mtoa hoja Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo, kwa saa moja kuanzia 12.00 hadi 1.00 usiku na hapo tutaingia kwenye Kamati ya Matumizi kwa dakika 45.

Baada ya kusema hayo, kwa sababu muda umewadia, naomba kusitisha Shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, kutoa mawazo yake, nina heshima na furaha kutangaza kwamba, kwenye *Speaker's Gallery,* tunaye mgeni mashuhuri Mheshimiwa Zakaria Dominick Muhuri Mhita, ambaye ni Balozi wa Kenya anayeaga, Balozi wa Kenya hapa nchini amefika kuja kutuaga. Amefuatana na Afisa wa Wizara yetu ya Mambo ya Nje.

Ahsante sana, Mheshimiwa Balozi, umeitumikia nchi yako vizuri sana hapa Tanzania, tunakutakia mema huko unakokwenda. Karibu sana. *(Makofi)*

Nimepata *note* sasa hivi, siku nyingine mambo haya nitakuwa siyasemi maana yake yamechokoza mambo. Kumbe leo pia ni siku ya kuzaliwa ya Mheshimiwa Dorah H. Mushi, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Manyara. Hongera sana Mheshimiwa Mushi. *(Makofi)*

Sasa namwita Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, atafuatiwa na Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya na pengine tutamfikia Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nitoe mchango wangu katika Wizara hii ya Mifugo. Kwanza, natanguliza kusema kwamba, kwa kweli nampongeza sana Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuunda Wizara hii muhimu sana kwa wafugaji. *(Makofi)*

Nawapongeza tena Mawaziri wote wawili, Katibu Mkuu, pamoja na Naibu Katibu Mkuu, wote ni Madaktari, kwa hiyo nategemea kwamba, Wizara hii itakuwa na ufanisi mkubwa. Wameanza vizuri kwa sababu naona wamesikiliza mawazo ya wadau, nawapongeza kwa hilo. Nimesoma hotuba yenu, lakini ningependa kusema kwamba, hotuba imeelekeza sana yaliyofanyika mwaka 2005/2006, machache sana mmeweka yatakayofanyika mwaka 2006/2007, ambayo sisi tuliyategemea sana yale yamekwishapita.

Mheshimiwa Spika, nataka kujielekeza katika mambo mawili kuhusu mifugo na kuhusu wafugaji wenyewe. Mifugo ni zao kubwa linalotegemewa na wananchi wengi. Kwa hiyo sio zao dogo, ambalo linaweza likabakizwa nyuma, ni zao ambalo ni uchumi kwa watu wengi. Wengine tukisikia mkisema kwamba, punguzeni mifugo, tunaona ni kosa kubwa, hatuwezi kuwaadhibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia pale Dar es Salaam, watu wameshindwa kufanya kazi, ofisini wengine wanakwenda saa 11.00 asubuhi akichelewa mpaka saa 12.00 au saa 1.00, hatakwenda tena kwa ajili ya wingi wa magari. Magari yamejaa bandarini, bado yanakuja kuongeza magari yaliyoko Dar es Salaam, lakini sikusikia mnasema kwamba, magari yasiagizwe, bado mnaongeza magari lakini mnasema punguzeni mifugo, ongezeni kilimo. Mwenye eka 10 aongeze eka 100 na maeneo hayo ni ya wafugaji, ndio mnawaambia kwamba, waende kupora maeneo ya wafugaji. Mimi nasema mnataka kupunguza mifugo kwa njia nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mifugo ina mahitaji mengi sana, inahitaji malisho ya kutosha, inahitaji maji ya kutosha wakati wote wa masika na kiangazi, inahitaji madawa yanayohitajika katika magonjwa yanayoikumba mifugo, lakini nashangaa hakuna utaratibu wowote wa kupata hayo madawa. Kwa hiyo, wanahitaji masoko kupata haya madawa, wanahitaji masoko, wanahitaji wataalamu, lakini wataalamu vijijini hakuna, kwenye kata hakuna mtaalamu wa mifugo mpaka Wilayani unakwenda kumkuta mmoja na huyo mmoja ana *base* sana upande wa kilimo. Kwa hiyo, ni upungufu mkubwa sana. Hata elimu kwa wafugaji, nani atawapa elimu wafugaji kama hakuna wataalamu. Naomba suala la wataalamu lizingatiwe sana.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepunguza au imefuta kabisa kodi ya madawa ya mifugo, lakini toka ilipofutwa kodi wanaofaidika ni wafanyabiashara wanaoingiza madawa ya mifugo. Kwa sababu bado madawa ni bei ghali, wafugaji hawawezi kununua. Nitoe tu mfano, *Dominics* lita moja ni shilingi 60,000, *bytical* lita moja ni shilingi 80,000, *superdeep* lita moja ni shilingi 65,000, *Decatic* lita moja ni shilingi 60,000, halafu tunasema kwamba tumesamehe ushuru wa madawa. Bado madawa ni ghali sana, Serikali imefaidisha wafanyabiashara na hakuna chombo chochote kinachoangalia kwamba, haya madawa baada ya kusamehewa kodi ni kweli wafugaji wanapata kwa bei nafuu, hakuna.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali itoe madawa kwa kila josho, lita 200 ya dawa za kuogeshea mifugo. Lita 200 kwa kuanzia ili vijiji vianze ku-*charge* mifugo inapoingia kwenye josho. Kwa hiyo, Serikali ianze kununua madawa kwa kila josho lililopo. Madawa mengine yanayohitajika ni madawa ambayo hayapatikani kwenye maduka. *ECF*, wafanyabiashara hawanunui dawa hiyo. Dawa ya ugonjwa wa miguu na midomo, hakuna madukani. Tunaomba Serikali inunue kila mwaka, wafugaji wapate madawa hayo kwa sababu ndigana ndiyo inapunguza mifugo kwa wingi sana hasa ndama wanapozaliwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuuliza kwamba, tulipata *amendmen*t ya Wizara hii majuzi tu kwamba, dawa ya mifugo sasa wamegawa ni shilingi bilioni 2.2. Lakini katika kitabu cha Waziri, ameandika hapa ni shilingi milioni 500. Sasa hizo shilingi bilioni 2.2 zimetoweka wapi? Juzi, jana na leo, zimeenda wapi na *amendment* tunayo, imekuwaje? Naomba tupate ufafanuzi, hamuwezi mkatudanganya halafu mtuambie tena mahesabu ya ajabu ajabu.

Dozi 120,000 ya Ndigana kwa mikoa 14, hivi jamani yaani mimi naona mnacheza, mnatufurahisha tu. Mikoa 14 kwa dozi 120,000, inatosheleza Wilaya ya Monduli tu. Sasa hapa imeandikwa ni kwa ajili ya mikoa 14, jamani yaani leo nimegundua kabisa kwamba, mnapunguza mifugo kwa njia hii na mahitaji yote yanayohitajika hakuna kitachopatikana pale.

Mheshimiwa Spika, zamani kulikuwa na Kitengo, ambacho kilikuwa kinashughulikia masoko ya mifugo *(TLMP),* siku hizi hakipo. Naomba kuuliza tu mbadala wa chombo hicho ambacho kilikuwa kinashughulikia minada yote masoko ni nini? Mmeunda chombo gani kwa ajili ya kushughulikia na kufuatilia masoko ya mifugo? Naomba majibu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia Soko la Afrika Mashariki. Nilitegemea kwamba, soko hili la Afrika Mashariki na sisi tungeingia kufaidika nalo, lakini sioni utaratibu wowote. Kenya wana mifugo na sisi tuna mifugo na Uganda wana mifugo. Naona muda unakimbia. Lakini ni utaratibu gani wafugaji watafaidika na hili soko? Mimi niko Namanga mpakani, malori ya mahindi yanapita ya mchele, maharage yanapitishwa, lakini zao la mifugo haliwezi kupita pale mpakani kwa sababu hakuna utaratibu. Ukija na ng'ombe kwenye malori, hakuna utaratibu wowote uliowekwa, waende Kenya mpaka wavuke wakienda Namanga Kenya ndio wanapakiwa kwenye

malori. Hivi sisi ni nini na sheria gani au kwa nini haukuundwa utaratibu wafugaji wa kwetu waende kwenye masoko kama wanavyokwenda wafanyabiashara wa mazao mengine?

Mheshimiwa Spika, naona Serikali yetu haijali mifugo na usipojali mifugo, hata wale wananchi wanaotegemea mifugo huwajali. Naona Serikali inajali Vyura wa Kihansi, kuliko mifugo mingine. Inawajali kwenye bajeti, vyura walioko Marekani wanaletewa mamilioni lakini sisi wafugaji hatuna chochote. Hivi ni Watanzania wangapi wameona hao vyura? Nashangaa vyura wamepangiwa mabilioni, sisi tunapangiwa madawa ya mifugo shilingi milioni 500, ajabu; dozi 120,000 kwa mikoa 14 ajabu nashangaa!

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia Mashamba ya *NARCO*. Mashamba ya *NARCO* ni mapori ambayo hayatumiki, bado Serikali wanasema sijui tubinafsishe, sijui tuuze. Naomba sana na naomba Serikali yetu itusikie, mashamba hayo muanzishe huu ufugaji wa kisasa, muwagawie wananchi, lakini wapewe mafunzo ya kufuga kwa kisasa. Msibinafsishe, kama mnataka kutufundisha ufugaji wa kisasa na eneo lipo, kwa nini msianzishe ranchi za wananchi kuliko kumpa mtu ambaye sijui anatoka Afrika ya Kusini na sijui anatoka wapi.

Mheshimiwa Spika, nilitarajia kwamba, nitaona mabwawa kwenye kitabu hiki. Mnatuandikia mabwawa ya mwaka 2005/2006, mabwawa ya kipindi hiki cha bajeti hii yako wapi? Ni kwamba, tungetosheleza wakati ule mkumbuke kwamba, hata wakati huu pamoja na kuchimba malambo hayo hayajatosheleza bado wananchi wanahitaji malambo lakini hakuna katika kitabu hiki hata lambo moja, ndio mnataka kumaliza mifugo au kupunguza mifugo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nielezwe. Naenda kwenye mikopo ya wafugaji. Ni kwa nini mifugo haina Bodi, kuna Bodi za Wanyamapori lakini hakuna Bodi za Mifugo? Kuna Bodi ya Korosho, Pamba, hata nasikia Mfuko wa Samaki umeundwa na kuna Bodi ya Samaki. Hivi mnaona kwamba, mifugo sio zao ambalo lingepaswa nalo liwe na Bodi? Hamwoni kwamba ni zao ambalo linategemewa na wananchi wengi sana? Nikisema wasimame Wabunge ambao wamechaguliwa kwa kura za wafugaji hapa ni wachache sana watakaokaa, Wabunge wengi mmechaguliwa na wafugaji. Lakini tunaona bajeti, inapitishwa tu bila wafugaji kujadiliwa. Hakuna bajeti, hii bajeti haikumjali mfugaji, kilichoandikwa hapa ni ranchi .

Mheshimiwa Spika, nashukuru. *(Makofi)*

**MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia kuhusu mifugo ya Tanzania, ingawa wengi walinihoji kama jimboni kwangu kuna mifugo gain, mimi nipo hapa kwa ajili ya Watanzania. Ikiwa wao wanafuga, Shinyanga wanafuga, lakini ni kuwatetea wafugaji wa mifugo ambao ni Watanzania. *(Makofi)*

Mimi nashukuru kwa hii hotuba iliyotolewa, Ripoti ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Mifugo na kwa Hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, hivi vitu vyote vinakwenda sambamba, vinaoana kwa ajili ya kumtengenezea maslahi na maendeleo ya mifugo yake, mwananchi wa nchi hii ya Tanzania. Tuanze na kuku. Mifugo iko mingi Tanzania, tunafuga kuku, mbuzi, kondoo, ng'ombe na nguruwe.

Mheshimiwa Spika, kuku leo Tanzania unapokwenda kwenye mahoteli tunapokea watalii kwa malaki kutoka Ulaya, wanakula kuku kutoka Brazil. Angalieni Tanzania miaka 40 ya uhuru, ardhi ipo, watu tunao, siasa safi ipo, lakini uongozi ni mbovu. Kwa nini nikasema uongozi ni mbovu? Sikusudii Uongozi wa Serikali. Uongozi wa Taasisi wanazopewa watu kuongoza ili kuleta maendeleo katika jamii ya Watanzania. Hivi kweli kuku watoke Brazil, waende mpaka Dubai, wasafirishwe mpaka Zanzibar au mpaka Dar es Salaam ili ale mtalii aliyekuwepo Serengeti au Arusha; vijana wetu wako wapi? Tumewajengea mazingira gani ya kwamba, wawe wafugaji? Ndiyo maana nikazungumza kwamba, kama hatujaanzisha chombo cha kuwasaidia wakulima na wafugaji cha kuwapa mikopo katika Mabenki yenye riba nafuu, hatuwezi tukakomboa kilimo wala ufugaji katika nchi ya Tanzania.

Leo akina mama wanao-*retire* mara nyingi huwa wanaanzisha miradi ya kufuga kuku, lakini bei ya kuku ipo pale pale wakati bei ya chakula cha kuku inapanda kila mwaka. Haimsaidii yeye, ndiyo pale Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, akatuambia kwamba, mkulima hanenepi na mifugo hainenepi.

Hakukusudia kunenepa kimwili kwamba, hauna faida naye na ule mfugo mpaka unajiuliza hivi huyu bwana mimi ananifuga kwa kunizungusha humu Tanzania nzima. Mimi hivi ng'ombe nimeumbwa kwa ajili ya kuzungushwa tu, nitoke Mbeya nije Serengeti niingie Tabora, anataka kuchinjwa nyama isafirishwe, iliwe na Watanzania wanachinjwa? Wanasafirishwa? Mayai yanatushinda ku-*produce* ya kutosha.

Tuna Mabalozi hapa wa nchi ambazo zina neema kubwa na maendeleo makubwa katika ukulima au ufugaji wa kuku, mojawapo ni Israel. Hapa Kibaha palikuwa na Meja Jenerali Mstaafu Karubi, alikuwa akiendesha JKT moja, walikuwa wanatoa kuku wa mayai, huwezi kumbeba kwa ukubwa wake, anafika kilo saba mpaka nane. *From* Israel sisi tumelala.

Tunangojea kuku watoke Dubai ndiyo wapelekwe kwenye hoteli za kitalii, kwa nini tusianzishe mifugo midogo midogo, tukawahimiza vijana, tukawapa wataalamu, tukafanya utafiti wa ardhi inayoweza kuwaweka kuku wale wakazalisha kuku waka-*supply* kwenye mahoteli? Tuachane na kuku twende kwenye mbuzi.

Mheshimiwa Spika, mbuzi ni mnyama ambaye hachukui maradhi sana kama ng'ombe, ana *demand* kubwa sana duniani. Mfano mdogo nitakupeni, Saudi Arabia kila mwaka wanakwenda mahujaji zaidi ya milioni mbili na kwa sheria zetu sisi Waislam, unapokwenda kuhiji lazima uchinje kondoo au mbuzi mmoja. Wanachinja mbuzi karibu

milioni tatu kila mwaka. Amekuja mjukuu wa Mfalme wa Saudi Arabia na ameonesha nia nzuri juu ya kuanzisha miradi mbalimbali Tanzania.

Ni nafasi nzuri Mheshimiwa Waziri, akachukua wataalamu wake, wakamwona Rais Jakaya Mrisho Kikwete, wakapata njia ya kupenya, wakamwona mjukuu yule angalau na sisi kwa mwaka mara moja tukasafirisha mbuzi na kondoo tukapeleka Saudi Arabia na hatukosi soko la kiasi cha mbuzi laki tano mpaka laki sita, iwapo wanachinja milioni tatu. Tena hao wanachinjwa kwa *sacrifice* ni kwamba, kutokana na imani ya kidini. Jiulize na wale wanaokwenda kuhiji hawali nyama.

Saudi Arabia haizalishi mbuzi, haizalishi kuku au ng'ombe, wote wanatoka Brazil, Australia, New Zealand, tena ni mbali zaidi kimasafa. Sisi hapa kama tutakuwa na mpango mzuri wa kutenga eneo kama Dodoma liko *Central of Tanzania,* tukazalisha mbuzi wazuri, tukapata mkataba na Saudi Arabia angalau tukasafirisha mbuzi laki tano au milioni moja kwa mwaka, tungewainua na tukawaonesha wakulima kwamba, Serikali inawajali na inawatafutia soko la uhakika. Ni rahisi sana suala hilo na hizi ni *arid areas;* Dodoma, Singida, Tabora, waweze kuweka ng'ombe wengi tu lakini mpango wa kuweka ng'ombe upo, kwa nini haupo?

Majosho yako 2,050 na juzi tukaambiwa kila mwaka Serikali yetu itakuwa na uwezo wa kuyafanyia ukarabati majosho 150, ina maana kwa miaka 13 ndiyo tuyamalize. *It means* hakuna programu ya majosho mengine ya kuwaoshea hao ng'ombe. Basi miaka 13 tumalize majosho 2,050; kwa nini jambo kama hilo tusilichukulie nguvu za pamoja, tukaondoa hii dhiki ya wafugaji wa ng'ombe ili tukawaondolea haya matatizo ya kupe, tukawapa madawa, tukaweka *bore holes*, tukaweka wataalamu wakawaongoza hawa watu?

Leo maziwa nimeyakuta hapa Dodoma, eti yanatoka Australia, New Zealand, Zimbabwe, tena nusu lita kwa shilingi 1,000, *approximately is about one dollar, just imagine!* Tanzania tuna uwezo wa kuzalisha lita moja ya maziwa, tukawauzia wananchi wetu mia mbili. Leo maziwa yanatoka Zimbabwe, Kenya, New Zealand na wakati Dodoma *is a land of* maziwa.

Tulikuwa na viwanda *late 1970's* vya maziwa, kimoja kilijengwa Mbeya kwa ajili ya kukidhi haja ya kusafirisha kupeleka *DRC* na Arabuni. *Sorry* cha Shinyanga. Cha Mbeya, *South* ikawa kwa *Copper Belt* ipelekwe wapi nyama? Ipelekwe Zambia. Lubumbashi na tulifika asilimia 80 ya kuvijenga, viwanda vile vimekufa kiholela.

*Tanganyika Packers,* tulikuwa tunatengeneza nyama ya kwenye makopo ilipelekwa mpaka kwenye maonesho ya Geneva na tukapata soko zuri na tukapata nembo ya kwamba, sisi ni washindi wa kwanza wa nyama ile.

Vibali vya nyama leo vimejaa madukani, vinatoka Brazil hatuoni aibu kwamba, nyama tunayo wenyewe, tuagizie kutoka nchi za nje? *It is really shame*. Tujitahidi sasa

tuwajengee mazingira bora, tuwe na *subsidize*, tuwaondolee kodi ambazo hazina misingi ili watu waweze kufuga na waweze kusafirisha.

Kuna ngozi, sisi tunadharau tunazungumzia nyama na maziwa tu ngozi je? Ngozi ya mbuzi na kondoo ina bei nzuri sana China. Hivi viatu tunavyovaa na haya mabegi tunayobeba, hii mikanda ya suruali, inatokana na ngozi hizi. Tulikuwa na kiwanda cha kutengenezea viatu hapa Tanzania, hivi tunashindwa kuwaita *designers,* tukaweka *is just small scale industries* ya viatu tukatengeneza viatu wenyewe. Leo tunataka viatu vitoke Hongkong, Thailand, havina hata *standard* na wauzaji ni Wachina, wamejaa Lumumba leo pale. Wamachinga badala ya kuuza wao viatu, wanakuja Wachina kutoka kwao kuja kuuza viatu vya plastiki pale Lumumba na Serikali imekaa kimya.

Nenda China wewe Mtanzania, kaombe *visa* ya kufanya kazi au ya kuuza viatu au ya kuuza mbuzi hawakupi. Kwa sababu tumeweka *Free Market*, njoo, uza, chukua, peleka, nyang'anya basi *that is all*. Hatuku-*determine* kuwanyanyua vijana wetu, wakawa wao ndio waanzilishaji wa vitega uchumi, wakasafirisha bidhaa za nchi hii kupeleka nchi za nje.

Unakwenda sokoni umeshauza ng'ombe au mbuzi wako, anayenunua anachukua chuma la moto, anamtia alama mbuzi fyaa kwenye ngozi yake, hana habari ameshaua uchumi. Unapoipeleka ile ngozi katika Kiwanda cha *TANARI*, baada ya kusafishwa ikivutwa kutengenezwa inaanza kuchanika.

Kwa hiyo, elimisheni watu kama wale kwamba, waweke *stitches* maalum za kuwachoma kwenye masikio, kama wanavyofanya wenzetu ili ngozi tuweze kui-*proces*s na kuisafirisha kupeleka nchi za nje.

Ngozi ni mali, tena waelimishwe wasifanywe *air drying,* wafanye kitu kinachoitwa *wet salt* ambacho ndicho kinachoipa thamani ngozi na kusafirishwa kupelekwa nchi za nje. Leo kiatu unakinunua kwa dola 100. Ilikuwa nipate nusu saa leo. *(Makofi/Kicheko)*

Kongwa hapa leo ina uwezo wa kuchukua ng'ombe 15,000, kuna 9,000 tu. Hapana *laboratories*, hapana majosho, hapana madawa, wataalamu ndugu zangu wanapiga kelele tu, igeni mfanye *process* kama wanavyofanya Botswana. Muwapatie wafugaji wadogo wadogo na wakubwa wenye uwezo wa kuendesha.

Mheshimiwa Spika, tunapatoka kuendesha watalaam wapo ndiyo maziwa yatakapopatikana pale, pale ndiyo utakapopata ngozi nzuri, nyama ya kusafirisha, utapata watu wa kuamka na kujua kumbe wenzetu wanafanya hivi na sisi tufanye hivi sio kuchukua ng'ombe kutembea nchi nzima kwenda huku na kule, mwishoni unamwambia mfugaji unaharibu mazingira, ng'ombe wanakunya barabarani, tena akanye wapi avalishwe suruali. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ndivyo tulivyofanya, ndiyo namna wafugaji wetu wanavyofuga, sisi hatuna wafugaji, tuna wachungaji tu wanatembea tu. Ni bora hata

hivyo vyura vilivyokuweko Marekani labda haviharibu mazingira, maana vingekuwepo hapa tungeambiwa sasa kutengwe pesa, vyura vinaharibu mazingira Kihansi. Watu wanatafuta njia za kula, hatuja- *determine* watu wetu na wafugaji wetu wa kuweza kutumia ardhi yetu vizuri tukawa na *land use map* kwamba hapa kwa wafugaji hii *reserve,* hii ya wakulima, hatuna. Lazima tuamke kibiashara, mbuzi wasafirishwe wakiwa hai au nyama zao, maziwa yapatikane, tuya-*process* yatiwe kwenye vitungi au kwenye *plastics,* yauzwe. Lakini maziwa unakwenda kuagizia toka Zimbabwe, kwa nini, ni aibu.

Nenda Zimbabwe utakuta maziwa ya Iringa, utakuta maziwa ya Arusha halafu unasema eti tuwaelimishe watu wetu, kuna siku ya maziwa atakunywa maziwa na hujamtayarishia maziwa? Unamwambia mtu ale nyama atakulaje na hana pesa ya kununulia nyama, Dodoma hapo Nunge nendeni kuna maduka zaidi ya 20 na yana nyama mpaka saa mbili usiku hawana uwezo watu wa kula nyama. Tuwaelimeshe kwanza wapate vipato vya kuweza kula hiyo nyama. Nenda kaangalia historia ya Tennessee. *Tennessee Valley Authority* iliyoanzishwa ya mwaka 1939 Amerika, toka 1920's wafugaji Amerika wanatembea kwa farasi ndiyo wanamfuga ng'ombe. Leo mfugaji wetu anatembea kilometa 50 hadi 60 anatembea kwa miguu hana viatu, hana nguo mwilini, halafu bado unamwambia eneo hili usiingie, eneo hili si lako, hili mbuga za wanyama unamtaabisha kichwa chake, anaona bora afe yeye na hao ng'ombe wake. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika,Watanzania hatujawa *serious,* mimi nasema kama tume-*determine* kweli tuwe na wataalam, tugawe maeneo tufuge ng'ombe kwa njia za kisasa, tufuge kuku kwa njia za kisasa. Ndugu yangu Mzee Malecela yule pale vimbuzi vyake vitatu juzi vimekufa hapo kwa maradhi ya mapafu, huyo hapo muulizeni. Katafuta wataalam wiki nzima kuna Mheshimiwa Mbunge mmoja akamshauri akamwambia hao waliobakia watoe ndani ya banda wasije wakamalizika kwa sababu yanaweza yakaambukiza wengine, yule pale muulizeni. Hana hata mtaalam wa kuangalia mbuzi wake kumi na tano anaofuga nyumbani kwake.*(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi naomba hasa hili suala la kusafirisha kuna kijana hapa juzi kasafirisha mbuzi 400 na leo amepata *fax* kutoka Dubai anaambiwa kwamba mbuzi wako kinachohitajika sasa hivi ni barua kutoka Wizarani kwako, hali ya afya ya uchinjaji, eneo lenyewe, wanaochinja wanavaa nguo vizuri, tutachukua *order* nyingine. Sasa yule bwana amezungumza na mimi anasema kwamba *problem* sasa hivi *capital* yangu ni ndogo na kama Waziri anataka nimletee huyu kijana, nitamletea, amesafirisha mbuzi 400 watu wamechinja mbuzi kutwa nzima pale. Wakatiwa ndani ya gari la baridi wakasafirishwa mpaka Dar es Salaam mpaka *Airport* ndani ya *Emirate* wamesafirishwa mpaka Dubai, *within a single day.* Yupo hapa mimi ninaye wakati wowote Waziri akitaka nimpeleke, nitampeleka au nimlete ili apate nyezo, apate uwezo asaidiwe na serikali asafirishe mbuzi wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, akisafirisha mbuzi wengine yule anayeuza mbuzi atanunua bati, saruji na ataanza kujenga, atamsomesha mwanawe, atakula vizuri na atalala mahala pazuri, lazima tujenge imani watu ambao wanataka kuinua uchumi wa Tanzania. Leo Kenya ile pale kuna kampuni kama za *Cadbarys* wanatengeneza *chocolate* kwa maziwa

yao ya Kenya tumetolewa *data* hapa leo, Kenya wanakunywa maziwa kiasi gani sie tunakunywa kiasi gani. Ukishanyonya maziwa ya mama yako mzazi ndiyo ushamaliza tena hunywi maziwa mpaka ufe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hiyo miaka miwili bahati yako, maana hata yeye mama afya yake mbovu hivyo hivyo. Kwa hiyo, sisi Watanzania tutegemee kunyonya maziwa kwa mama zetu. Tukimaliza miaka miwili itabidi tubakie hatunywi maziwa mpaka kiama. Lazima tujenge mikakati ya kuweza kuwainua wakulima wa nchi hii ili waweze kusafirisha, wauze mifugo yao wapumzishe mifugo yao na watengewe maeneo yao kwa ajili ya kufuga mifugo yao. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Tanzania inaweza ikawa na uhaba wa maziwa lakini haina uhaba wa wataalam wa ufugaji. Tumekwisha sikia kutoka kwa mfugaji wa Longido sasa tumesikia vitu vipya kabisa kutoka kwa mfugaji wa Mji Mkongwe Zanzibar kwa hiyo, basi tumalizie kutoka kwa mfugaji wa Simanjiro, Mheshimiwa Ole Sendeka. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nichukue nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo, na nianze kwa kweli kuungana na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, kwa kutupati Wizara ya Maendeleo ya Mifugo kama Wizara kamili. Kwa niaba ya wafugaji pia naomba niwapongeze wachangiaji wote waliochangia siku ya leo ambao kwa kiasi kikubwa wameonyesha kutuhurumia wafugaji na kwa kweli wameonyesha upeo mkubwa wa kuelewa tatizo au matatizo yanayowapata wafugaji. *(Makofi)*

Ningependa pia nichukue nafasi hii kuwatakia *birthday* njema kwa wale ambao wamezaliwa tarehe ya leo na kwa kusema kweli ninachowaonea wivu ni kwamba sehemu kubwa ya wale ninaowawakilisha hawajui *birthday* zao nikiwemo mimi mwenyewe. Kwa sababu bahati mbaya wazazi wetu hawakujua kusoma na kuandika na hawakuweka rekodi. Mimi mwenyewe niliamua kuchukua tarehe ile ya Uhuru wa Tanganyika kuwa tarehe yangu ya kuzaliwa kwa kuamua na mke wangu wa kwanza naye alichukua siku ile ya Muungano kwa sababu hajui tarehe yake ya kuzaliwa. Kwa sababu watoto walikuwa wanatuuliza baba wewe *birthday* yako ni lini. Sasa ikabidi tutunge siku na tukaweka siku zile ambazo kunakuwa na kumbukumbu za kudumu ambazo inatufanya tukumbuke kila siku. Ninahakika wafugaji wengi wako hivyo.*(Makofi /Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nigependa nichukue nafasi hii kuwapongeza madaktari wote watatu Waziri wetu wa Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu, kwanza kwa kuaminiwa na Rais na kupewa dhamana ya kuongoza Wizara yetu hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, kwa kweli wameonyesha kwa kiasi kikubwa ufahamu wa kuijua kazi yao kwa kiwango kikubwa na cha kuridhisha na kwa maana hiyo

lazima nieleza faraja yangu kwamba kadri siku zinavyozidi kwenda na Wizara zinapowasilisha hotuba zao kila siku naendelea kuona kwamba Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, hajafanya makosa hata kidogo kwa kuwateua makada wenye uwezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipindi kilichopita tulikuwa na Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo ambaye kwa sasa ni Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania, Mheshimiwa Edward Lowassa, alitufanyia kazi nzuri sana na nafikiri pia kutokana na uzoefu alioupata yeye na Rais pengine na mtandao wao, mimi sijui wanateuana vipi. Lakini nafikiri walishauriana wakatupa watu makini na watu ambao wanafahamu mifugo pamoja na kwamba watu wengine wanaweza kufikiri hawatoki maeneo ya wafugaji. Lakini niseme tu kwamba wanafahamu kwa kiwango cha kutosha.

Mheshimiwa Spika, hata kitabu chao cha bajeti, imewekwa picha ya ng'ombe mzuri, dume la mbegu kubwa ambaye kila mmoja hata wale wanaopenda kukutana na ng'ombe mezani kwenye sahani, nina hakika wanamezea mate dume hili ambalo liko hapa, wanafikiri na wanajiuliza atachinjwa lini. Sasa ningependa kusema kwamba sasa nielekee kuchangia baadhi ya mambo muhimu kwanza nikitambua kwamba hotuba ya Waziri inathibitisha wazi kiasi cha ufahamu wake katika suala zima la mifugo. Kwa sababu katika ukurasa wa nane kwa ridhaa yako naomba kunukuu Waziri akielezea juu ya tatizo la ukame lililolikabili Taifa letu na wafugaji katika ukurasa wa nane anasema: "Ili kunusuru mifugo, wafugaji walilazimika kuhamia katika maeneo yaliyokuwa na unafuu wa malisho na maji ikiwa ni pamoja na Mikoa," akataja hiyo Mikoa. Wafugaji walilazimika kuhamisha mifugo ili kunusuru mifugo yao.

Mheshimiwa Spika,wale wanaofikiri wafugaji wana hama kwa kupenda, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu amewaelimisha kwamba mkituona tunahama sio kama tunapenda tunahama ili kunusuru mifugo yetu isije ikafa au ikaisha.

Mheshimiwa Spika, ninyi nyote ni mashahidi kwamba juzi Waziri wa Maji alipokuwa akitoa hotuba yake alisema maji ni uhai na kwa sababu mifugo inahitaji maji mengi zaidi kuliko binadamu, pale ambapo pana upungufu wa maji na kwa kuwa maji ni uhai ni lazima mfugaji ajitahidi kwa kadri ya uwezo wake kuhamisha mifugo yake ili kufuata malisho katika eneo ambalo malisho yanapatikana lakini ili pia kufuata maji maeneo ambayo maji yanapatikana.

Kwa hiyo, ningependa Watanzania wenzentu waendelee kutuelewa kwamba wafugaji wanapohama hawahami kwa sababu ya kupenda, ila wanahama kwa sababu wanalazimika kuhama na sababu moja wapo ni kutafuta malisho na maji kwa ajili ya mifugo yao.

Mheshimiwa Spika, Rais alieleza masikitiko yake katika hotuba yake ya kufungua Bunge, aliposema kwamba mfugaji anakonda na mifugo inakonda, watu wengine wanatafsiri vibaya. Lakini ni ukweli kwamba Rais alikuwa anatuonea huruma na mimi nilifikiri kwamba kupitia bajeti ya leo, Serikali ingejielekeza zaidi kutenga fedha nyingi zaidi kwa ajili ya mifugo na wafugaji. Nimemshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kupewa Wizara lakini kupewa Wizara ni jambo moja na kuwezeshwa kwa Wizara ni jambo

lingine muhimu tena muhimu kuliko. Mwaka jana hatukuwa na Wizara ya Mifugo, tulikuwa na Wizara iliyochanganya mifugo na maji.

Lakini leo rejea yote ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo inaeleza mafanikio ya majosho, malambo na mabwawa ambayo yalichimbwa katika kipindi cha bajeti ya mwaka 2005/2006. Nikiangalia kwenye bajeti ya mwaka 2006/2007 hakuna kitu, kwa mfano kwenye Wilaya yangu sioni josho lolote, sioni bwawa lolote na kwa maana hiyo tunarejea yale ya Mheshimiwa Edward Lowassa, mambo aliyoyafanya mwaka jana ndiyo leo tunayajaza kwenye kitabu, tunasahau kwamba wafugaji bado wanahitaji majosho, malambo, wanahitaji dawa za mifugo, lakini badala yake tunaeleza yale yaliyopita badala ya kueleza watatufanyia nini kwa bajeti ya mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kuiomba Serikali na kuishauri ione uwezekanao wa kutafuta fedha kwa ajili ya kuwasaidia wafugaji. Haieleweki na Watanzania hawawezi kutuelewa tukisema tunawasaidia wafugaji wakati hakuna hata fungu au fedha zilizotengwa kwa ajili ya majosho wala kwa ajili ya malambo. Kama alivyosema Mbunge wa Longido, Mheshimiwa Michael Laizer, alielezea bayana juu ya zile shilingi milioni 500. Hivi milioni 500 unapowapa wafugaji maana yake nini? Milioni 500 ni sawa sawa na fedha mnazowapa zilizotengwa kwa uwezeshaji kwa kila Mkoa, haziwezi kutosha chochote.

Dawa za mifugo ni ghali na zinahitaji fedha nyingi zaidi kwa ajili ya kusaidia mifugo hiyo na mifugo ile inahitaji fedha nyingi zaidi kwa ajili ya kusaidia mifugo hiyo na mifugo hiyo inahitaji maji na bwawa moja halipunguwi shilingi milioni 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sababu nyingine inayofanya wafugaji kuhama ambayo ningependa kuweka bayana hapa ni kutokana na maeneo yao ya kufugia kubadilishiwa matumizi ikiwa ni pamoja na kuanzishwa mashamba makubwa katika maeneo hayo na kuanzishwa kwa hifadhi za Taifa katika maeneo ya wafugaji. Ukiangalia leo wafugaji wa jamii ya Watotoga au Wabarbeig unaowaona kule, yako maeneo yao ambayo yalichukuliwa katika mashamba yale ya *NAFCO* yaliyoko kule Basutu ambayo ni maelfu ya mahekari ambayo yangeweza kuwasaidia sana. Lakini cha kushangaza ni kwamba wakati mnarejesha haya mashamba kabla ya kubinafsisha mngewakusanya Wabarbeig mkawagawia wangefurahi sana wangeweza kuendesha ufugaji katika eneo hilo kuliko kuwaacha watangatanga. Haya sijatumwa na mtu yeyote, lakini nimeona mimi kama Mbunge nigusie hayo, maana hilo Jimbo ni la Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, mkasema kanituma.

Mheshimiwa Spika, napenda kusema kwamba kuna kitu kinachoitwa kilio cha wafugaji wa Tanzania. Barua ambayo imeandikwa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imeandikwa na wafugaji na ikapewa kichwa cha Kilio cha Jamii ya Wafugaji wa Tanzania. Sina hakika kama Waziri wa Maendeleo ya Mifugo amewahi kuiona lakini namwomba sana tukitoka sasa hivi nitamkabidhi nakala, kwa sababu walimwandikia Rais. Lakini kama mnavyojua, walisema wenyewe walipeleka pale geti la Ikulu ipelekwe kwa Rais lakini kama imefika kwa Rais hatuna uhakika. Lakini tukikukabidhi wewe kilio hicho cha wafugaji wa Tanzania kitafika kwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina haja ya kurejea sana yaliyoko humo ndani maana yake ni mengi, lakini kikubwa ni kwamba wanaeleza jinsi ambavyo watu wamekuwa wakipotosha dhana nzima ya ufugaji na kuwaona wafugaji kama ni waharibifu wa mazingira na wengine kabisa bila kuona haya wanasahau kwamba mifugo hiyo hiyo ndiyo inayohuisha mazingira na kama mifano mingine iliyotolewa kwa kupitia mbolea inayotokana na mifugo kwamba mbolea ile inarutubisha ardhi.

Mheshimiwa Spika, nina hakika wenzangu wa Kusini nikianzia kada mwenzangu Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, ningefurahi sana kama angepata ng'ombe kama kumi kwake na akatumia mbolea ya ng'ombe hao kumi pamoja na kaka yangu Mheshimiwa Raynald Mrope wakawa na ng'ombe kumi kila mmoja kwenye mashamba yao binafsi, nina hakika mbolea ya kununua hawatanunua kwa sababu watakuwa wanatumia samadi na watakuwa wamesaida jamii hizo kunywa maziwa kwa kiwango cha kutosha. Nimesema niwatolee mfano hao kwa sababu ni rafiki zangu.

Mheshimiwa Spika, liko jambo lingine muhimu sana kwa upande wa wafugaji ambalo linahitaji kipaumbele, nalo ni dawa za mifugo na chanjo. Magonjwa yanayomaliza mifugo ni ugonjwa wa *Ndigana ECF* na kama tungepatiwa chanjo na dozi ikaongezwa kutoka zile dozi za shilingi 120,000, inaweza ikatusaidia kwa kiasi kikubwa. Lakini mkatusaidia pia kupata dawa za kuogesha mifugo Serikali ikawasaidia wananchi kama kianzio na baada ya hapo watakuwa wamepata mifuko ya kuendeleza, basi nina hakika ufugaji ungewezekana vizuri.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine ni kwamba wale wenye leseni za kuuza dawa wangeruhusiwa kuendelea kuuza dawa katika maeneo mbalimbali. Kwa mfano ukingalia jiografia ya Wilaya ya Simanjiro kutoka kijiji kimoja mpaka kingine ni kilometa 70 au 50.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama kuna watu ambao wanafanya *mobile veterinary services* ingeweza kusaidia zaidi ndivyo ilivyo kwa Wilaya nyingine ambazo jiografia yake inafanana na hiyo ya Simanjiro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni maji hasa kwenye maeneo makame kama ya wafugaji kama Wilaya yangu ya Simanjiro. Tunavyo vijiji ambavyo vimesajiliwa tangu mwaka 1993, lakini mpaka sasa vimeshindwa kufanya uchaguzi wa Serikali ya kijiji, kwa sababu makazi hayo watu wanaishi wakati wa masika na wakati wa kiangazi wanahama na kwa maana hiyo vijiji hivyo vimeshindwa kuanzishwa ikiwemo kijiji cha Losokonoi na kijiji cha Londrekes.

Mheshimiwa Spika, wafugaji wanahama wakati wa kiangazi na shule wakati mwingine shule zinalazimika kufungwa na haya ni maeneo mazuri sana kwa wafugaji ningefurahi sana kama Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa angewezeshwa na Serikali ili hii Wizara yake iweze kutoa huduma ya maji kwa wafugaji na mifugo yao.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua nafasi hii kwa mara nyingine, kumwomba Waziri anayehusika aendelee kuwaelimisha wale ambao hawaelewi juu ya dhana nzima ya ufugaji kwa mazingira yetu ya sasa ili upotoshaji uweze kuondoka na watu waweze kufahamu kwamba wafugaji ni watunzaji wazuri wa mazingira na si waharibifu wa mazingira kama ambavyo wengine wanajaribu kutaka tuamini hivyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kutamka kwamba naunga hoja. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Maendeleo ya Mifugo, Naibu Waziri na watendaji wote kwa ujumla kwa hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ufugaji wa kuku wa nyama na mayai, kumekuwa na idadi kubwa ya uagizaji nyama na kuku wa mayai ya kisasa toka nje ya nchi na hasa kutoka Afrika Kusini. Mwenendo huu unadhoofisha juhudi za kuwaondolea umaskini wananchi wetu hususan wanawake ambao wengi wao ni wafugaji wa kuku wa mayai na nyama.

Mheshimiwa Spika, wawekezaji kama wenye mahoteli makubwa na *supermarkets* huagiza mazao hayo toka katika nchi zao walizotoka na nchi jirani kama mazao ya nyama ya kuku, mayai, machungwa, uyoga, vitunguu swaumu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hali hii ni hatari sana kwa wafugaji wetu, hivyo Serikali ingetoa tamko rasmi la kuwaagiza wawekezaji hao wanunue vyakula vya aina yote ambavyo hupatikana hapa nchini ili kulinda soko la ndani na hatimaye wananchi wafaidike na utaratibu huu hususan wanawake ambao ni wafugaji wa kuku. Hii ikiachwa hivi hivi kila *investor* aaagize chakula toka nje ya nchi, umaskini wetu hautaweza kupungua.

Mheshimiwa Spika, Wizara iangalie bei ya vyakula vya kuku kwani ni aghali kupita uwezo wa wafugaji. Wizara iweke utaratibu wa kukutana na wenye viwanda vya chakula cha kuku kwa lengo la kudhibiti upandishaji holela wa vyakula hivi.

Nampongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuunda Wizara ambayo itashughulikia mifugo pekee kwa lengo la kuleta ufugaji wenye tija. Kwa maana hiyo, Wizara iangalie upya suala zima la kulinda masoko ya ndani kwa lengo la kuinua kipato cha wananchi wanyonge wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la maziwa nchini, tatizo kuu ni *packaging*. Ingefaa tatizo hili lipatiwe ufumbuzi wa haraka. Ukienda katika *supermarkets* unakuta maziwa yanatoka Afrika Kusini, Uarabuni na kadhalika. Hivi kweli tutaendelea kuthamini mazao yanayotoka nje ya nchi mpaka lini?

Naomba wataalam wetu waliangalie suala zima la kuthamini na kuwa na uzalendo wa kuhimiza utumiaji na ulindaji wa soko la ndani na utaalam wa kutosha kupaki katika

ubora wa Kimataifa wa mazao yetu. Kuwe na mipango ya utekelezaji wa muda mfupi na muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwamba Wizara iweke kila Mkoa uwe na vitengo vifuatavyo: -

(i) Elimu ya mifugo na jinsi ya kupata masoko;

(ii) Ufuatiliaji wa ukiukwaji katika mahoteli kutoagiza vyakula nje ya nchi; na

(iii) Kuhakiki ubora wa mazao ya mifugo ili wananchi wapate kuelewa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, kabla ya yote naomba kuunga mkono hoja hii kwa jinsi ilivyoandaliwa vizuri na kwa utaalam wa hali ya juu.

Pia naomba niwapongeze Waziri wa Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa na Katibu Mkuu, Dr. Charles Nyamrunda, pamoja na timu ya wataalam wote wa Wizara wakiongozwa na Dr. Jonas Melewas ambaye niliwahi kufanya naye kazi na kujua uwezo wake ulivyo mkuu katika masuala yote ya kuendeleza mifugo nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, bado ninakusudia kutoa malalamiko yangu kwa niaba ya wananchi kwa maamuzi yanayotuletea mifarakano kati ya Serikali na wananchi kwa kudhani Serikali haijawatendea haki wananchi waishio karibu na shamba la Malonje (Sumbawanga). Matamshi na maelekezo mbalimbali yaliyotolewa na Serikali yalianza kuwapa matumaini ya kuona Serikali itagharamia upimaji wake na kulipa mafao ya wafanyakazi wa *DAFCO.*

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo ya awali ya Wizara, lakini sasa Wizara inatutaka tugharamie upimaji na kuwalipa wafanyakazi! Hali hii inatuacha sisi Wabunge tuonekane kama walaghai mbele ya uso wa jamii kwa kubadili badili maamuzi. Namwomba Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo akubali kufanya yafuatayo: -

Kwanza, Wizara iwalipe stahili ya wafanyakazi wote wa hapo Malonje kuliko kutuachia sisi mkoani. Pili, Wizara ikitumia wataalam wapima ambao walitumika kupima mashamba mengine, waendelee kutumika na ofisi ya Mkoa ije iwalipe baada ya kuuza maeneo yatakayokuwa yamepimwa katika mashamba madogo madogo ya hekta 40 hadi 50 kila moja kwa ajili ya ufugaji.

Tatu, Wizara itumie wataalam wake waje kusimamia zoezi lote hili kwa kuzingatia pia kuwa wananchi wachache wanaozunguka maeneo ya shamba wanahusishwa kikamilifu ili kujua kwa undani hatma yao katika kumiliki sehemu ya shamba hilo.

Mheshimiwa Spika, Mkuu wa Mkoa wetu, Ndugu Daniel Ole Njoolay, anajitahidi sana kutafuta fedha, lakini inakuwa vigumu kwa Taasisi ya Fedha kutoa mkopo kwa shamba ambalo halina hati rasmi. Tunaomba suala la hati ya shamba lipewe umuhimu wake, maana shamba hilo linagombewa pia na Magereza Mollo, ambalo nao wanasema shamba hilo sehemu kubwa ni lao na walipewa na Wizara. Sisi hatuna uthibitisho huo, labda Wizara itusaidie.

Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa machinjio ya kisasa na ya Kimataifa Mjini Sumbawanga kunahitaji maandalizi ya mipango ya malisho bora katika maeneo yote yanayozunguka machinjio hayo ili upatikanaji wa mifugo bora ambayo inaweza kuchinjwa kwa ajili ya soko nje ya mkoa na nje ya nchi. Udhibiti wa magonjwa na uimarishaji wa malambo na majosho ni budi upewe kipaumbele ili fedha nyingi za Serikali zilizotumika kugharamia mradi huu zisipotee bure na kuitia hasara nchi hii.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri ajitahidi sana kuwawezesha watumishi wake wote wapewe maslahi mazuri, wapewe zana nzuri za kufanyia kazi zao vizuri na kuimarisha utafiti wa mifugo na dhana nzima ya huduma za ugani kwa wafugaji wote hapa nchini. Tusikubali wafugaji wakabakia wachungaji tu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii na kuwatakia kheri na mafanikio katika azma hii muhimu kwa afya ya Watanzania.

**MHE. TATU M. NTIMIZI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na kupongeza hotuba nzuri yenye mwelekeo.

Mheshimiwa Spika, naomba nipate maelezo, kwanza, wafugaji hawatembelewi na wataalam ili kuwapa elimu ya ufugaji bora. Wataalam hawaendi kuwatembelea hadi wakati wa chanjo bila kujua historia ya magonjwa katika eneo hilo au kumwelimisha mfugaji. Ni faida ya kuwa na wataalam wasiofanya kazi ya elimu na kutembelea maeneo ya kazi zao ili wawe watekelezaji bora.

Pili, kusafirisha mifugo kutoka Bara kuelekea Dar es Salaam ni hatari na gharama. Je, Wizara hii haina mawasiliano mema na Wizara ya Miundombinu? Usafirishaji kwa treni ni ghali mno, usafiri wa malori ni gharama na ajali nyingi, usafiri wa kuswaga ni hatari kwa mifugo na binadamu, barabara zinaharibika na wanyama wakali njiani huhatarisha maisha ya watu na wanyama.

Tatu, unyanyasaji wa wafugaji kutoka Mikoa ya Bara kuelekea Mikoa ya Kusini na Mashariki kuna nini mpaka wapigwe, wanyang'anywe mifugo na kuonekana kama ni wakimbizi ndani ya nchi yao iliyo huru? Ubinadamu uko wapi, waende wapi? Kwa nini hekima isitumike kuwaelimisha na kuwaendea kiutaratibu na kisheria badala ya kuwatia bakora?

Nne, watendaji walioko vijijini chini ya TAMISEMI wamechoka kazi, wasiliana na Wizara hiyo ili watendaji waliokaa zaidi ya miaka mitano kwenye Kata wahamishwe kwani hakuna kazi wanayofanya hivi sasa badala ya kujijengea mazingira ya ulaji na

ukaaji. Mazoea na wananchi yamekuwa makubwa kuliko ufanisi wa kazi. Naomba maelezo na ufafanuzi na majibu ya kuelimisha ili wafugaji katika Jimbo langu waelewe.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. HEMED MOHAMMED HEMED:** Mheshimiwa Spika, ni vyema kabisa nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake ambayo imeniwezesha kufahamu wafugaji wa nchi yetu sasa wamepata wakili. Tegemeo hili litatoa mategemeo makubwa kwa wafugaji wetu.

Mheshimiwa Spika, wakati umefika sasa Serikali ibadilike juu ya wafugaji kwani wanakabiliwa na matatizo mengi sana. Wana matatizo ya kufuga wanyama wao kienyeji. Wafugaji ni maskini, pia mifugo inakabiliwa na ukame. Wafugaji wetu wengi wanafuga wanyama wao kienyeji. Hii inatokana na Wizara kushindwa kuwahamasisha wafugaji kwenda na wakati. Kuna tofauti kubwa kuhusiana na wanyama wetu kuanzia utoaji wa maziwa, wingi wa nyama na kadhalika. Bado wafugaji wetu wanafuga ng'ombe wale wale wa enzi za mababu zetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umaskini, wafugaji wetu ni maskini kama wanyama wenyewe kiakili. Kwa nini Serikali ishindwe kuwasaidia wafugaji kwa kutumia mikopo pamoja na kuwapatia wataalam wa mifugo wafugaji wetu?

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukame, kama alivyo mwanadamu yeyote hapa nchini anahitaji chakula na maji. Ni lini Serikali itaondoa tatizo hili? Kuna ukubwa wa maeneo makubwa nchini mwetu, lakini wakulima hawapewi. Jiografia ya nchi yetu Serikali inaijua, kuna uchumi kwa baadhi ya mazao kieneo. Korosho sehemu yake, majani ya chai sehemu yao, mpunga sehemu yake na kadhalika, kwa nini iwe hivi? Kila eneo limejipangia zao lao kutokana na ardhi yenyewe. Sehemu gani ni ya wafugaji? Kwa nini Serikali ishindwe kuwapa maeneo yao?

Mheshimiwa Spika, wanyamapori wamepewa heshima kubwa sana hata kudiriki kupewa madaktari wa kuwatibu, lakini kwa wafugaji Serikali haijali. Serikali kusema wafugaji wanaharibu mazingira ni kuwaonea. Kusema wapunguze wanyama wao hii pia ni kuwaonea. Serikali haijui kama ikiweka soko mifugo itapungua. Serikali inapaswa iwafahamu ni Watanzania wangapi waliojiajiri kupitia mifugo. Pia inapaswa kujua ni Watanzania wangapi wameweza kusoma kupitia mifugo, vile vile inapaswa iwajue ni Watanzania wangapi wanatunza familia zao kupitia mifugo. Serikali pia inapaswa kujua ni wakulima wangapi wanaolima kwa kutumia mifugo.

Mheshimiwa Spika, wakulima na wafugaji ni baba mmoja, mama mmoja katika nchi yetu. Ni vyema basi Serikali kama baba wa watoto hawa ingewaenzi sawa. Wizara kama ni wakili, mtetee mteja wako ili aondokane na kesi. Wafugaji nao wanayo haki. Ahsante.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba naweza kuchangia kwa kuongea, bado naona muda hautoshi kuelezea mengi ambayo nilitaka kuchangia.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Mifugo haina watumishi kwenye ngazi za vijiji, kata na hata maeneo mengine hawana Afisa Tawala wa Mifugo. Taarifa ya mifugo pamoja na huduma zinatakiwa ziendelee vizuri, hivyo wapatikane wahudumu/watendaji kwenye ngazi ya vijiji.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni utaratibu wa wafugaji kupata dawa za mifugo. Dawa za kuogeshea, dawa ya *ECF,* dawa ya miguu na midomo hazipatikani madukani, kwa hiyo, ni vizuri kila mwaka dawa za chanjo hizo zipatikane. Bei ya dawa ni juu sana kutokana na Serikali kupunguza au kufuta ruzuku ya dawa hizo, wanaofaidika ni wafanyabiashara. Wizara iunde chombo cha kupanga bei ya dawa ili punguzo liwasaidie walengwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu masoko ya nje, Tanzania ni moja ya nchi za Afrika Mashariki ambayo imeruhusu soko la nchi zote tatu. Lakini nasikitika kwamba utaratibu wa kupeleka ng'ombe Kenya kupitia kituo cha Namanga haupo, lakini mazao mengine yamewekewa utaratibu wa kupitishwa. Kila mwaka nauliza kuna utaratibu gani wa mifugo kwenda Kenya lakini sipati majibu. Ng'ombe wanaouzwa Kenya ni wengi sana, kwa mfano ng'ombe wa mikoa ifuatayo wanauzwa Kenya, Mikoa ya Arusha, Mara, Kilimanjaro, Manyara, Shinyanga na Singida.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ng'ombe wengi kwenda Kenya, hakuna utaratibu wowote unaotumiwa kwenda, ni njia za panya tu. Kwa nini mifugo hawapitishwi mpakani kwa magari kama mazao mengine?

Mheshimiwa Spika, kuna mgogoro mkubwa kati ya wananchi wanaozunguka mashamba ya *NARCO.* Ombi langu ni kwamba mashamba hayo yagawiwe kwa wananchi, waanzishe ufugaji wa kisasa, mafunzo yaanzishwe kwenye maeneo hayo yawe mfano.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba kujua kwa nini fedha za dawa zimepunguwa tena kutoka milioni ambazo zimeandikwa kwenye *amendment* ya shilingi bilioni 2.2 na kuwa shilingi milioni 500. Fedha hizi ni chache sana hazitoshi, ziongezwe.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, maendeleo ya mifugo ni muhimu sana katika maendeleo ya nchi yetu na watu wake hususan wafugaji ambao pamoja na kuwa na mifugo mingi, lakini bado mifugo yao haijawasaidia kuwaondoa katika umaskini.

Mheshimiwa Spika, ipo haja ya makusudi ya kujiangalia na kujipanga vizuri ili mipango na mikakati yetu iweze kuwa chanzo cha kubadilisha hali ya maisha ya wafugaji wetu. Kwa kutumia raslimali hii, ni vyema itabadili hali ya Watanzania kwa ujumla wao katika kuchangia pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, ipo haja na ulazima katika kuwaelimisha wafugaji wetu waweze kuondoka katika kuchunga na kuwa wafugaji kwa kuhakikisha huduma za lazima na za muhimu zinapatikana karibu yao na wakati wote. Wafugaji wanastahili pia kupata huduma za kijamii kama zahanati na shule kwa kusomesha jamii ya wafugaji. Naamini ufugaji wa kisasa na bora utaendelezwa baada ya jamii kupata elimu ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, upo ulazima usio na hiari wa kuangalia wafugaji wanapata huduma za ugani, dawa, malambo na majosho kulingana na idadi ya mifugo katika kila eneo na kuhimiza na kutoa bure mbegu za malisho ya mifugo. Kwa kufanya hivyo wafugaji wataacha kuhangaika na kuhama toka eneo hadi eneo na hii itasaidia pia kuhifadhi mazingira yetu.

Mheshimiwa Spika, nimepata kuona kitabu ambacho kimetolewa na Chama cha Mapinduzi kuhusu Mipango ya Utekelezaji wa Serikali yake kwa mwaka 2006/2007 kuhusu Mikoa. Pamoja na kwamba kitabu hicho si *official document,* lakini kimenipa hofu kubwa sana kwa namna ya utekelezaji wa mipango ya Serikali kama ilivyoainishwa katika kitabu hicho.

Mheshimiwa Spika, katika mipango kama ilivyo katika *document* hiyo, Serikali haisemi chochote kuhusu mradi uliotelekezwa wa kiwanda cha nyama Shinyanga kilichoachwa kuendelea kuoza na mitambo kuharibika na fedha za wananchi kupotea na sasa Serikali hii inafikiria kujenga kiwanda Bagamoyo. Jamani, wapi na wapi, Shinyanga na Bagamoyo katika suala la mifugo?

Mheshimiwa Spika, sishangai sana katika hili, daima ndio *vision* ya Serikali yetu. Tumbaku inalimwa Urambo na Mpanda, kiwanda kipo Morogoro. Lakini katika hili ni vyema Serikali ikaeleza vigezo na vipaumbele vya Bagamoyo na siyo Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo kubwa la vifo vya mifugo kutokana na ukame na maradhi, hatua zinazochukuliwa hazitoshelezi katika kujenga malambo na majosho. Wilaya ya Mpanda inayo mifugo ambayo ninayo hakika Serikali inafahamu vyema. Naomba katika hitimisho, Serikali itamke bayana katika suala la kujenga malambo na majosho katika maeneo yenye ng'ombe wengi Wilayani Mpanda.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa uteuzi wao ili kusimamia Wizara hii. Pia niwapongeze wataalamu wote wa mifugo kwa kazi yao nzuri na kwa kushiriki kwao katika kuandaa hotuba hii nzuri.

Pamoja na kuunga mkono hoja ya Waziri, naomba kutoa maombi na ushauri yafuatayo:-

(i) Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara nyingine waandae ramani *(atlas)* ya nchi nzima ya matumizi ya ardhi na kutenga nchi katika maeneo ya kilimo na kufugia mifugo. Badala ya mtindo wa sasa wa kutumia kila eneo la ardhi kwa kilimo na ufugaji mifugo.

(ii) Kama (i) inakubaliwa, Taifa likubali kuwa Mikoa ya Dodoma, Tabora, Singida na sehemu za Mikoa ya Arusha na Manyara zitumike kwa ufugaji wa ng'ombe wa nyama kwa asilimia 90 na Mikoa ya Morogoro itumike kwa kilimo. Ramani ya matumizi ya ardhi Kitaifa ionyeshe wazi maeneo ya kilimo na utafiti.

(iii) Sheria itungwe kuzuia *nomadism* baada ya kutekeleza (i) juu.

(iv) Mpaka sasa ufugaji mifugo unafanywa na Watanzania wasio na elimu na utaalam wa kufuga ingawa uzoefu umewapa elimu ya ufugaji au uchungaji wa ng'ombe. Kwa namna gani Wizara itavutia wasomi kushiriki katika ufugaji?

(v) Kwa nini Wizara isianzishe mashamba madogo ya mifugo vijijini na kutumia mashamba ya mifugo yaliyomo kama shule. Ni kosa kubwa kuuza na kugawanya mashamba ya mifugo yaliyoko.

(vi) Ni kosa kubwa kuendeleza mtindo huu wa kila Mtanzania kumfanya mfugaji na mkulima. Nini sera ya Wizara kuhusu *nomadism and shifting agriculture?* Ufugaji hauko nchini ila ni uchangiaji mifugo, njia ambayo haitatupeleka popote. *There is need for change.*

Mheshimiwa Spika ombi na mapendekezo kuhusu Njombe ni:-

(i) Kutokana na mafanikio ya mpango wa kopa ng'ombe, lipa ng'ombe katika vijiji vya Kata ya Igongolo hasa kijiji cha Ibumila ambacho Waziri alitembelea hivi karibuni, vipi Wizara hii isisaidie kusambaza ng'ombe katika vijiji vyote vya Kata au Tarafa hii ili vitumike kama shule kwa vijiji vingine katika Wilaya au Mkoa.

Mheshimiwa Spika, nakumbushia ombi langu la wananchi wa kijiji cha Ibumila la kupatiwa ng'ombe zaidi wa maziwa kutoka *Sao Hill.* Kiwanda cha maziwa cha Njombe kina uwezo wa lita 40,000 lakini kinapokea lita 500 tu.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, naomba kujua kinachofanya vituo vingi vya mifugo vinazidi kurudi nyuma kimaendeleo kwa mfano kama Mkoa wa Kagera unakuta ulipewa kipaumbele ningeomba kujua, ni kwa sababu gani? Unakuta sehemu nyingi ambapo kuna wafugaji Serikali inazidi kuwahamisha na hiyo inakua shida mojawapo, hivi Serikali haioni kama ni tatizo kubwa kwa wafugaji? Wangefanyiwa mpango kuwapa sehemu kubwa.

Mheshimiwa Spika, kuna wananchi wengi wanajitahidi kufuga lakini sasa inafika mahali wanakata tamaa. Kulikuwa na kituo cha kununua maziwa lakini mpaka sasa hakifanyi kazi hivi Wizara inaliona. Naomba jibu zuri.

Mheshimiwa Spika, kuna wanaofuga nguruwe, kuku na mbuzi, lakini hawapati elimu ya kutosha na hii itakuwa wale ambao wanapenda kuunda vikundi vya kufuga.

Pamoja na hayo wafugaji wa Karagwe na Wilaya hizo za Karagwe, Biharamulo, Ngara, Muleba na wananchi wanojitahidi kufuga sana.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara hii ijitahidi kuboresha wafugaji waweze kujipatia kipato, wawe na faida na mifugo yao. Kagera hawana hata josho moja la kuogeshea ng'ombe. Naomba kuwasilisha.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, Shirila la Ranchi za Taifa likarabatiwe kwa kaisi kikubwa sana, nampongeza Waziri kwa kuunda Bodi mpya, kazi ni kubwa wafanye:-

Mheshimiwa Spika, watumishi wanaopaswa kustaafu na kupisha wenzao wapya hawafanyi hivyo, wanaendelea na kazi kwa visingizio vya *consultants* wenye madawati ya kudumu, mikataba isiyoisha. Hakuna mipango imara wa *succession,* mtawapa mikataba wastaafu hao mpaka lini? Je, siku Mwenyezi Mungu atakapowatwaa hao waja wake hizo ranchi mtazifunga? Je, ahadi ya Serikali ya ajira kwa vijana inatekelezwe vipi endapo waliopo hawaondoki na wala mpango wa hawana? Mlipeleka vijana wa kuwa-*understudy* wakubwa, hawa vijana wamekuwa *frustrated* sana, baadhi wameacha kazi na baadhi wameona bora waajiriwe na Halmashauri. Wameondoka.

Mheshimiwa Spika, ranchi ya Kongwa inahitaji *overhaul* ya uongozi. *Rangeland deterioration* ni kubwa, *pasture development strategy* hakuna, fensi imeanguka zamani, majengo ni chakavu sana, *capacity* ya shamba ni ng'ombe 14,000, waliopo ni wachache kwa mbali na baadhi ya waliomo ni watu binafisi, mpango wa mahusiano na wanavijiji kwa kuwezesha *extension services* kwa vijijiji jirani hakuna mchango wa ranchi kwa maendeleo ya wananchi ni kidogo sana na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, badilini uongozi kwa kuruhusu wastaafu kustaafu, pia kuhamisha baadhi ya watumishi na kuajiri *graduates* wapya na kuwapa madaraka na majukumu mapya.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu kuwa suala hili litachukuliwa hatua za haraka kwa vile wanachi wa Kongwa wamechoka na *Management* iliyopo *for the past 30 years.*

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kuhusu uwekezaji katika malisho ya mifugo. Kwa kweli wenye mifugowanahamahama kutafuta malisho kwa vile wananchi hawajahamasishwa kuhusu njia bora na za kisasa za ufugaji.

Mheshimiwa Spika, nashauri wananchi wahasishwe na pia wapate mafunzo kuhusu njia za kisasa za ufugaji. Wananchi watengewe maeneo ya malisho na kuhakikisha nifugo yao inalishwa kwa maeneo *(portion)* sio mifugo huachiwa kula kila mahali. Wawe wanakula sehemu kwa sehemu wakati wakiendelea kula sehemu nyingine mpya, ile waliyokula awali majani yanaendelea kukua.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usindikaji, Serikali ihakikishe inaanzisha viwanda vya kusindika nyama Kikanda *(zones)* ili mifugo iliyopo katika kila Kanda iweze kupungua kutokana na usindikaji hii itasaidia kupunguza idadi kubwa ya mifugo kuweza kuisaidia kupata maeneo ya kukidhi idadi iliyopo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la maziwa, katika Mkoa wa Tanga, kuna viwanda vya *Tanga Fresh* na *Azania Dairies,* kwa kweli wananchi wanapenda sana kunywa maziwa, lakini kutokana na hali ya ukata wanashindwa kununua maziwa hayo.

Mheshimiwa Spika, ningeshauri bei ya maziwa ingepunguzwa kwa kiasi fulani na wananchi wahamasishwe kunywa maziwa kwa afya zao. kwa kweli kwa wastani wa unywaji maziwa, ulaji nyama na mayai ni mdogo sana kwa wananchi wa Tanzania hii ni hali mbaya kwa afya za wananchi. Bei zipunguzwe wananchi wamudu kununua na kula. Katika Mkoa wa Tanga, Wilaya ya Muheza kulikuwepo na ranchi inayoitwa *Geiglitz* ambayo miaka ya nyuma ilikuwa ikifuga ng'ombe na mbuzi ambao walikuwa wakisaidia sana katika utoaji wa maziwa na nyama kwa wananchi.

Je, Serikali bado inaendelea kuwa na ranchi hiyo au tayari imeitelekeza? Ranchi hii inaimarishwa ili kuleta ufanisi katika ufugaji wa kisasa.

Mheshimiwa Spika, mwisho naiomba Serikali iwawezeshe wakulima wadogo wadogo (wafugaji) kwa kuwapatia mafunzo ya njia bora za ufugaji na pia kuwapatia mikopo ili kuwawezesha kumudu shughuli zao za uzalishaji mali kwa maendeleo yao na nchi kwa jumla na kutekeleza lengo la MKUKUTA

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE: SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, mifugo ni muhimu sana si tu kwa maendeleo ya nchi, bali pia mazao ya mifugo yanajenga miili ya binadamu kama vile nyama na maziwa. Mifugo katika nchi hii hawa ng'ombe na mbuzi wamekuwa wakizagaa ovyo hivyo kuharibika sana kwa mazingira.

Wafugaji wadogo ambao ndiyo wengi wanahama hama ili kutafuta malisho ya mifugo yao. Lakini ni ukweli uliodhahiri kuwa mifugo inaingizia nchi hii pato kubwa sana na pia wafugaji wamekuwa kimbilio la wenye taabu, hivyo ni vyema kuwe na mikataba ya kusaidia wafugaji hawa ili wawe na mifugo yenye kutoa *product* nzuri.

Mheshimiwa Spika, kama walivyo binadamu, wanyama nao wanahitaji chanjo na dawa. Lakini cha ajabu pembejeo za uzalishaji wa mazao yatokanayo na binadamu ikiwemo dawa zimekuwa aghali kiasi kwamba wafugaji kushindwa kumudu gharama hizo. Hali hii imepelekea wafugaji kutokupata mazao mazuri ya mifugo hiyo badala ya ng'ombe mmoja kutoa lita 10 za maziwa kwa siku wanatoa lita moja hadi tatu tu.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na tatizo kubwa sana la vurugu, kupigana kati ya wafugaji na wakulima. Hii inatokana na kutotenga maeneo maalum ya wafugaji na matokeo yake kumekuwa na mwingiliano usio wa lazima kati ya makundi haya mawili.

Mheshimiwa Spaka, elimu ni muhimu sana si tu kwa wafugaji, lakini kundi hili ni muhimu sana kwani familia nyingi za wafugaji wako mbali sana na elimu. Ni muhimu basi waelimishwe ili waweze hata kutambua dalili za magonjwa, tiba na dawa za maradhi hayo.

Mheshimiwa Spika, kuna haja ya kuboresha mifugo hii ili iweze kuongeza tija. Wafugaji wapewe ruzuku ili waweze kufuga zaidi.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kushangaza kuona maduka makubwa hapa nchini *(supermarkets)* yakiuza nyama ya ng'ombe na kuku kutoka Afrika Kusini wakati nyama zetu zinalala na kuharibika kwenye maduka ya nyama *(Butchery).* Hivi hili ni halali na kwa mtindo huu kweli wafugaji hawa watapata fedha wapi?

Mheshimiwa Spika, tulikuwa na kiwanda chetu cha kusindika nyama *(Tanganyika Packers)* pale Kawe. Kiwanda kile kimekufa na hatujui hatma yake. Je, Serikali haioni kubinafsishwa kwa kiwanda kile na kukiacha kuwa gofu ni hatari kubwa kwa wafugaji?

Mheshimiwa Spika, suala la uhamasishaji wa kunywa maziwa ni zuri, lakini cha jabu maziwa mengi yanatoka nje ya nchi. Ni kwa nini Serikali imethamini zaidi maziwa ya nje ya nchi wakati yetu ya yanadorora na kuharibika?

Mheshimiwa Spika, suala la wataalam wa mifugo ni la msingi, siku za nyuma tulikuwa na wataalam wa mifugo *(veterinarians).* Siku hizi hawapo wala hawawatembelei wananchi kabisa. Tunaomba wataalam hawa wawepo ili kutoa ushauri na tiba kwa wafugaji.

Mheshimiwa Spika, mwisho nashauri kupitia Wizara hii wandeleze mifugo kwa kuiboresha ili wananchi waweze kunywa maziwa na nyama kwa afya bora. Lakini pia nashauri kuwa bajeti hii ni ndogo sana kwa kuboresha maisha ya Mtanzania. Ahsante sana.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kutujalia afya njema. Nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo, Naibu Waziri na wataalam wake wote kwa jinsi walivyoiandaa bajeti vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nitaanza na tatizo la uhaba wa mabwawa, malambo na majosho. Tatizo la uhaba wa mabwawa, malambo na majosho kwa ajili ya kuogesha na maji ya mifugo limekuwa ni kero kwa wafugaji na wachungaji katika maeneo mengi ya Tanzania, hivyo wafugaji na wachungaji wanatembea kilometa kadhaa ambapo pia inaathiri mifugo kupunguza muda wa kula majani. Hivyo naishauri Serikali ili kujenga majosho na malambo kwa kila kata na bwawa kwa kila Tarafa kukabiliana na tatizo hilo, hii pia itaongeza muda wa wanyama kupata malisho ya kutosha na kunenepa.

Mheshimiwa Spika, tatizo la mchanganyiko wa maeneo kwa pamoja na barua ya wafugaji na wakulima limekuwa kero kubwa la mgongano katika jamii, hivyo ni ushauri

wangu kwa Serikali kutenga maeneo maalum kwa wafugaji, kwani athari ya kutowawekea maeneo maalum wanaweza kuvamia hata ranchi za Serikali kulingana na taratibu.

Mheshimiwa Spika, nasisitiza wafugaji watakapotengewa maeneo maalum yawe ni maeneo mazuri na yenye majani ya kutosha na sio jangwa sambamba na upatikanaji wa maji, hivyo hili litaondoa ugomvi kati ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, vituo vya utafiti wa kuboresha mifugo ni muhimu sana, kwani hapa ni sehemu ya taaluma, hivyo ni vyema nikashauri wataalam wakadhibitiwa kwa kupatiwa mishahara mizuri na marupurupu ili kuepukana na wimbi la wataalam kukimbia sehemu zao za kazi na hasa wakapatiwa fedha, posho ya kazi ngumu kama ilivyokuwa zamani.

Mheshimiwa Spika, nazungumzia uboreshaji wa mifugo katika uzalishaji nyama na maziwa. Imebainika ng'ombe wa huzalisha nyama kidogo na maziwa ukilinganisha na nchi nyingine kama Botswana, hivyo wanashauri Serikali kuwa na kampeni maalum ya kuwapatia wafugaji na wachungaji ng'ombe bora wa kisasa kama wale *FI* wanaotokana na *Boran* (dume) na *Frisian,* ambapo wafugaji watagundua faida ya mara moja na wataachana na mazoea ya kuwa na mifugo mingi wakiamini ndio mtaji wao wa kupunguza umaskini, hivyo naishauri Serikali pia katika hili kutoa elimu ya kutosha kwa wafugaji na wachungaji.

Mheshimiwa Spika, lingine ninalotaka kueleza ni uzalishaji wa majani kwa ajili ya mifugo. Nchi yetu kwa kila kipindi huwa tunakabiliwa na ukame na unapelekea hata wakati mwingine ng'ombe kufa, kutokana na ukosefu wa majani na kulingana na idadi ya ng'ombe ilivyo kubwa Tanzania inahitaji malisho ya majani ni makubwa hivyo naishauri Serikali kulifanya shamba la Vikuge mkoa wa Pwani likazalisha zaidi kwa kukamilishiwa tatizo la maji, kwani shamba hilo linategemea maji ya mvua tu.

Ushauri wangu pia kwa Serikali katika hali ya kukabiliana na tatizo la uhaba wa malisho ya majani kwa mifugo ni vyema Serikali ikaanzisha mashamba mengine yaliyo na vyanzo vya maji ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, sababu ya Watanzania kutokunywa maziwa yanayotosheleza inatokana na umaskini wa kipato kwani mkulima aliyepata shilingi 1,000/= au shilingi 3,000/= anapanga matumizi ya familia bila kuangalia umuhimu wa maziwa na tatizo ni vijijini ambako ndiko kwenye idadi kubwa ya wananchi watimie, hivyo Serikali ilenge au ielekeze kampeni ya unywaji wa maziwa vijijini. Pia naishauri Serikali kutengeneza miundombinu ya barabara vijijini kwa mazao ya mifugo ili kuweza kufikisha mazao yao mahali kwenye soko na bei ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali katika hili kujenga viwanda vidogo vidogo vitakavyochuja maziwa kuwa siagi au mtindi na pia itapelekea vyama kupata ajira na hatimaye kupunguza umaskini. Hivyo nashauri Serikali wakati wa kujenga viwanda hivi wajenge kwenye maeneo yenye mifugo mingi mfano Shinyanga na Mwanza.

Mheshimiwa Spika, mwisho nataka kuuliza Serikali je, ng'ombe, mbuzi waliokufa wa wafugaji wadogo wadogo na wachungaji kipindi cha ukame uliopita ambao hali hiyo imepelekea kuwa maskini zaidi, hivyo Serikali ina mpango gani angalau wa kuwapatia kifuta machozi cha kuongeza tena mifugo yao katika hali ya kukuza ushuru na kupunguza umaskini. Naomba kuwasilisha.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza Wizara hii kwa hotuba nzuri iliyoainisha mikakati thabiti ya kuendeleza sekta ya mifugo. Naunga mkono hoja hii. Hata hivyo ninayo maoni yafutayo:-

(i) Utengenezaji wa malambo ya maji. Maeneo mengi ya mifugo ikiwemo Wilaya yangu ya Manyoni ni maeneo kame, hakuna maji ya kutosha kwa binadamu na pia kwa mifugo. Kwa hiyo, wafugaji hulazimika kuhama hama kutafuta malisho na maji ya mifugo. Tunaiomba Wizara iweke programu maalum ya kuchimba malambo kwa wingi na pia kufukua *(desilt)* malambo ya zamani yaliyojaa mchanga.

Katika bajeti ya leo, Wilaya ya Manyoni tumepangiwa fedha za kutengeneza lambo moja, tunashukuru sana kwa hilo, lakini kasi mpya inatakiwa katika kuongeza idadi ya malambo, iwapo Wizara italeta *catapillers,* wafugaji wapo tayari kuchangia dizeli na posho za madereva na mashine hizo kwa ajili ya kufukua malambo ya zamani yaliyojaa mchanga ambayo ni mengi sana. Manyoni yapo 40!

(ii) Mikakati ya ufugaji wa kisasa na kuboresha mifugo. Programu ya Waziri ya kuboresha aina ya mifugo itapata kasi iwapo huduma za uhamilishaji *(artificial insemination)* itasogezwa karibu na mfugaji katika Kanda au Mikoa. Hivi sasa wafugaji wengi vijijini hawaioni huduma hii wala hawajui namna ya kuipata. Jitihada zifanyike kumsogezea huduma hii pamoja na ile ya usambazaji wa mitamba. Hakika hatuwezi kuendelea na mifugo ya jadi katika karne hii.

(iii) Ukarabati wa majosho. Magonjwa yatokanayo na kupe bado yanaua mifugo kwa wingi sana vijijini. Uogeshaji wa mifugo kwenye majosho haufanyiki kwa kiwango cha kutosha kwa vile majosho mengi yameharibika, yanahitaji ukarabati. Wilaya ya Manyoni tunayo majosho zaidi ya 30 lakini yanavyofanya kazi ni chini ya hapo. Halmashauri peke yake haina uwezo wa kufufua majosho hayo kwa mara moja, inafufua majosho matatu hadi matano kwa mwaka! Tunaiomba Wizara iweke nguvu kubwa kusaidia Halmashauri kufufua majosho yote Wilayani ili kupigana vizuri vita dhidi ya kupe. Wafugaji wapo tayari kujinunulia dawa za kuogeshea mifugo pindi majosho yakikarabatiwa. Naunga mkono hoja hii.

**MHE. GAUDENTIA M. KABAKA:** Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Waziri Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa, Mbunge, Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Mbunge, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara yao kwa kazi ngumu lakini kazi nzuri wanayoifanya ili kuboresha mifungo na mazao yake. Ni vema nika-*share* na ninyi machache kuhusu eneo hili nikiwa kama mfugaji wa mjini, lakini pia kama mzawa ndani ya ufugaji. Mkoa wa Mara una mifugo mingi sana hasa tarafa za

Nyancha, Bunda, Gorango na Luoimbo kuna mifugo wengi sana ambao ni zao muhimu la biashara kwa wananchi hao.

Mimi mwenyewe bila ng'ombe nisingesoma. Lakini sasa majosho yote yaliyokuwepo yalikwisha kufa, wakati huo huo ndiyo chanzo kikubwa cha magonjwa karibu yote ya ng'ombe na mifugo wengine. Naomba Mheshimiwa Waziri, chonde chonde, hebu fufua majosho hayo ili mifugo isife ovyo na kuleta umaskini kwa ndugu hawa.

La pili ni kile kilichokuwa kinaitwa *Mara Milk.* Mradi huu ulisaidia kuwapatia wafugaji wa Mara soko la maziwa yao mengi sana. Vituo vile vilikuwa karibu na wananchi na hivyo kuwawezesha akinamama kubeba maziwa ya ziada na kwenda kuuza.

Je, kilitokea nini hadi mradi huu ukafa? Unaonaje ukafufuliwa maana watu binafsi wanajaribu kuleta kitu *similar* lakini hawakidhi haja ya mradi huo wa awali. Jamani hebu rudisheni *Mara Milk Project* kwa ustawi wa akina mama na familia zao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchangia hayo niwapongeze sana kwa mikakati mizuri na naunga mkono hoja!

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Spika, bila ya kuelekeza juhudi zetu kwenye mapinduzi ya ufugaji nchi yetu itaendelea kufaidika kidogo na rasilimali ya mifugo ambayo tumejaliwa kuwa nayo. Ni lazima kuwe na mikakati maalum wa kuanzishwa maeneo mbalimbali ya kupandwa malisho kwa ajili ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu Serikali, lazima Serikali ipange maeneo maalum katika nchi ambayo inaruhusiwa ufugaji wa ng'ombe hatika kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, katika kuleta mapinduzi ya kilimo ni lazima wapatikane wataalam wa mifugo (Wagani) bila hivyo juhudi zozote hazitazua matunda yanayohitajika.

Mheshimiwa Spika, kuwa na mifugo mingi pekee si njia ya kuhakikisha kipato zaidi kwenye sekta hiyo ya mifugo. Wizara ya Mifugo ndio nchi yetu itaweza kupata maendeleo ya haraka katika sekta hiyo ya Mifugo.

Mheshimiwa Spika, suala la Watanzania kutokunywa maziwa, kula nyama halisababishwi pekee na kuwa hawana mazoea ya kunywa au kula nyama bali pia uwezo na ughali wa bidhaa hizo pia unachangia kwa hivyo, njia pekee ya kuwa na bei nafuu ya bidhaa hizi ni kuwa na uzalishaji mkubwa. Njia bora ni ufugaji wa kisasa.

Mheshimiwa Spika, kama inavyoonekana, dawa kwa matumizi ya binadamu wakati wengine zinakuwa hazina kiwango kinachotakiwa kwa matumizi ya binadamu kwa hali hiyo, vile vile inawezekana hakuna kuingizwa dawa za mifugo ambazo hazina viwango.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Wizara husika ipo haja ya kufuatilia kuona ubora wa dawa hizo. Ahsante.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie juu ya ufugaji ng'ombe/uchungaji.

Mheshimiwa Spika, kuchunga kunaharibu mazingira, lakini kufuga kwa utaalam kunalinda mazingira. Kuwe na sheria mkulima/mfugaji awe na eneo lake. Kisheria ili mfugaji asimwingilie mkulima na mkulima asimwingilie mfugaji utaratibu huu utasaidia kukuza amani. Mkidharau ugomvi (vita) kati na mkulima na mfugaji utaendelea. Tabia ya kupigana, kuuwana kati ya wakulima na wafugaji itabadili tabia ya amani, undugu na kupendana, kutaendeleza uadui.

Naomba Serikali isilidharau suala hili. Tusifike tulipofikia kati ya wananchi na wezi/majambazi kwa kutoridhika na hukumu za Mahakama. Hivi sasa wananchi wamechukua sheria mikononi mwao. Imebadili tabia za huruma za wananchi hasa vijana wetu kuwa hivi sasa ni jambo la kawaida. Baada ya miaka mingi vijana hawa wanaweza kutumiwa ili kuondoa amani nchini.

Mheshimiwa Spika, tusipokuwa na majosho tunawafanya wafugaji watumie malambo yanayotumiwa kwa maji ya kunywa. Hii inasababisha afya ya binadamu kuathirika.

Mheshimiwa Spika, Kibaha hivi sasa ng'ombe wengi mwaka huu wanakufa kwa sababu ya ugonjwa wa *fungus* ya midogo na miguu. Wafugaji wanalazimika kununua dawa. Je, kwenye *epidemic* dawa hazitolewi bure? Kibaya zaidi maziwa ya ng'ombe hawa wagonjwa yanauzwa mitaani. Je, usalama na wananchi upo wapi?

Kuhusu kiwanda cha ngozi Kibaha, kinawaudhi wananchi. Kinatoa harufu sana. Je, atatusaidiaje Waziri kwenye tatizo hili?

Mheshimiwa Spika, kuhusu maziwa, je, maziwa yanayouzwa kutoka kwa wafugaji moja kwa moja (kwa wananchi) yana usalama kiasi gani? *Perstutazation* haifanyiki. Maziwa hayapimwi, yanauzwa mitaani, je, hii ni afya salama?

Mheshimiwa Spika, kuhusu mashamba ya majani, ningeiomba Wizara iandae mpango wa kuanzisha mashamba ya majani. Wafugaji waelimishwe na wakopeshwe ili wanunue majani badala ya kuvamia maeneo ya watu.

Mheshimiwa Spika, naomba nishauri kuwa Mkoa wa Pwani ni Mkoa mzuri wa kuanzisha mashamba ya majani. Hali ya hewa ya Mkoa huu ni nzuri kwa majani. Uotaji wa majani umesababisha ukulima wa mkoa huu kuwa mgumu. Wanalazimika kupalilia mashamba zaidi ya mara tatu. Naomba wakulima wa Mkoa wa Pwani wafunzwe kulima mashamba ya majani. Majani yatakuwa bidhaa ya biashara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu shamba la *Narco,* Vigwaza, je, mpaka sasa shamba hilo limeamuliwaje? Shamba lina maeneo makubwa ambayo hayatumiki, ni maficho ya majambazi, chatu na wanyama wakali, je, wananchi wanaolizunguka shamba hili wananufaikaje?

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote Wizarani kwa kazi nzuri mnayofanya.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu la Hai tunao wafugaji wa aina mbili, kwanza wale wanaofuga kwa wingi maeneo ya tambarare hasa Masai na pili wale wanaofuga kwa uchache *(zero grassing)* maeneo ya milimani hasa wachaga.

Mheshimiwa Spika, ninachoomba au kushauri ni huduma kutoka Wizarani kwa maeneo yote mawili. Kwa maeneo ya tambarare kuna mahitaji mengi ya majosho, madaktari wa mifugo pamoja na dawa. Kwa upande wa milimani tunaomba kwa kushirikiana na Wizara tupate mbegu mpya ya ng'ombe wa mfano waliopo Seliani , Arusha ambao wanatoa maziwa na nyama kwa wingi na hawa ni wa *zero grassing*.

Mheshimiwa Spika, upande wa mifugo, mbuzi tunaomba kushirikiana na Wizara kupata na kusambaza mbuzi wa kisasa wenye kutoa maziwa mengi na nyama. Kwa ujumla Wizara kwa kushirikiana na Wizara zingine kutoa elimu kwa wafugaji nchi nzima juu ya umuhimu wa kupunguza mifugo kwa maana ya kwamba ni shughuli zipi za maendeleo wanazoweza kuzifanya kwa kutumia pesa zitakazopatikana baada ya kuuza mifugo yao kwa mfano, biashara mbalimbali na ujenzi wa nyumba bora pamoja na kuweka akiba.

Pili, kuhusu maeneo ya ufugaji. Naishauri pia Wizara kwa kushirikiana na Wizara nyingine kutenga maeneo ili kuepusha migogoro na wakulima. Naomba kupatiwa wawekezaji katika biashara ya mazao ya mifugo hususan maziwa kwani Wilayani kwangu upatikanaji wa maziwa ni mkubwa na wa uhakika maeneo ya uwekezaji huo yapo. Je, kiwanda cha ngozi kule Mjini Moshi kitafufuliwa, kwani hakifanyi chochote. Karibuni sana Hai na tunawaahidi kuwapa ushirikiano wa aina zote. Mungu awabariki nyote.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii walioshirikiana kuiandaa hotuba hii na ni hotuba inayoashiria kwa uwazi maendeleo ya mifugo.

Ni imani yangu kuwa watendaji na watumishi wa Wizara hii katika ngazi zote za utumishi watashirikiana huku wakitumia uzoefu na utaalamu wote kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya kuyatekeleza yale yote waliyoyaainisha katika kitabu cha hotuba ya bajeti ya Wizara hii. Nami kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya wapigakura wa Jimbo la Kwimba tunawaahidi kuwaunga mkono na kushirikiana nao kwa karibu kadri taratibu na uwezo wetu utakavyoruhusu.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja hii. Pamoja na hayo napenda nichangie maoni yangu kama ifuatavyo:-

Moja, kuwapo kwa Wizara hii kama lilivyo jina lake Maendeleo ya Mifugo, inaonesha haja ya kuendeleza mifugo na huna budi kutumia gharama kutekeleza maendeleo hayo. Taswira unapoongelea juu ya maendeleo ya mifugo huna budi kuwa na makundi matatu kichwani ya kuendeleza.

Pili, kuhusu mifugo. Mifugo ya aina mbalimbali kama hotuba ya Waziri inavyoainisha na mifugo hii ina mahitaji mbalimbali kwangu mimi mahitaji muhimu kwa mifugo ni pamoja madawa, maji na vyakula.

Kuhusu dawa, naipongeza Wizara kwa kuonesha kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya dawa. Nafikiri ingefaa kwa nia njema ya kuwasaidia Waheshimiwa Wabunge na wananchi ingeonesha kiasi hicho ni wastani wa Tanzania shilingi ngapi kwa mifugo. Hii itaonesha uwazi zaidi kiasi kitakachotengewa kwa kila Halmashauri ya Wilaya. Pia itaweza kumsaidia anayetaka kujua Wizara itajikita katika maeneo yapi kwa upande wa dawa na maeneo mengine kuachwa kwa wafanyabishara na watunza mifugo wenyewe.

Kuhusu maji, ni hitaji lingine la mifugo vile vile ingefaa Wizara ioneshe imetenga kiasi gani cha fedha kwa ajili ya maji na hiyo itatolewa kwa malambo /mabwawa kadhaa, malambo makubwa, ya kati kadhaa kwa wastani wa lambo kubwa moja kwa mifugo kadhaa na hivyo fedha hizo zikagawiwa kwa Halmashauri ya Wilaya kulingana na mifugo iliyoko. Kama inavyojulikana kuwa si vyema kutumia sehemu moja kwa binadamu na mifugo mpaka pale inapokuwa lazima, nafikiri japokuwa ni njia moja ya kupunguza gharama siyo jambo rahisi kuafutilia na kuratibu kwa urahisi kusambaza fedha ya maji kwa Wizara za Kilimo, Maji na Maendeleo ya Mifugo. Kilimo wangetengewa fedha za kilimo cha umwagiliaji. Wizara ya Maji ingeshughulikia maji kwa ajili ya binadamu na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo ikashughulikia malambo na majosho tu na hivyo ingekuwa rahisi kugawa fedha hiyo katika Halmashauri za Wilaya kulingana na mifugo waliyonayo. Utaratibu huo utarahisisha ufuatiliaji kwa upande wa Wabunge na wananchi miradi waliyonayo kuhudumia mifugo katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu watunza mifugo. Watunza mifugo wako wa aina mbili, wafugaji na wachugaji. Hitaji kuu kwa watunza mifugo wa aina zote ni elimu kuhusiana na mifugo yao. Mtunza mifugo anatakiwa kuelimishwa kuhusu uhusiano kati ya malisho na mazingira na hifadhi ya chakula hususan ukame unapotokea. Ili mtunza mifugo apate elimu hii muafaka hana budi kukutana mara kwa mara na mtaalamu wa mifugo/afisa ugani kwa njia ya warsha, semina na mikutano mbalimbali na ili afisa huyu aweze kutekeleza shughuli zake kikamilifu licha ya haki zake za kiajira, hana budi kuwezeshwa kuweza kumfikia mtunza mifugo huyo aweze kuwa na chombo cha usafiri cha uhakika na awe na taaluma muafaka kwa kazi zake. Hivyo elimu yake iwe inarutubishwa mara kwa mara kwa mafunzo na kozi fupi.

Mheshimiwa Spika, hali halisi ya Wilaya ya Kwimba hivi sasa Wilaya hii ina ng'ombe 390,891, mbuzi 105,048, kondoo 79,330, punda 79,300, kuku 196,311, bata 65,436, mbwa 14,401 na nguruwe 100.

Mheshimiwa Spika, mifugo hii yote inamilikiwa na wananchi waliona katika vijiji 111 lakini tunao maafisa ugani 27 tu, hivyo tuna upungufu wa watumishi katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na upungufu huo wa watumishi yanahitajika malambo makubwa mapya matano, malambo ya kati 10, kama tungaliezeshwa tunayo malambo makubwa 5 na malambo ya kati kumi. Takwimu hizi zinaonesha kuwa maendeleo ya mifugo hayataweza kwenda sambamba na matarajio ya mipango ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo kutokana na upungufu huo. Hivyo kwa niaba ya wafugaji na wachungaji wa Wilaya ya Kwimba, naomba Wizara ituwezeshe kupunguza upungufu huu. Naunga hoja mkono.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Waziri Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa, Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Katibu Mkuu na watendaji wote katika Wizara hii kwa kuandaa bajeti hii. Naamini wametumia muda wao vizuri kuhakikisha kuwa yale yote yaliyo ndani ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 yanaanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie katika maeneo yafuatayo, maeneo ya kuchungia ni kweli kabisa wafugaji wetu wanahangaika, lakini Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 ilibainisha kutenga maeneo.

Mheshimiwa Spika, wasi wasi wangu ni namna ya upatikanaji wa maeneo haya kwani maeneo mengi ambayo yanafaa kutengwa ni maeneo ambayo tayari ni hifadhi za Halmashauri .

Mheshimiwa Spika, endapo maeneo hayo tutayagawa, tutaanza kupingana na sera ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anijibu katika Jimbo la Bukombe tunazo hifadhi za Halmashauri ya Wilaya ambazo pia ni hatari sana kwa usalama wa wananchi.

Je, anakubaliana na mimi kwamba maeneo hayo tuyatenge kwa wafugaji? Mfano msitu kati ya Ushirombo na Runzewe, msitu wa Runzewe huko Ilyamchele.

Mheshimiwa Spika, nichangie eneo la mabwawa/majosho. Pamoja na kuandaa utaratibu wa kutenga maeneo ya wafugaji, naomba tupatiwe malambo makubwa katika kijiji cha Bulega, Ibambilo, Nampalahala na ikiwezekana kila Kata ili kuondokana na upungufu wa tatizo la maji.

Mheshimiwa Spika, Serikali ituangalie sisi Wilayani Bukombe kwa sababu *growth rate* ni kubwa 7.4 ikisababishwa na ongezeko la wafugaji.

Mheshimiwa Spika, niongelee ongezeko la wafugaji katika Wilaya/Jimbo la Bukombe, ni kweli kabisa wafugaji wanaongezeka sana katika Wilaya ya Bukombe. Tunalo wimbi la ndugu zetu aidha, Wanyarwanda au Warundi wenye asili ya Kitusi wanahamia katika maeneo yetu husasan yaliyo jirani na hifadhi zetu za Kigosi/*Myowosi Game Reserves.*

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ifanye utaratibu wa kuwasiliana na wananchi wa Kata ya Runzewe na Uyovu ili kuweza kuwabaini wafugaji wahamiaji wenye asili ya Kitusi waondoke. Pasipo kufanya hivyo hata harakati za kutenga maeneo hazitasaidia, kwani wanayo mifugo mingi na uharibifu wao ni mkubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee suala la kuondoa wafugaji katika vyanzo vya maji. Tuandae utaratibu mbadala na tutoe muda wa kutosha kwa nini wafugaji tunawafukuza bila kuwaandalia wapi waende.

Mheshimiwa Spika, nilipata taarifa si rasmi kuwa wafugaji waliofukuzwa maeneo ya vyanzo vya maji wameelekea sehemu za Masasi, huko nako wamefukuzwa. Je, Serikali haitambui kwamba mifugo ni moja ya utajiri wetu? Au tunataka mifugo hii Mungu atunyang’anye?

Mheshimiwa Spika, tusipoangalia hili kwa makini maisha bora kwa kila Mtanzania hatutayafikia. Kwa sababu mifugo yetu inaondoka kwenda nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, wafugaji ni watanzania ndani ya nchi hii tuwahamishe, tuwaandalie sehemu nzuri na tuweze kupata wawekezaji haraka wanaoweza kupandishi bei ya mifugo hii na mfugaji awe tayari kuuza na kubadili shughuli.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja ila Mheshimiwa Waziri anipatie majibu ya maswali yangu. Ahsante.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, mimi napenda kukufahamisha Mheshimiwa Waziri kwamba Mkoa wa Kagera ni miongoni mwa Mikoa ya Tanzania yenye mifugo mingi, hasa ng’ombe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ubinafsishaji wa ranchi ya Kagoma katika Wilaya ya Muleba, Jimbo la Muleba Kaskazini, Kata ya Ngenge umewaacha wananchi zaidi ya 10,000 wakiwa hawana mahali pa kulima, kuchunga mifugo yao, wala umiliki wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Ngenge na Kata yenye jumla ya vijiji vinne vikiwemo Rutoro, Ngenge, Kishuro na Rwigembe. Vijiji vyote isipokuwa Rwigembe vimeathirika vibaya sana na umilikishaji wa ranchi ya Kagoma.

Mheshimiwa Spika, vijiji vya Rutoro, Ngenge na Kishuro vimesajiliwa kisheria na viko hapo zaidi ya miaka 12. Kila kijiji kina shule ya msingi na wananchi wamejenga makazi yao ya kudumu. Licha ya kuwa ni wakulima, pia ni wana mifugo mingi ya ng’ombe na mbuzi na kondoo.

Mheshimiwa Spika, unaposema au unapoagiza kuwa wenyeji waondoke, je, watakwenda wapi hawa sio wageni ni Watanzania wenyeji? Vitalu 291/7, 291/6, 291/8, 291/9, 291/10, 291/11, 291/12, 291/13 na 291/5, Serikali ione uwezekano wa kuwaachia wananchi wenyeji wanaoishi katika vitalu hivyo waendelee kuishi na kufanya shughuli zao za kilimo, ufugaji na makazi.

Mheshimiwa Spika, haikuwa rahisi kwa wananchi kununua vitalu hivi kutokana na jambo lenyewe, halikuwa wazi kwa wenyeji wahusika, pia gharama kubwa za kuomba vitalu hivyo. Zaidi haikuonyeshwa wazi athari ambazo zingejitokeza baada ya ubinafsishaji kama ingekuwa wazi, tungechukua tahadhari mapema.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ilitazame hili kwa jicho la huruma na dhana ya kuwawezesha Watanzania kuinua hali zao za maisha ukiwaondoa wanavijiji hawa sasa, kwa vyovyote watarudi nyuma kimaisha kwa miaka mingi. Naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Spika, kwanza nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika katika Kikao cha Bunge cha leo tukiwa wazima na wenye afya njema. Namwomba Mwenyezi Mungu atuzidishie uzima na afya njema.

Napenda kukupongeza wewe binafsi pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuliongoza Bunge letu kwa ufanisi mkubwa. Aidha, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa hotuba nzuri iliyowasilishwa mbele yetu. Pia nawapongeza wananchi wa Jimbo la langu la Mtambwe kwa kunichagua kwa kura nyingi kuwa Mbunge wao. Naahidi kushirikiana nao katika suala zima la maendeleo ya Jimbo letu na Taifa kwa jumla.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina rasilimali kubwa ya mifugo kiasi cha milioni 66.3. Miongoni mwa mifugo hiyo ni ng’ombe, mbuzi, kondoo, nguruwe, kuku na kadhalika. Sekta ya mifugo inachangia kwa kiasi kikubwa pato la wafugaji pamoja na Taifa kutokana na mazao ya mifugo kama vile nyama, maziwa, ngozi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mifugo mingi iliyopo nchini, lakini hali ya wafugaji ni ya umaskini mkubwa. Hii inatokana na ukosefu wa taaluma ya ufugaji. Naiomba Serikali na Wizara iwe na utaratibu wa kukutana na wafugaji ili kutoa taaluma ya ufugaji bora ili ufugaji uwe na manufaa zaidi kwao binafsi na pia kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, wananchi pia wapewe taaluma ya kutumia mazao ya mifugo kama vile nyama, maziwa, mayai na kadhalika kwa ajili ya kujenga miili yao pamoja na afya zao.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na malalamiko mengi kuhusu uharibifu wa mazingira kutokana na mifugo. Uharibifu wa mazingira unamgusa kila mtu kwa njia moja ama nyingine. Ni vyema tukakaa chini

Mheshimiwa Spika, kuhusu wataalamu wa ugani ni muhimu sana wawepo wa kutosha, wenye ujuzi na maarifa, wenye vitendea kazi, wenye kulipwa vizuri, wenye njia nzuri za mawasiliano na kadhalika. Haya yatasaidia kuwa na ufugaji bora na wenye kuleta tija. Ahsante sana.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi zangu za dhati kwa Waziri, Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa, Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa na Katibu Mkuu kwa kuwasilisha hotuba yao ya bajeti ambayo ni nzuri. Nawatakia kila la kheri katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu mkubwa niuelekeze kwa kuiomba Wizara ifanye kazi kubwa kuelimisha jamii juu ya mifugo endelevu. Mpaka sasa kwa bahati mbaya jamii ya wafugaji bado wanaendeleza dhana ya kuwa na mifugo mingi ambayo haina faida. Wafugaji wengi bado ni watumwa wa mifugo yao. Hawaelewi kuwa wao ni matajiri na wakiuza mifugo yao ya ziada watakuwa mamilionea, lakini wafugaji wengi ni maskini wa kutupwa. Naona Wizara bado haijafanikiwa kuwafanya wafugaji wabadilike ili ufugaji uwabadilishe wawe na maisha bora ziadi kuliko ya kutangatanga.

Hivi karibuni tumeona jinsi gani mifugo ya Kusini ilivyoharibu Bonde la Usangu Mbeya hasa katika Wilaya ya Mbarali. Chanzo kikubwa cha mito ya *Great Ruaha,* Ruaha, Bwawa la Mtera na Kidatu yaani Ziwa la Ihefu, limeharibiwa na uvamizi wa wingi wa mifugo. Nchi sasa imegutuka na kuanzisha *special operation* kuondoa mifugo katika maeneo hayo kutokana na kukauka kwa chanzo cha Ihefu, Bwawa la Mtera na Kidatu. Ng'ombe kwa malaki wameharibu kwa kiasi kikubwa vyanzo vya maji na kuleta uharibifu mkubwa wa mazingira unaopelekea kuleta jangwa katika maeneo haya ya ukulima wa mpunga.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuzidi kwa mifugo katika maeneo ya wafugaji nchini kumekuwa na minong'ono mingi kwamba mifugo hii sasa ihamishwe mikoa ya Kusini ambako bado kuna maeneo mengi mazuri ya malisho.

Mheshimiwa Spika, napenda kutamka kuwa minong'ono hiyo iishie kuwa minong'ono, hatua zozote za kuhamishia mifugo hii Kusini isichukuliwe. Hatua ya namna hiyo itapelekea kuhamisha tatizo kutoka maeneo hayo kuhamishia Kusini. Hii sio

busara hata kidogo. Ufumbuzi wa tatizo la mifugo mingi ni kuuza mifugo hiyo. Kule Usangu malaki ya mifugo iuzwe na hata nyama yake iuzwe nje ya nchi. Hakuna maana wala sababu ya kueneza uharibifu wa mazingira katika maeneo mengine ya Tanzania ambayo bado ni mazuri. Tusieneze jangwa nchini kutokana na wafugaji wachache wenye uroho wa kuwa na mifugo mingi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo Wizara ya mifugo iwe na mipango endelevu ya kuwa na mashamba ya ng'ombe wa kisasa na ufugaji wa kisasa uenezwe Kusini. Nasisitiza kuwepo na utaratibu mzuri wa kisayansi wa kueneza mifugo katika maeneo haya na sio kuswaga tu ng'ombe toka maeneo yanayowafukuza hao ng'ombe wa ziada na kuja kuharibu mazingira ya Kusini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa mawaidha haya, naunga mkono hoja.

**MHE. ESTERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Dr. Shukuru Jumanne Kawambwa, kwa kuwakilisha hotuba nzuri. Nawapongeza Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, wafugaji waliokuwa wameingia kwenye bonde la Ihefu wameitikia wito wa kuhama eneo hilo kwa hiyo, pamoja na uongozi wa mkoa wanastahili kupongezwa kwa kuitikia wito wa Serikali. Tatizo wanalopata wafugaji hawa ni maeneo ya kwenda. Serikali itamke mikoa ambayo wafugaji wanapaswa kwenda na njia ya kupita. Hali kwa sasa haielekei kuwa nzuri hasa ikifika mwezi wa nane wakati ambao mito yote ya muda itakuwa imekauka hali itakuwa mbaya sana. Kwa sasa kuna kundi kubwa sana la ng'ombe liko kwenye vijiji vya Kata ya Madibira, Ubaruku, na Utengule Usangu wanalisha kwenye mashamba ya wakulima. Mbarali hakuna maeneo yanayoweza kutengwa kwa mifugo kwa mwaka huu sababu ya ukame.

Mheshimiwa Spika, Wizara isaidie katika kuboresha masoko ya mifugo na mazao ya mifugo kwani ndio njia pekee katika kupunguza mifugo.

Mheshimiwa Spika, elimu ni muhimu kwa wafugaji, niishauri Serikali iweke mkakati wa haraka wa kutoa elimu kwa wafugaji ili waone umuhimu wa kuuza mifugo na kuwekeza kwenye hisa na sehemu mbalimbali ambazo zitazalisha faida za akiba zao.

Mheshimiwa Spika, wataalam wa mifugo ni wachache sana kwenye Halmashauri zetu na hawana vyombo vya usafiri kwa mfano Mbarali wana mtalaam mmoja tu, wengine wote ni wa kilimo. Nashauri sasa iangalie upya jinsi ya kuwa na maafisa mifugo wa kutosha kwenye Halmashauri zetu ili wasaidie kutoa elimu.

Mheshimiwa Spika, uchimbaji wa malambo, kiasi cha shilingi 3,000,000/= kinachotolewa na Serikali kwa lambo moja ni kidogo sana kwani gharama za lambo moja ni zaidi ya shilingi 9,000,000/=. Wakati kama huu ni muafaka katika kuhamasisha uchimbaji wa malambo ila masika ikifika maji yaweze kuvunwa. Naunga mkono hoja.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii kwa namna alivyoandaa hotuba yake na alivyoiwasilisha.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imejaliwa kuwa na mifugo mingi sana, lakini bado Serikali yetu haijawaandalia mazingira mazuri wafugaji wetu jambo ambalo linapelekea kuendelea kuwa na wafugaji ambao pamoja na kumiliki mifugo mingi lakini bado mfugaji ni maskini sana na afya yake pia kuendelea kuwa mbaya.

Mheshimiwa Spika, ulimwengu wetu huu wa kileo kila jambo linaendeshwa kisayansi hivyo tunahitaji Serikali kwanza ifanye sensa ya kujua tuna idadi gani ya wafugaji na idadi gani ya mifugo tuliyonayo na hatimaye iwe rahisi kuwafikia katika maeneo yao ili kuwapatia taaluma ya kutosha na kuwapatia huduma zilizo bora, ili kuinua hadhi ya mfugaji.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha na kuboresha huduma za wafugaji naiomba Serikali itenge maeneo makubwa ya ardhi na kuyaendeleza kuwa mashamba ya malisho.

Mheshimiwa Spika, tukipanua shughuli za ufugaji ina maana tunaongeza ajira. Pamoja na wingi wa mifugo tulionao nchini bado kuna haja ya kupanua sekta hii kwa nia ya kuongeza ajira ili kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, ili kulifanikisha hili, Serikali ingeanzisha mfuko maalum kwa ajili ya wafugaji na wananchi wengine nchini kote wote wenye nia ya kujiajiri katika sekta hiyo kwa ajili ya ufugaji wa kibiashara. Mfuko utaweza kuwasaidia wafugaji kuanzisha ufugaji wa kisasa wa kibiashara utaweza kuwapa uwezo wa kununulia mitambo bora na kuanzisha mashamba ya malisho, visima, ujenzi wa mabanda na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, wafugaji wetu kama hawa na wale wadogo wadogo wanaweza nao kupatiwa mikopo ili kujiendeleza.

Mheshimiwa Spika, wafugaji wetu wana usumbufu hata wa kupatiwa chanjo ama tiba kwa ajili ya mifugo yao. Naomba tuwaangalie kwa jicho la huruma wafugaji wetu kwa faida yao na Taifa letu. Nashukuru sana.

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze Waziri kwa hotuba nzuri. Suala la kuboresha ufugaji katika nchi yetu ni muhimu sana na tunamshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, kwa kuunda Wizara kamili ya Maendeleo ya Mifugo.

Mheshimiwa Spika, matatizo ya muda mrefu yanayoathiri mifugo kwanza ni maeneo ya wafugaji kuingiliwa na wakulima. Kwa mfano katika jimbo langu la Babati Vijijini maeneo ambayo kwa asili ni ya wafugaji, wakulima wameyavuruga kwa kilimo ambacho hata hivyo hakina tija.

Mheshimiwa Spika, maeneo yenyewe ni hususan katika kata ya Nkaiti - Minjingu, Olasiti (Oltukai) na maeneo karibu yote kutokea/kuanzia Kibaoni (Olasiti) hadi Makuyuni Wilayani Monduli. Kwa hakika maeneo yote hayo hayazalishi chochote kwa kilimo, lakini ni maeneo yanayofaa kwa mifugo. Naomba waachiwe wafugaji na mifugo yao.

Tatizo la pili ni upatikanaji duni wa maji. Maji hayapatikani wakati wa kiangazi, lakini wakati wa masika maji mengi yanabaki yakitiririka baharini, je, Serikali ni lini itaweka mkakati wa kujenga malambo na mabwawa mahsusi kwa ajili ya wafugaji na mifugo? Naiomba Serikali izingatie umuhimu huu.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ni la ukosefu wa uhamasishaji wa ufugaji wa kisasa hasa ng'ombe wa maziwa. Lakini pia Serikali iwezeshe/irahisishe usindikaji wa maziwa ili kuboresha thamani ya maziwa (kwa njia ya viwanda vidogo) vijijini ili yaweze kusafirishwa mbali kwenye soko.

Mheshimiwa Spika, baada ya machache haya naunga mkono hoja ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, kimuundo Wizara ya Maendeleo ya Mifugo inajitegemea lakini kwenye Manispaa na Halmashauri za Wilaya muundo wa Idara bado umeziunganisha kilimo na mifugo na kwamba Mkuu wa Idara ni mmoja. Muundo huu unapunguza ufanisi na kasi inayostahili ya kuendeleza mifugo yetu.

Mheshimiwa Spika, je, Wizara haioni sasa kuwa ni wakati muafaka kwa kuwepo na Idara ya Mifugo inayojitegemea ili kuongeza tija?

Mheshimiwa Spika, mwisho, nampongeza sana Waziri Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa. Wote mmetoka kwenye kazi za kitaalam, sasa mnajifunza Ubunge na Uwaziri, pamoja na vikwazo vingi mnatimiza wajibu na majukumu yenu vyema, hongera sana.

**MHE. MUSTAFA H. MKULO:** Mheshimiwa Spika, Jimbo la Kilosa limeingiliwa na jamii za wafugaji, kuna wafugaji zaidi ya 4,000. Mifugo inaharibu mazao ya wakulima na wakulima wanawachukia wafugaji. Kumewahi kutokea mapigano mara kadhaa na mara moja walikufa zaidi ya wakulima 30 katika kijiji cha Mkuyuni, Kata ya Rudewa kuna uharibifu mkubwa wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, nashauri Mheshimiwa Waziri apange kutembelea Jimbo langu na Wilaya ya Kilosa ili ajionee hali ilivyo ili aweze kutafuta ufumbuzi wa matatizo haya. Nashukuru na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nawatakia kazi njema.

Je, ni lini kutajengwa kiwanda cha nyama hapa nchini hasa kile cha Shinyanga?

Mheshimiwa Spika, dawa za kuogeshea mifugo zinauzwa kwa bei kubwa, je upo utaratibu wa kuweka ruzuku?

Mheshimiwa Spika, mpango wa ujenzi wa mabwawa au malambo Wilaya ya Nzega unahitajika sana hasa katika Tarafa za Puge na Nyasa.

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa, Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa na wafanyakazi wote wa Wizara hii muhimu kwa umahiri, ufanisi na kwa uzalendo wa hali ya juu. Hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa moyo wake na utaratibu alioweka wa kuwa karibu na Waheshimiwa Wabunge katika kutatua mataizo mbalimbali yanayowakabili wafugaji hapa nchini.

Napenda kukumbusha tena kuwa Jimbo la Rorya lina jumla ya mifugo 418,308 ikilinganishwa na idadi ya mwaka 2000 hadi 2004, biashara ya mifugo kupitia minada imeweza kuwaingizia kiasi cha shilingi 3,881,531,400 pato kwa wananchi. Hata hivyo, huduma za sekta ya mifugo bado unakabiliwa na matatizo makubwa. *DADPS* wale *THSAF* peke yake haiwezi kutanzua hata baada ya miaka 15 ndiyo maana nilikuletea ombo maalum katika barua yangu niliyokuandikia Februari 16, 2006.

Mheshimiwa Spika, nilipokuwa naandika barua yangu nilijua kuwa Serikali ya awamu ya tatu katika mwaka wa fedha 2003/2004 ilitenga shilingi milioni 25.0 kwa ajili ya majosho ya Wilaya ya Tarime kwa ajili ya ukarabati. Mimi mwenyewe nilimwomba Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Maji ambaye sasa ni Mheshimiwa Waziri Mkuu na alisaidia sana kufanikisha ombi la wananchi wa Jimbo la Rorya, namshukuru sana.

Mheshimiwa Spika, najua pia mwaka 2005/2006 Serikali ilitenga shilingi milioni 14.1 kwa ajili ya ukarabati wa majosho ya Obwera ambayo ukarabati haujakamilika, Komuge - Ranyamamulike, Nyanduga - Ranyamamulike na majosho mengine yaliyotajwa katika barua ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo.

Napenda kukuhakikishia kuwa pamoja na wafugaji, wananchi wa Jimbo la Rorya kukabiliwa na tatizo hili la majosho mabovu yapatayo 17 na majosho 11 ambayo yanafanya kazi chini ya 30% bado wataendelea kutoa michango yao mikubwa katika kuendeleza na kuboresha huduma za mifugo hata baada ya majibu ya kukatisha tamaa niliyoandikiwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo.

Mheshimiwa Spika, nimetoa taarifa kwa wafugaji wa Jimbo la Rorya kuwa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wamekubali kushughulikia matatizo yao ya zaidi ya miaka 30 kwa kuendelea kujadiliana na Mbunge wao kuona jinsi gani Serikali ya awamu ya nne inaweza kuwaunga mkono katika jitihada zao.

Mheshimiwa Spika, nimefarijika sana kwa jinsi mlivyonitia moyo katika majibu yenu, nasema ahsante sana na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napongeza Serikali ya awamu ya nne chini ya usimamizi wa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete. Pia sina budi kupongeza Wizara hii kwa hotuba nzuri, nampongeza sana Waziri.

Mheshimiwa Spika, mradi wa kopa ng'ombe, lipa ng'ombe ni mradi mzuri sana kwa wananchi lakini bado mradi huu una uchache katika utekelezwaji wake. Naomba Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na kwa usimamizi wa Waziri mradi huu uongezeke kusambazwa kwa Wilaya zote vijiji, mitaa na hata kwa kila mfugaji ili ufugaji ukue kwa kiwango na dawa wapelekewe msaada au kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Mifugo itoe elimu (semina) Mikoani, Wilaya na Majimboni kwani ufugaji bila elimu ufugaji ni mfupi, wafugaji waelimishwe kwa ufugaji mzima.

Mheshimiwa Spika, wafugaji wakubwa ni wafugaji wa kupongezwa na kutunzwa sana kwani wanawezesha wananchi kupata maziwa, nyama (kitoweo), mbolea na kadhalika.

Kwa hiyo, naomba Serikali kuwa wananchi/wafugaji waenziwe, wawezeshwe kifedha na wapewe maeneo ya kufugia na wasisumbuliwe ili kuboresha ufugaji kwa manufaa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mabwana mifugo wapewe uwezo wa kitalaam na kuwawezesha kutembelea kila mfugaji katika maeneo yao na kuwasaidia wafugaji kutoa ushauri na kuwahamasisha kwa utalaamu mzima na kuondokana na ufugaji wa zamani na tuwe waboreshaji wa kileo kuendana na wakati.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Magogoni naunga mkono hoja hii.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ili nami nichangie hoja iliyopo hapo juu.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niende moja kwa moja kwenye hoja hii. Tatizo kubwa kabisa katika Wizara hii ni chanjo, kwani ng'ombe wanapopata chanjo, ng'ombe wengi wanakufa pale pale, wakichomwa kama leo, kesho yake wanakufa. Hii ndiyo sababu wafugaji wengi wanashindwa kupeleka ng'ombe/mifugo yao kwa ajili ya chanjo.

Mheshimiwa Spika, mimi nashauri wataalam wetu, kama wapo hawazingatii dawa ipi kwa maradhi yapi. Enzi za ukoloni mambo kama haya hayakuwepo au yalikuwa kidogo.

Hivyo mfugaji anakuwa anashindwa kupeleka mifugo yake kwa chanjo kwani mifugo itakufa na ukiacha apigwe faini mfano Kata ya Sigili, Kitongaji cha Bulende, wafugaji walichangia gharama za chanjo lakini hawakupeleka ng'ombe kwa chanjo, sababu ya kuogopa ng'ombe wao watakufa na walilipa faini. Wafugaji wengine kama ana ng'ombe 20 anapeleka ng'ombe watano kwa sababu ya kuogopa ng'ombe wake watakufa.

Mheshimiwa Spika, hivyo Wizara ya Maendeleo ua Mifugo ifanye utafiti hasa ili wanapotoa chanjo ilenge ugonjwa husika mfano ugongwa wa midomo, miguu na sotoka, wafanye utafiti kamilifu na hivyo kutoa chanjo inayohusika na hivyo kuzuia vifo visivyo vya lazima, sababu hiyo ndiyo itasababisha wafugaji warudishe imani na hivyo kupeleka mifugo kwa chanjo siyo kuficha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu majosho, Serikali ijenge majosho mapya na ya zamani yakarabatiwe na dawa ya kuongesha ng'ombe au mifugo zitolewe bure.

Mheshimiwa Spika, wafugaji hununua dawa feki na wakiogesha ng'ombe au mifugo, kupe au viroboto hawafi. Naomba Serikali itoe dawa bure kama ilivyokuwa zamani enzi za wakoloni na enzi za Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Naomba turudi nyuma tutoe dawa hizi bure.

Mheshimiwa Spika, kuhusu malambo, tutakapoboresha majosho yanaendana na malambo. Hivyo unapoweka majosho ni lazima maji yaani malambo yawepo pia ili mifugo inapoogeshwa dawa, basi mifugo iwe na malambo ili mifugo iweze kunywa maji pale pale.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Jimbo langu la Bukene lina mifugo karibu lote, kwa kuwa nimeshayataja katika hotuba za Kilimo na Chakula na hotuba ya Waziri Mkuu na kwa kuwa nilipata elimu pale Chuo cha Uvunaji wa Maji ya Mvua pale *Sokoine University,* Morogoro kwamba malambo ya kisasa yatakuwa na sehemu tatu yaani kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji, kwa ajili ya majosho/kwa ajili ya mifugo na kwa ajili ya matumizi ya nyumbani. Kwa misingi hiyo naomba malambo au mabwawa ya Kageongwa, Shighamba, Itobo, Mwamala, Ikinelwa yafufuliwe ili yakidhi matumizi niliyoyataja. Kwa misingi hiyo basi, naomba Wizara hii ishiriki kikamilifu kukarabati malambo haya na ikiwezekana yachimbwe malambo au majosho mapya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafunzo ya wahudumu wa mifugo vijijini, naomba Serikali itoe mafunzo *(short training)* kwa vijana vijijini ili wawe wataalam angalau kukidhi mahitaji ya pale kijijini kwao.

Mheshimiwa Spika, tukifanya hivyo tutakuwa tume-*create* ajira kwa vijana kwani vijana watakapopewa utalaamu huu watakuwa tayari wamejiajiri wenyewe, kwani baada ya kozi hiyo atakuwa anachoma sindano mifugo katika kijiji chake, wafugaji wanawalipa mfano shilingi 1,000 kwa dozi hivyo keshajiajiri na hivyo tutakuwa tumewapa au tumebuni ajira kwa vijana wafugaji.

Mheshimiwa Spika, tunaomba nasi tupate ule mradi wa kukopa ng'ombe/mbuzi lipa ng'ombe/mbuzi kwenye Jimbo langu la Bukene. Naomba kuwasilisha.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa maoni yangu kuhusu Wizara hiyo. Kwanza napenda kumpongeza Waziri wa Maendeleo ya Mifugo kwa hotuba yake nzuri hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Mwanza ni miongoni mwa mikoa ya wafugaji, hivyo basi naomba ufafanuzi juu ya haya yafuatayo kwanza, katika mkoa huu kuna minada mingapi ya kisasa? Pili, kuna viwanda vinangapi vya kisasa vya maziwa na nyama? Tatu, kuna majosho mangapi ya kisasa?.

Mheshimiwa Spika, kusema hivyo ni kwa sababu mkoa wa Mwanza una mifugo mingi na pia huduma hizo zina umuhimu sana. Pia wafugaji wengi ni maskini, pia wapo matajiri kwani utakuta mfugaji ana ng'ombe zaidi ya mia mbili, lakini nyumba anayoishi haiendani na utajiri wa mifugo yake, pesa hana, mtu huyu anahitaji elimu ya kutosha na anahitaji mkopo wa kuweza kuendeshea shughuli zake za ufugaji.

Naomba Serikali iweze kutoa mikopo kwa wafugaji, mfano wafugaji wenye mifugo mingi wakopeshwe vifaa vya kusindikia maziwa, pamoja na elimu ya kutosha ili waweze kujikwamua katika ufugaji wao. Pia napenda kupata ufafanuzi kuhusu shamba la ufugaji lililokuwa katika eneo la Mwabuki, kwani sasa halipo tena kama miaka ya 1979 na 1978. Hivyo naomba ufafanuzi ili nipate kuelewa shamba hilo lilipata madhara gani mpaka likafika hatua hii mbaya ya sasa. Hivyo basi naomba maelezo wakati wa majumuisho kuhusu shamba hili na naomba kwasilisha.

**MHE. ASHA MSHIMBA JECHA:** Mheshimiwa Spika, wafugaji waelimishwe kuanzisha vikundi ili iwe njia rahisi ya kutambuliwa na kupatiwa mikopo/misaada. Wakianzisha vikundi itakuwa ni rahisi kusajiliwa na kuwa na vituo vinavyoeleweka na kuweza kufikishiwa pembajeo mbalimbali kama elimu ya ufugaji bora, uandaaji malisho bora, kuwa na sauti ya pamoja, kumiliki masoko ya uhakika, kutambuliwa kisheria, kupatiwa uhusiano wa ndani na nje ya nchi na kuweza kukuza ufugaji na kipato chao. Pia wafugaji waelimishwe ili waweze kutumia ufugaji kuwa ni njia mojawapo ya kukuza kilimo, afya bora na kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Spika, wafugaji wawe na malengo endelevu na yenye kuleta maendeleo kwa jamii na Taifa kwa jumla, wafugaji wawezeshwe ili wamiliki viwanda vidogo vidogo na kuweza kusindika mazao yatokanayo na mifugo na kutumika kwa muda mrefu zaidi na kuongeza kipato.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, kwanza Mheshimiwa Waziri hongera kwa hotuba nzuri. Pili, ombi langu ni Wizara itoe tamko la kusitisha ubaguzi wa kikabila katika Mkoa wa Mbeya, Iringa na Rukwa hii ni kansa ya amani.

Tatu, naomba Serikali isitishe amri ya wafugaji katika Mikoa ya Rukwa, Iringa na Mbeya, kuzuia ng'ombe katika maeneo madogo mfano, *two acres* na kadhalika. Ma-*DC* wasiwaonee wafugaji kwa kuwakataza wafugaji kuhamisha mifugo mpaka Serikali itakapowaeleza waende wapi kuchunga mifugo yao.

Mheshimiwa Spika, nne, Serikali ianzishe na iunge mkono utaratibu wa kulisha ng’ombe, kutumia *cake* na *shelvings* za mbegu za pamba na tano sera ya kupunguza ng’ombe ni sawa na kujenga umaskini.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kama ifuatavyo, fedha zilizotengwa shilingi milioni 20 kwa ajili ya kuchimba malambo na mabwawa Mkoa wa Singida hazitoshi. Jawabu la matatizo ya maji kwa mifugo yetu ni malambo na mabwawa, naomba Wizara itupatie fedha za kutosha kwa ajili ya malambo na mabwawa kwa ajili ya vijiji vya wafugaji vya Gurungu, Sanjaranda, Doroto, Kitaraka, Muhanga, Idodya Ndole, Agluandi, Itagata na kadhalika, vyote hivi havina maji ya uhakika na kusababisha ufugaji wa kuhama hama.

Pia tunahitaji pia majosho kwenye vijiji hivyo kuepukana na ugonjwa hatari wa kupe na tatizo la ndorobi. Pia kuanzishwa kwa mbuga ya hifadhi ya Chaya imezidisha upungufu mkubwa wa maeneo ya malisho ya mifugo na kuwafanya wafugaji wasielewe ni wapi watalisha mifugo yao msimu huu kabla ya mvua ya mwezi Novemba.

Mheshimiwa Spika, tunashauri ruhusa/kibali maalum kitolewe na Halmashauri ili wafugaji watengewe maeneo maalum ya malisho kwenye mbuga hiyo ambako hakuna vyanzo vya maji, mbuga hiyo ni pana sana.

**MHE. OMARI S. KWAANGW’:** Mheshimiwa Spika, kuhusu umuhimu wa mifugo na dhana ya uharibifu wa mazingira, Tanzania tunajivunia kuwa na mifugo mingi na kwamba ni nchi ya tatu Barani Afrika. Wakazi wote wa mijini kwa sehemu kubwa wanatumia nyama ya mifugo. Mifugo ndio tegemeo la maisha ya wote walio kwenye sekta ya mifugo. Mifugo pia hutegemewa na Taifa kwa sababu ya kipato kinachotokana na mazao ya mifugo kama nyama, maziwa siagi, ngozi na mbolea. Kwa desturi, wafugaji hawakati miti kwa ajili ya kuchoma mkaa. Wao hukata matawi tu kwa ajili ya kujenga maboma. Mifugo inarutubisha ardhi kutokana na mbolea inayotokana na wanyama wenyewe.

Mheshimiwa Spika, uharibifu mkubwa wa ardhi hufanywa kwa njia ya kilimo hasa kisichozingatia kanuni za uhifadhi wa ardhi. Kutokana na amri ambazo zimekuwa zikitolewa kila mahali kwa mwavuli wa uharibifu wa mazingira umeanza kujenga dhana potofu juu ya mifugo na sasa kila mahali wafugaji wanafanyiwa kila aina ya uonevu wakati wa kutekeleza amri hizo. Wafugaji wamekuwa wakikamatwa kila mahali na kupigwa faini isiyozingatia sheria na wakati mwingine ng’ombe au mifugo imekuwa ikizuiwa ndani ya eneo kwa siku zaidi ya moja (ng’ombe kuwekwa rumande) mfano, pale Babati wafugaji kando kando ya Mji wa Babati na Ziwa Babati wamepata kila aina ya uonevu. Mbaya zaidi hata fedha zinazokusanywa haijulikani zinatumikaje na yapo pia malalamiko kuwa hata risiti zilikuwa hazitolewi. Taarifa zote amepewa Mkuu wa Wilaya ya Babati.

Kwa kuwa Wizara hii ndiyo inayoshughulika na maendeleo ya mifugo, nashauri kwa Serikali ifanye yafuatayo:-

(i) Wafugaji wanayo haki ya kuishi na kutegemea mifugo yao hivyo uonevu unaofanywa na watendaji wa Serikali popote ukomeshwe na Serikali, vinginevyo tunavunja haki ya kuishi na kupata mapato kwa wafugaji hawana hatia yoyote. Wameishi maeneo hayo tangu enzi za mababu zetu kwa sheria za nchi hii na si wakimbizi.

(ii) Endapo tunahitaji kuwapa maeneo mengine wafugaji basi, maeneo yatengwe kwanza yakiwa na mahitaji ya kutosha ya ardhi, malisho na maji kabla kabisa ya kufikiria kuwaondoa.

(iii) Wizara hii ifuatilie sheria zote ndogo zilizotungwa na Halmashauri za Wilaya ili kuona kama zimetungwa kusaidia utunzaji wa mazingira na siyo kukataa tu mifugo.

(iv) Wizara iweke mkakati wa kuwaelimisha wafugaji ili waweze kuibadilisha mifugo yao kuwa bora zaidi hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nakutakia wewe na wasaidizi wako kazi njema.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia hotuba ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo. Aidha, nampongeza sana Waziri wa Wizara hii pamoja na Naibu wake pamoja na watalaam wao kwa kuandaa hotuba hii na kuwasilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, naomba niende moja kwa moja kwenye mchangu wangu. Wafugaji wengi hapa nchini hawanufaiki na kazi yao ya ufugaji kwa sababu ya kukosa masoko ya mazao ya mifugo yao. Bei za mazao ya mifugo ni ndogo sana wakati huo huo bei za vyakula vya mifugo na dawa zinapanda kila siku. Bei za maziwa, kuku wa nyama, mayai hazijapanda tangu mwaka 1996 hadi leo ila vyakula na dawa zimepanda mara mbili mfano mwaka 1996 bei ya kuku *broilers* mwenye kilo moja mpaka moja na nusu ilikuwa shilingi 2200 hadi 2400/=.

Mheshimiwa Spika, bei ya mayai *tray* moja ilikuwa shilingi 2,000 mpaka 2,500 wakati huo mfuko wa kilo 50 wa chakula cha kuku ni kati ya shilingi 6500 hadi 7500. Leo miaka 10 bei ya kuku ni shilingi 2200 hadi 2500, mayai *tray* shilingi 2500 hadi 2,800 wakati mfuko wa chakula cha kuku ni kati ya shilingi 9,500 hadi 11,500.

Mheshimiwa Spika, bei ya maziwa mwaka 1996 ilikuwa shilingi 200 hadi 300 kwa lita. Wakati gunia la *cotton seed cake* (Mashudu) lilikuwa shilingi 5,000 hadi 6,000. Leo maziwa bei yake ni shilingi 300 mpaka 400 kwa lita wakati gunia la chakula ni shilingi 10,000 mpaka shilingi 13,000/= na gharama za chanjo na dawa nazo zimepanda sana.

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine maziwa yanamwagwa kwa kukosa soko kabisa. Tungependa Wizara itueleze ina mipango gani ya kusaidia wafugaji hawa ambao wamefuga miaka mingi, lakini hawanufaiki wala kujikomboa na ufugaji huo? Kina mama wengi wanaoachishwa kazi kwenye mashirika mbalimbali na wale wanaostaafu

Serikalini wanajiingiza kwenye ufugaji wa kuku na ng'ombe lakini maisha yao ni magumu sana.

Mheshimiwa Spika, Tanzania hatuna viwanda vya kutosha kusindika maeneo ya mifugo. Kiwanda kikubwa cha *Tanganyika Packers* kilichopo Kawe, Dar es Salaam ilisaidia sana ku-*process* nyama na hivyo kusaidia wafugaji kupata soko la uhakika, leo kiwanda kile hakifanyi kazi. Naomba Wizara itueleze kuna mpango gani wa dhati wa kufufua kiwanda hiki muhimu ili kuleta tija kwa wafugaji kwa kusaidia uwepo wa soko la mazao ya wafugaji?

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni Serikali kuvunja nguvu wafugaji kwa kuruhusu uagizaji wa nyama na maziwa nje ya nchi kwa ajili ya hoteli yetu wakati wakijua kabisa tuna wafugaji na nyama na maziwa hayo yanapatikana hapa nchini. Hili limepelekea hata *supermarket* kubwa hapa nchini wanauza nyama za kuku, ng'ombe, mbuzi na nguruwe kutoka nje. Serikali haitakiwi kuacha kila kitu huria kwa wafanyabiashara wakati inatambua fika wananchi wake ni maskini na wanatakiwa kujikomboa na umaskini huo kwa kujishughusha na kilimo na ufugaji na shughuli nyingine.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu mashamba ya mifugo *(ranches)* zilizokuwa zimeajiri vijana wengi kutoka vyuoni na hata vijiji. Mashamba hayo mengi yamekufa na mengine kugawiwa kwa wakulima na mengine yapo tu hayafanyi kazi iliyokusudiwa. Tunaomba Wizara itueleze ina mikakati gani ya kutafuta mashamba haya ya mifugo ili yaweze kufufua tena ajira kwa vijana wanaomaliza masomo na pia kusaidia utafiti mbalimbali wa mifugo.

Mheshimiwa Spika, ili ufugaji uwezo kuleta tija hii kama Serikali ijikite kwa uhakika kusaidia kutoa elimu kwa wafugaji wafuge kisasa kusaidia upatikanaji wa mazao ya mifugo na kufanya tafiti mbalimbali ikiwa ni pamoja na kupambana na kuteketeza magonjwa yanayosumbua mifugo.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kuomba Serikali iangalie kwa makini uingizaji wa nyama ya kuku na bata nchini, tusije tukakumbwa na ugonjwa wa hatari wa mafua ya ndege.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii.

**MHE. RITA L. MLAKI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa natoa pongezi sana kwa Waziri na Naibu Waziri kwa hotuba yao nzuri sana. Ni mategemeo yangu kuwa kweli kama yote waliyoandaa na kuyasema katika bajeti hii ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo itatekelezwa basi nchi yetu itaendelea.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa kuipa Wizara hii ya maendeleo ya Mifugo, uzito unaostahili. Napenda kuchangia mambo matatu.

Kwa kuwa nchi yetu ni ya tatu kwa wingi wa ng'ombe, ningeomba Wizara isaidie nchi ifaidike na zao hili. Kwanza ku-*process* nyama na kuuza nje, Wizara isaidie watu

wanaopenda ku-*process* nyama na kuuza nje ili waweze kufanya hivyo na hii itawezekana kwa kupata maeneo ya kuweka viwanda hivyo kama Ruvu na msaada wa mikopo kupitia *export guarantee scheme* iliyoko chini ya Benki Kuu.

Pili, pamoja na kuuza nyama nje, Wizara yako ihimize uzalishaji wa ngozi na kuhakikisha zao hili linapelekwa nje. Ufugaji wa kisasa ukiendelezwa tutaweza kupata ngozi nzuri na kuongeza thamani kabla ya kupeleka nje.

Tatu, ni kuhusu maziwa. Tuna ng'ombe wengi lakini bado tunaagiza maziwa kutoka *South Africa* na Ulaya. Serikali isaidie tutumie maziwa yetu na kuongeza thamani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Waziri wa Mifugo Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa, Mbunge na Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Mbunge pamoja na watalaam kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu kwanza nielekeze kwenye maeneo ya majosho, dawa ya chanjo, malambo na kuboresha minada.

Naomba Serikali ifikirie kuboresha na kuongeza malambo katika Wilaya za Tabora ambazo zina wafugaji na kuna mifugo mingi kama vile Sikonge, Igunga, Nzega, Igalula, Uyui na Urambo, kwa kweli sehemu hizi hazina malambo ya kutosheleza na sehemu nyingine hapa nchini. Mahitaji ya mifugo na kusababisha wafugaji kutanga tanga ovyo kutokana na ukame.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa majosho Serikali iangalie kuwafikiria wananchi huduma hiyo karibu na wafugaji ili mifugo ipate kuhudumiwa kwa urahisi kwani bila majosho kutaleta madhara makubwa kwa mifugo.

Mheshimiwa Spika, majosho kwa ajili ya kuogesha mbona yanaangaliwa kwenye maeneo ya mijini na vijijini ili kuondokana na maradhi yatokanayo na wanyama hao yaani mbwa. Kwa kufanya hivyo kutazuia au kueleweka kuna dalili za mbwa mwenye kichaa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ugonjwa wa kichaa cha mbwa unazuilika vipi wakati Serikali imeacha mpango wa kuua mbwa wanaozurura mitaani kwenye majalala ya taka na kama upo ni maeneo gani yanafanyika kwa kupigwa risasi?

Mheshimiwa Spika, dawa za chanjo zitolewe bure au kupunguziwa gharama za dawa hizo. Dawa hizo kama vile za magonjwa ya mapafu. *East Coast Fever(ECT)* ambayo ni tishio la wanyama hao (sotoka).

Mheshimiwa Spika, wafugaji wamepewe elimu ili waweze kujua kutoa huduma ya kwanza pale mnyama anaanza kununua. Kama vile *first aid,* kuboresha minada angalau kuweka uzio ili kusaidia wafugaji wasikimbizane na mifugo kwenye soko na

kuweka mizani ili wafugaji waweze kuuza kwa thamani ya kilo kuliko ilivyo sasa kwa kutizama ndipo bei itolewe na mnunuzi.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali itusaidie kukarabati kiwanda kilichokuwa kinasindika maziwa na samli ambacho kilikuwepo kwa miaka ya nyuma ili tuweze kusindika na kupata soko maeneo mengine na ajira. Kwa miaka ya nyuma kulikuwa na mashine za kubeketa samli ambazo zilikuwa zinasaidia kusindika kwa wingi.

**MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

(a) Mzeri Ranchi - Handeni ni moja ya Ranchi maalum na yapo maeneo yaliyomilikishwa wananchi. Inafanya kazi vizuri. Wizara isaidie kukarabati barabara kutoka Misima hadi Mzeru.

(b) Wafugaji wa kutoka maeneo mengine wamevamia maeneo mengi ya Wilaya ya Handeni kwa mfano Sindeni, Misima, Mkata Kwamsisi na kadhalika, uharibifu wa mazingira na *imminent.* Wizara ina mkakati gani *specific* kuhusu tatizo hili?

Mheshimiwa Spika, sekta ya maendeleo na mifugo imepewa *priority* na inaendelea vizuri. Wizara i-*facilitate* Wilaya ya Handeni kuwa *a big producer of cattle products.* Kwa mwaka 2005/2006 ukarabati/ujenzi wa majosho katika Mkoa wa Tanga ni miwili tu. *How possible?*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutamka kwamba naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu katika hoja hii ni mdogo sana na hii inatokana na jinsi hoja ilivyoandikwa kwa umahiri. Lakini pia jinsi ilivyoletwa mbele ya Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, mimi napenda kuiomba Serikali iendelee kuelekeza nguvu zake katika kutatua tatizo la uhaba au upungufu wa majosho na malambo katika Mkoa wa Shinyanga na hususan tatizo lililopo katika Wilaya ya Kahama.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kahama ambayo ni miongoni mwa Wilaya zenye ng'ombe wengi ina tatizo kubwa la malambo. Yapo machache yaliyochimbwa na Serikali lakini karibu yote yameharibika na yaliyo afadhali yamejaa tope au mchanga yakihitaji ukarabati mkubwa.

Aidha, naomba Serikali ilipe kipaumbele suala la upungufu wa majosho yaliyopo ambayo ni mabovu, yakarabatiwe. Aidha, katika maeneo mengi ambako hakuna majosho basi Serikali ione umuhimu wa kujenga majosho mapya.

Mwisho, kama nilivyosema hapo awali sina budi kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na wakuu wote wa idara kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya tangu Wizara hii iundwe. Ni imani yangu kubwa kabisa kwamba kwa ushirikiano wao, Wizara hii itatekeleza kwa tija majukumu yake.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Serikali ya Awamu ya Nne kuunda Wizara ya Maendeleo ya Mifugo.

Pili, nampongeza sana Waziri wa Maendeleo ya Mifugo, Naibu wake na Makatibu Wakuu kwa hoja nzuri ya yenye mwelekeo ya kukidhi matarajio ya wafugaji Tanzania.

Mheshimiwa Spika, maeneo niliyotaka kuchangia yamezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, sioni busara kurudia. Lakini basi naomba nizungumzie kidogo kuhusu maendeleo ya wafugaji kiujumla hususan wanawake wafugaji.

Mheshimiwa Spika, wanawake wa maeneo ya wafugaji ni wanawake wenye maendeleo duni sana Tanzania ukilinganisha na wanawake wengine nchini.

Mheshimiwa Spika, wanawake hawa wana haki yao ya kmsingi ya kuendelezwa, kupata elimu na kadhalika. Mfumo dume umekithiri sana maeneo ya wafugaji na kwa ajili hiyo, nina wasiwasi kuwa hata mipango mizuri ya Taifa kama ya MKUKUTA na MKURABITA haitaweza kuwanufaisha wanawake wafugaji kama wenzao wa maeneo ya wakulima na mijini. Wanawake hawa hawamiliki ardhi, mali wala rasilimali yoyote ya kuweka dhamana ili wapate mikopo. Kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM sehemu ile inayozungumzia uwezeshaji wanawake kiuchumi, inazungumza kuwa: "Hatuwezi kuendelea na maendeleo yenye mitizamo ya jadi. Lazima kwanza tubadili tabia."

Mheshimiwa Spika, naomba sana Wizara ya Maendeleo ya Mifugo itafute pia namna ya kuwasaidia wanawake hawa ili kuwapa elimu ya miradi ya mifugo itakayowaendeleza.

Mheshimiwa Spika, mpango wa MKURABITA utawapita pembeni kwani hawana mali ya kurasimisha na isitoshe wanawake hawa hawana asili ya kufanya biashara. Hawako *exposed* kwa sababu hawana hata nafasi ya kutembea tembea huku na kule kuona wenzao Tanzania wanafanya nini.

Mheshimiwa Spika, kwa ajili hiyo basi, natoa wito kwa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo kuwa bajeti wanayoweka kwa Wizara siyo tu iboreshe Wizara, bali itenge fungu la fedha kwa makusudi ya kuwafikia wafugaji katika maeneo yao ili wayaone matatizo na wasaidie kutatua ili nao wafanane na binadamu wengine wa Tanzania kimaisha bora.

Mheshimiwa Spika, si hivyo tu, bali naomba sana Wizara iwasaidie wanawake wafugaji katika kutafuta soko la bidhaa zao ndogo ndogo kama siagi na shanga. Kama nilivyosema wanawake hawa asili yao ya kufuga haiwapi fursa na kutembea kutafuta

soko, hivyo naomba Wizara ya Maendeleo ya Mifugo, siyo tu iboreshe ufugaji (mifugo) bali pia iboreshe maisha ya wafugaji, hususan wanawake wafugaji.

Mheshimiwa Spika, narudia tena, naunga mkono hoja na ahsante kwa kupokea mchango wangu.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza Waziri na uongozi wake kwa mipango mizuri ya shughuli za mifugo hasa kwa kuangalia sheria mbalimbali na miongozo na kuifanyia maboresha au kurekebishwa.

Mheshimiwa Spika, mimi wazo langu ni kutenganisha kilimo na mifugo, sasa kumeingiliana sana na shughuli za mifugo na shughuli za killimo, Wakuu wa Idara, watenganishwe.

Mheshimiwa Spika, dawa ziuzwe katika Mikoa, sasa hivi kuna uhaba sana wa dawa za mifugo halafu zikionekana dawa zinakuwa ghali sana hasa katika Mikoa ambayo haina mifugo kama Lindi na Mtwara. Kwa hiyo dawa za mifugo zionekane ili zitumike.

Mheshimiwa Spika, bidhaa za mifugo kama kwato, nyama, ngozi na pembe za wanyama ya ng’ombe, mbuzi, kondoo na kadhalika ni muhimu sana kwa nchi za nje. Nchi za nje zimeonekana kupenda sana bidhaa za Tanzania. Kama mifugo hii ingeangaliwa vizuri, kutunzwa vizuri, kutibiwa vizuri, tungeuza sana katika nchi za nje, kwa hiyo, tuwatibu wanyama wetu vizuri ili tuendelee kuuza nje mazao yetu ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, maeneo yote yanayofuga wanyama (ranchi) zimekuwa zikisuasua hasa ya Nachingwea, Ngongo na Nangaramo (Kusini). Tunaomba zifufuliwe ili kuendeleza mifugo Kusini. Mifugo bora na ya kisasa tunaipenda Kusini na sio mifugo holela. Kwa maeneo ya ufugaji ya ranchi za Serikali zifufuliwe ili kueneza mifugo nchini. Ranchi nchini zifufuliwe Kusini.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa fursa hii. Ningependa kuchukua fursa hii kuwapongeza kwa dhati Waziri wa Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Dr. Shukuru Jumanne Kawambwa, Naibu wake, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Katibu Mkuu Dr. Charles Nyamrunda, Naibu Katibu Mkuu pamoja na watumishi wote wa Wizara na taasisi zinazoongozwa na Wizara hii kwa kazi nzuri na hotuba safi na yenye mwelekeo mzuri sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada nzuri za Wizara hii kuendeleza sekta ya mifugo, yapo maeneo ambayo yanaweza yakachangia kupunguza kasi ya maendeleo iwapo hayatapata msukumo unaostahili. Ningependa kugusia baadhi yake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilayani Mkinga, kuna upungufu mkubwa wa dawa hazipatikani kwa utaratibu ulio wazi na bei zake ziko juu sana. Majosho mengi ya zamani yanahitaji ukarabati wakati ambapo mengi mapya yanastahili kujengwa maaneo mapya yanayoendeleza ufugaji kwa kasi kubwa. Vivyo hivyo malambo yanastahili kujengwa maeneo mengi. Naomba Wizara iichukulie Wilaya ya Mkinga kama eneo jipya lenye nafasi kubwa ya kuendeleza mifugo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na wataalamu wa mifugo na kilimo kuchanganywa, huduma za ugani kwa wafugaji hazipatikani kwa kiwango cha kuridhisha. Ipo haja ya kuongeza idadi wa wataalamu na kuwahitaji wawe na ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya inayoendana na Serikali ya Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Spika, pamoja na sera nzuri za uwezeshaji, bado wafugaji wengi wanapata ugumu katika kupata mikopo.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana kuona miundombinu iliyojengwa na Shirika la Mifugo kwa ajili ya kuendeleza usindikaji kama vile *Tanganyika Packers, Tanga Dairy* na kadhalika imegeuzwa kuwa maghala kwa ajili ya shughuli tofauti kabisa baada ya kubinafsishwa. Nashauri kwamba zaidi ya kuhimiza uwekezaji wa miundombinu mipya na ya kisasa, jitihada maalum zifanyike ili kuirejesha miundombinu kwa ajili ya maendeleo ya mifugo ambayo kwa sasa inatumika isivyostahili.

Mheshimiwa Spika, kinyume cha matarajio ya kuhimiza wawekezaji kuongeza uwekezaji katika kusindika bidhaa za mifugo, Chama cha Ushirika cha Uendelezaji Maziwa Mkoani Tanga *(Tanga Dairy Cooperative Union)* na washiriki wao, *Tanga Fresh,* wamelazimishwa na Afisa wa *TRA* wa Tanga kulipia kodi ya mauzo kwa maziwa ya mgando (Mtindi). Sio tu kodi ya ongezeko la thamani haitozwi popote hapa nchini, lakini *Tanga Fresh* wanadaiwa zaidi ya shilingi 150,000,000/= kiwango ambacho ni kikubwa kuliko mtaji wa *TDCU* na *Tanga Fresh.*

Mheshimiwa Spika, kulipa kodi hiyo kutaamanisha kufilisika na kulazimika kufunga *Tanga Fresh* na *TDCU,* taasisi hizo zimefikisha rufaa yao Wizarani. Nashauri Wizara kwa kushauriana na Hazina na *TRA* ichukue hatua za kuzuia hatma mbaya ya *Tanga Fresh* na *TDCU.*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. FATMA ABDALLA TAMIM:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuandika mwandiko wangu huu.

Pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuchaguliwa kwa ushindi mkubwa katika Wilaya ya Bagamoyo na kumwezesha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kumteua kuwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo. Nampongeza sana na Mungu amzidishie afya njema na maisha marefu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote kwa kazi wanazozifanya.

Mheshimiwa Spika, nikianza mchango wangu, nampa pole sio pole kwake yeye tu, bali kwa wananchi wote wa Tanzania kwa mtihani wa ukame uliotufika katika nchi yetu na kusababisha vifo vya wanyama na kupata hasara ya mamilioni ya fedha.

Mheshimiwa Spika, ukame huo sio kwa upande wa wafugaji tu, bali pia kwa upande wa kilimo na kukosa chakula na wananchi kufikwa na njaa.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa dunia inakabiliwa na tatizo la kuenea kwa ugonjwa wa mafua makali ya ndege ambao husababisha vifo kwa ndege na binadamu. Kwa mujibu wa taarifa za Shirika la Afya ya Wanyama Duniani, nchi zilizoripotiwa kuwa na ugonjwa huo ni 50 zikiwamo nane za Bara la Afrika.

Mheshimiwa Spika, ijapokuwa Serikali imechukua hali ya tahadhari ya kutopitishwa kwa mifugo ya aina ya ndege kwani dalili zinaonyesha ni mbaya kwa nchi nane za Afrika kukumbwa na maradhi hayo.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwani nina hofu kubwa sana na Mwenyezi Mungu atatunusuru na janga hili, lakini watu wamesema tahadhari kabla ya hatari au kinga bora kuliko tiba.

Mheshimiwa Spika, basi bora tuendelee na njia hiyo ya kinga ya kuzuia kutoingia aina yoyote ya wanyama jamii ya ndege ili kuja kuepusha tiba itakapoingia na kusababisha vifo vya wanadamu pamoja na wanyama.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu ni mdogo. Naipongeza hoja ya Mheshimiwa Waziri kwa asilimia mia moja. Mwenyezi Mungu akulinde wewe na familia yako na akupe maisha marefu. *Amin.*

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo kwa hotuba yake yenye mpangilio fasaha na mvuto wa kipekee. Napenda pia nichukue fursa hii kuwapongeza kwa pamoja, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa kazi na juhudi kubwa waliyoonyesha wakati wa ukame na katika kuchukua tahadhari za kuzuia mlipuko wa ugonjwa wa ndege.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Mbozi Magharibi, Wilayani Mbozi lenye maeneo ya uwanda wa juu na uwanda wa chini (Bonde la Ufa la Rukwa au *Msangano Trough* na *Uwanda Plains)* lina sifa asilia ya kuwa na mifugo yenye nyama yenye ladha ya kipekee kutokana na wanyama hawa kula nyasi na majani aina ya matete na *elephant grass* na kulamba magadi ambayo yametapakaa Jimboni.

Mheshimiwa Spika, hadi miaka ya hivi karibuni eneo hili lilikuwa na ng'ombe aina ya Zebu ambao hawakuwa na magonjwa mengi ya wanyama. Lakini kufuatia uvamizi wa wafugaji kutoka mikoa ya kanda ya Ziwa waliokuja pamoja nao ng'ombe aina ya Ankole, magonjwa mengi ikiwa ni pamoja na homa ya mapafu, Ndigana, *Brucellosis,* Kifua kikuu cha ng'ombe, Kimeta na Ugonjwa wa miguu na midomo, yameibuka na kuanza kuangamiza mifugo asilia.

Mheshimiwa Spika, athari ya ujio huu inaonekana wazi katika Kata za Kamsamba, Ivuna na Chilumo zilizoko Tarafa ya Kamsamba. Hapa wale ng'ombe asilia

wenye afya na nyama safi karibu wanatoweka na kubadiliwa na ng'ombe waliokonda ambao karibu nusu ya uzito wao ni mapembe ambayo hayana fadia kwa wananchi wetu. Pia kutokana na wingi wao ardhi kando kando ya Ziwa Rukwa imeharibika kutokana na kumalizika kwa uoto asilia.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Mbozi Magharibi linapakana na nchi za Malawi na Zambia Kusini mwake. Pia lina barabara kuu kuelekea nchi hizo. Mpaka wa Tunduma ni ni njia kuu ya kuingizia mifugo nchini, kama kuku. Hali hii inafanya Jimbo hili kuwa na uwezekanao wa kupata mlipuko wa ugonjwa wa mafua ya ndege. Mlipuko wa ugonjwa huu pia katika jimbo hili unaweza kuwa mkubwa kutokana na uhamiaji wa makundi makubwa ya ndege aina ya bata maji, *flamingo* kwenye Ukanda wa Bonde la Ufa la Ziwa Rukwa kati ya mwezi Novemba na Januari kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, miaka ya nyuma, maeneo mengi ya Jimbo hili yalikuwa na vituo vya ushauri wa ufugaji bora na majosho. Lakini kwa zaidi ya miaka 15 sasa vituo vingi vimefungwa au kubomoka.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hoja hizo, maombi ya wananchi wa Jimbo la Mbozi Magharibi ni kama yafuatayo:-

(i) Wataalam wa Mifugo angalau kwa ngazi ya *Extension Officers* wapelekwe kwa ajili ya kusaidia kuwaelimisha wananchi ufugaji bora na kutoa msaada wa tiba ya mifugo pale panapotokea milipuko.

(ii) Maeneo hasa ya Bonde la Ufa ya jimbo la Mbozi Magharibi yafanyiwe utafiti na ufatiliaji maalum wa kubaini kuwepo na kuchukua hatua muhimu kudhibiti magonjwa *(Surveillance)* ya mifugo hususan homa ya mapafu, kifua kikuu na Ndigana.

Pia wakati wa majira ya mvua za kwanza (Novemba – Januari) mlipuko wa ugonjwa wa mafua ya ndege kwenye kata za Kamsamba, Ivuna, Chilulumo, Chitete, Msangano, Myunga na Kapele.

(iii) Kusaidia vituo vya uzalishaji wa mifugo bora hasa Kata ya Kapele, Myunga, Chitete na Msangano ambazo bado zina uoto mzuri kwa ajili ya malisho ya mifugo.

(iv) Serikali isaidie kufufua vituo vya ushauri vilivyokuwepo hapo nyuma kata za Msangano, Chitete, Chilulumo, Ivuna, na Kamsamba na kurejesha huduma za majosho zilizokuwapo maeneo hayo kwani sasa hivi zinahitajika zaidi kuliko hapo nyuma kutokana na uvamizi uliofanywa na wafugaji toka nje ya Jimbo hili.

(v) Huduma za ukaguzi wa mifugo hasa kuku wanaoingizwa pale mpakani Tunduma iongezwe nguvu kuliko hivi sasa ili kuhakikisha kuwa ugonjwa wa mafua ya ndege hauingii nchini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Wizara ya Maendeleo na Mifugo asilimia mia moja.

**MHE. RAMADHANI A. MANENO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia hotuba ya Wizara hii. Naipongeza hotuba ya Wizara hii kwa mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie ufugaji bora. Ufugaji bora ni kupata mifugo bora, lakini upatikanaji wa mifugo bora ni pamoja na mfugaji apatiwe hifadhi, malisho, dawa na majosho.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ni mchungaji na mfugaji, Wizara ijitahidi kuona hili. Wafugaji wengi lugha hii ya kisiasa haiwaingii akilini, nani mfugaji na nani mchungaji. Kuchunga ni kupeleka mifugo kwenye malisho. Unakuta mwenye mifugo pale alipo hakuna majosho, nyasi, mabwawa wala Bwana Mifugo hayupo, unategemea nini kama asiitwe mchungaji! Atakaa hapo alipo, hizo huduma atazipata wapi?

Mheshimiwa Spika, maeneo yenye Ranchi kama ya Ruvu, inatoa elimu au msaada gani kwa wananchi wanaoishi pembezoni mwa Ranchi hiyo! Unakuta Ranchi ipo, lakini hazina msaada wowote kwa wananchi hao. Si ushauri, si dawa, hata kuwapa maziwa ya kunywa!

Mheshimiwa Spika, Wizara sasa ihakikishe inatoa wasimamizi watakaotoa na kusimamia hasa jambo la mifugo. Mifugo haikai mjini. Inakaa shamba. Hawa Mabwana Mifugo wafike kwa wafugaji.

Mheshimiwa Spika, ufugaji kwa wananchi au mfugaji mmoja mmoja, anaelekezwa na kuhimizwa mifugo kama ng'ombe, mbuzi, nguruwe na kusahau mifugo mingine.

Mheshimiwa Spika, Wizara sasa ifikie hatua iweke sheria ya mifugo inayozagaa mijini.

Mheshimiwa Spika, mwisho, zipo Ranchi kwa baadhi ya watumishi au wafanyakazi wa ranchi wanachukua sheria mkononi kuwanyang'anya wachungaji wanaoingiza mifugo ndani ya ranchi .

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Waziri na wasaidizi wake kwa kutayarisha bajeti ambayo inaleta mwelekeo mzuri wa maendeleo ya mifugo nchini.
Mheshimiwa Spika, naomba nichangie katika maeneo yafutayo:-

Upatikanaji maji kwa jili ya mifugo, wananchi wa Dodoma pamoja na kilimo, pia ni wafugaji wakubwa wa ng'ombe, mbuzi na kondoo. Kutokana na ukame uliopo Dodoma wakati wa kiangazi mifugo hii inaathirika sana, hata kufa na kumpunguzia mfugaji pato.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana kwamba Serikali haijalichukulia *seriously* suala la kuvuna maji ya mvua kwenye malambo kwa ajili ya mifugo Dodoma.

Mheshimiwa Spika, ni ombi langu kwamba Wizara hii itengeneze mradi kabambe wa kuhakikisha kwamba kila kijiji kinachimbiwa lambo la maji ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru kwamba mnada wa Kizota, Dodoma utaboreshwa kufikia hadhi ya kituo cha biashara ya mifugo. Tutafuatilia kwa karibu sana kuhakikisha hili linafanyiaka kama lilivyoahidiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Chuo cha Ukataji na Usindikaji Nyama Dodoma, Ujenzi wa Chuo hiki ambao uliendа sambamba na ule wa Machinjio ya Kisasa ulikamilika Agosti 2004. Malengo ilikuwa ni kutoa mafunzo ya kukata na kusindika nyama. Ninaomba Serikali itoe maelezo kwa nini Chuo hicho bado hakijaanza kazi hadi hivi leo pamoja na gharama kubwa za uwekezaji ambazo zimebebwa na wananchi kupitia kwenye mikopo mbali mbali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu machinjio ya kisasa Kizota. Ujenzi ulikamilika tangu mwaka 2004 na hivi sasa yanatumika. Kuna taarifa kwamba nyenzo mbali mbali za kisasa hazitumiki kutokana na uendeshaji hafifu. Serikali inatakiwa kutamka ni lini ubinafsishaji wa Machinjio haya utafanyika kama ilivyoazimiwa tangu awali ili kuleta ufanisi zaidi katika utendaji na biashara.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mchango wangu, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Katibu Mkuu na watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii yenye mwelekeo wa kuboresha ufugaji kwa lengo la kuinua uchumi kupitia za la mifugo.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizi, sasa niunge mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja na kuanza kutoa ushauri wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iweke utaratibu mzuri juu ya wafugaji wadogo wadogo wa mjini, Manispaa na majiji. Ni ukweli usiofichika kuwa ufugaji wa maeneo haya ni kero kubwa kwa wakazi, hivyo Serikali itenge maeneo rasmi ya kufugia kwani kufuga mijini ni kuchafua mazingira, kero kwa wakaazi na kuleta mizozo mingi,

kusababisha ajali mifugo inapozurura hovyo, kusababisha maambukizo ya magonjwa mfano *TB*.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itenge maeneo maalum ya hifadhi ya malisho kwa ajili ya tahadhari ya ukame kwani mara nyingi unapotokea ukame, mifugo mingi hufa kwa kukosa malisho. Vile vile maeneo hayo yakitengwa yawe na uangalizi wa kutosha ili yasitumike mpaka wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali ihakikishe inapeleka wataalam vijijini ili waweze kutoa huduma kwa wafugaji hasa chanjo, kuandaa majosho ya kuogesha mifugo, dawa na kutatua kero mbali mbali zinazojitokeza.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Serikali kuwashauri wafugaji kutumia rasilimali waliyonayo yaani mifugo kwa ajili ya kuboresha maisha yao, kwa mfano; kujenga nyumba, kusomesha watoto, chakula na mavazi na .kadhalika.

Mheshimiwa Spika, wakifanya haya watapunguza idadi ya mifugo na itawasaidia kumudu kufuga katika mazingira mazuri na watakuwa na afya bila shaka hata soko lao litakuwa kubwa.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwani sasa inaenda sambamba na wananchi katika kuchimba malambo ya kunyweshea mifugo ili kupunguza tatizo la mifugo kutembea umbali mrefu kwenda kunywa maji. Ikiwezekana kila kijiji chenye mifugo kiwe na lambo la kunyweshea mifugo hali hii itawasaidia sana wafugaji kwani wananchi suala la kuchangia gharama wanalitambua na wako tayari.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru sana Halmashauri zetu zinajitahidi kuweka maeneo ya Gulio la mifugo mijini mara moja kwa wiki na vijijini ni mara moja kwa mwezi ili wafugaji waweze kuuza mifugo yao na wananchi kuuza bidhaa mbali mbali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa na magulio ya kuuza mifugo, bado hatujapata wanunuzi wazuri wa mifugo. Hivyo basi naomba Serikali iandae utaratibu wa kununua mifugo ili wafugaji wasiendelee kuuza kwa bei ya hasara.

Mheshimiwa Spika, vile vile naishauri Serikali iweke sheria kali kwa watanzania wanaosafirisha mifugo yao kwa kuwaswaga barabarani kwani wanaharibu sana barabara zetu ambazo Serikali inatumia gharama kubwa kutengeneza.

Mheshimiwa Spika, Serikali itoe tamko kuwa sasa mifugo isafirishwe kwa malori na mabehewa ya treni kupitia Bunge lak, nina hakika wafanyabiashara wataheshimu tamko hili ambalo litasaidia sana kulinda barabara zetu.

Mheshimiwa Spika, sasa nimalizie mchango wangu kwa kuunga mkono tena bajeti hii kwa asilimia mia kwa mia. Mungu awatangulie waweze kutekeleza mikakati yao.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii iliyoko mbele yetu. Nianze mchango wangu kwanza kwa kutamka kwamba naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaingia kwenye majibu ya hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge, naomba kwanza nitoe pongezi zangu nyingi kwa Rais Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa ushindi wake wa kishindo katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika Desemba, 2005. Nimpongeze pia kwa kuendeleza historia hiyo hiyo tarehe 25 Juni, 2006 wakati alipochaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi kwa kupata asilimia karibu mia ya kura zote zilizopigwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nimpongeze Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais na baadaye kupitishwa na Bunge lako Tukufu kwa kura nyingi sana kuwa Waziri Mkuu. Niwapongeze Wabunge wote kwa ushindi wao katika Majimbo na Mikoa yao na kwa uteuzi kwa wale walioteuliwa na Mheshimiwa Rais. Niwapongeze sana Waheshimiwa Mawaziri kwa kupewa dhamana na Mheshimiwa Rais kwa kuziongoza Wizara. Niwapongeze pia Naibu Mawaziri wenzangu kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais katika nafasi hiyo.

Aidha, niwapongeze sana kwanza wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Wenyeviti wetu Mheshimiwa Job Ndugai na Mheshimiwa Jenista Mhagama, kwa jinsi mnavyoongoza kwa umahiri mkubwa vikao vya Bunge letu hapa ukumbini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kwa namna ya pekee kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa imani aliyonipa kwa kuniteua kuwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo, uteuzi niliupokea kwa unyenyekevu mkubwa sana. Naahidi nitakuwa mwaminifu kwake na kwa Taifa langu katika utumshi wangu.

Namshukuru sana Waziri wangu Mheshimiwa Dr. Shukuru Jumanne Kawambwa, kwa kunishirikisha kikamilifu katika majukumu ya Wizara yetu. Pia nimpongeze Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa, kwa ushindi wa Medali ya Fedha katika mbio za Waheshimiwa Wabunge za kilometa tano zilizofanyika tarehe 22 Julai, 2006 hapa hapa Dodoma, ambapo mimi nilikuwa namfatia kwa karibu na nikapata Medali ya Shaba. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu, Dr. Charles Nyamrunda, Naibu Katibu Mkuu Dr. Jonas Verawasi, Wakurugenzi, Wakurungenzi Wasaidizi na wafanyakazi wote wa Wizara nzima kwa ushirikiano wa hali ya juu wanaonipa katika kazi yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru sana wananchi wa Shinyanga Mjini kwa kunichagua kuwa mwakilishi wao hapa Bungeni, naendelea kuwaahidi utumishi mwema kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya, *inshallah* kwa kipindi cha miaka mitano. Kwa namna ya pekee naomba niishukuru sana familia yangu hususan mke wangu

Leonsia Mlingwa, kwa kunipa moyo wakati nilipoamua kuomba kuwa Mbunge wa Shinyanga Mjini, namshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba nitoe maelezo ya hoja za baadhi ya Waheshimiwa Wabunge zilizojitokeza katika hotuba ya bajeti ya Waziri wangu, nasema baadhi kwani Mheshimiwa Waziri atawatambua wote muda mfupi ujao atakapokuwa anahitimisha hoja yake.

Naomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia na kuhakikishia kwamba tunaithamini michango yao na tuna waahidi kuwa itazingatiwa katika utekelezaji wa mipango ya Wizara yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ziko nyingi na kwa vyovyote vile wakati mwingine kwa sababu ya ubinadamu si wote wanaoweza kutajwa. Masuala yote yaliyoongelewa na Waheshimiwa Wabunge angalau tumejaribu kuyaweka katika mafungu makuu ya hoja na kama tunavyofahamu hoja hizi nyingine zilikuwa zinasemwa kwenye hotuba zilizotanguliwa na hoja hizi nitataja tu baadhi kwa sababu Waziri wangu atasimama hapa kuhitimisha hoja yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kwenye eneo la huduma za ugani. Suala lililozungumziwa ni pamoja na kufuatilia utendaji wa maafisa ugani kwa upande wa mifugo, kuwapatia nyenzo, vitendea kazi, mafunzo na kuboresha maslahi yao, watoe elimu kwa wafugaji na kuwepo kwa elimu ya tahadhari kuhusu ukame *(Livestock Early Warning Systems)*.

Katika eneo hili waliochangia kwa leo ni Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Michael Laizer, Mheshimiwa Job Ndugai, waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Janeth Masaburi, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Teddy Kasela-Bantu na Mheshimiwa Ali Khamis Seif.

Mheshimiwa Spika, waliochangia huko awali ni Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Hilda Ngoye, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Sameer Lotto na Mheshimiwa Hassan Kigwalilo.

Mheshimiwa Spika, maelezo ni kwamba Serikali imekuwa ikiboresha huduma za ugani kupitia miradi ya *National Agriculture Extension Project*, kwa kifupi *(NAEP)* na *Southen Highlands Extension and Rural Financial Services* kati ya mwaka 1996 na 2001 kwa kutoa mafunzo na vitendea kazi kama magari, pikipiki, baiskeli na vifaa vingine vya kutolea ugani. *(Makofi)*

Aidha, kuanzia mwaka 2002 hadi sasa Wizara kupitia Mradi wa Kudhibiti Magonjwa ya Mlipuko ya Mifugo imetoa pikipiki 47 na baiskeli 400. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2003/2004 Serikali inaboresha huduma za ugani kupita mipango ya maendeleo ya kilimo ya Wilaya *(DADP's)*. Katika mwaka 2006/2007 Wizara yangu itatoa mafunzo kwa wafugaji 20,000 na wataalam wa ugani 250. Utaalam kuhusu tahadhali ya majanga hususan ukame umeshafanywa utafiti katika Kituo cha Utafiti cha Mpwapwa na utasambazwa katika Mikoa ya Arusha, Dodoma, Singida Shinyanga, Mwanza kuanzia mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine lilikuwa ni uwezeshaji wa wafugaji wadogo wadogo. Waliochangia kwa leo ni Waheshimiwa wafuatao, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Michael Laizer, Mheshimiwa Luhaga Mpina na Mheshimiwa Ibrahim Sanya. *(Makofi)*

Waheshimiwa wafuatao walichangia hoja za awali, nao ni Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Martha Umbulla.

Mheshimiwa Spika, maelezo ni kuwa Serikali inahamasisha wafugaji kutumia fursa zilizopo za kuwawezesha kufuga kibiashara. Kwa mfano, matumizi ya Mfuko wa Maendeleo Vjijijini, Mfuko wa Pembejeo za Kilimo, Mipango ya Kopa Ng'ombe, Lipa Ng'ombe, kuanzisha na kuendesha *SACCOS*, Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo *(PADEP)*, zote hizi ni fursa za kuwawezesha wafugaji kuendesha ufugaji wa kibiashara kwa njia ya uwezeshwaji.

Mheshimiwa Spika, wanawake wafugaji katika Mkoa wa Manyara, Mheshimiwa Anastazia J. Wambura, alizungumzia sana hili suala. Pia, wanashauriwa kutumia fursa zilizotajwa hapo juu ikiwa ni pamoja na fedha za Mfuko wa Ujasiriamali wa Mkoa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na ombi la kuitisha Mkutano wa Wadau wa Mifugo na hapa leo asubuhi tumesikia Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha na Mheshimiwa Michael L. Laizer wamelizungumzia. Lakini awali, kwenye hotuba zilizotangulia, Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti na Mheshimiwa John M. Shibuda, pia walilizungumzia.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu alishakubali ombi hili na kwa vyovyote vile, Wizara yangu itaratibu maandalizi ya Mkutano huu ili hatimaye Mkutano huu uweze kufanyika.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa majosho, Waheshimiwa wengi sana wamezungumzia. Naomba nitaje baadhi. Inawezekana wengine nisiweze kuwataja, lakini naomba radhi katika hilo, lakini kwa vyovyote vile Waheshimiwa wote tutawapatia majibu hata pale ambapo hatutawatamka hapa na majibu yote yanayojitosheleza yatapatikana.

Mheshimiwa Spika, kwenye masuala ya majosho, ukarabati wa majosho ulizungumziwa, ujenzi wa majosho mapya, uendeshaji wa majosho, upatikanaji wa dawa za majosho na kwamba Serikali ichukue jukumu la kukarabati na kujenga majosho

pamoja na kupunguza gharama za uogeshaji. Kwa leo, Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mheshimiwa Prof. Philemon M. Sarungi, Mheshimiwa Ponsian D. Nyami, Mheshimiwa George M. Lubeleje, Fuya G. Kimbita, Mheshimiwa Mbaruk K. Mwandoro, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mheshimiwa Michael L. Laizer, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo, Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni, Mheshimiwa Maria I. Hewa, Mheshimiwa Fatma A. Mikidadi, Mheshimiwa Riziki O. Juma, Mheshimiwa Sevelina S. Mwijage, Mheshimiwa Kaika S. Telele, Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba, Mheshimiwa Teddy L. Kasella-Bantu, Mheshimiwa Dr. Zainabu A. Gama, Mheshimiwa James D. Lembeli, Mheshimiwa Emmanuel J. Luhahula, Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda, wote walizunguzmia suala la majosho.

Mheshimiwa Spika, maelezo ni kuwa juhudi za Serikali katika kukarabati majosho zinaendelea ambapo mwaka 2003/2004 Serikali ilitenga jumla ya Shilingi milioni 975 kwa ajili ya ukarabati wa majosho 195. Shilingi milioni 441.8 kwa ukarabati wa majosho 141. Mwaka 2004/2005 na Shilingi milioni 347 kwa ajili ya ukarabati wa majosho 84 kwa mwaka 2005/2006. Serikali itaendelea kuhamasisha wananchi kupitia Halmashauri zao kuibua miradi ya majosho kupitia *DADPS*. Serikali imeanza kutoa ruzuku mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, Waheshimiwa waliochangia walikuwa ni wengi, lakini kwa sababu ya nafasi yangu, naomba niishie hapo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa mara nyingine tena, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, napenda kwanza kuchukua nafasi hii, kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. Napenda pia kusema kwamba Wabunge wote waliochangia hotuba ya Wizara yangu ni 64 na kati ya hawa, 51 wamechangia kwa maandishi na 13 wamechangia kwa kuzungumza. Lakini pia wapo Waheshimiwa Wabunge 55 ambao walichangia kupitia Bajeti za Wizara mbali mbali hasa Ofisi ya Waziri Mkuu, Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Waziri wa Fedha, Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Waziri wa Maji, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira, Waziri wa Maliasili na Utalii na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Sekta ya Kilimo na Ardhi, Mheshimiwa Gideon Asimulike Cheyo, Mbunge wa Ileje na Wajumbe wote wa Kamati pamoja na Mheshimiwa Joyce N. Machimu, Mbunge wa Viti Maalum ambaye siku ya leo aliwasilisha maoni ya Kamati. Wote nawashukuru na nasema ahsanteni sana kwa sababu yale yaliyozungumzwa wakati wa Kamati yamesaidia sana kuboresha hotuba yetu hii leo.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumshukuru Msemaji wa Kambi ya Upinzani na Waziri Kivuli wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mbunge wa Wete.

Mheshimiwa Spika, Wabunge waliochangia kwa kuzungumza na maandishi ambao nitawataja hivi karibuni, wamezungumzia masuala mbalimbali ya maendeleo ya mifugo. Masuala mengine yanahitaji ufafanuzi, lakini pia mengi yanalenga katika kuendeleza na kuboresha shughuli za Wizara hii. Michango mingine kwa kweli imekuwa mahsusi ambayo inaweza kuchukuliwa na kuwekwa katika mikakati ya utekelezaji. Kwa hiyo, nasema ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda moja kwa moja kuwatambua wote wale waliochangia katika hotuba yangu leo hii, ambao wamechangia hoja katika maeneo yafuatayo:- Kabla ya kufanya hivyo, naomba kumshukuru Mheshimiwa Dr. Chales O. Mlingwa, Naibu Waziri kwa maelezo mazuri na kufafanua baadhi ya hoja.

Mheshimiwa Spika, maeneo ambayo yametolewa mchango ni mengi, nimeyajumuisha katika michango mikuu na ninaomba kwa ridhaa yako kuwatambua wale waliochangia mmoja mmoja kwa kadri michango mikuu ambayo imetolewa. Kwanza, naomba kuwatambua waliochangia katika hoja ya kutenga maeneo ya wafugaji. Waliochangia kwa kuzungumza ni hawa wafuatao:- Mheshimiwa Maria I. Hewa, Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mheshimiwa Kaika S. Telele. Waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Jackson M. Makwetta na Mhshimiwa Omar S. Kwaangw'. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia wako Waheshimiwa ambao walichangia katika hoja hii ya kutenga maeneo kwa wafugaji lakini wao walichangia kupitia hotuba zilizopita, naomba nao pia niwatambue:- Mheshimiwa John Samwel Malecela, Mheshimiwa Said J. Nkumba, Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti, Mheshimiwa Michael L. Laizer, Mheshimiwa Joyce N. Machimu, Mheshimiwa Fatma A. Mikidadi, Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, Mheshimiwa Juma S. Nh'unga, Mheshimiwa Dr. Mary M. Nagu, Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mheshimiwa Christopher O. Ole-Sendeka. Ni hao tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja kubwa ambayo ilichangiwa hapa ni ya kutenga maeneo kwa wafugaji na katika hoja hiyo kuu, Wabunge wamechangia katika maeneo kwa mfano, maeneo ya wafugaji yatengwe kabla ya kuhama, Serikali itoe hati miliki za maeneo hayo, wafugaji wa wezeshwe ili waweze kukopa kutoka Benki, itungwe Sheria ya Kusimamia Maeneo ya Malisho.

Mheshimiwa Spika, nitaomba nitoe maelezo ya jumla ya kujibu hoja hizi mbalimbali nikitegemea kwamba katika kila hoja *specific* nitakuwa nimeigusia.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitenga maeneo ya wafugaji kupitia Serikali za Vijiji na Wilaya na kuyamilikisha kwa wafugaji ili wayaendeleze kulingana na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na.5 ya mwaka 1999 na kazi hii inaendelea.

Kama hatua ya kwanza, Hati Miliki ya Mipaka ya Vijiji imetolewa kwa Vijiji vya Wilaya za Babati, Iringa Vijijini, Mbozi, Handeni na Kilindi. Hatua inayofuata ni upimaji wa maeneo kwa ajili ya shughuli mbalimbali ikiwemo shughuli ya ufugaji.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na.5 ya mwaka 1999 imetamka bayana baada ya kupimiwa maeneo hayo, hati miliki zinatolewa na Baraza Ardhi la Kijiji *(Village Land Council)* kwa kushirikiana na Halmashauri husika. Hati miliki hizo zitawawezesha wafugaji kukopa katika Benki. Aidha, wafugaji wanashauriwa kujiunga katika vikundi ili waweze kukopesheka.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine kuu ambalo limechangiwa na Waheshimiwa Wabunge ni eneo la ufugaji holela kuwa chanzo cha uharibifu wa mazingira. Ndani ya eneo hilo, michango mahsusi ilikuwa inajumuisha pia eneo la mifugo kueneza magonjwa ya mifugo, pia mchango wa mifugo usiharibu Bonde la Usangu kule Mbarali. Hii ni michango mahsusi.

Mheshimiwa Spika, naomba niwatambue wale waliochangia kwa kuzungumza kuhusu eneo hilo, nao ni:- Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami, Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine pia ambao walichangia katika eneo hilo lakini walichangia kupitia hotuba zilizopita ni Mheshimiwa Raynald A. Mrope, Mheshimiwa Estherina J. Kilasi, Mheshimiwa Ezekiel M. Maige, Mheshimiwa John M. Cheyo, Mheshimiwa Benedict K. Losurutia, Mheshimiwa John M. Shibuda na Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maelezo ya jumla ambayo naomba niyatoe kwa michango hiyo, ni kuwa, Serikali inawatambua na kuwathamini wafugaji nchini kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri Mkuu katika majumuisho ya hotuba yake. Aidha, Serikali imeandaa mkakati wa Taifa wa kuhifadhi mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji unaolenga kudhibiti uharibifu wa mazingira. Vile vile, Serikali kupitia Wizara yangu imetoa mwongozo kuhusu taratibu za kuhamisha mifugo kutoka eneo moja la nchi hadi eneo lingine. Utaratibu huu una lengo la kuzuia migogoro, uharibifu wa mazingira na kueneza magonjwa na kuhamasisha kufuga kisasa na kufuga kibiashara.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo limechangiwa sana na Waheshimiwa Wabunge ni eneo la maji kwa mifugo. Katika eneo hili hili kuu, imekuwemo michango pia inayohusu ukosefu wa maji kusababisha wafugaji kuhamahama na kuharibu mazingira, eneo la maji safi ya mifugo, eneo la kujenga malambo ya maji ya mifugo na ukarabati wa mabwawa na malambo.

Mheshimiwa Spika, naomba niwatambue Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia kwa kuzungumza katika maeneo haya, nao ni Mheshimiwa Mwadini

Abbas Jecha, Mheshimiwa George M. Lubeleje na Mheshimiwa Kaika S.Telele. *(Makofi)*

Waheshimiwa wengine ambao walichangia kwa njia ya maandishi katika hoja hiyo, naomba niwatambue. Ni Mhehimiwa Lucas L. Selelii, Mheshimiwa Damas P. Nakei, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati na Mheshimiwa Said Amour Arfi.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe maelezo ya pamoja kwa hoja hii kuu pamoja na hoja *specific* katika hiyo hoja kuu ya maji kwa mifugo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuipatia mifugo maji na imekuwa ikichangia asilimia 50 ya gharama za ujenzi au ukarabati wa malambo. Kuanzia mwaka 2001/2002 hadi sasa, jumla ya malambo 340 yamejengwa na kukarabatiwa kwa gharama ya Shilingi bilioni 1.2. Katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu imetenga jumla ya Shilingi milioni 360 kwa ajili hiyo. Aidha, wananchi kupitia Halmashauri zao wanaombwa kuibua miradi ya ujenzi na ukarabati wa malambo na mabwawa kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo Wilayani *(DADPS)* na mipango mingine katika Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine kubwa ambalo limechangiwa na Waheshimiwa Wabunge ni eneo la malisho na vyakula vya mifugo. Ndani ya eneo hili kuu, michango mahsusi ilikuwa ni mbegu bora za malisho, uzalishaji wa malisho, kuwawezesha wafugaji kuzalisha malisho.

Mheshimiwa Spika, naomba niwatambue Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia kwa kuzungumza katika eneo hili nao ni Mheshimiwa Maria I. Hewa, Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni na Mheshimiwa Job Y. Ndugai. *(Makofi)*

Waheshimiwa waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Janeth M. Massaburi, Mheshimiwa John M. Cheyo, Mheshimiwa Zainab A. Gama, Mheshinmiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Said Amour Arfi na Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili. *(Makofi)*

Waheshimiwa wengine ambao walichangia kupitia hotuba zilizopita ni Mheshimiwa Christopher O. Ole-Sendeka na Mhehimiwa Martha J. Umbulla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe maelezo kuhusu hoja hii. Katika mwaka 2006/2007 Wizara yangu inatarajia kuzalisha tani 25 za mbegu za malisho na marobota ya *Hay* 150,000 katika mashamba ya Serikali na Sekta Binafsi na kusambaza kwa wafugaji. Hadi sasa kuna wafugaji 293 wanaozalisha malisho. Aidha, uendelezaji wa malisho kwa njia ya asili ya hifadhi ya malisho ya Ngitiri, Olalili (nadhani nimelitamka vizuri katika Kimasai) na Milaga utapewa kipaumbele kwa kushirikiana na Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, mafunzo kwa wafugaji kuhusu uzalishaji na hifadhi ya malisho ikiwa ni pamoja na shamba darasa, yatatolewa katika Vituo vya Babati,

Buhemba, Kahama, Kikulula, Kihinga, Kibaha, Mabuki, Mpwapwa, Mogadili, Monduli, Nachingwea, Newala, Njombe, Nzega, Nkundi, Shinyanga, Simanjiro na Singida.

Mheshimiwa Spika, vyakula vya mifugo ni bidhaa zinazozalishwa na Sekta Binafsi na uzalishaji wake unategemea upatikanaji na gharama za malighafi.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo limechangiwa sana na Waheshimiwa Wabunge ni kuhusu masoko ya mifugo. Katika eneo hili kuu, michango mahsusi ilikuwa: Masoko ya mifugo yatafutwe ndani na nje ya nchi, viwanda vya kusindika mazao ya mifugo, kulinda viwanda vya usindikaji, viwanda vya ngozi havifanyi kazi, machinjio ya kisasa Dar es Salaam yamechelewa kuanzishwa, bidhaa za mifugo, kwato, ngozi na pembe ni muhimu kwa soko la nje na Chuo cha Mafunzo ya kukata nyama Dodoma hakijaanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba niwatambue Waheshimiwa ambao wamechangia kwa kuzungumza katika eneo hili kuu linalohusiana na masoko ya mifugo kama ifuatavyo: Mheshimiwa Joyce N. Machimu, Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mheshimiwa Kaika S. Telele na Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni. Wale waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga, Mheshimiwa Rita L. Mlaki, Mheshimiwa Fatma A. Mikidadi, Mheshimiwa Fuya G. Kimbita na Mheshimiwa Epraim N. Madeje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wako ambao wamechangia katika eneo hilo la masoko ya mifugo lakini kwa kupitia hotuba zilizotangulia, ambao ni: Mheshimiwa Michael L. Laizer, Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mheshimiwa William M. Ngeleja, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwaga, Mheshimiwa Richard S. Nyaulawa na Mheshimiwa Halima O. Kimbau.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya jumla ambayo ningependa kuyatoa kufuatana na hoja hii ni kuwa, Serikali kwa kushirikiana na Sekta binafsi imefanya mawasiliano na nchi za Comoro, Misri, Burundi, nchi za Falme za Kiarabu, Mexico na Oman.

Mheshimiwa Spika, kutokana na juhudi hizo, katika mwaka 2005/2000, ambao tunaumaliza sasa, jumla ya ng'ombe 1706 wenye thamani ya Shilingi milioni 647.9 na mbuzi 800 wenye thamani ya Shillingi milioni 28 waliuzwa nchini Comoro na Burundi. Vile vile, tani 3.5 za nyama ya mbuzi yenye thamani ya Shilingi milioni 6.8 ziliuzwa kwenye nchi ya za Falme za Kiarabu na hizi tani ni zile ambazo Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya amezitamka ambazo zilipelekwa Falme za Kiarabu mwezi wa tano kupitia ajenti wao Bwana Taji ambaye ni mkaazi wa hapa Dodoma na rafiki yangu mzuri sana, baada ya kuweza kusaidiana na mimi kwa kila hali kuhakimisha kwamba soko hili la Falme za Kiarabu tunaanza kulifungua. *(Makofi)*

Soko hilo la Falme za Kiarabu kupitia mfanyabiashara huyu mmoja ambaye tumeanza naye, tunategemea mpaka kufikia Mwezi wa Ramadhani mwaka huu, badala ya mbuzi 500 kwa wiki wanaoenda Falme za Kiarabu, tukifikia mwezi wa Ramadhani kupitia kwa mafanyabiashara huyu peke yake tunatarajia kupeleka mbuzi 1,500 kwa wiki katika mwezi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa masoko ya ndani, Serikali kupitia Halmashauri inasimamia jumla ya Minada 300 kwa ajili ya biashara ya mifugo. Kati ya hiyo, Minada nane ni ya mipakani. Aidha, kuna viwanda 19 vya kusindika maziwa, viwanda viwili vya kuchinja na kusindika nyama, viwanda viwili vya kuchinja kuku ambavyo ni Mkuza na *Interchick* na viwanda sita vya ngozi. Bado Serikali inahimiza uwekezaji katika viwanda vya mazao ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, katika kulinda viwanda vya ndani, Serikali iliondoa kodi ya *VAT* katika vifungashio vya maziwa, kuongeza kodi katika maziwa yanayotoka nje kwa asilimia 20 na Ushuru wa Forodha kwa asilimia 15 kuanzia mwaka 2001. Viwanda sita vya usindikaji ngozi vya Moshi, Himo, Morogoro, Kibaha, Arusha na Mbagala vinafanya kazi. Kiwanda kimoja tu cha Mwanza ndicho ambacho hakifanyi kazi.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Machinjio wa Jiji la Dar es Salaam ama *East Africa Meat Corporation Limited* utakaoendeshwa kwa ubia kati ya Manispaa za Jiji la Dar es Salaam na Kampuni ya *Leynod and Mayer Limited* ya Ujerumani, imechelewa kuanza kutokana na Manispaa ya Ilala, Kinondoni na Temeke kuchelewa kuchangia asilimia 33 ya hisa hizo. Hadi sasa Manispaa hizo zimeshachangia asilimia 18 ya hisa zinazotakiwa. Ujenzi wa machinjio kwa hiyo, unatarajiwa kuanza mwezi Oktoba, 2006.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nijulishe eneo lingine kuu ambalo limechangiwa na Waheshimiwa Wabunge. Hili ni la Viwanda vya Nyama vya Mbeya na Shinyanga na viwanda vya Maziwa. Michango mahsusi ilikuwa kiwanda cha Shinyanga ni kama gofu, mahitaji ya kutumia eneo la Kiwanda cha Mbeya kwa ajili ya kilimo na malalamiko kuhusu Kiwanda cha Maziwa Tanga.

Mheshimiwa Spika, ninaomba niwatambue waliochangia katika eneo hili la Viwanda vya Nyama, Mbeya na Shinyanga na Kiwanda cha Maziwa Tanga kwa njia ya mazungumzo kama ifuatvyo: Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni, Mheshimiwa Mabaruk K. Mwandoro, Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga na Mheshimiwa Fatuma A. Mikidadi. Waheshimiwa wengine waliochangia katika mada hii kwa kupitia hotuba nyingine ni Mheshimiwa Joyce M. Masunga na Mheshimiwa Richard S. Nyaulawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maelezo ya jumla kwa hoja hii ni kama ifuatavyo: Serikali kupitia Kamati ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma *(PSRC)*, hivi karibuni imetangaza tena kwenye Vyombo vya Habari, zabuni za kubinafsisha Viwanda vya Nyama vya Mbeya na Shinyanga, baada ya waombaji wa zabuni wa awali kushindwa. Tangazo lilitolewa tarehe 30 Mei, 2006. Zabuni zitafungwa tarehe 25 Agosti, 2006.

Kwa kuwa mchakato wa kumpata mwekezaji wa kununua viwanda hivyo, unaendelea, hatudhani kwamba itakuwa busara kubadili maeneo ya eneo hilo na hasa hapa nazungumzia kiwanda kile cha Mbeya.

Mheshimiwa Spika, tukumbuke kwamba, Kiwanda cha Nyama kutokuwa na eneo la *holding ground* ndio ambayo ilisababisha matatizo katika ubinafsishaji wa Kiwanda

cha Kawe ambacho baadaye kilikuja kubadilishwa matumizi kwa kufanyiwa matumizi mengine. Kiwanda cha *TDL*, Tanga tayari kimeshapata mwekezaji na ameshaanza kuzalisha maziwa.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo limechangiwa na Waheshimiwa Wabunge ni kuhusu mashamba ya mifugo ama Ranchi za Taifa. Michango mahsusi katika eneo hili kuu ni kuhusu Ranchi zenye migogoro, ulimaji wa miwa katika Ranchi za Kagera na Morogoro, kubadilisha matumizi ya Shamba la Iwambi.

Mheshimiwa Spika, naomba niwatambue ambao walichangia katika eneo hili kwa kuzungumza, nao ni Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami na Mheshimiwa Michael L. Laizer. Waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga, Mheshimiwa Nuru A. Bafadhili, Mheshimiwa Ruth B. Msafiri na Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya.

Mheshimiwa Spika,Waheshimiwa waliochangia hoja hii pia kupitia hotuba nyingine ni Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mheshimiwa Benson M. Mpesya na Mheshimiwa Richard S. Nyaulawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe maelezo kuhusu hoja hii kuu. Serikali inahakiki matumizi ya maeneo ya Ranchi ndogo ndogo zinazogawiwa kwa Wawekezaji zenye migogoro ili kupata ufumbuzi wa kudumu. Hili zoezi tumelianza muda mrefu kidogo. Mimi mwenyewe binafsi katika Ziara ambayo niliambatana na Waziri Mkuu katika Mkoa wa Kagera. Nilifanya maongezi maalum na Mkuu wa Mkoa wa Kagera pamoja na Wakuu wote wa Wilaya katika Mkoa wa Kagera kubainisha matatizo ya migogoro ya wananchi inayohusiana na Ranchi za *NARCO* ambazo ziko katika Mkoa huo, hasa na migogoro katika Ranchi hizo.

Mheshimiwa Spika, makubaliano ambayo tulikuwanayo katika Kikao hicho ambacho nilifanya na Uongozi wa Mkoa, yaani Mkuu wa Mkoa na Wakuu wote wa Wilaya Mkoa wa Kagera, ulizaa matunda ambayo baada yake Mkuu wa Mkoa wa Kagera aliwasilisha Wizarani kwangu mapendekezo ya Mkoa katika utatuzi wa migogoro hiyo ya mipaka katika Ranchi ambazo tunazibinafsisha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kupata wasilisho hilo la Mkuu wa Mkoa, mimi kama Waziri mwenye dhamana na Wizara hii, nilisita kidogo kuyatolea maamuzi mapendekezo yale kwa sababu niliendelea kupata malalamiko na maelezo yanayotofautiana kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Madiwani kutoka Mkoa huo huo. Nikaona ni busara basi nioanishe mapendekezo yanayotoka kwa Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa na yale ambayo nayapata kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge, ili kama kuna kitu chochote ambacho kazi nzuri ambayo ameifanya Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, kimeachwa, niweze kukijumuisha katika maamuzi ambayo tutayatoa kama Wizara.

Mheshimiwa Spika, napenda kusema kwamba kufikia sasa nimeweza kuainisha vizuri yale mapendekezo ya Mkuu wa Mkoa ambayo yalijumuisha mapendekezo yote ya kazi nzuri aliyofanya kila Mkuu wa Wilaya katika Mkoa wa Kagera kuhusiana na mgogoro huu wa mipaka na Ranchi katika Wilaya zile. Nimeoanisha mapendekezo hayo na kazi nzuri hizo zilizofanywa na yale mapendekezo na malalamiko ambayo nimeyapokea kwa Mbunge mmoja mmoja na hivi sasa niko tayari kuweza kutoa msimamo wa Wizara, msimamo wa Serikali kuhusiana na migogoro hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, naomba niwahakikishie pia wananchi wa Mkoa wa Kagera wote ambao wamekumbwa na matatizo hayo kwamba nia na madhumuni ya Serikali ni kuhakikisha kwamba wao wanaweza kuishi kwa usalama na amani na wanaendelea na shughuli zao za uzalishaji ama katika kilimo ama katika ufugaji na kamwe hatutachukua hatua ambazo zitawaweka katika hali ngumu sana. Pale ambapo tutashindwa kabisa kuwatengea maeneo hata katika wale ambao wako katika Ranchi, basi tutakuwa tumewahamisha katika sehemu ambazo zinajulikana.

Mheshimiwa Spika, tumejifunza kutoka wafugaji ambao wamekwenda Ihefu, wamehamishwa bila kujua watakwenda wapi, lakini wao kwa wale wachache na nasema watakuwa wachache sana ambao itawabidi kuondoka katika maeneo yao, watakuwa wametengewa mahali pakwenda. Niwatoe hofu kabisa katika jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, kama Mheshimiwa Waziri Mkuu alivyoagiza, Serikali imekubali kubadilisha matumizi ya Shamba la Iwambi katika Halmashauri ya Manispaa ya Mbeya. Maombi yalitumwa na Mheshimiwa Mbunge alizungumza kuomba mabadiliko ya matumizi ya shamba hilo na Mheshimiwa Waziri Mkuu alishalitolea maelekezo. Naomba niwahakikishie kwamba mimi kama Waziri mwenye dhamana hiyo, nimekubalina, nimeafiki kabisa na maelekezo ya Waziri Mkuu na tutamsaidia kuhakikisha kwamba Manispaa ya Mbeya inamudu kutekeleza mahitaji yao hayo.

Kuhusu hoja ya Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami, Mbunge wa Nkasi, naomba kumthibitishia kwamba orodha ya Wawekezaji wa Shamba la Kalambo, ipo na ninayo hapa. Kwa hiyo, hii orodha haina tatizo kabisa baada ya Kikao hiki tu Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami wala Shilingi ile usiishike nitakukabidhi orodha hiyo ambayo ilishawahi kwenda Mkoani, lakini nitakupa kama nakala yako uweze kuitumia kule Jimboni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Shamba la Malonje, nilitoa maelekezo kwa uongozi wa Mkoa nilipotembelea maeneo ya Mkoa wa Rukwa Mwezi Aprili kuhusu jinsi ya kukamilisha kazi ya kukamilisha shamba hili. Nilitembelea Shamba la Malonje Mwezi wa Nne, ni kipindi hicho hicho ambapo nilitembelea Kalambo ambapo ilikuwa na migogoro na nilitembelea kwa sababu ya sauti kali ya Uongozi wa Mkoa wa Rukwa ambao ulikuwa ukihitaji fedha kutoka Serikalini.

Baada ya kukabidhi Shamba la Malonje kwa Mkoa wa Rukwa, Uongozi ukataka Serikali itoe fedha ili Mkoa uweze kumilikisha Shamba la Malonje kwa wananchi. Serikali yetu ina Mfuko wa kiasi fulani, ni nchi ambayo inaendelea, haina hela nyingi

zisizokuwa na kifani. Lakini shamba la Malonje baada ya kukabidhiwa kwa Utawala wa Mkoa, limekabidhiwa pamoja na mali ambazo zimo ndani ya Shamba. Shamba lina ukubwa wa hekta 15,000 na lina ng'ombe hivi sasa au mpaka nilipotembelea mwezi wa Aprili, kuna ng'ombe wa maziwa wapatao 175 wenye thamani ya haraka haraka ya Shilingi milioni 35.

Nimezungumza na Mkoa wa Rukwa kwamba Serikali haina pesa ya kuwapa ili mmilikishe mashamba, lakini pia Uongozi wa Rukwa niliwaelekeza kwamba hawana sababu ya kung'ang'ania na kukaa na shamba kwa muda mrefu bila ya kulimilikisha kwa sababu fedha wanazo. Wana ng'ombe 175 ambao tuliwatathmini pamoja nao *on sight* shambani nilipotembelea, wakiwa na thamani ya Shilingi milioni 35. Shamba linatakiwa kugawiwa kwenye hekta 50, 50. Hivyo ni vitalu 300 ambavyo vikitangazwa kwa zabuni kama tulivyofanya katika mashamba mengine ya Kalambo na na Ranchi za Kagera, kila anayechukua zabuni alikuwa anachukua Shilingi laki moja. Wakifanya hivyo hivyo maana yake zabuni tu zitakazochukuliwa kwa ajili ya kubinafsisha zitaingiza Shilingi milioni 30. Kuna Shilingi milioni 65 za haraka.

Mheshimiwa Spika, gharama ambayo wapimaji wa Wilaya (Sumbawanga) wameitaka kwa ajili ya kupima maeneo yale ni Shilingi milioni 49. Nikawaambia: "Mna milioni 65 za haraka, milioni 49 wanazotaka watumishi wa Halmashauri ya Sumbawanga wanaweza wakapewa nusu kufuatana na hela za mauzo ya ng'ombe wale ambao wanaweza wakanunuliwa mara moja na zinazobaki wakamaliziwa baada ya kumaliza kazi ambayo itakuwa zabuni zote zimeishauzwa." Kwa maana hiyo, wana hela. Kwenye vitalu 300 hatuuzi zabuni 300, tunauza zaidi ya zabuhi 300 ili tuchambue tupate hao watu 300 ambao tutawamilikisha hivi vitalu. Kwa namna hiyo ni kwamba, wana uwezo moja kwa moja wa kubinafsisha bila senti 10 kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Spika, lakini zaidi ya hapo, kama vile kwenye mashamba ya Kalambo kule Rukwa na mashamba ya Kagera, wale wanaobinafsishiwa hivi vitalu wanalipia gharama za upimaji. Kwenye mashamba haya niliyoyataja ya Kagera na Rukwa waliobinafsishiwa walitakiwa walipe Shilingi milioni nne kwa kila kitalu, nikawaambia: "Ninyi nitakapowabinafsishia vitalu 300 hivi msitake Shilingi milioni nne kama sehemu nyingine. Fanya biashara ya haraka haraka, mdai milioni noja tu, kwa maana hiyo mtaingiza milioni 300 za haraka haraka kwa kuuza mashamba haya, tusisubiri hela kutoka Serikalini ili tubinafsishe mashamba haya ya Malonje."

Mheshimiwa Spika, naomba niwajibu uongozi wa Mkoa pamoja na Wabunge wa Mkoa wa Rukwa kwamba, *resources* zipo mikononi mwenu. Tulikubaliana katika Kikao ambacho tumekaa shambani Malonje mwezi Aprili na utawala wa Mkoa na wakaafiki kwamba kweli hakuna tatizo lolote katika umilikishaji huo. Waliniahidi, Mkuu Wilaya ya Sumbawanga kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa ambaye hakuwepo aliniahidi kwamba hawatachukua muda mrefu, watabinafsisha kwa sababu wamekubaliana na mimi kwamba kubinafsisha hilo Shamba la Malonje kwa kulikata katika vitalu kubinafsisha kwa wananchi hela nyingi wanazo na hela nyingi zitabaki kwa ajili ya maendeleo ya Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nielekeze mchango wangu katika maoni na ushauri wa Kambi ya Upinzani kuhusu hotuba ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo iliyotolewa na Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mbunge wa Wete. Huu ni ushauri wa Kambi ya Upinzani. Kuna maeneo makubwa ambayo nilidhani inafaa niyatolee maelezo. Eneo moja linazungumzia kuhusu wiki maalum ya unywaji maziwa ya mifugo na kwamba Serikali ianzishe wiki ya ulaji wa nyama na mayai badala ya kukazania maziwa peke yake.

Majibu ni kuwa, Wizara yangu inakubaliana na ushauri huo wa Kambi ya Upinzani. Nawashukuruni sana. Pamoja na wiki maalum ya uhamasishaji wa unywaji wa maziwa, naomba niwajulishe kwamba kuna Sherehe ya Siku ya Chakula Duniani ambapo pamoja na mambo mengine ulaji wa nyama na mayai pia huhamasishwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu eneo la ubinafsishaji wa Mashamba ya Iwambi, Malonje na Kalambo, hayo nimeyatolea maelekezo tayari na naomba yawe maelezo kwa Waheshimiwa wa Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la mashamba yaliyobinafsishwa ambayo imeelezwa katika ukurasa wa nane *paragraph* ya 13 kuhusu mikakati iliyowekwa kuhakikisha waliomilikishwa wanafuga kisasa. Naomba nieleze kuwa, ili kuhakikisha mashamba yaliyobinafsishwa kwa wananchi yanafanya kazi kama ilivyokusudiwa, Serikali imeunda Kamati ya wataalam kuhakiki matumizi ya mashamba hayo. Sio kwamba mashamba hayo tutayaacha tu yafugwe kiholela, tunachokikusudia katika mashamba yale ni kuwa mashamba ya mifano katika ufugaji wa kisasa na ufugaji wa kibiashara na tutayafuatilia kwa karibu na kwa yule ambaye atashindwa kufuata yale masharti ya kimkataba, basi Serikali haitasita kuyachukua mashamba hayo.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo wamelichangia Waheshimiwa wa Kambi ya Upinzani ni kuhusu mafunzo kwa wafugaji na kupanua Vyuo vya Mafunzo ili kuongeza idadi ya wanafunzi na kwamba mafunzo yalenge wachungaji badala ya kulenga wafugaji wa ng’ombe wa maziwa. Naomba nieleze kwamba, Wizara imeimarisha Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo nchini ili kuongeza idadi ya wanafunzi kutoka idadi ya sasa hivi ya 748 hadi kufikia idadi ya 800 katika mwaka huu mpya wa fedha.

Ili kuongeza Elimu kwa Wafugaji nchini, Wizara itashirikiana na Halmashauri kuanzisha mashamba darasa 10 kwa wafugaji pamoja na kuwaelimisha wafugaji 20,000 kwenye vituo mbalimbali nchini.

Waheshimiwa Wabunge, Kambi ya Upinzani pia wametoa hoja kuhusu sensa ya mifugo na hasa wamezungumzia umuhimu wa kufanya sensa kamili ya mifugo. Naomba nitolee maelezo haya. Wizara yangu inakubaliana kwanza na ushauri wa Kambi ya Upinzani, nasema nawashukuruni sana. Juhudi zinafanywa na Wizara kuwasiliana na Wahisani ili kupata fedha za kufanya sensa, kwa kuzingatia kuwa gharama zinazohitajika ni kubwa sana. Zinahitajika gharama zinazokaribia Shilingi bilioni 17.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya kujibu hoja hizo, kuna hoja ambazo zimekuja saa 11.00 wakati tunaingia kwenye Kikao hiki na ambazo sikuweza kuzijibu kupitia maandishi haya. Naomba nipitie haraka haraka kama yalivyokuja. Kwanza Mheshimiwa Michael Laizer nimshukuru kwa pongezi ambazo amenipa mimi binafsi na Mheshimiwa Naibu Waziri. Namshukuru kwa kutupa moyo, ametuambia tunajitahidi.

Ni kweli, kama tulivyoonyesha siku ya Jumamosi kwamba na sisi tunaweza kwenda katika *speed* ya wafugaji kwa kuchukua medali zile mbili za shaba na fedha na kwa hali hiyo hiyo, tutaendelea kwenda na ninyi bega kwa bega kwa hatua ambazo ninyi mnazipiga.

Pia, Mheshimiwa Mbunge amezungumzia kuhusu bei ghali sana ya dawa za mifugo. Ametoa mfano wa *super dip* ambayo inauzwa Sh. 65,000/= kwa lita. Sisi tunaelewa Serikalini kuhusu matatizo hayo ya wafugaji na kama ambavyo ameona katika Bajeti ya mwaka huu ya Wizara, tumeomba ruzuku kwa ajili ya dawa za kuogeshea mifugo. Tumeomba ruzuku ambayo imefikia kiasi cha Shilingi milioni 500 na kwa baraka zenu nategemea kwamba ruzuku hii ipite kwa sababu kilio cha wafugaji ni kikubwa.

Nakubali kwamba ruzuku hiyo siyo kubwa, lakini tukumbuke vitu viwili. Moja ni kwamba, ruzuku ambayo Bunge hili Tukufu likiipitisha itapunguza makali ya bei kali ya hizi dawa za kuogeshea ambazo zitapunguza vifo vya wanyama. Tunategemea kwamba itapunguza kwa kiasi kizuri. Lakini pia tukumbuke kwamba, Wizara yangu ilileta maombi ya Bajeti ya ruzuku kwa miaka miwili mfululizo iliyopita, lakini hatukuweza kupata hata senti 10 kwa ajili ya ruzuku ya dawa za kuogeshea mifugo. Kwa hiyo, nishukuru kwamba kama Bunge hili litapitisha, hii itakuwa mara ya kwanza kuweza kupitisha ruzuku katika dawa za kuogeshea mifugo.

Lakini pia Mheshimiwa Laizer ameuliza kwamba, mbona waliona *adendum* ambayo ilijulisha kwamba ruzuku hiyo ni Shilingi bilioni mbili na wala siyo Shilingi milioni 500? Suala hili Mheshimiwa Michael Laizer naweza kusema kwamba kama aliiona, aliiona kwa bahati mbaya. Ni suala ambalo liliwasilishwa katika ngazi mbalimbali za Bunge na kwa makosa ya kiutendaji, halikuweza kufikishwa Bungeni kwa wakati muafaka, kwa namna hiyo ikabidi *adendum* hii isisomwe.

Mheshimiwa Spika, naomba niwahakikishie Mheshimiwa Laizer na wafugaji nchi nzima kwamba, kwa ruhusa ya Bunge hili nitajitahidi kwa taratibu zitakazowezekana kumfuatilia Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuhakikisha kwamba hiyo ruzuku tuipate kwa njia nyingine ama *supplement budget* katika *media review* au sehemu nyingine na yeye tayari ameshanihakikishia kwamba atanisaidia katika juhudi hizo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Michael Laizer naweza kusema kwamba, hata ile hoja ya Serikali kutoa lita 200 kwa *dip* ni kwamba itakuwa imesaidiwa kwa ruzuku hii kwa vile sasa dawa zitapatikana kwa bei nafuu zaidi.

Mheshimiwa Laizer ameulizia pia suala la mradi gani mbadala baada ya *TLNP* ambayo imemalizika. Ni kweli mradi huu ulikuwa umefadhiliwa chini ya Benki ya *ADB* na wamefikia ukomo mwaka 2005, lakini sasa shughuli zile ambazo zilikuwa zikifanywa

na *TLNP* za kuboresha miundo ya masoko ya mifugo, shughuli hizi zimechukuliwa moja kwa moja na Serikali kwa gharama ya Serikali na pesa zimetengwa kwa mwaka huu ili kuboresha miundombinu. Bahati nzuri kwa kipindi cha mwaka unaokuja, badala ya kuangalia Kaskazini, maana tumelalamikiwa sana na Wabunge na hasa wa Kusini kwamba Mheshimiwa Waziri kwa vile ni Muislam anafuata taratibu zile za kila anaposali anaangalia Kaskazini; Je, Kusini lini Serikali itaiona?

Kwa hiyo, katika mpango ambao tumeutengea fedha mwaka huu kuboresha miundombinu ya masoko, kiasi kikubwa kitakwenda katika kuboresha miundombinu ya masoko katika Mikoa ya Kusini. Nabadilisha dini kidogo.

Mheshimiwa Mbunge amezungumzia pia kuhusu mabwawa, kwamba yako wapi mabwawa ya mwaka 2006/2007? Mbona mnazungumzia mambo ya mwaka 1947, ambayo ameshafanya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Edward Ngoyai Lowassa? Nini hapa mnakifanya mwaka huu? Naomba Mheshimiwa Laizer pamoja na Waheshimiwa Wabunge niwapeleke katika ukurasa wa 31 wa kitabu cha hotuba yangu. Katika ukurasa huo kuna *paragraph* mbili na nadhani na mimi ninacho kitabu hapa, kuna *paragraph* mbili zinazungumzia kuhusu malambo na mabwawa.

Mheshimiwa Spika, aya ya 50 inazungumzia kwamba Serikali ili kuendeleza ufugaji wa asili katika mwaka wa 2005/2006, Wizara ilichangia kukamilisha uchimbaji na ukarabati wa malambo 20 katika Wilaya zilizotajwa. Lakini kwenye aya ya 51 nilieleza kuwa katika mwaka 2006/2007, huu mwaka ambao tunakwenda, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri itajenga mabwawa mawili katika Wilaya za Mwanga (bwawa moja) na Kishapu (bwawa moja).

Aidha, Wizara yangu itachangia ujenzi wa malambo 20 katika maeneo ambayo yameorodheshwa hapa. Hii ni kusema kwamba kazi imefanywa na ndugu yetu kipenzi Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa katika kuendeleza mifumo ya ufugaji. Mwaka 2005 Wizara imesaidia kujenga na kukarabati malambo 20, lakini katika mwaka huu unaofuata wa fedha 2007/2008 siyo tu malambo 20 ambayo tuna-*match* kama mwaka 2005, lakini pia kuna idadi ya mabwawa ambayo yana gharama kubwa zaidi, ambayo ni mawili katika hayo maeneo yaliyotengwa. Juhudi za Serikali siyo tu kwa kazi ambayo imeshafanywa, lakini na kwa kazi ambayo tunaendelea kuifanya. Kazi hiyo haiishii kwa awamu zilizopita.

Mwisho kabisa, naomnba nigusie haraka kwa sababu hili amelizungumzia Mheshimiwa Mbunge kwa manung'uniko makubwa sana, hili la kutokuwa na Bodi ya Mifugo. Mheshimiwa Mbunge amesema, mbona hata samaki wana Bodi ya Samaki, inakuwaje mifugo? Naomba nimwondolee wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwa kumweleza kwamba, tuna Bodi mbalimbali zinazohusiana na mifugo. Kwa mfano, mwaka 2005 tumezindua Bodi ya Maziwa ambayo imeshaundwa tayari na ambayo imo katika sheria na pia kuna Bodi ya Nyama ambayo iko njiani kuundwa baada ya kupitishwa Sheria Bungeni. Kwa hiyo, kuna Bodi kadhaa ambazo zitafuata na zote zinalenga moja kwa moja eneo hili la mifugo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Sanya amezungumzia kwa ukali sana yale mapungufu ambayo tumekuwanayo katika kuimarisha ufugaji wa mifugo midogo midogo na pia katika kufuatilia soko la nje. Naomba kumjibu Mheshimiwa Sanya kwamba, kwanza Serikali ina mkakati mahsusi wa kuboresha mifugo midogo midogo pamoja na utafiti na pia inafanya kazi kubwa.

Kama nilivyoanza kugusia kuhusu kufungua masoko ya nje. Soko la nje tunalitambua kwamba ni soko ambalo litatupa faida kubwa kwa vile ndiyo soko ambalo lina uwezo wa kununua mifugo kwa idadi kubwa. Soko ambalo amelitaja la Uarabuni kupitia *agent* ambaye ni mkazi wa hapa hapa Dodoma, nimelieleza kwa kina na kwamba huyu bwana sina haja ya kwenda kwake. Ni rafiki yangu na leo kwa kudhihirisha urafiki ambao ninao kwa kazi kubwa hii ambayo amefanya kutusaidia kufungua masoko ya Uarabuni, hata Waheshimiwa wageni wangu Wenyeviti, Makatibu wa CCM na Makatibu wa Jumuiya za CCM pamoja na Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo ambao wamekuja kuhudhuria Bunge, nimewapeleka huko wakala chakula cha mchana kwenye hoteli yake. Hayo ndiyo mahusiano ya karibu, siyo kwa takrima, bali kwa kulipa mimi mwenyewe, lakini kwa kumuunga mkono kwamba wewe ni rafiki wakati wa shida na wewe ni rafiki ambaye nataka tufanye nawe kazi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tunafanya maongezi mahsusi na Balozi wa Egypt ambaye ananisaidia kufanya ziara mara baada ya Bunge kwenda Egypt kujaribu kukamilisha taratibu za kulipata Soko la Misri ambalo ni soko kubwa. Kwa wastani wameshaweza kutuwekea katika mabano kama tutatekeleza yale mahitaji yao au masharti yao tani zipatazo 22,000 kwa mwaka za nyama. Tani hizi 22,000 ni mzigo mkubwa sana ambao tukiweza kuutekeleza maana yake litakuwa ni soko kubwa kwa wafugaji wetu. Tani 22,000 kwa mwaka kwa nchi ya Misri ni sawa sawa na ng'ombe waliofugwa vizuri 110,000 kwa ajili ya soko hilo. Lakini pia tumefuatilia kwa karibu na hivi karibuni wakati Rais wa Comoro alipokuja nchini mimi binafsi nilikaribishwa na Mheshimiwa Rais, Jakaya Mrisho Kikwete kwenda kumpokea na tumeongelea kuhusu kuboresha soko la Comoro. Mwaka 2005 tuliweza kuuza ng'ombe wapatao 3,481 katika soko hilo na tuna mkakati wa kuboresha uuzaji katika soko hilo unaozidi ng'ombe 6,000 kwa mwaka huu, lakini kuzidisha maradufu baada ya hapo.

Mheshimiwa Spika, naomba nipitie pia hoja ambazo Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka amezitaja katika Kikao hiki cha jioni. Moja, namshukuru sana kwa kutupongeza. Inatupa moyo na tuna uhakika kwamba kwa pongezi hizo na kupewa moyo hivyo, tutahakikisha kwamba tunakwenda kwa kasi ambayo wafugaji wameizoea. Amezungumzia pia kuhusu mabwawa na malambo, nadhani hii sitairudia kwa sababu nimeizungumza tayari katika hoja ya Mheshimiwa Laizer.

Lakini amezungumzia pia hoja ya kilio cha wafugaji wa Tanzania. Namshukuuru sana kwa kunijulisha kuhusu andiko hilo ambalo aliandaa wafugaji. Nimelisikia katika redio mbao, sijapata nakala. Lakini sikushangaa sana kwa sababu nimeambiwa kwamba hili andiko limepelekwa kwa Mheshimiwa Rais na andiko ambalo linapelekwa kwa Mheshimiwa Rais bila shaka kwanza linamfikia Mheshimiwa Rais na kwa kawaida mara zote yale ambayo yamenihusu Wizarani kwangu Mheshimiwa Rais angeharakisha

kuniletea. Nina uhakika kwamba nitalipata katika taratibu hizo. Nitashukuru akiweza kunipatia kabla, ingawa najua kwamba hii itakuwa katika mlango ambao sikuutegemea kupata, lakini nitalifanyia kazi kwa kadri ambavyo nitaweza.

Mheshimiwa Spika, najua hoja zilikuwa nyingi na muda wetu wa kuzipitia zile hoja ulikuwa mchache na kwa kuzingatia upya wa Waziri, Naibu Waziri na wataalam katika Wizara na nakiri inawezekana sana, kwamba kuna hoja za muhimu ambazo sikuzigusia, lakini nahisi kwamba nimezishika zote zile ambazo zilikuwa muhimu. Kama imetokea kwa mapungufu ya kibinadamu nimeacha moja au mbili, basi naomba msamaha, lakini siyo kwamba tumezidharau.

Mheshimiwa Spika, hoja ambazo hatukuzitolea maelezo ya mdomo sasa hivi tutazitolea majibu kwa maandishi kwa kila Mbunge ambaye amewasilisha na kwa kutambua mapungufu hayo, basi naomba nimtambue. Nimepewa kikaratasi sasa hivi wakati naongea, nimtambue Mheshimiwa Martha Mlata, Mbunge wa Viti Maalum Singida, ambaye ametoa mchango wake kwa kuzungumza katika nyanja ya Viwanda vya Nyama, majosho na ufugaji wa kuku pamoja na maji kwa mifugo. Nakushukuru sana Mheshimiwa na samahani kwa kusahau kukutambua katika eneo hilo. *(Makofi)*

Naomba pia niwatambue wale ambao walichangia katika Kikao hiki cha jioni kwa kuhisi kwamba pengine sikuwatambua katika orodha hii ambayo ilikuwa imeishaandaliwa. Naomba niwatambue Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, Mheshimiwa William Ngelela, Mheshimiwa Juma Njwayo, Mheshimiwa John Magufuli, Mheshimiwa Martha Mlata (ambaye nilishamtaja kumbe, nilikuwa nimemwandika), Mheshimiwa Mary Nagu na mwingine ni Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, waliochangia kwa maandishi. Ahsanteni sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Bado una dakika tano. Kwa hiyo, kama una jambo lingine, unaweza kuendelea.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Tayari.

**SPIKA:** Tayari eeh, inatosha.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Kabla sijawahoji kuhusu hoja hii nimebadili utaratibu kidogo. Mtoa hoja atakuwa anakaa karibu hapa kwenye chombo cha kusemea.

Waheshimiwa Wabunge, vile vyombo viwili vya kusemea baada ya mabadiliko ya viti, havipo. Mtakumbuka mara ya kwanza tulikuwa tumemweka Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa, sasa tulivyobadili ile mitambo iliyokuwa inaungana kwenye vyombo hivi viwili, imeondolewa au tuseme imeharibika.

Kwa hiyo, imeagizwa kutoka nje na hivi punde, nadhani kabla hatujamaliza Mkutano mwezi Agosti, 2006 tunaweza kuwa tumerejesha hali hiyo. Lakini kwa sasa hivi Waheshimiwa Mawaziri, naona wanapata taabu kwa sababu ama inabidi waondoke wasogee huku kwa Mzee Ngombale au warudi kwenye ile *microphone* ya nyuma. Sasa nimeona ni bora nibadilishe.

Mheshimiwa Mtoa Hoja, ningekuomba uje hapo kwani itakuwa rahisi zaidi kuliko kuwasumbua Waheshimiwa Mawaziri wetu. Watanong'onezana tu, si wanaonana hapo! Sogeza Kiti nyuma kidogo, siyo lazima kiwe hapo hapo.

Sasa, huo ndiyo utakuwa utaratibu hadi hapo mitambo ile itakapokuwa imepona. Hoja iko mbele yetu, kama mnavyofahamu inahitaji tuingie kwenye Kamati, ndiyo mwisho, tuweze kuikamilisha.

Lakini kwa hatua hii ya kuingia kwenye Kamati kwa mujibu wa Kanuni, inabidi niwahoji. Kwa hiyo, nitawahoji sasa.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**Fungu 99 – Wizara ya Maendeleo ya Mifugo**

Kifungu cha 1001 – *Administration and General* ... ... ... ... ... ... Sh.3,271,258/=

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Niko *program* 10, *sub vote* 1001, 250100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia, nimeomba kupata ufafanuzi. Ukiangalia karibu Mikoa saba ya nchi yetu wanapeleka ng'ombe Kenya bila utaratibu wowote, wanapita njia za panya na kwa kuwa sasa nchi zetu zote tatu ziko katika nchi za Afrika Mashariki, napenda kujua ni utaratibu gani utakaotumika ili ng'ombe wanaokwenda kwenye Minada ya Kenya wasiende tena kwa njia za panya, waende kwa njia ya halali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningeomba Serikali watueleze ni utaratibu gani ambao wananchi watatumia?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu hoja ya Mheshimiwa Laizer kama ifuatavyo: Serikali inatambua suala ambalo lipo katika Mikoa ya mipakani Kaskazini mwa Tanzania na hasa Longido ambapo wafanyabiashara wengi wanatumia Minada ambayo iko upande wa Kenya kwa sababu mbalimbali. Tumejaribu kufuatilia, moja ya sababu ni miundombinu ambayo

tulikuwa tunashughulikia chini ya Mradi wa *TLMP. TLMP* baada ya kumalizika kama nilivyosema awali ni kwamba Serikali itatumia fedha zake zenyewe kuweza kujenga miundombinu katika Mikoa ya Kaskazini na hasa katika Mikoa ambayo ipo mipakani.

Kama nilivyozungumza awali kuwa safari hii pia tutatumia kiasi cha fedha kuweza kuboresha miundombinu upande wa Kusini, sasa hicho ni kishawishi mojawapo. Lakini kishawishi kingine pia ni wafugaji kwa maeneo haya ya Kaskazini, walikuwa wakisema kwamba bei za mifugo yao kwa upande wa pili wa mpaka ni kubwa zaidi kuliko bei ambazo wanapata nchini Tanzania. Sasa tutafanya kazi kwa juhudi kufuatana na fungu dogo la hela tulilokuwanalo katika kuboresha miundombinu.

Lakini kuhusu kishawishi cha kuuza upande wa pili wa mpaka kwa sababu ya bei kubwa, njia pekee ambayo Serikali itatumia ni kuwaelimisha wananchi na kama nilivyosema kabla kwa juhudi kubwa ambayo Serikali inafanya sasa ya kufungua masoko ya nje, Masoko la Uarabuni, Soko la Mexico na nchi kwingine ambako sikutaja kabla, tutategemea kwamba tutaweza kupata bei nzuri ambayo itawezesha pia kishawishi cha kuuza nje au kupata pigo, wa mpaka nacho pia tuweze kukiondoa. Hiyo ndiyo mikakati ya Serikali kwa sasa. Ahsante.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali yangu siyo marefu, ningependa tu kujua kwa vile wafanyabiashara wengine wanaruhusiwa kupitisha mazao, mfano mahindi, kila aina ya mazao yanapita.

Je, ni kwa nini wafugaji wasiruhusiwe kupita mpakani pale Namanga na mifugo waende kwenye Minada ya Kenya, wapate *officially* na magari yabebe mifugo na kwenda kwenye Minada ya Kenya kama wanavyokwenda wakulima wengine, hata vitunguu kutoka Karatu vinapita, hata soko hili la mahindi la Kibaigwa wanakwenda, lakini mifugo hawaruhusiwi kupita Namanga na magari, kwa nini wasiruhusiwe? Nilitaka kujua sababu ni zipi? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Laizer ulitaka mifugo ipite kwenye bararabara ya lami? Mifugo ipite kwenye barabara!

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mifugo wapite kihalali hata kama wamebebwa na magari wapite kihalali, lakini hawawezi kupita kwa sasa.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe maelezo mafupi tu kwa swali ambalo ni la msingi ambalo Mheshimiwa Laizer ameliuliza. Ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, hicho anachokiomba Mheshimiwa Laizer ndicho tunachotaka kifanyike. Wafanyabiashara ndani ya nchi zetu tatu, biashara ya mifugo, biashara ya mahindi, biashara ya maharage, yote hiyo tunataka ifanyike kwa taratibu ambazo tumekubaliana. Sasa kwa mifugo bado tunajadiliana kwa suala hili kwa sababu ya wasiwasi wa kuhamisha magonjwa kutoka upande mmoja na kuyapeleka upande wa pili.

Katika Kikao kilichopita cha *sector council* inayoshughulika na masuala haya, suala hili lilikuwa miongoni mwa *agenda* ambazo zimewasilishwa. Kwa hiyo, tunaomba wananchi wa Afrika Mashariki wavute subira kidogo wakati tunaitafutia suala hili ufumbuzi wa kudumu. Lakini, tutapata jibu la kutosheleza ili biashara ya mifugo iweze kufanyika katika nchi zetu tatu. *(Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nina maswali matatu. Kifungu *programu 10 sub-vote* 1001 *sub-vote* - Mshahara wa Waziri 250100. Wakati nachangia kwa maandishi, nilimwuliza Mheshimiwa Waziri anieleze ni hatua gani ambazo anazochukua kuhakikisha kwamba hakuna ubaguzi katika sehemu ambazo mifugo inahamishwa kwa haraka sana. Kuna malalamiko ya wananchi mengi ambapo wengine wanahamishwa kwa mfano lile Bonde la Usangu, kuna mifugo zaidi ya laki sita. Sasa ukihamisha mifugo laki sita bila kuwaambia unapeleka wapi na hiyo mifugo thamani yake tunazungumza kwa laki moja, ni karibu bilioni 60. Ndiyo kusema unataka kuwafanya watu maskini kwa bilioni 60! Hii ni hela! Unafanya nini?

Sasa nataka kupata jibu, kwa sababu wengine wanasema nendeni mlikotoka, kama wametoka Umasaini waende walikotoka Umasaini, kama unatoka *Sukuma Land* waende *Sukuma Land*. Lakini wanaambiwa msipite katika Wilaya *A, B and C.* Sasa hawa watarusha ng'ombe kwa helkopita wazirudishe au kwa kitu gani? Ninachotaka kusema hapa, utaratibu ambao umefanywa sasa hivi kuhamisha wale ng'ombe haujafikiriwa vizuri na kwa kuwa hii ni mali, nataka kujua aniambie Waziri atafanya nini kuhakikisha linafanikiwa. Kwanza hii haiwi chanzo cha ubaguzi katika Taifa hili la Mwalimu Julius K. Nyerere. Pia, wale watu hawapotezi mali zao hilo la kwanza. *(Makofi)*

Pili, juu ya masoko, pamoja na majibu mazuri ambayo yametolewa na Mheshimiwa Chenge, lakini ukweli ni kwamba ng'ombe *corridor* ya *Sukuma Land* tunakouza, tunauza sasa hivi ng'ombe wengi Kenya. Wazuiaji basi wangekuwa wa Kenya ingelikuwa sawa sawa, lakini wanaotuzuia ni Watanzania. Ukishaingiza ng'ombe wale, Wakenya wanafurahi sana, hawazungumzii juu ya maradhi , wanakupa fedha, unarudi.

Sasa, kwa kuwa kuuza ni mojawapo ya njia ya kuwasaidia wakulima kupata faida na pia ku- *diestock* hao ng'ombe, basi atueleze Waziri atafanya utaratibu gani kuhakikisha kwamba matatizo haya ya njiani ukienda Kisasa unakamatwa, ukienda Magu unakamatwa, njiani unakamatwa kila wakati yatakomesha lini ili watu wengi waliokubali kuweza ku-*diestock* au kupunguza hawa ng'ombe huwezi ukafanya bila usumbufu. *(Makofi)*

La tatu, malisho. Kusema kweli watu hawajaliangalia hili jambo la mifugo kwa uzito unaostahili mifugo tuliyonayo hata kwa bei ya kawaida kama laki mbili, ni sawa sawa na trioni 3.7 ambayo ni sawa sawa na Bajeti nzima ya nchi hii. Hii hela ipo ni *savings* za watu, lakini halijapewa uzito unaostahili. Kwa hiyo, *investment* yake ndiyo tunayoiweza, ndiyo MKUKUTA. Tunachohitaji ni maji na mahali pa kuchungia na malisho lakini hakuna lolote ambalo limefanywa. Nataka kujua atafanya nini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cheyo dakika tano zimekwisha.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa John Cheyo amezungumzia kuhusu ubaguzi kwa wafugaji na hasa katika sehemu ambazo wafugaji wanahamishwa na kuwa Serikali imeandaa mkakati gani wa maeneo ambayo wafugaji hawa watakwenda.

Kwanza, niseme kwamba, hakuna ubaguzi kwa wananchi wa Taifa hili moja, labda kama ubaguzi umekuwepo ni ubaguzi wa haki ya kimataifa wa mtu kuwa na nchi yake ambapo, tulipoamua kuwarudisha makwao kutoka katika Mkoa hasa wa Kagera, Kigoma ambao hawakuwa na haki ya kupunguza malisho na maji katika nchi yetu wakati wameingia bila kufuata taratibu. Huo ndio ubaguzi ambao unaruhusiwa na tumewarudisha kwa vile pia tunasema kwamba maeneo hayo lazima tuyalinde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Cheyo, amezungumzia wafugaji wa Usangu. Nikiri kwamba Serikali tulifanya makosa ya kutotenga maeneo kabla, hawa wafugaji kuwaomba waondoke kule. Lakini mara tu katika kipindi kifupi tulielewa kwamba kulikuwa na tatizo hilo na Serikali imekaa kwa Wizara yangu, Wizara ya Ardhi, Wizara ya TAMISEMI na Wizara ya Usalama wa Raia, kuzungumzia na kubainisha na namna ambazo tutazifanya ili wafugaji hawa sasa wasiwe kama wahamiaji katika nchi yao waweze kuelekezwa maeneo ya kwenda.

Hiyo kazi inafanywa sasa hivi kwa kasi kubwa sana na Wizara ya Ardhi imetengewa fedha na kuyatambua maeneo yale na kuyapima. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi ambao wameondoka katika sehemu hizo kwamba Serikali yao inafanya kazi usiku na mchana kuhakikisha kwamba wanapata maeneo ya kwenda. *(Makofi)*

Swali la pili la Mheshimiwa Cheyo, linasema, kwa nini tunazuiwa kuuza Kenya na kero ambazo wafugaji wanazipata wakati wanaswaga mifugo yao kwenye masoko?

Kuuza Kenya sehemu hii ya swali ni tosha majibu ambayo Mheshimiwa Waziri wa Afrika Mashariki kwa sababu alizozitoa na kwamba kama alivyotoa ahadi Serikali inashirikiana na nchi jirani kuhakikisha kwamba taratibu zinapangwa haraka iwezekanavyo ili kuondoa kero kwa wafugaji lakini pia kuhakikisha kwamba tunaboresha pato la Taifa kupitia mifugo. Napokea kero aliyozungumzia ya wafugaji hao wanapokuwa wanapeleka ng'ombe masokoni, katika maeneo ambayo ameyataja, kero hizi zilikuwa hazijanifikia mimi Waziri, nazipokea na namuahidi Mheshimiwa Mbunge kuwa tutazishughulikia Wizarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Mbunge John Cheyo, amezungumzia kuwa mifugo hii ina thamani kubwa sana, Serikali ina mikakati gani katika kuhakikisha kwamba tunaboresha ufugaji nchini Tanzania? Naomba kusema kupitia kwa hotuba ambayo tumeitoa na taratibu mbalimbali zikijumuishwa utengaji wa maeneo, zikijumuisha ruzuku kwa madawa ya kuogeshea, ukijumuisha pia ujenzi wa miundombinu ya masoko na miundombinu mingine ambayo inasaidia kuboresha ufugaji

kwamba, Serikali ina mkakati mzuri na kufuatana na keki ambayo tunayo kuhakikisha kwamba tunaboresha ufugaji nchini kwetu. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cheyo, hapa ni kupata tu ufafanuzi. Hebu kaa chini. La kwanza ulilouliza ulisema kwamba labda ni ubaguzi kwamba ng'ombe na wafugaji waliokwenda katika maeneo ya mabonde ambapo ilionekana kwa hali ya mazingira ya nchi yetu pengine ingekuwa na athari kubwa, wametimuliwa tu bila kuelekezwa waende wapi.

Nilivyomwelewa Mheshimiwa Waziri, amesema kwamba, wamekutana Wizara zote tatu, wanapanga utaratibu mchana na usiku ili hilo liwezekane.

La pili, kwa nini wafugaji wanazuiwa kwenda Kenya? Mheshimiwa Waziri wa Afrika Mashariki ameelezea juu ya utaratibu ambao utawekwa kisheria, lote hilo liweze kufanyika.

Hili la tatu nadhani ulikuwa unatoa maoni tu, kwanza niliruhusu kwa makosa, unasema tu ng'ombe wana thamani, mipango gani, tuko hapa kuzungumza hiyo, mipango si ndiyo hiyo imo kwenye Bajeti? Sasa sijui kama una jipya, lakini nakuruhusu maana yake una nafasi, unaruhusiwa kwa Kanuni usimame tena uulize. *(Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sio adabu kugombana na Spika na mimi ni mtu mzima, nauliza ili kujaribu kusaidia watu. Unaposema unafanya mipango kwa wale watu ambao umewahamisha ng'ombe, siyo sawa sawa na mawe kwamba unaweza kuyaweka kwa siku 20 au 30 hawajui watakunywa maji wapi, hawajui watachungwa wapi. Angekuwa kwamba, wakati wanafanya utaratibu, ng'ombe waliopo waende kunywa kule ambapo walikuwa wanakunywa zamani, wachunge kama walivyokuwa wanachunga, hilo ningeridhika.

Lakini kuniambia tunafanya utaratibu, hujaniambia sasa yule mfugaji ambaye ana ng'ombe wake sasa hivi anafanya nini, mimi nikwambie basi. Sasa watu wanakwenda usiku kunywesha katika sehemu zile ambazo zimekatazwa na njiani wanahonga ili kwenda kunywesha maji.

Kwa hiyo, jibu lake halinipi au wafugaji wale haliwapi raha hata kidogo kwamba tunaambiwa wanafanya mipango. Sasa wale wapi wanyweshe mifugo yao? *This is what I want to know, very specific.*

**MWENYEKITI:** Hilo ni halali kabisa. Hawa ng'ombe sijui laki sita sijui kweli wako wapi sasa, wanahudumiwa vipi!

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi kwa hoja ambayo Mheshimiwa John Cheyo ameitoa. Ufafanuzi ni kama ifuatavyo: Lilikuwa muhimu kwa kipindi hiki ni kuhakikisha kwamba chanzo kile cha maji kinakuwa huru ili kiwe na manufaa siyo tu kwa wafugaji, bali kwa wananchi wote wa nchi ya Tanzania. *(Makofi)*

Serikali kwa umakini wake imehakikisha kwamba zoezi hili imelifanya kipindi kizuri, kipindi ambacho wafugaji maeneo yetu hayana uhaba wa malisho wala maji. Wafugaji hawa katika maeneo walipo wana malisho ya kutosha na wana maji ya kutosha, kuna wafugaji wachache ambao wameingia maeneo ambayo wamepata migogoro na wananchi wengine waliokuwa huko, lakini inatatuliwa kupitia kwa uongozi uliokuwepo na hakuna tatizo kubwa la aidha malisho au maji kwa sehemu ambazo wafugaji wamekwenda kuchungia.

Wasiwasi wetu mkubwa ni wa kipindi kijacho na hiki tumekitolea kauli na ufafanuzi kwamba tunajitahidi kwa kila linalowezekana kuhakikisha kwamba unyonge wa wafugaji kwamba hawana pa kwenda usikae kwa muda mrefu. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Niko katika *vote 99 program ten - Administration sub-vote* 1001 kifungu 250100. Nilikuwa naomba ufafanuzi kutoka kwa Waziri. Wakati Kambi ya Upinzani inatoa maoni yake na katika maoni yangu kwa maandishi nilikuwa nimeomba kupata maelezo ni kwa nini Wizara haijafanya sensa ya wanyama kwa muda wa zaidi ya miaka 20? Yaani sasa hivi miaka 22 na je wanafanyaje *estimate* zao hasa tukijua kwamba bila kujua idadi ni vigumu sana kufanya *budget estimates*. Sasa naomba kujua Wizara hii inafanyaje *estimate* zake za pembejeo hali ambapo hawajui idadi ya mifugo waliyonayo?

La pili, naomba kujua kuhusu hatma ya Kiwanda cha *Tanganyika papers*. Tunatambua kwamba kiwanda kile kilikuwa kinasindika nyama na tulikuwa tunapata nyama kwa bei nafuu sana, lakini kiwanda kile kimebinafsishwa na sasa hivi kimeachwa holela hakifanyi kitu chochote, sasa nilikuwa naomba kujua Wizara ina mipango gani ya kiwanda kile?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, sensa ya wanyama na hatma ya kiwanda cha *TBPL*.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi wa hoja alizozitoa Mheshimiwa Susan Lyimo kama ifuatavyo: moja Wizara inafanyaje makadirio yake ya huduma kwa Sekta bila ya sensa ya mifugo. Sensa ambayo Mheshimiwa Lyimo hapa anaizungumzia ni ile ya *(head count)* kichwa kwa kichwa ambayo mara ya mwisho tumeifanya mwaka 1984. Naomba kumjulisha Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi kwa ujumla kwamba sensa hii kama nilivyoongea ina gharama kubwa sana na kufuatana na keki yetu mara kadhaa wakati tulipotakiwa kufanya sensa hatukuweza kuwa na hizo *resources* za kufanya sensa. Kwa hiyo, ikabidi turuke kufanya sensa.

Lakini hiyo haikwazi Serikali kushindwa kuweka mipango ya kuihudumia Sekta kwa sababu *head count* ni aina moja ya sensa, lakini kuna taratibu tofauti ambazo naweza kuzitumia kwa ajili ya kufanya sensa. Kwa mfano kuna *sample census* ambayo inafanywa na tumeshawahi kuifanya baada ya mwaka 1984 tumefanya *sample census* mwaka 1993, tukafanya tena *sample census* mwaka 1998 halafu tukafanya tena *sample*

*census* mwaka 2003. Hizi *census* zinatusaidia vizuri kuweza kuweka mikakati ambayo ni halisi, mikakati ambayo haina matatizo katika kuhudumia Sekta ya Mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe pia ufafanuzi kuhusu suala la Kiwanda cha Nyama cha *(Tanganyika Packers Dar es Salaam).* Hiki kiwanda kama nimemwelewa vizuri kilibinafsishwa kwanza kwa madhumuni ya kuendelea kwa kazi ya nyama. Lakini kama anakumbuka nilipokuwa natoa jibu kuhusu kutokuwa tayari kwa Serikali kutumia eneo la Kiwanda cha Mifugo Mbeya litumike kwa kilimo halafu tubinafsishe kiwanda peke yake kwa sababu kiwanda kinatakiwa kiwe na *holding ground* kubwa kuweza kukidhi mahitaji ya uchinjaji na ubora wa wanyama ambao wanachinjwa. Kwa hiyo, moja ya matatizo ambayo yaliyotokea ni kwamba kiwanda kile hakikuwa na *holding ground*.

Kwa hiyo, kwa taratibu za uchinjaji na usindikaji wa nyama kwa ajili ya soko la nje kwa mfano ilikuwa haiwezekani tuweze kukiendeleza kile kiwanda kwa kazi hiyo hiyo. Lakini sasa tuna mradi wa machinjio mapya Dar es Salaam, kwa hiyo, tunatarajia kupata nyama kutoka machinjio hayo na kiwanda hiki sasa kimebadilisha matumizi kwa matumizi mengine.

**MWENYEKITI:** Nadhani inatosheleza.

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kifungu 50 *sub-vote 1001* kifungu kidogo 250100 - Mshahara wa Waziri, mimi nilikuwa nahitaji maelezo ambayo ameshauliza Mheshimiwa Cheyo. Lakini nataka niseme hali ya Mbarali siyo ilivyo kama Waziri anavyozungumza hapa.

Nimetoka huko juzi na Naibu Waziri ana taarifa, Jumamosi nimekutana na wafugaji wapatao kama 50 wa jamii ya Kisukuma, malalamiko ni makubwa sana kwa sababu wameondoka Ihefu kwa kutii amri ya Serikali. Uongozi wa Mkoa kwa kweli umejitahidi sana kuelimisha wafugaji.

Sasa tatizo lilitokea kwamba wametoka sehemu ya Ihefu wamekuja kwenye Vijiji vinavyozunguka Ihefu. Kwa hiyo, kuna Kata kama tatu ambazo zimevamiwa na mifugo mingi sana. Kuna vita ya kichinichini, kwa hiyo kuna watu ambao wanaumizana na huwezi kujua.

Sasa nilitaka kujua maelezo au kujua tamko nilipochangia kwa maandishi nikasema nipate tamko la Serikali kwamba ni lini sasa kazi itafanyika angalau kama ni mwezi mmoja kwa sababu hali ya Mbarali, maji hakuna, mwaka huu hatukupata mvua kabisa, siyo kama miaka mingine inavyokuwa. Sasa ni mwezi mmoja ambao ni wa nane ndipo tutapata angalau maji na sasa wanalisha sehemu zile ambazo wamevuna mazao ikishaisha hiyo tayari vurugu inaanza upya na nina wasiwasi kama mkachelewa mpaka mvua zikianza tayari wataanza kulisha mifugo kwenye sehemu zile ambazo wanalima. Lakini pili, tumepata tenda ya kupandisha Hadhi ya Ihefu kuwa *National Park* kwa maana kwamba hekta zimeongezwa sasa, lile eneo la hekta 80 sasa zitakuwa ni 5140.

Mheshimiwa Spika, hizo sehemu ambazo wafugaji wapo itabidi waondoke tu na hilo zoezi la mwaka mmoja maana yake mwaka kesho 2006 mwezi Juni itabidi tuwe tumeshakamilisha kuwa chini ya *National Park* sasa, ndiyo niliomba tamko la Serikali kwamba je, huu mwezi mmoja hiyo kazi itakuwa imekamilika ili hawa wafugaji wawe na uhakika kwa sababu kuwalundika mahali pamoja na hali kwa kweli ni mbaya siyo kama mnavyofikiri. Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Estherina Kilasi, kama ifuatavyo: Moja, namshukuru kwa taarifa hii ambayo ametupa kwamba hali ya Mbarali siyo nzuri. Ni taarifa ambayo mimi naipokea kwa mikononi miwili, siyo kwa kutokujua, ni mwezi wa Tano ambapo Naibu Waziri Maendeleo ya Mifugo ametembelea eneo hilo kwa siku tatu kamili na kuzungumza na wafugaji wengi na kama wanavyojua, Naibu Waziri anaweza akaongea nao wananchi si tu kwa lugha yetu ya Taifa ya Kiswahili, bali anaweza akaongea nao katika lugha ya kwao kwa sababu yeye mwenyewe ni mmoja wa hao. Baada ya hapo, mimi nilikuwa na mawasiliano ya karibu na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya na taarifa hii ambayo ananipa naona ni taarifa mpya na kwa namna hiyo, naipokea kwa mikono miwili nitaifanyia kazi. *(Makofi)*

Kuhusu ahadi ya lini kazi ya kubainisha na kutenga maeneo itakamilika, naomba niseme kwamba hii kazi tunayoifanya kama alivyozungumza awali kwa ushirikiano wa karibu na Wizara hizi ambazo nimezitaja ikiwemo Wizara ya Ardhi na Wizara ya TAMISEMI, tunaifanya kwa hali ya dharura kwa kutambua kwamba wafugaji hawa inabidi wawe na sehemu ya kwenda. Sasa mara itakapokamilika, tutatoa maelekezo muafaka.

Mheshimiwa Spika, siwezi kusema kwamba katika wiki hii kwa sababu sasa hivi watalaam wako katika *field* katika maeneo mbalimbali na matokeo yake ndiyo ambayo tutakuja kuyajadili na kuyafanyia uamuzi, itategemea kitachopatikana kutoka *field* itakuwaje, nisingependa kusema kitu ambacho kiwe tofauti baadaye kije kiwe tofauti na kilete matatizo makubwa siyo tu kwa Wizara bali kwa Mheshimiwa Mbunge. Nakushukuru. *(Makofi)*

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia Kifungu cha 1001 na Kifungu kidogo cha 250100. Wakati nachangia kwa maandishi nilipenda kujua juu ya mgao wa fedha za uchimbaji wa mabwawa na malambo kwa Mkoa wa Singida.

Kama mnavyojua Mkoa wa Singida ni kati ya Mikoa ambayo inakumbwa mara kwa mara na ukame. Halafu ni Mkoa wa wafugaji, ina mifugo mingi. Sasa nashangaa na ndiyo maana nasimama ili nipate ufafanuzi wa sera kuhusu mgao wa fedha kwa ajili ya uchimbaji wa malambo na mabwawa. Ninavyofahamu, hata Mikoa mingine ambayo sio ya ufugaji lakini imepata pesa nyingi sana katika eneo hilo kuliko Mkoa wa Singida. Sasa mimi ningependa kupata ufafanuzi. Ahsante sana.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lwanji ameuliza kuhusu zile *material* ambazo zimetumika katika kugawa fedha za ujenzi wa malambo na maeneo mbalimbali kama tulivyoainisha. Moja ya vigezo ambavyo vimetumika ni mahitaji ambayo tumeyapokea kutoka Halmashauri mbalimbali kwamba kuna maombi ambayo yamefanywa, ilibidi tuyafanyie uchambuzi, lakini pia kuangalia maeneo mbalimbali ambayo kwa kipindi kilichopita yalikuwa yameathirika na ukame.

Sasa kufuatana na keki ambayo ilikuwepo, ilikuwa hamna njia ya kupeleka lambo au bwawa katika kila sehemu ambayo tulidhani ilikuwa muhimu kufanya hivyo, keki ambayo ilikuwepo iliruhusu maeneo hayo tu ambayo yametajwa. Naomba Mheshimiwa Mbunge avute subira ya Serikali kwamba huu sio mwisho wa harakati na nguvu ya Serikali katika kuwahudumia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 1002 - *Finance and Accounts...* Sh. 559,230,000/=
Kifungu cha 1003 - *Policy and Planning...* Sh. 616,642,200/=
Kifungu cha 1004 - *Livestock Research and Training Institute...* Sh.2,148,364,100/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa na wewe umechelewa. Sijui mnaniona! Naangaza hivi ili kuona lazima uwe na kitabu na unafuata. Vinginevyo, kazi ya Kamati itakuwa ngumu sana. Endelea!

Kifungu cha 1005 - *Information, Communication and Education Techn....* Sh. 106,000,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 7001 - *Veterinary Services ...* Sh. 2,819,122,400/=

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko *programu 70, Sub-Vote 7001,* Kifungu kidogo 260400- *Medical Supply and Services*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliwahi kupata *amendment* ya madawa ya mifugo. Nadhani vifungu hivi vinabadilishwa wakati ikionekana kwamba kuna kosa. Kwa hiyo, hiyo tuliyoipata ndiyo sahihi. Kwa sababu ndiyo mabadiliko. Mheshimiwa Waziri alisema kwamba vimetolewa kwa makosa lakini bado atafuatilia kumwomba Waziri wa Fedha hizo fedha kwa ajili ya madawa. Nakumbuka kwamba Bajeti zote tulizozipitisha kwa kila Wizara hizo fedha hazipo. Ni kwamba, siyo kwamba ni pesa *cash* zilizoko Benki. Ni kwamba zinakusanywa na baadaye zinagawanywa. Kwa nini hii ikafutwa tusisubiri tu ikiwa hizo bilioni 2.2 tusubiri mpaka zipatikane, lakini kwenye maandishi ionekane. Ningeomba tu ufafanuzi kwa nini ile haikubali kama vile mlivyosahihisha? Naomba ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Laizer, katika hatua hii, Kamati hii haina uwezo wa kujitafutia nyongeza kwa kutafuta kifungu na kusema sasa iwe Shilingi bilioni mbili, haiwezekani. Ufafanuzi Mheshimiwa Waziri alikwishautoa. Ziko namna na wewe kama mzoefu unazifahamu, iko *reallocation warrants,* zipo *supplimentary estimates.* Hizo ndiyo nilizomsikia anajibu hoja zako alikuwa anajielekeza huko na mimi nilidhani ni jibu zuri tu, kwamba kiwepo hiki 588 milioni halafu majadiliano yanavyoendelea kwa kutambua hiyo hoja unayoisema ili kwa taratibu, tunaelewa miradi yote Bajeti ndiyo, lakini kama unavyofahamu Bajeti ikishapangwa kuna miradi mingine inakwenda haraka kuliko mingine. Sasa ile inayochelewa mara nyingi tunaokoa fedha na kupeleka kwingine, ndiyo zile *reallocation warrants* na pia *supplimentary estimates.* Naomba tuwe na subira.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Sasa zimebaki dakika 10. Kwa mujibu wa Kanuni, tutapitisha mafungu moja kwa moja bila kwenda kwenye vifungu moja kwa moja. Hiyo inaitwa *Guillotine. (Makofi)*

Kifungu cha 8001 – *Animal Producation...* Sh. 3,116,132,300/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**VOTE 99 – WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO**

Kifungu cha 1001 – *Administration and General... ... ... ...* Sh. 150,000,000/=
Kifungu cha 1003 – *Policy and Planning...* Sh. 3,501,849,000/=
Kifungu cha 1004 – *Livestock Research and Training Institute...* Sh. 3,732,811,000/=

Kifungu cha 7001 – *Veterinary Services...* Sh. 1,784,600,000/=
Kifungu cha 8001 – *Animal Producation ...* Sh. 745,400,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

## T A A R I F A

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi ya Bunge Zima imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo ya mwaka 2006/2007 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila ya mabadiliko. Hivyo naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali Makadirio hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.
**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja iliyopo mbele yetu ni kuyapitisha na kuyakubali Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo kwa mwaka 2006/2007. Hoja hiyo imetolewa na Mheshimiwa Waziri na imeungwa mkono. *(Makofi)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo kwa Mwaka 2006/2007 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nimepata taarifa chini ya Kanuni ya 21(6) , nimepokea taarifa ya Mheshimiwa Mbunge mmoja ambaye anataka kutoa maelezo binafsi. Kwa hiyo, nitamwita. Kabla ya kumwita, nitamwomba Waziri wa Nchi, aweze kutoa hoja ya kuahirisha Bunge ili tupate nafasi ya kumsikiliza huyo mwenzetu.

## KUAHIRISHA BUNGE KABLA YA WAKATI WAKE

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa liahirishwe mpaka kesho saa tatu asubuhi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Pamoja na kuwa hoja hiyo imeungwa mkono, lakini kwa sababu Kanuni ya 21 (6) inatuhitaji tumsikilize huyo mwenzetu. Namwita Mheshimiwa Charles M. Kajege.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nasimama kutoa maelezo yangu binafsi kwa mujibu wa Kanuni Na. 21(6). Wakati nikichangia hotuba ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Julai, 19 mwaka huu wa 2006, mojawapo ya masuala niliyozungumzia ilikuwa ni tuhuma za Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mahige, iliyopo Kwimba kumbaka mwanafunzi wa kike. Katika maelezo yangu, nilisema, pamoja na mambo mengine, kwamba yule msichana alipata *mis carriage,* yaani mimba ilitoka kabla ya kujiunga na Kidato cha Kwanza, ukweli ni kwamba ile mimba haikutoka na yule msichana alijifungua mtoto wake salama. Hivyo nakubaliana na maelezo yaliyotolewa na Serikali kwamba yule msichana alijifungua mtoto salama. Nachukua fursa hii kuomba msamaha kwa wale wote waliopata usumbufu wa aina yoyote kutokana na maelezo niliyotoa.

Kosa nililolifanya ni kuamini walalamikaji na kuyaleta hapa Bungeni bila kuyafanyia utafiti kwanza, kufahamu usahihi wake, *I was mis leaded.* Hata hivyo, kwa vile maelezo yangu mengine ni sahihi kuhusiana na tukio hili, naiomba Serikali ilifuatilie kwa uzito unaostahili ili wahusika wote wawili Mwalimu Mkuu na msichana anayemtuhumu waweze kutendewa haki mbele ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Kwa mujibu wa Kanuni, maelezo kama hayo hayana mjadala. Kwa hiyo, sasa tutarejea kwenye ile hoja ya kwanza ya Mheshimiwa Waziri ya kuahirisha Bunge hadi saa tatu asubuhi. Kwa hiyo, kabla sijatangaza tu kuahirisha, napenda kusema kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu kesho asubuhi atasafiri kwenda Dar es Salaam na tunamtazamia kurejea kwa kile kipindi cha saa 11.00. Wakati akiwa kazini Dar es Salaam, amemteua Mheshimiwa Mohammed Seif Khatib, Mbunge, Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, kuwa Kaimu Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni. Napenda kwa niaba yenu nimpongeze Mheshimiwa Mohammed Seif Khatib, kwa sababu sasa imekuwa ni kama mazoea. Kwa hiyo, inaonyesha anamudu mambo haya. *(Kicheko/Makofi)*

Mimi pia nitalazimika kwenda Dar es Salaam asubuhi na Mwenyekiti - Mheshimiwa Jenista Mhagama atashughulikia Kikao cha Asubuhi. Baada ya kusema hayo sasa naliahirisha Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 01.44 Usiku Bunge liliahirishwa Mpaka siku yaJumanne,*
*tarehe 25 Julai, 2006 Saa Tatu Asubuhi)*